**6 FEBRUARI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Tano – Tarehe 6 Februari, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. VINCENT P. MBOGO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi zitokanazo na UVIKO–19 kupitia Ufadhili wa Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF) (Report of the Controller and Auditor General on Implementation of* Tanzania *COVID – 19 Socio – Economic Response and Recovery Plan (TCRP))*.

**MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo aulize swali lake.

Na. 68

### Ujenzi wa Kituo cha Afya Mchomoro – Namtumbo

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa Shilingi Milioni 100 kumalizia Kituo cha Afya Mchomoro zilizoahidiwa na Rais wa Awamu ya Tano?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Jimbo la Namtumbo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Mchomoro kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kimejengwa kwa nguvu za Wananchi, fedha za Halmashauri, Mfuko wa Jimbo, pamoja na wadau. Ujenzi wake ulianza mwaka 2019 na kiasi cha Shilingi Milioni 52.5 zimetumika, kujenga jengo la wagonjwa wa nje ambalo limekamilika na linatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kituo hiki hakina miundombinu muhimu ya kukiwezesha kutoa huduma za ngazi ya kituo cha afya, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024, itatenga Shilingi Milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niishukuru Serikali, kwa kuamua kwamba itatenga *shilingi* Milioni 400 katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 ili kukimalizia kituo cha afya cha Mchomoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, sisi pia tuna vituo vitatu, Kituo cha Mkongo, kituo cha Rusewa na kituo cha Mputa vya afya, ambavyo ni vya siku nyingi sana. Tuliahidiwa katika Bunge lako tukufu hapa kwamba vitafanyiwa ukarabati.

Je, Serikali ni lini itafanyia ukarabati vituo vya afya vya Mkongo, Rusewa na Mputa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Jimbo la Namtumbo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Namtumbo ina vituo hivi vitatu vya afya, amabvyo ni vya siku nyingi vimekuwa chakavu, Serikali imeweka mpango wa kuainisha vituo vyote chakavu lakini kutenga fedha kwa awamu, kwa ajili ya kuvikarabati. Kwa hiyo, ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge wakati tunatekeleza utaratibu huo, vituo hivi vya afya pia vitaingia kwenye mpango na kukarabatiwa kwa awamu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na sasa ninamuita Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang aweze kuuliza swali lake.

Na. 69

**Ujenzi wa vyumba vya kujifungulia kwenye Zahanati za Dirma, Laghanga na Getanus - Hanang**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga vyumba vya kujifungulia akina Mama kwenye Zahanati za Dirma, Laghanga na Getanus?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa vituo vya kutolea huduma za afya kutoa huduma ya kujifungua, zikiwemo zahanati za Dirma, Laghanga na Getanus zilizopo Halmashauri ya Hanang. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitia Halmashauri ya Hanang itatenga kiasi cha shilingi milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha kujifungua katika jengo la Zahanati ya Laghanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, upanuzi wa vyumba vya kujifungua katika zahanati za Dirma na Getanus utafanyika katika mwaka wa fedha 2024/2025. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, changamoto ya ufinyu wa maeneo ya kutolea huduma ya afya ya mama na mtoto hasa eneo la kujifungulia ipo maeneo mengi ndani ya Wilaya yangu ya Hanang.

Je, sasa Serikali haioni ni wakati muafaka kufanya tathmini ya jumla wakati tukiendelea kupanga mpango wa kujenga kituo cha afya kila Kata ili kufanya maboresho katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili fedha zilizotengwa kwa zahanati ya Laghanga, milioni 10. Je, Serikali haioni kwamba hizo fedha ni kidogo haiwezi kutosheleza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba zahanati zile ambazo zilijengwa miaka ya nyuma zilikuwa ndogo na vile vyumba vya kujifungulia vilikuwa finyu lakini kwa sasa Serikali imeboresha sana ramani zetu, ramani zetu ni kubwa zina vyumba vya kutosha vya kujifungua, lakini pia vya kupumzika wakina mama baada ya kujifungua. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba kwa ramani za sasa tutajenga zahanati zenye nafasi za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga vituo vya afya kila Kata utaratibu wa Serikali tutajenga vituo vya afya vya kimkakati katika maeneo ya kimkakati ambayo yana idadi kubwa ya watu lakini umbali mkubwa kutoka kituo cha huduma cha Jirani zaidi. Lakini hii shilingi milioni 10 imetengwa kutoka mapato ya ndani na chumba kinakwenda kuongezwa katika jengo lile ambalo linatumika kwa sasa, kwa hiyo tunaamini itatosha na kama haitatosha basi Serikali itaongezea kuhakikisha kwamba chumba hicho kinakamilika. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Jerry Silaa, swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kituo cha afya cha Nguvukazi - Chanika kinahudumia mama na mtoto na Serikali, ni lini sasa itaona umuhimu wa

kujenga majengo wezeshi kama wodi za wanawake, wanaume na chumba cha kuhifadhia maiti ili kituo cha afya hiki kipate hadhi ya kuwa Hospitali na kuwahudumia wananchi wa Kata za Chanika, Buyuni, Zingiziwa na Msongola?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa JImbo la Ukonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kituo cha Afya hiki cha Chanika kinahudumia wananchi wengi na tulishatoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam kwa maana ya Manispaa ya Ilala, kutenga fedha kati ya asilimia 60 kwa ajili ya kufanya upanuzi na ujenzi wa wodi katika kituo hiki. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumuelekeza Mkurugenzi kwamba hiki ni kipaumbele cha wananchi ahakikishe anatenga fedha kwenye mapato ya ndani ili tuweze kujenga wodi hizo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Sasa ninamuita Mheshimiwa Asha Abdullah Juma aweze kuuliza swali lake.

Na. 70

**Huduma za afya ya uchunguzi na kujikinga mashuleni**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kushughulikia huduma za afya kwa uchunguzi tiba na kujikinga katika Shule za Msingi na Sekondari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri – TAMISEMI, Mheshimiwa Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya afya kinga na tiba shuleni ni afua muhimu inayotekelezwa na Serikali kuwajengea watoto uelewa wa kujikinga na magonjwa. Huduma hii inahusisha utoaji wa elimu ya afya, utambuzi wa magonjwa katika hatua ya awali pamoja na uratibu wa kupata matibabu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri imeendelea kuratibu utolewaji wa elimu na huduma za afya kwa watoto walioko shuleni, hususani kwenye magonjwa ya malaria, minyoo, kichocho, saratani ya mlango ya kizazi, afya ya kinywa, meno pamoja na macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya iligawa vyandarua 3,104,401 kwenye shule za msingi 7,639 kwa uwiano wa chandarua kimoja kwa kila mtoto. Pia, chanjo ya kuzuia maambukizi ya saratani ya mlango wa kizazi ilitolewa kwa wasichana 623,501 dozi ya kwanza na 472,460 dozi ya pili. Aidha, kila mwaka hufanyika kampeni ya utoaji dawa za minyoo na matone ya vitamini ‘A shuleni, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Serikali.

Kwa kuwa mchakato wa bima ya afya kwa wote umo mbioni kukamilishwa, na kwa kuwa miaka ya nyuma kulikuwa na utaratibu mzuri wa kwenda kuchunguza afya za watoto mashuleni kwa vipindi kadhaa kwa mwaka. Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha mpango huu wa kuchunguza afya za vijana wetu shuleni walau mara mbili kwa mwaka, katika jitihada za kupunguza gharama kwa kugundua maradhi mapema ili kukinga na kuwapunguzia wanafunzi hawa shida au wazazi wao kupeleka hospitali wanapokutwa maradhi yameshawatokea?

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri – TAMISEMI, majibu kwenye swali hilo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni muhimu sana kuwa na utaratibu wa ku-*check* afya za wanafunzi shuleni angalau mara mbili kwa mwaka, utaratibu huo uko kwenye miongozo yetu, ni kweli kwamba hapa katikati ufanisi wake umepungua kidogo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwanza tumepokea ushauri wake tutakwenda kutekeleza, pia nitoe maelekezo kwa Wakuu wa Shule na Halmshauri zetu kuhakikisha wanaweka utaratibu kwa kutumia Waratibu wa Elimu, pia na Waratibu wa Huduma za Afya katika shule ili watoto wetu wachekiwe mara kwa mara afya zao na kupewa matibabu mapema. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahasnte. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na sasa namuita Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, aulize swali lake.

Na. 71

**Kuwawezesha wachimbaji wadogo wanawake**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuwawezesha wachimbaji wadogo wanawake kwa kuwapa mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha wachimbaji wadogo hususan wanawake wanapata mikopo, Serikali kupitia *STAMICO* imepanga kununua mitambo mitano (5) midogo ya uchorongaji (utafiti madini) ambapo taratibu za ununuzi wa mitambo hii zinakamilishwa hivi sasa. Mitambo hiyo itawazesha wachimbaji wadogo kujua kiasi cha mashapo yaliyopo katika maeneo yao. Aidha, *STAMICO* imeingia makubaliano ya ushirikiano (*MoU*) na baadhi ya mabenki nchini kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo wakiwemo wanawake. Benki hizo ni *CRDB*, *NMB* na *KCB* ambapo katika utekelezaji wa makubaliano hayo, benki hizo zimejengewa uelewa wa sekta ya madini na namna nzuri ya utoaji mikopo kwa sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini imekuwa ikiwahamasisha wachimbaji wadogo hususan wanawake kujiunga katika vikundi ili kurahisisha utoaji huduma mbalimbali zinazolenga kuwawezesha kupata fedha, vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo: -

(a) Je, Mhesnimiwa Naibu Waziri, anaweza kunieleza ni vikundi vingapi na kwa kiasi gani vya wanawake wa Mkoa wa Ruvuma wamekopeshwa fedha hizo?

(b) Serikali ina mpango gani wa kutumia *survey data* ili kuwa ni dhamana ya kuweza kuwakopesha hao wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu wachimbaji wengi hawana dhamana ya kuweka kwenye mikopo yao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili madogo au swali moja lenye kipengele (a) na (b) la Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Ruvuma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa idadi ya waliokopeshwa kutoka Mkoa wake, hatujaweka mchanganuo wa kimkoa lakini kwa ujumla wakiweko wachimbaji wadogo wanawake na wanaume hadi sasa zaidi ya vikundi na wachimbaji wadogo 110 wameshafikiwa na mikopo kutoka mabenki ya ndani ambayo yamekubali kukopesha wachimbaji waliokidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili kuhusu *data* za jiolojia kutumika kama dhamana ya kupata mikopo ya benki, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba, tutakapokuwa tumepata hivi vifaa vya kuwasaidia wachimbaji wadogo kwenye utafiti, *data* zile sasa zitatumika kama mojawapo ya vigezo ikiwepo pia wao kuweka kumbukumbu za uchimbaji wao, ndiyo maana hata waliofanikiwa kufanya hivyo hadi sasa, watu 110 walio

kwenye mnyororo wa thamani wa madini wameshakopeshwa zaidi ya Bilioni 80 na Benki ya *NMB* na Benki ya *CRDB* pia imeshawakopesha kiasi cha Bilioni 65. Kwa hiyo, Bilioni 145 zimeshawasaidia wachimbaji waliojipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa wanavikundi walioko katika Mkoa wake nao wajipange, waweke taarifa zao sahihi na mitambo hii ikija tutafanya utafiti na wataweza kutumia kama moja ya vigezo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Masache Kasaka, nimekuona.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali pamoja na kuwa imeweka utaratibu wa kutoa mikopo kupitia taasisi za kifedha, lakini mikopo hii imekuwa na masharti magumu amabyo wachimbaji wetu wadogo wengi wameshindwa kuweza kuyafikia.

Je, Serikali haioni haja sasa ya kupunguza masharti na ikiwezekana iweze kutoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo ili tuweze kuwasaidia katika uchumi wa madini.

**MWENYEKITI:** Mhehsimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kasaka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya kibenki yanaonekana kuwa ni magumu kwa sababu wachimbaji wadogo hawajapata uelewa mzuri wa namna ya kujipanga kupata mikopo hii. Kazi yetu kama Wizara imekuwa ni kutoa

elimu ya vigezo muhimu ambavyo wanatakiwa wazingatie ili waweze kukopeshwa au waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Wizara tutaendelea kujadiliana na mabenki na kuona namna ya kutengeneza masharti rafiki na rahisi kueleweka ili wachimbaji hawa waweze kupata mikopo bila usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na wanawake hawa kupata mikopo kuna shida kubwa sana kwenye biashara ya madini wanawake kupata masoko. Serikali ina mpango gani wa kujipanga kuhakikisha wanawake hawa pamoja na kwamba wanapewa mikopo lakini pia watafutiwe masoko ili bishara zao ziende vizuri?

**MWENYEKITI**: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri Madini, majibu kwa ufupi.

**NAUBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti suala la masoko sio *issue* tena nchini kwetu baada ya Wizara kuanzisha masoko ya madini na vituo vya kununua madini nchini. Kwa sasa tuna zaidi ya masoko 47 na vituo 84 na bei elekezi hutolewa na Wizara kila wakati na kwa madini ya dhahabu bei ya dunia hutumika katika kuwapa bei stahiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Namuita Mheshimiwa Yustina Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 72

**Uwanja wa Ndege Manyara**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanja cha Ndege katika Mkoa wa Manyara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utaratibu wa kutwaa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Manyara.

Mheshmiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imeshamaliza kuandaa hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata mhandisi elekezi atakayefanya upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina ili kubaini gharama za ujenzi. Hivyo, ujenzi wa kiwanja hicho utaanza baada ya usanifu kukamilika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali madogo ya nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa

hatua hiyo, sasa tunaelekea kwenye upembuzi yakinifu pamoja na usanifu. Sasa hamu ya wana Manyara ni kuwa na kiwanja cha ndege. Sasa Serikali imejipangaje kukamilisha hatua hiyo ya usanifu?

Swali langu la pili, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kufidia wananchi ambao maeneo yao yatatwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege baada ya kukamilisha uthamini huo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza, kama nilivyosema, tumeshatafuta mhandisi elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina; na huyo ndie atakayetupa sasa gharama halisi ya fidia. Baada ya hapo Serikali basi itatafuta fedha ili kabla hatujaanza ujenzi tuwafidie hao wananchi amabo watapisha ujenzi wa eneo hilo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea namuita Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 73

**Mafao ya wastaafu wa ATCL**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza: -

Je, ni lini wastaafu wa ATCL watalipwa mafao yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Malembeka Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kabla ya kuanza kwa juhudi za ufufuaji wa *ATCL* Septemba 2016, *ATCL* ilikuwa ikikabiliwa na changamoto za uendeshaji kwa kukosa mtaji, kuwa na ndege mbovu, kushindwa kulipa madeni ya wazabuni na kutowasilisha michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii. Aidha, baada ya mwaka 2016, *ATCL* imekuwa ikiwasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia uhakiki uliofanyika, *ATCL* ina madeni ya jumla Shilingi 4,864,673,387.85 yanayotokana na kutowasilisha michango ya wanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Fedha za kulipa madeni hayo zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023. Hivyo, madeni hayo ya michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya jamii yatalipwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Malembeka, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nampongeza kwa jibu lake zuri ambalo

linaridhisha. Swali langu la kwanza; kwa kuwa deni hilo la wastaafu lilirithiwa kabla ya mpango maalum wa kufufua *ATCL,* nilitaka kujua sasa hivi Serikali ina mpango gani wa kuzuia kuzalisha madeni mengine mapya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali imejikita zaidi katika kutoa mafunzo mbalimbali katika vyuo vyake ikiwepo Chuo cha Usafirishaji, nilitaka kujua hadi sasa tuna marubani wangapi wazalendo ambao wako katika ndege zetu za *ATCL*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami niweze kujibu maswali mawili ya nyongeza, ya Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala haya ya *ATCL.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua mpango wa kuzuia madeni mapya baada ya kuanza mpango ule wa ufufuaji wa kampuni hii yetu ya ndege nchini. Serikali imejipanga kuzuia ama kutozalisha madeni mengine. Hadi sasa tangu mwaka 2016 tumekuwa tukilipa wafanyakazi wote na hakuna deni jipya; lakini kwenye mwaka wa fedha huu 2022/2023 ambao tunaendelea nao tumetenga takribani kiasi cha shilingi bilioni 10 ili kulipa wafanyakazi wote waliokuwa wa *ATCL* kama deni la nyuma.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anataka kujua idadi ya marubani tulio nao hapa nchini hususan wanawake na wanaume. Tuna takribani ya marubani 106. Kati ya hao marubani 11 ni wanawake na marubani 95 ni wanaume; kwa maana ya kwamba hawa wanawake wanarusha ndege

zote kwa sababu hapa nchini tuna ndege aina tatu ambapo tuna *Dash 8Q400, Bombardier al* maarufu *Bombadier* ama sasa hivi inaitwa *DeHaveland* lakini pia tuna *Airbus 220-300* ambapo pia wanawake wanarusha na tuna *Boeing* 787-8 ambayo pia wanawake wanarusha hizi ndege. Na kati ya hao 106. 105 wote ni watanzania, ni mmoja tu ambaye sio Mtanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Namuita Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi aulize swali lake.

Na. 74

**Ukarabati Mahakama ya Wilaya - Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Mahakama ya Wilaya ya Lushoto.?

**MWENYEKITI:** Majibu ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshmimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania inaendelea kutekeleza kwa awamu Ujenzi na ukarabati wa majengo yake sehemu mbalimbali hapa nchini. Katika mpango huu, yapo majengo ambayo yanahitaji kujengwa upya kutokana na hali yake na ufinyu wa jengo ikilinganishwa na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kulingana na hali ya jengo la Mahakama ya Wilaya ya Lushoto, imeamuliwa kuwa jengo hili lijengwe upya badala ya kukarabatiwa lile jengo lililopo kwani ni la zamani sana, finyu na baadhi ya miundombinu yake hairuhusu ukarabati mkubwa. Hivyo, kulingana na Mpango, jengo jipya la Mahakama ya Wilaya ya Lushoto litajengwa kwenye kipindi cha fedha 2024/2025. Aidha, kwa sasa jengo lililopo litaendelea kufanyiwa matengenezo madogo madogo hadi litakapopatikana jengo jipya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa mwenyekiti, nakushukuru, pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lushoto lina Mahakama za mwanzo mbili, kwa maana Mahakama ya Mlola na Mahakama ya Gare. Lakini hii ya Gare takribani miaka 20 sasa haifanyi kazi yani jengo lake limekeuwa ni gofu.

Je, Serikali in ampango gani wa kujenga upya Mahakama ya Gare pamoja na kata jirani ili waweze kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshmimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi kama ifuatavyo: -

Mheshmimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mahakama ya Tanzania katika mpango wake inajenga Mahakama za Mwanzo katika Makau Makuu ya Tarafa zote hapa nchini.

Kata ya Gare haipo kama sehemu ya Makao Makuu ya kata kwa sababu iko ndani ya Tarafa ya Lushoto yenyewe. Hivyo tunaangalia uwezekano wa kuzipa umuhimu kata ambazo zina uhitaji maalum. Baada ya Bunge hili tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge kujua uhalisia wa tatizo la Gare lakini kwa sasa tunaelekeza nguvu zetu Makao Makuu ya Tarafa hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Mahakama ya Mwanzo ya Mbagala ambayo ina hali ngumu sana, mazingira yake na idadi ya watu wanaopata huduma pale ni wengi sana?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri, Katiba na Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tumelichukua ombi lake na tutakwenda kulifanyia kazi ili tuweze kuiweka katika mazingira mazuri ya matumizi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wiazra ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mnamuita Mheshimiwa Neema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu aweze kuuliza swali lake.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ubadilishe jina siitwi Neema naitwa Rehema.

Na. 75

**Ujenzi wa minara yenye kasi kubwa – Kata za Ulyankulu**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza: -

Je, ni lini Minara yenye Kasi Kubwa itajengwa Kata za Nhwande, Kanoge, Uyowa, Silambo, Makingi, Ichemba, Igombemkulu na Mwongozo?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Babari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetekeleza miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata tano ambazo ni Kata ya Kanoge, ambapo kuna mnara wa Airtel umejengwa katika eneo la Ulanga, Uyowa katika eneo la Uhindi, Ichemba eneo la Ichemba yenyewe, Igombemkulu katika eneo la Imara na Mwongozo katika eneo la Mwanditi ambapo minara hii imekamilika na inatoa huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Minara ya Kata za Kanoge, Ichemba, Igombemkulu na Mwongozo inatumia teknolojia ya 2G/3G hivyo inatoa huduma za mawasiliano yenye kasi kubwa; na mnara huu uliopo Kata ya Uyowa unatumia teknolojia ya 2G pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Uyowa imengizwa kwenye mpango wa kuboreshewa huduma za mawasiliano

yenye kasi na zabuni yake itatangazwa katika awamu ijayo kulingana na upatinaji wa fedha. Aidha, Serikali itafanya tathmini ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu yenye kasi kubwa katika Kata za Nhwande, Silambo, na Makingi katika mwaka wa fedha 2023/2024, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali linguine la nyongeza. Pamoja na mjibu mazuri ya serikali lakini nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa minara ya simu au huduma za simu zinafanywa kibiashara, na mwananchi anaponunua vocha yake au *internet* anadhamiria apate huduma kulingana na pesa aliyoweka. Hata hivyo, cha ajabu kutokana na kasi ndogo ya hii minara au hizi huduma za simu, wananchi wanafikia mwisho wa muda wa kutumia ile fedha yake ilhali hajapata huduma aliyokusudia. Sasa swali langu;

Je, kwa kuwa hizi fedha za hawa wananchi wangu zinazokuwa zimetumika ilhali hawajapata huduma, je hizi kampuni za simu ziko tayari kuwafidia hao wananchi wetu ambao pesa zao zimetumika bila kupata huduma kwa sababu inaonekana huu ni wizi kama wizi mwingine?

**MWENYEKITI:** Mhehsimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa labda niseme kuwa minara amabayo imejengwa katika hizi kata 4 ambapo

Mheshimiwa Mbunge ameonesha kulalamikia huduma inayotolewa pale, inatoa huduma ya 2G peke yake, haijaanza kutoa huduma ya 3G. Sasa mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaenda ku-*upgrade* minara hii amabyo ilikuwa inatoa huduma ya 2G kwenda kwenye 3G, ambapo tukishafikia kwenye 3G na 4G maana yake kwamba Mtanzania na mwananchi wa Ulyankulu ataweza kutumia huduma ya *internet* bila kuwa na changamoto yoyote ile, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsasnte, Mheshimiwa Nyamoga, nimekuona.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kata ya Masisiwe haijawahi kuwa na mnara wala mawasiliano tangu uhuru wa nchi yetu.

Je, ni lini Serikali itajenga mnara katika kata hiyo ili wananchi waweze kupata mawsiliano?

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi kabisa, tunategemea na majibu pia mafupi hivyo hivyo. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2021/2022 Serikali ilileta vijiji ambavyo vinaenda kupatiwa mawasiliano ikiwemo kata ya Masisiwe. Mheshimiwa Mbunge tayari tushawasiliana na iliingizwa kwenye mradi wa Tanzania ya Kidigitali, mradi amabao umefunguliwa tarehe 31 Januari, 2023. Hivyo basi mchakato wa tenda utakapokamilika tutajua kwamba ni mtoa huduma gani ambaye amepatikana kwa ajili ya kufikisha mawasiliano katika kata ya Masisiwe.

Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Tumbakose na kata ya Kimaha mawasiliano ni hafifu sana, naomba kujua *commitment* ya Serikali kwenda kujenga mnara maeneo hayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo hayana kabisa huduma ya mawasiliano tunatumia Sheria yetu Namba 11 ya mwaka 2006 iliyoanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote kwenda kufikisha mawasiliano kwenye eneo hilo. Lakini kama mawasiliano ni hafifu na kuna changamoto ya ubora wa mawasiliano kwa Sheria yetu Namba 12 ya mwaka 2003 iliyoanzisha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, tunaielekeza Mamlaka ya Mawasiliano *TCRA* iende ikapime ubora wa mawsiliano ili tujiridhishe changamoto ipo wapi, ili tuhakikishe kwamba wananchi wa Chemba wanapata mawasiliano ya hakika na ubora unaotakiwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Katika Jimbo la Newala Vijijini kuna changamoto kubwa ya mawasiliano hasa katika

kata za Chitekete, Makukwe na baadhi ya vijiji vya Nambali na Mkomatu.

Je, ni lini Serikali italeta mawasiliano katika maeneo husika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa jimbo la Newala Vijijini lina changamoto, na mimi nilishafika kule; lakini Jimbo hili baadhi ya kata tuliziingiza katika utekelezaji wa miradi wa *Special Zones and Border,s* lakini vile vile baadhi ya kata tumeziingiza kwenye Mradi wa Tanzania ya Kidigitali. Pamoja na hayo yote Mheshimiwa Waziri pia amepanga timu moja ya kuzunguka na kujiridhisha katika maeneo ambayo yana changamoto kubwa ili tuyapatie kipaumbele, tunaamini kwamba timu hiyo itakapoleta majibu ya tathmini Waheshimiwa Wabunge tutaweza kuwahudumia kwa sababu ni dhamira ya Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata huduma ya mawasiliano, ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini swali la mwisho la nyongeza kwenye Wizara hii.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Katika Jimbo la Kilwa Kusini Kata za Kikole, Kata za Kiranjeranje hususani Kijiji cha Makangaga, Kata ya Nanjilinji hususani Kijiji cha Nakiu na Kata ya Lihimalyao hususani Kijji cha Mangisani na Kisongo hakuna kabisa mawasiliano. Je, ni nini mpango

wa Serikali kwenda kujenga minara kwa ajili ya mawasiliano katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali dhamira yake ni kuhakikisha kwamba inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025. Sisi kama Serikali maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja naomba niyapokee ili twende tukayatazame kwa upana, tutume Timu Maalum ikafanye utafiti na tathmini ili tujiridhishe kwamba tatizo kubwa ni mawasiliano hafifu au hakuna kabisa ili tuweze kuona kwamba ni njia ipi itaenda kutatua tatizo hili, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Injinia Kondo. Wizara hii inaonekana maswali yapo mengi sana, kwa hiyo nafikiri ni vizuri mkajipanga namna ya kuweza kufanyia kazi.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, namwita Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 76

**Kusafisha maji kabla ya kuyasambaza- Arumeru**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kusafisha maji kabla ya kusambazwa ili kuondoa *Floride* ambayo huleta ulemavu kwa Wakazi wa Arumeru?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia katika maeneo mbalimbali yaliyoathirika na madini hayo. Mikakati hiyo ni pamoja na kujenga Miradi ya Kusambaza Maji Safi na Salama kutoka kwenye vyanzo vya maji vya uhakika ambavyo havijaathirika na madini ya *fluoride*; kusambaza teknolojia ya kuondoa madini ya *fluoride* kwa kutumia chengachenga za mkaa wa mifupa ya ng'ombe; na kuweka mitambo ya *reverse osmosis* kwa ajili ya kusafisha maji ikiwa ni pamoja na kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia katika Kata za Oldonyosambu, Ngaramtoni, Embasenyi katika Wilaya za Arumeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara kupitia Kituo cha Utafiti cha Kuondoa Madini ya *Fluoride* cha Ngurdoto imeendelea kutoa elimu kuhusu madhara ya kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na matumizi sahihi ya teknolojia ya kuondoa madini hayo kupitia vyombo vya habari, mikutano na makongamano mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake haya, nimkumbushe tu upatikanaji wa maji ni jambo moja, lakini upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wetu ni haki yao ya msingi na wanahitaji maji haya safi na salama muda wote.

Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha mikakati hii ya kusafisha maji katika Wilaya ya Arumeru ili wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kuwa madhara ya madini haya ya *fluoride* ni makubwa sana kwa wananchi wetu yanayopelekea kupata udumavu na ulemavu.

Je, Serikali haioni sasa haja ya kuanzisha *program* maalum kwa ajili ya kuwatibu wananchi hawa? Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee pongezi zake, lakini vilevile naye nimpongeze kwa namna ambavyo ni mfuatiliaji mzuri na kwa sababu ni mama ndiyo maana anaongelea hata masuala ya ulemavu kwa watoto kwa sababu ni kweli watoto wanaathirika na watu wazima pia. Kama Wizara tunaendelea na utaratibu wa kuona namna njema ya kuwa sehemu ya kuwafariji hawa walioathirika na madini ya *fluoride*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la lini mradi huu utakamilika. Tayari mradi upo katika utekelezaji, mradi

mkubwa ambao utaleta maji katika maeneo yote ambayo yameathirika. Sasa hivi tunatarajia tu mgao ujao wa fedha tuendelee kuleta fedha katika Jimbo la Arumeru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nancy Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante; je, ni lini Serikali itajenga mtambo wa kusafisha na kutibu maji katika Chanzo cha Mgombezi - Ilula?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyalusi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chanzo cha Mgombezi ni moja ya vyanzo muhimu sana katika eneo la Iringa. Katika mwaka ujao wa fedha tuna mradi mkubwa sana wa USD Million 88.4. Kupitia mradi huu tunatarajia chanzo kile pia kiwe sehemui ya wanufaika kwa kupata eneo la *treatment plant,* lakini vilevile maeneo ya Kilolo pia yatapata kunufaika na tunatarajia pia kuwa na uboreshaji wa huduma ya maji safi na maji taka katika eneo la Iringa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa kutibu maji ni gharama sana ili yafikie hatua ya kuwa maji safi na salama na wananchi kuyatumia kwa uhakika, lakini maji hayo hayo yanayogharamiwa sana na Mamlaka za Maji na *RUWASA* na wote ambao na Wizara pia yanatumika kuonyeshea magari, yanatumika kwenye kuzima moto, yanatumika kwenye kufrashi vyoo.

Je, ni lini sasa Serikali hii ya Tanzania italeta mpango mzuri wa kutumia maji safi na salama kwa ajili ya wananchi na maji hayo mengine kwa ajili ya takataka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Wizara ni kuhakikisha maji yote ambayo yanatumia gharama kubwa katika kuyatibu yaweze kutumika kwa matumizi sahihi ya majumbani na kwa kazi kama alizozitaja za uoshaji wa magari, tayari Wizara tuna mpango wa kuona kwamba *raw water,* maji ambayo bado hayajatibika yaweze kutumika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUM M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wananchi wa Wilaya ya Handeni Mjini wanapata maji kutoka kwenye Kisima cha Nderema ambao ni Mradi wa Serikali, tunaishukuru sana Serikali. Hata hivyo, kisima hicho maji yake yana chumvi sana, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanaenda kuchuja maji yale ili yawe maji safi na salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Eng*. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zodo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisima chochote ambacho kimechimbwa na maji yake bado yana tope Serikali kupitia Wizara tumeendelea na mipango madhubuti ya kuhakikisha tunapata *treatment plant* kwenye maeneo hayo, hivyo Mheshimiwa Mbunge, pamoja na hiki kisima ulichokitaja na chenyewe kipo kwenye Mpango wa kuweza kujengewa *treatment plant*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, ahsante sana kwa majibu.

Tunaendelea, sasa namuita Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba, aulize swali lake.

Na. 77

**_Task Force_ zilivyopunguza tatizo la uvuvi haramu katika Ziwa Victoria**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, ni kwa kiwango gani *task forces* zimepunguza tatizo la uvuvi haramu katika Ziwa Victoria kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2017/2018 - 2019/2020, Kikosi Kazi kilifanya

doria na operesheni katika maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Ziwa Victoria. Utekelezaji wa doria hizo uliwezesha kukamatwa kwa zana haramu zilizokuwa zikitumika katika shughuli za uvuvi ikiwemo nyavu za makila, makokoro, nyavu za timba *(monofilament*) na nyavu za dagaa. Pia, vifaa vilivyokuwa vinatumika kwenye uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi ikiwemo injini pamoja na boti na magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa doria hizo katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria uliwezesha kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu, biashara ya samaki wachanga na utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi kwa asilimia takribani 80; ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali la nyongeza, Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Kutokana na Takwimu za Serikali yenyewe, hali ya Ziwa Victoria hususani upatikanaji wa mazao ya samaki ni mbaya sana. Kulingana na viwango ambavyo tumejiwekea katika Ziwa lolote samaki wazazi wanapaswa kuwa kati ya asilimia 3-5 lakini kwa Takwimu ambazo zimetolewa na Serikali hii katika Ziwa Victoria samaki wazazi wako chini ya asilimia 0.85. Swali la kwanza; sasa naomba Serikali inipe majibu upungufu huo hausiani na uvuvi haramu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; *Task Force* zimekuwa zikiendelea Ziwa Victoria, hawa ambao wanatumwa kwenda kufanya hiyo kazi ni wasomi, lakini hawana weledi wowote na masuala ya uvuvi. Matokeo yake wamekuwa wakikamata hizo zana haramu wanawapiga faini zisizo na Kanuni wala Sheria wala sijui nini, baada ya kuwapiga faini wanawarudishia zile zana haramu ambazo zinasadikiwa kuwa ni zana haramu.

Je, Serikali haioni kwamba inaendekeza huo uvuvi wa haramu kwa kutumia self pesa ya walipakodi wa Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, upungufu hauhusiani na uvuvi haramu? Kwa namna yeyote ile upungufu wa samaki wazazi unahusiana na uvuvi haramu na ndiyo maana tumeweka mkakati shirikishi kama Serikali kupitia Vyombo vyetu vyote na sasa tunakwenda katika kutekeleza mkakati ule ambao utakwenda kunusuru na kulinda moja; samaki wazazi lakini mbili rasilimali nzima na kwa hivyo itapelekea kupatikana kwa uendelevu wa rasilimali hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, amehusianisha juu ya vitendo vya baadhi ya maafisa wetu wasiokuwa waaminifu na waadilifu. Nakiri yawezekana wako maafisa wanaofanya vitendo vya kinyume na maelekezo na maagizo ya Serikali. Tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge, ikiwa anafahamu watumishi wanaofanya hivyo, Taratibu, Sheria na Kanuni za Kiutumishi zipo, nataka nimuahidi yeye kwamba tutachukua hatua madhubuti kwa yeyote ambaye anashiriki katika kuharibu *operations* na shughuli za Kiserikali zenye lengo jema kabisa la kulinda rasilimali za nchi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kutoa mikopo ya zana za kisasa za uvuvi kama boti pamoja na pesa kwa ajili ya kufanya uvuvi wa kuvua samaki kwa njia ya vizimba kama njia ya kuzuia uvuvi haramu. Je, ni lini sasa mikopo hii itawafikia wavuvi wetu? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joeseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imejidhatiti katika kuondoa uduni na kero ya Wavuvi kutumia vyombo hafifu na kwa hivyo kupelekea kupatikana kwa vyombo vya kisasa sasa ni lini tunawapitia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari hatua za kimanunuzi zimekalika. Tunazo boti takribani 160 za kisasa zitakazogawiwa kwa wanufaika Wavuvi waliotimiza viwango ambavyo viliwekwa na Serikali na miongoni mwa Wavuvi hao wapo wa kule Ukerewe. Boti hizo zitakuwa ni za kisasa zenye *fish finder,* kwa maana kifaa maalumu kinachoelekeza wapi samaki alipo lakini pia vilevile kitakuwa nae neo la kuhifadhia samaki lisilopungua tani moja, kitakuwa na *GPS* na vifaa vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa pesa takribani bilioni 20 kwa ajili ya zoezi la ufugaji wa samaki kuongeza uzalishaji wa samaki aina ya sato. Walengwa ni pamoja na vikundi vya vijana na akinamama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kuniona. Wizara katika siku za karibuni ilitoa nafasi kwa Vikundi Mbalimbali vya Uvuvi viweze kuomba mikopo katika Wizara hiyo. Swali langu, je, ni lini fedha hizo zitatoka ili ziweze kuwanufaisha wananchi wetu wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Kilwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa wanufaika wa mikopo ile ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Wavuvi inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Wavuvi wa Kilwa, watapata boti hizo na tayari taratibu zimekwishakamilika, orodha ya wanufaika iko tayari tuta-*share* na Waheshimiwa Wabunge wote ili muweze kuona kile mlichokiomba ni hiki kimepatikana na kwa kusudi hilo muweze kuwafikishia walengwa wajipange ili tuweze kutekeleza kazi ya uzalishaji, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi ahsante sana, unaweza kwenda kuketi.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, aweze kuuliza swali lake.

Na. 78

**Hitaji la Kituo cha Polisi – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Kilindi?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua hitaji la Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Kilindi. Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi imeshatoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 15,760 kwa ajili ya kujenga kituo daraja B, pamoja na nyumba za kuishi askari. Fedha za Ujenzi zinatarajiwa kutengwa kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2023/2024; nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nimshukuru pia Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa majibu yenye kutia matumaini kiasi, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Wazari kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi imetenga eneo kwa ajili ya Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa sababu eneo hilo limetengwa takribani miaka ishirini iliyopita je, ni utaratibu upi au mipango ipi au ni *parameter* zipi ambazo zinatumika kuhakikisha kwamba mnajenga Vituo vya Polisi kwa kuangalia uhalisia wa mahitaji ya eneo husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye sasa hivi ni Waziri wa Mambo ya Ndani alikwishatembelea Wilaya ya Kilindi na kujionea uhalisia wa changamoto ya Kituo cha Polisi jinsi kilivyo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kutoa *commitment* kwa wananchi wa Wilaya ya Kilindi kwamba mwakani watajenga Kituo cha Polisi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na ahadi zinatolewa na zimechukua muda mrefu, hususan kituo hiki, eneo limetengwa muda mrefu kama alivyosema miaka 20, na ametaka tuseme tutazingatiaje uhalisia wa maeneo husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, tunapotaka kujenga eneo lolote lazima tuzingatie uhalisia wa eneo. Ndiyo maana wataalam wetu wanakwenda kule kufanya tathmini ya udongo ili kuweza kujiridhisha vifaa na kiwango gani cha ujenzi utakaohitajiwa. Kwa hiyo, watakapokuwa wanaanza ujenzi, mahitaji halisi ya eneo la Mheshimiwa Mbunge yatazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hili la *commitment* nimesema, tutatenga kwenye bajeti ya 2023/2024. Sasa bajeti yetu ikishapita hapa, namwomba Mheshimiwa Kigua asome maeneo yatakayojengewa vituo, atajiridhisha kwamba eneo lake litakuwa na mpango huo wa ujenzi. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naona karibu Bunge zima limesimama sasa. Haya, Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Jimbo la Mlalo, Vituo vya Polisi vya Mlalo na Mtae vipo katika majengo ambayo ni ya Serikali za Vijiji: Je, Serikali ina mpango gani sasa kujenga majengo ya Polisi katika tarafa hizi mbili?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Shangazi, moja, kwa kujenga mahusiano mema na Serikali za Vijiji hata wakapata majengo ya kuazima. Pia, nikiri kwamba majengo yale hayakidhi haja ya vituo vya kisasa vya Polisi. Nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa vile yeye analo fungu kidogo kwenye Mfuko wa Jimbo, nimshauri aweze kutenga kidogo kwa sababu, tumesema vituo vilivyoko kwenye maeneo ya kijamii kadiri wanajamii wanavyoanza kutoa na Serikali inawaunga mkono kumalizia. Kwa hiyo, akianza tu anipe taarifa na sisi Wizarani tutajipanga ili Jeshi la Polisi liweze kuongezea, vituo hivi vya Mlalo na Mtae viweze kukamilika, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba niulize swali la nyongeza kwa niaba ya Jimbo la Mchinga. Kituo cha Polisi cha Mchinga kina ukubwa wa kilometa 30 kwa 40 na bahati nzuri kiwanja kimepimwa, lakini kinakabiliwa na changamoto kadhaa nyingi tu. Changamoto ya kwanza ni uchakavu wa jengo, ikiwa na maana kwamba, paa linavuja kabisa, ukosefu wa usafiri na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, nini kauli ya Serikali juu ya kuboresha Kituo hiki cha Jimbo la Mchinga? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba vipo Vituo vya Polisi vina hali mbaya sana. Kwa kuwa tulishatoa ahadi hapa ya kutembelea Jimbo lile na Wilaya ya Lindi kwa ujumla ili kuangalia uchakavu wa vituo vya Magereza, niahidi kwamba baada ya Bunge hili, nitatimiza ahadi hiyo ya kutembelea Lindi, Mchinga kwa madhumuni ya kuona kiwango cha uchakavu na hatimaye Mkuu wa Jeshi la Polisi aelekezwe kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama atapata nafasi niko tayari kuongozana naye, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi. Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa Wilaya ambazo hazina Kituo cha Polisi, wanatumia Kituo cha Polisi kwenye jengo la Ofisi ya Kata. Halmashauri ya Wilaya la Tanganyika kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wameomba wadau kuchangia, nami nikiwa miongoni mwa wadau kujenga Kituo cha Polisi. Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi ambao wamejitolea ili waweze kukamilisha hicho Kituo cha Polisi ambacho kipo katika hatua ya awali ya msingi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tumpongeze kwa kazi nzuri aliyofanya kama mmoja wa wadau na wadau wengine walioanza ujenzi wa Kituo hiki cha Polisi pale Tanganyika. Kwa niaba ya Waziri wangu, niahidi tu kwamba, tunamwelekeza *IGP* kupitia Makamanda wake waweze kufanya tathmini ya kiwango kilichofikiwa na kiasi gani kinatakiwa kama pungufu ili waweze kuingiza kituo hiki cha Tanganyika kwenye mpango wao wa ujenzi, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika kata 29 zilizopo katika Jimbo la Tabora Mjini kuna upungufu mkubwa kwenye vituo vya Polisi vilivyoko kata za nje. Kata ya Kazima haina kabisa Kituo cha Polisi na uhalifu mwingi unafanyika maeneo yale katika Jimbo la Tabora Mjini: Ni lini Serikali itaweza kuweka mkakati wa kujenga Kituo cha Polisi katika kata hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge Mwakasaka kwa dhamira yake ya kujenga vituo vya Polisi kwenye maeneo ya Tabora. Unajua Tabora wakati fulani ilikuwa na wimbi kubwa sana la uhalifu, hapo katikati wakapoa sana, tukaamini pamekuwa eneo lenye utulivu. Sasa kama wameanza matukioya uhalifu, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Tabora, waangalie maeneo yanayoweza kuwekwa vituo vya kimkakati kama Kazima, basi wayaingize kwenye mpango wao ili Serikali Kuu kupitia Jeshi la Polisi iweze kuwasaidia kukamilisha vituo hivyo. Wakifanya hivyo, tutawaunga mkono, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 79

**Wimbi la mauaji nchini**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuzuia matukio ya mauaji, kujiua na ukatili uliokithiri hasa kwa wanawake na watoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kuwakamata watu wote wanaotenda makosa yakiwemo ya mauaji na ukatili na kuwafikisha Mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake. Uchunguzi wa Jeshi la Polisi unaonesha kuwa matukio haya kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na watu kujichukulia sheria mkononi, imani za ushirikina, wivu wa mapenzi, migogoro ya ardhi, migogoro kwenye ndoa, kugombania mirathi, ulevi na mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kutekeleza mkakati wa kutoa elimu na mafunzo kwa jamii ili wananchi wafuate sheria za nchi katika kutatua migogoro inayojitokeza au wanapodai haki zao. Aidha, wananchi wanaombwa kuwashirikisha viongozi wa kijamii, kimila, kisiasa na kiserikali, wazee au watu maarufu wanaotambulika na kuheshimika ili kuwaasa ipasavyo na hivyo kuepuka kuvunja sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Niishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na *program* maalum hasa kwa kutumia mapolisi kata ili waweze kutoa elimu kwa jamii kuweza kupunguza masuala ya ukatili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi wamekuwa wakisambaza picha ambazo zinaonesha matukio mbalimbali ya ukatili katika mitandao ya kijamii na picha nyingine zimekuwa zikikiuka haki za binadamu na kutweza utu wa wale ambao ni wahanga wa ukatili: Je, Serikali haioni upo umuhimu wa kuwa na namba maalum ya Serikali ambayo matukio yale yatapelekwa kule badala ya watu wachache kusambaza picha hizi katika mitandao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua umuhimu wa kuendelea kuimarisha elimu kwa ajili ya jamii nzima kupitia Polisi wetu wa Kata. Kwa kutambua hilo, ndiyo maana kuanzia mwaka 2022 Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeridhia kutoa ajira zaidi ya Askari Wakaguzi Sasaidizi 3,200 na kupangiwa kwenye kata. Tumeanza kuona baadhi ya kata wameanza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na viongozi wetu kwenye Wilaya na Halmashauri kuwatumia Polisi Kata hawa, hasa wanapokuwa na vikao vyao, mikutano ya hadhara ili waendelee kutoa elimu. Hii itasaidia kupunguza uhalifu kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya ushauri alioutoa wa udhibiti wa usambazaji wa picha zinazokiuka haki na maadili, tunapokea ushauri huo ili tuweze kuufanyia kazi. Ni kweli, baadhi ya picha zinazooneshwa kwenye mitandao ya kijamii nyingine ziko vibaya sana, badala ya kusaidia zinaharibu kabisa. Kwa hiyo, tunaupokea ushauri huo ili tuweze kuufanyia kazi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hakuna swali la nyongeza kwenye swali hili; ooh, Mheshimiwa Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hili wimbi kubwa la ukatili na tabia zote mbaya katika jamii: Je, Serikali haioni sasa iko haja ya kuimarisha Polisi Jamii kwenye vijiji ili angalau huo ukatili uweze kutambulika kwa haraka zaidi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba swali hili linakaribiana sana na swali lililoulizwa na muuliza swali la msingi. Ni kweli, sasa hivi tumeweka hawa Wakaguzi wa Polisi kama viongozi kwenye ngazi hizo za kijamii, lakini pia wapo Polisi wa kawaida wenye vyeo vya chini ili kushirikiana na hawa Polisi Kata. Kwa hiyo, ushauri alioutoa Mheshimiwa

tunauzingatia na ndiyo maana tutaendelea kuimarisha eneo la Polisi Kata kweye kata zetu zote ili waweze kutimiza wajibu wao huu wa msingi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, aweze kuuliza swali lake.

Na. 80

**Hitaji la Kituo cha Polisi Mji wa Mangaka, Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Mji wa Mangaka?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua hitaji la kujengwa Kituo cha Polisi kwenye mji wa Mangaka Wilaya ya Nanyumbu. Tathmini kwa ajili ya ujenzi imeshafanyika na kubaini kuwa kiasi cha shilingi 569,091,050 kinahitajika kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Daraja B. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kwenye Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2023/2024; nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru…

**MWENYEKITI:** Samahani kidogo Mheshimiwa Hokororo, nimpe mwenye swali lake la msingi maswali yake ya nyongeza mawili.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Jimbo la Nanyumbu liko mpakani mwa Tanzania na nchi ya Msumbiji. Sisi sote ni mashahidi kwamba hali ya usalama sisi na ndugu zetu wa Msumbiji siyo nzuri kwa wakati huu. Majibu ya Serikali nayashukuru sana. Sasa swali kwa Mheshimiwa Waziri:-

Je, ni *commitment* gani ambayo unaitoa kwa wananchi wa Jimbo la Nanyumbu kuwahakikishia kwamba katika mwaka huo ujao wa fedha 2023/2024 watapata Kituo cha Polisi ili kuwa na uhakika na usalama wao na mali zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri umemwelewa Mheshimiwa Mhata. Anataka *commitment* ya Serikali kwenye hiki ambacho amekisema.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YANNDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* ni kiwango cha asilimia mia moja. Kama bajeti yetu itapitishwa mwezi Juni, uhakika ni kwamba Kituo cha Mangaka ni moja ya vituo vilivyopangwa kujengwa katika mwaka wa 2023/2024. Kwa hiyo, huo ni uhakika, naomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, nilimeita Mheshimiwa Hokororo Agnes aulize swali lake la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. naomba kuuliza swali dogo la nyongeza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza majengo na kukarabati Kituo Polisi Masasi ambacho kilijengwa wakati wa ukoloni 1959?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongea la Mheshimiwa Hokororo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua vituo vilivyojengwa kabla ya uhuru kama hiki cha Masasi ni vya muda mrefu, vimechakaa, vinahitaji ukarabati. Kupitia Bunge hili namwomba *IGP* kupitia wasaidizi wake walioko mikoani waweze kufanya tathmini ya kiwango cha uchakavu wa Kituo cha Polisi ngazi ya Wilaya pale Masasi ili baada ya kubaini kiwango cha uchakavu kiweze kutengewa bajeti kwa ajili ya matengezo kulingana na mpango wetu wa matengezo na ujenzi wa vituo vyetu vya Polisi, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Nyanghwale, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Tarafa ya Nyijundu tuna ujenzi wa Kituo cha Polisi, nami kama Mbunge nimeweza kushirikiana na wananchi hao kwa kuchangia matofali zaidi ya 2,000: Je, Serikali iko tayari kuchangia nguvu za wananchi ili tuweze kukamilisha kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Nyanghwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo *spirit* ya Wizara kwamba pale ambapo wananchi na wadau wao wamejitokeza kuanza ujenzi wa vituo hivi vya Polisi kwa ajili ya usalama wetu, sisi tutawaunga mkono. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama ametoa matofali 2,000 na wadau wengine wametoa na ujenzi umeanza, basi katika ukamilishaji tutawanga mkono. Wakati wowote mtakapokuwa mmefikia hatua ya ukamilishaji, tafadhali tuwasiliane ili tuweze kukuunga mkono kituo hicho kikamilike na kuanza kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Namwita Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, aweze kuuliza swali lake.

Na. 81

**Kuwajengea uwezo wahitimu wa Vyuo Vikuu nchini**

**MHE. BAHATI K. NDINGO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwajengea uwezo Wahitimu wa Vyuo nchini ili waweze kushindana katika soko la ajira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Omari Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi ujulikanao kama, *Higher Education for Economic Transformation (HEET),* inaendelea na maandalizi ya uboreshaji wa mitaala iliyopo na uandaaji wa mitaala mipya zaidi ya 290 katika programu za kipaumbele cha Taifa ili kuwajengea uwezo wahitimu kuhimili ushidani wa soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayoendelea ni ukusanyaji wa maoni *(tracer study and needs assessment)* kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu ili kubaini mahitaji halisi. Mitaala hiyo iliyoboreshwa inatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka wa masomo 2023/2024, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, wameshaanza mapitio ya mitaala, ni kwa namna gani wameweza kushirikisha sekta binafsi katika mapitio ya mitaala hiyo ikiwa wao ndio waajiri wakubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunatambua kwamba elimu ya ufundi kwa sasa ni muhimu ili kuwawezesha wahitimu kujiajiri na kuajiriwa. Sasa Serikali ina mkakati gani kuhakikisha wanaanza kutoa mikopo kwenye vyuo vyetu vya ufundi nchini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bahati Keneth, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi, kwamba kupitia mradi huu wa *HEET* ambao ni wa zaidi ya Dola milioni 425, tunafanya maboresho makubwa na mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu. Miongoni mwa mapinduzi hayo ni katika kuboresha mitaala yetu iliyopo sasa. Katika uboreshaji wa mitaala hii, ushirikishaji wa wadau, kama nilivyozungumza kwenye jibu la msingi, ni wa kiasi kikubwa ikiwemo na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu, ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wakiwemo sekta binafsi tunauzingatia kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana tunafanya kitu kinaitwa *tracer study and needs assessment.* Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba tunapata mahitaji, lakini vilevile tunawashirikisha wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la pili, nazungumzia suala la mikopo katika kada ya kati. Hili suala tayari tulishalizungumza hapa Bungeni na tulisema wenzetu wa *NMB* tayari wameshaingia kwenye utaratibu huu. Wametenga zaidi ya Shilingi bilioni 200 katika mwaka huu wa fedha 2022/2023, lakini sisi kama Serikali katika mwaka 2023/2024 tunakusudia sasa kutenga fungu kwa ajili ya mikopo katika kada hii ya kati, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea namwita Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge Viti Maalum aweze kuuliza swali lake.

Na. 82

**Kauli ya Serikali kuhusu masomo ya dini**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza: -

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya masomo ya dini kutokuwa *principal pass* ya kujiunga na Stashahada na Shahada?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa uendeshaji wa elimu ya Chuo Kikuu hapa nchini na katika nchi nyingine duniani, Mabaraza ya Vyuo Vikuu (Seneti) yamepewa mamlaka ya kisheria kuweka vigezo mahsusi vya udahili kwa kila programu ya masomo kwa ngazi husika *(Specific Program Requirements)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hapa nchini, *principal passes* za masomo ya dini zinatambuliwa kama vigezo mahsusi vya kujiunga na baadhi ya program za masomo kwa ngazi ya Stashahada na Shahada ya kwanza. Mfano, baadhi ya Vyuo Vikuu ambavyo vimekuwa vikitumia masomo ya dini kama kigezo kimojawapo cha kujiunga na *program* za masomo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Kiislam cha Morogoro; Chuo Kikuu cha Zanzibar; Chuo Kikuu cha Arusha; Chuo Kikuu cha Mt. Yohana cha Tanzania; Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi; Chuo Kikuu Huria cha Tanzania; Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, swali la nyongeza.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, sasa Serikali imetuelezea kwamba kuna vyuo mbalimbali ambavyo vinatoa elimu ya juu ambayo inazingatia hiyo *principal pass.* Je, hamuoni sasa Serikali kuandaa Mpango maalum kupitia *TCU* ambao ndiyo wadhibiti ubora wetu wa Elimu ili waweze kuwashauri sasa Vyuo Vikuu vyetu waweze kuliingiza ili somo la dini liwe kama ni miongoni mwa *Principal pass*?

Swali langu la pili, kwa kuwa masomo haya ya dini yanawajenga vijana wetu kimaadili lakini pia yanawajenga wanafunzi wetu wetu kimaadili lakini na kiimani. Je, hatuoni sasa kulitoa hili somo la dini kwamba siyo miongoni mwa *principal pass* ambazo zitamsaidia mwanafunzi kujiunga na Chuo Kikuu, hatuoni sasa tunawaandaa wanafunzi wengi ambao wakimaliza Vyuo Vikuu watakuwa hawana maadili mazuri kwa sababu wanafunzi hawatalisoma hili kama ni somo la msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Latifa Juwakali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwisha kueleza kwenye majibu ya msingi kwamba masomo haya ya dini yanatumika kwenye baadhi ya Vyuo na kwenye baadhi ya *program*. Hatuwezi *program* zote tukasema kwamba ziingize masomo ya dini, kwa sababu itategemea na *program* gani mwanafunzi anayokwenda kusoma. Kwa hiyo, tumebeba ushauri huo alioutoa lakini ninaomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba *TCU* jukumu lake ni kudhibiti, kufanya Ithibati ya ubora wa masomo yanayotolewa na siyo

kupanga kwamba *program* gani iingizwe na kwa *requirement* zipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza zile *Senate* ndizo zenye wajibu wa kupanga namna gani *requirements* zinazotakiwa kwenye *program* husika. Kwa hiyo, tunalibeba suala hili la kuona namna gani masomo yetu ya dini yanaweza yakaingizwa kwenye baadhi ya hizo *program* kwa kadri tutakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, namwita Mheshimiwa Anton Albert Mwantona aweze kuuliza swali lake.

Na. 83

**Kumaliza Mradi wa *REA II* Vijiji 25 vya Jimbo la Rungwe**

**MHE.ANTON A. MWANTONA** aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa *REA II* utamalizika kwa Vijiji 25 vilivyobakia katika Jimbo la Rungwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji 25 vilivyobaki katika Jimbo la Rungwe vitapatiwa umeme kupita Mradi wa *REA III* mzunguko wa pili ambapo kwa sasa Mkandarasi yupo eneo la mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mkataba, Mkandarasi wa kazi hiyo *(ETDCO)* atakamilisha kazi kwenye vijiji hivyo Mwezi Desemba, 2023. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mafupi. Mheshimiwa Anton Albert Mwantona swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe masikitiko yangu makubwa, nimekuja mara nyingi hapa kwa mradi wa *REA II* ambao ni Vijiji 25, ukizingatia huu mradi ulikuwa ni mradi wa mwaka 2014 ndiyo ulianza, hivi vijiji 25 vilitelekezwa. Nilikuja hapa mwaka jana mwezi wa Februari Bunge, Naibu Waziri mwenyewe hapa alisema kwamba Mwezi April mradi utakuwa umeshakamilika. Nimekuja Bunge la Mwezi wa Sita akaniambia mwezi wa Tisa mradi utakuwa umeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekutana na Waziri mwenyewe amekuja kufanya ziara kule nyumbani Jimboni kwangu, amefanya mkutano na wananchi pale Tukuyu akawaambia mpaka Disemba mradi utakuwa umeshakamilika. Leo hii naambiwa hapa kwamba mradi huu umechanganywa na *REA* Namba *III* Awamu ya Pili na utaisha Disemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Wizara haikuelewa vizuri swali langu. Huu ni mradi *REA II* ambao ni wa muda mrefu, nilikuwa naomba nipate majibu. Ni lini mradi wa *REA II* vijiji 25 utakamilika?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA III* Awamu ya Pili nilikuwa na Vijiji 36, mpaka ninavyoongea hapa ni Vijiji Vitatu tu ndiyo vimeshawashiwa umeme, kuna Kijiji cha Mboyo Kata ya Isongole, Kijiji cha Ndwati na Kijiji cha Lienje Kata ya Ikuti na *deadline* ilikuwa ni Disemba mwaka 2022. Leo naambiwa

hapa kwenye swali la msingi kwamba tunapeleka tena mpaka Disemba 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri ni lazima tuwe *serious* kwa sababu wananchi wetu wanatusikiliza, ahadi Serikali wanazotoa nasi tunawaambia, leo naambiwa 2023 ndiyo mradi utakamilika. Naomba nipate ufafanuzi wa Serikali, mambo gani yaliyopelekea kubadilisha *deadline* kutoka Disemba 2022 mpaka Disemba 2023?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati nafikiri umemuelewa Mheshimiwa Mbunge. Hoja yake ni *REA II* umezungumzia *REA III*, kwa hiyo anataka ufafanuzi na *commitment* ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anton Albert Mwantona kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama swali lilivyoulizwa ilikuwa ni kwamba ni lini Vijiji vilivyobaki katika *REA II* vitakamilishwa. Kule mwanzo vilipochukuliwa hivi Vijiji 25 vilitakiwa vifanyike katika *REA II* lakini havikufanyika vilibaki. Kwa sababu maelekezo ya Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kwamba hii Awamu ya *REA III* mzunguko wa pili usiache kijiji hata kimoja bila kupelekewa Umeme. Kwa hiyo, Vijiji hivi 25 vimeunganishwa kwenye Mkataba wa *REA III Round II* ili navyo vifanyiwe kazi na vikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua tutawaelekeza wenzetu wanaotekeleza mradi kwenye maeneo haya ili wahakikishe kwanza katika *scope* hii wanashughulika na vile Vijiji ambavyo ni vya muda mrefu halafu hivi ambavyo vilikuwa ni vya *REA III Round II* waje wavimalizie kwa kadri tunavyosogea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine ambalo ni la msingi ameuliza kuhusu kubadilika kwa muda wa kumaliza mkataba wa *REA III Round II* kutoka Disemba mwaka jana kwenda Disemba mwaka huu. Sababu kubwa ziko mbili, kwanza ni ile ambayo tulikwisha ieleza ya matatizo tuliyoyapata ya kuongezeka kwa bei na changamoto zilizotokana na UVIKO, tatizo jingine ni tatizo chanya ambalo ni kuongezeka kwa Kilometa Mbili kwa kila Kijiji katika mradi huu ambao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kwa *scope* ile ya zamani ambayo ilitakiwa iishe Disemba, baada ya kuongeza zaidi ya nusu ya ile *scope* imekwenda sasa kufikia mpaka Disemba mwaka huu, tutahakikisha kwamba tutavutana na kukabana na Wakandarasi ili hizi kilometa mbili ambazo zinaongezeka kwenye Vijiji vyetu Disemba mwaka huu kazi yote iweze kukamilika katika maeneo yetu.

**MWENYEKI:** Ahsante. Mheshimiwa Noah Mollel swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi wananchi wanahitaji umeme kwa asilimia 100. Kuna Mkandarasi ambaye yupo kwenye Jimbo hilo ambaye amekuwa akisuasua kuwapa wananchi umeme, kuna maeneo kuna maeneo amechimba mashimo, hakuna nguzo kwa muda mrefu, kuna maeneo ameweka nguzo hakuna nyaya kwa muda mrefu, maeneo mengine hakuna umeme kabisa....

**MWENYEKITI:** Sasa uliza swali lako Mheshimiwa.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi ambao wamesubiri umeme wa *REA* kwa muda mrefu bila mafanikio?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lemburis Noah Saputi, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ambayo tulichelewa kupata Mkandarasi eneo la Arumeru ni mojawapo, Mkandarasi tayari amepatikana na anaendelea na kazi, katika maeneo ambayo tunaangalia kwa macho ya Karibu Mkoa wa Arusha pia ni mmojawapo. Tunahakikisha kwamba katika muda ambao tumekubaliana nae wa kimkataba kazi yake ya kupeleka umeme kwenye maeneo hayo itakamilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tunaomba atupe subira kidogo na utatuona sana katika Jimbo lake tukiendelea kuvutana na Mkandarasi kuhakikisha kwamba kazi inakamilika katika muda tuliokubaliana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa tatizo hili la Makandarasi wa *REA* limekuwa ni tatizo kubwa nchini, Wizara haioni umuhimu wa kutusikiliza Kikanda ili kuona matatizo yalivyo kwenye Kanda zetu?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sikusikia vizuri mwisho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaweza ukarudia swali lako.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la usambazaji wa umeme kupitia Wakandarasi wa *REA III* mzunguko wa pili imekuwa tatizo kubwa katika Majimbo yetu. Je ,Wizara haioni umuhimu sasa wa kutusikiliza Kikanda kuona matatizo yalivyo kwenye Majimbo yetu katika mradi huu wa *REA*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalil la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilikuwa nyingi, zile za ndani ya uwezo na nje ya uwezo. Changamoto zilizo ndani ya uwezo zote tumeshazitatua. Siku chache zilizopita Mheshimiwa Waziri aliitisha kikao cha Wakandarasi wote na kutoa maelekezo, tayari wenzetu wa *REA* wameshapita kwenye Mikoa takribani Saba au Nane ambayo tuliona iko nyuma zaidi kuhakikisha kwamba wao, watu wa *REA* na watu wa *TANESCO* kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa lakini na Waheshimiwa Wabunge pia mlipata mialiko kwenye hayo maeneo tukae kwa pamoja ili tuone tatizo liko wapi na tuweze kusukuma shughuli hii ili tuweze kuikamilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewekeana makubaliano na tunaamini ndani ya muda tutayatekeleza na tutakamilisha kazi hizo.

**MWENYEKITI:** Swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona *REA* wanayo miradi mbalimbali lakini tunaotoka Majimbo ya Mjini na tunayo mazingira ya maeneo ambayo yana sifa za vijiji ingawa yako Mjini. Je, ni lini mtatupelekea umeme kwa sababu hata miradi hakuna huko, tunaona tu ya *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Iringa Manispaa mtaa wa Ugele, Mtaragara, Msisina, Kagrielo na Wahe, ni lini mtatuletea umeme maeneo ya pembeni?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wenye Majimbo ya Vijijini wamekuwa na miradi ya *REA* na *densification* na mingine, sisi ambao tuko kwenye Majimbo ya Mjini na mimi nikiwemo Jimbo la Bukoba Mjini, tumepata mradi unaoitwa *peri-urban* ambao kama nilivyotangulia kujibu kwenye siku zilizopita, mradi huu sasa umeenda kwenye awamu ya pili na tutakwenda kwenye awamu nyingine zinazokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilianza Mkoa wa Pwani na Kigamboni, awamu ya pili ikaja Mkoa wa Arusha, Dodoma na Mwanza, Awamu ya tatu imepata Mikoa mingine kama mitano au sita, sasa tutaenda awamu ya nne nimhakikishie Mheshimiwa Msambatavangu kwamba na Iringa pia itaingia kwenye awamu inayokuja kwa sababu pesa inapatikana taratibu lakini kila mmoja lazima apate pesa katika kufanya miradi hii kwenye maeneo yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Namuita Mheshimiwa

Abdullah Ali Mwinyi Mbunge wa Mahonda aulize swali lake, Mheshimiwa Edward Olelekaita naona ameinuka.

Na. 84

**Taarifa ya utekelezaji wa *Blueprint***

**MHE. EDWARD O. KISAU K.n.y. MHE. ABDULLAH ALI MWINYI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa taarifa ya utekelezaji wa *Blueprint for Regulatory Reforms* za mwaka 2018 ili zijadiliwe?

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdullah Ali Mwinyi, Mbunge wa Jimbo la Mahonda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianza rasmi utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini *(MKUMBI)* ujulikanao kama *blueprint* hapo Julai Mosi, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 24 Oktoba, 2022, Wizara iliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa MKUMBI kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Katika taarifa hiyo ambayo inaonesha utekelezaji wa hadi kufikia Agosti, 2022 ilijadiliwa, ambapo Kamati ilitoa maelekezo mbalimbali ya kufanyiwa kazi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mpango huo, maelekezo hayo yanaendelea kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Olelekaita Kisau swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninalo swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mpango huu wa *blueprint* ulitengeneza changamoto mbalimbali ambazo ziko kwenye Sheria mbalimbali na ucheleweshaji katika kuushughulikia imekuwa ni *issue*. Wizara ina mpango gani sasa kwamba makosa mapya hayajirudii kwenye sheria zinazotengezezwa mpya?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Olelekaita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli moja ya changamoto katika mambo yaliyokuwa kwenye andiko hili la *blueprint* ilikuwa ni Sheria na Kanuni zipatazo 88 ambazo zilikuwa na changamoto mbalimbali. Mpaka sasa zaidi ya Sheria na Kanuni 40 zimeshafanyiwa kazi ambayo ni takribani asilimia 45 ya utekelezaji ya mpango huu wa kuboresha mazingira ya wafanya biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunaendelea kupitia na kuhakikisha Sheria na Kanuni ambazo bado ni kinzani kwa ajili ya kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara nchini tunaendelea kuzitatua na kupitia Bunge lako Tukufu ninaamini mengi tutaendelea kuyarekebisha kadri ya muda unavyokwenda, kwa sababu pia tunavyotatua baadhi ya changamoto kuna changamoto zingine mpya zinaibuka. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kutatua kadri ambavyo hali halisi itakavyokuwa inajitokeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, tumekaa hapa tunaongea lakini huko Halmashauri zetu wanatunga Sheria Ndogondogo ambazo zilizopo nyingi zinakwenda kupunguza *attraction* ya wawekezaji hasa wa ndani.

Je, ni mkakati gani wa sasa ambao Wazira inao kuhakikisha inaratibu zoezi hili ili liweze kuhakikisha kwamba Wawekezaji hasa wa ndani wanaweza wakafanya kazi bila ya kuwa na Sheria Ndogondogo hasa za tozo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli moja ya changamoto tulizonazo kwenye utekelezaji wa mradi wa *blueprint* au *MKUMBI* ni katika ngazi za Halmashauri. Wizara tumeshaanza kuliona hilo na moja ya utekelezaji tumeanzisha madawati au kitengo mahususi kinachoshughulikia masuala ya viwanda, biashara na uwekezaji katika ngazi ya Halmashauri. Tunaamini kitengo hiki kitasaidia moja, kuhakikisha tunaharakisha utekeklezaji wa yale maboresho ambayo tumeyafanya, lakini pili kuwaelimisha wenzetu wa Halmashauri ili wawe wanatunga Sheria au Kanuni ambazo si kinzani na nia hii ya Serikali ya kuboresha mazingira ya

uwekezaji na ufanyaji biashara hapa nchini. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tarimba swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya 141 kati ya 190 kwa ugumu wa ufanyaji biashara. Majibu ya Mheshimiwa Waziri yananipa mashaka juu ya *commitment* ya Serikali juu ya kutumiza haja ya *reforms* katika *regulations* zetu. Hivi ni kwa nini hiyo taarifa ya utekelezaji msiilete Bungeni ili tuweze kuijadili, badala ya kuipeleka kwenye Kamati peke yake, tuleteeni Bungeni hapa tuijadili, tuna usongo na hali hii sisi, tunataka tumalize haya matatizo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Abbas Tarimba Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira, ni moja ya Kamati ambazo zimetungwa na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo namini kwa utaratibu ule ule kwamba Kamati hizo zinawasilisha Bunge hili na kwa maelekezo yenu nadhani inawezekana kama kutatakiwa kuleta hapa, basi ni maelekezo ya Bunge lako Tukufu ili tuweze kufanya hivyo.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Nusrat Hanje, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mpaka sasa hivi *Blueprint* inaonekana ni *document* ya Serikali na watu hawaimiliki. Ni yapi sasa mafanikio mpaka sasa hivi tangu tufanye *reforms* kwenye *blueprint,* Serikali imefanikiwa nini kiuchumi ili *at least* sasa tuanze kuona *value for money* na hayo marekebisho ambayo tumeyafanya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, napenda kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yako mengi kama ambavyo nimesema. Moja ya maeneo ambayo yalikuwa yana angaliwa ni zile Sheria zilizoanishwa kwenye mpango ule au kwenye *document* hiyo, ambayo kimsingi iko *public* na kila mtu anaweza ku-*access* na sio ya Serikali. Ni zaidi ya sheria na kanuni 88, ambazo katika hizo sheria na kanuni 40 zimeklwisha ratibiwa na kufanyiwa marekebisho. Hata hivyo katika mambo ambayo yalikuwa yameibuliwa ni mwingiliano kati ya taasisi za Serikali moja wapo mi *TBS* na *TMDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yameweza kurekebishwa; lakini moja ni uanzishwaji wa mifumo ambayo ilikuwa na changamoto kwa wafanyabiashara kwa mfano Wafanyabiashara wakitaka kulipia ilikuwa ni changamoto kubwa. Kwa hiyo mifumo 42 imerekebishwa, moja wapo tunaona ni hii *GEPG* ambayo ni malipo ya Serikali na yameboreshwa na hii imepunguza sana manung'uniko kwa wananchi kupanga foleni Kwenda kulipa katika taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi katika utekelezaji huo ndiyo tunaona kwamba tumeanzisha idara hizi na vitengo ambavyo vitakuwa mahususi sasa kusikiliza na kutatua kero za wafanyabiashara maeneo yote. Kuanzia wizarani kuna kitengo hicho lakini pia tunaenda kwenye halmashauri tunaweka kitengo ili kuhakikisha tunapunguza manung'uniko na changamoto ambazo wafanyabiashara wa Tanzania walikuwa wanakutana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo taarifa hizo au kitabu hicho au *document* hiyo ni ya wananchi wote. Kwa hiyo popote utakapotaka unaipata na taarifa hizi kama ulivyosema kama ukihitaji tutaileta hapa Bungeni; lakini Kamati yako ya Viwanda, Biashara na Mazingira wamekwisha ipata na wameijadili na mambo mengi yanaendelea kurekebishwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri, Wizara ya Uwekezaji,viwanda na Biashara. Tunaendela na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalumu. Namwita Mheshimiwa Ester Nicholus Matiko Mbunge wa Viti Maalumu aweze kuuliza swali lake.

Na. 85

**Kuanzisha madawati ya kijinsia katika ngazi za Kata na Vijiji**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, ni kwa nini Serikali isianzishe madawati ya kijinsia katika ngazi za Kata na Vijiji kutokana na ongezeko la vitendo vya ukatili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELELO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamaii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholus Matiko Mbunge wa viti maalumu kama ifuatvyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii ambapo imeratibu uanzishwaji wa madawati 420 ya Jinsia katika vituo vya Jeshi la Polisi, na 153 vya Jeshi la Magereza. Aidha, madawati ya ulinzi wa watoto yameanzishwa katika shule za msingi na sekondari. Vile vile, madawati ya jinsia yanaanzishwa kwenye vyuo vyote nchini pamoja na maeneo ya umma kama kwenye masoko. Kwa upande mwingine, kKamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zimeanzishwa katika ngazi ya mtaa/vijiji hadi Taifa kwa asilimia 88. Madawati haya yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia katika jamii. Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nasikitika kwa majibu ya Serikali, kwa sababu tunatambua kwamba ukatili wa kijinsia umeongezeka, sasa mpaka leo wanatuambia madawati ya kijinsia yako 420 na tuna kata takribani 4000. Ina maana takribani asilimia 10 tu ndio watu wanaopata hii huduma ambao wana athirika. Hata hivyo madawati ambayo wanasema wanatarajia kuanzisha Mashuleni wameanzisha *so far,* Madawati 1,300 na tuna shule zaidi ya 30,000 kwa Sekondari na Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati hizi anazodai kuamzishwa kwa asilimia 88, aidha hazijaanza kazi labda kwa

sababu ya changamoto ya kimuundo au kibajeti. Nataka kujua sasa, ni lini Serikali itazielekeza halmashauri ziweze kutenga bajeti ili kuhakikisha kwamba zinazipatia hizi kamati ambazo zimeanzishwa kwenye hivi vijiji ili ziweze kutekeleza kwa tija na kupunguza au kuzuia kabisa matukio ya ukatili wa kijinsia ambayo yamekithiri katika jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa sasa matukio haya ukatili wa kijinsia yanakuwa hayachukuliwi hatua mpaka pale labda vyombo vya habari au mitandao ya kijamii inapo ripoti kwenye jamii ndipo tunaona viongozi wa ngazi za juu wanafuatilia na kuchukua hatua. Nilitaka kujua Serikali imeweka utaratibu upi ambao utawezesha utolewaji wa taarifa na ufuatiliaji wa matukio ambayo yameripotiwa kwenye hizi kamati ambazo mmesema zimeanzishwa kwa asilimia 88 ili kuhakikisha …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swalo sasa

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Ndilo swali lenyewe, ili kuhakikisha sasa waathirika wa vitendo vya ukatili wanapata huduma na haki staki kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELELO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther ifuatvyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha kamati. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Esther kwa wazo zuri ambalo amelitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe waheshimiwa Wabunge ambao wanaingia katika Mabaraza ya Madiwani

walipe kipaumbele suala hili ili Kamati hizi ziweze kujiwezesha na baadaye kufanya kazi kwake kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifumo na utoaji wa taarifa. Kwa suala hili kwa kuwa utekelezaji wa MTAKUWWA ni mtambuka, Serikali itaendelea kutumia mifumo iliyopo kisheria. Kuhusu swali la Jeshi la polisi ndio muamala ambao unaweza kutoa taarifa za ukatili wakati upelelezi unapo kamailika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mwananchi aweze kuhukumiwa, Mahakama ndiyo itakayo toa hukumu katika vifungu ambavyo vilivyowekwa. Hata hivyo kesi ili iende haraka tunawaomba waathirika wote wawe na ushirikiano na vyombo vya sheria na pia kuwa wawazi katika kuleta maelekezo yao. Ahsante. (makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri naona Bunge zima linashangilia. Mheshimiwa Tendega

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba asilimia 88 ndio wameunda katika vijiji, kata na kwenye mitaa yetu. Hata hivyo Kamati hizi zimekuwa hazitekelezi majukumu yake ama hazifahamiki ipasavyo. Mimi nilitaka kujua, je, kamati hizi za ulinzi na usalama wa watoto zimeundwa na wajumbe gani ili tuwatatmbue tuweze kuwafuatilia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELELO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

napenda kujibu swal la nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Kuanzishwa Madawati ya Ulinzi na Usalama kwa Watoto ulianzishwa Juni, 2022 na kuanzishwa madawati hayo machache. Hata hivyo wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Elimu pamoja na Mamlaka ya Jeshi la polisi tutaendelea kuimarisha Kamati hizi ifikapo mwaka 2023 basi tutahakikisha shule zote zina madawati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu nimemuona Mheshimiwa Neema Lugangira.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matukio ya ukatili wa kijinsia yameendelea kukithiri hapa nchini, je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ya Ukatili wa Kijinsia hapa Bungeni kama ambavyo Tanzania iliridhia katika Mkutano wa 44 wa Bunge la *SADC (SADC Parliamentary Forum)?* Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELELO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, tutajipanga Wizara pamoja na Wizara mtambuka ambazo tunatengeneza miamala hii ya miswada kwa pamoja ili kuweza kuifikisha pale panapohitajika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunakushuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Unaweza kwenda kuketi. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili ninaomba tusikilizane vizuri. Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane vizuri kwa sababu yanatuhusu moja kwa moja.

Tangazo la kwanza, ni tangazo la Katibu wa Bunge. Naomba nilisome; Yahusu Wabunge kujaza fomu za maombi ya kujiunga na Kamati za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia kwamba Mheshimiwa Spika kwa kushauriana na Kamati ya Kanuni za Bunge katika kikao kilichofanyika Ijumaa tarehe 3 Februari, 2023 amefanya marekebisho ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 na kufuta na kuweka muundo mpya wa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta.

Kutokana na mabadiliko hayo, Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta zitakuwa 11 badala ya Kamati tisa za awali kama ifuatavyo: -

Waheshimiwa Wabunge, niliwaomba utulivu kwa sababu nilijua. Naomba kurudia kusoma tangazo la Katibu wa Bunge kwa Maelekezo ya Mheshimiwa Spika wetu.

1. Kamati ya Utawala Katiba na Sheria.
2. Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niliwaomba utulivu kwa sababu nilijua. Naomba kurudia kusoma Tangazo la Katibu wa Bunge kwa maelekezo ya Mheshimiwa Spika wetu.

1. Kamati ya Utawala Katiba na Sheria.
2. Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

3. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama
4. Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
5. Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii.
6. Kamati ya Maji na Mazingira.
7. Kamati ya Elimu,Utamaduni na Michezo.
8. Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii.
9. Kamati ya Afya na Masuala ya Ukimwi.
10. Kamati ya Miundombinu.
11. Kamati ya Nishati na Madini.

Orodha kamili ya Kamati zote za Bunge na Wizara zinazosimamiwa na Kamati hizo imewekwa kwenye Vishikwambi vyenu. Tusikilizane Waheshimiwa. Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 135(7) ambayo inaweka ukomo wa Ujumbe kwenye Kamati za Bunge kuwa ni Mwisho wa Mkutano wa Kumi ambao ni nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge. Wabunge wote sasa wanatakiwa kujaza fomu za maombi ya kujiunga na Kamati za Kudumu za Bunge kwa kipindi cha pili cha maisha ya Bunge.

Naendelea kusoma matangazo ya Katibu wa Bunge.

Fomu hizi zinapatikana humu Bungeni kwa Wahudumu kuanzia leo jumatatu tarehe 6 Februari, 2023. Siku ya mwisho ya kurudisha fomu zilizojazwa ni Jumanne tarehe 7 Februari, 2023 saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge wote mnasisitizwa kuchukua fomu hizo, kuzijaza ipasavyo na kuzirejesha ili mchakato wa kuwapanga kwenye Kamati za Bunge uendelee.

Tangazo limetolewa na Katibu wa Bunge leo tarehe 6 Februari, 2023.

Tangazo namba mbili ni kuhusu wageni. Wageni waliopo Bungeni ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kundi la kwanza ni wageni 22 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Waziri wa Madini, ambao ni Wanyeviti wa Kata kutoka Jimboni kwake Bukombe Mkoani Geita. Wenyeviti wa Kata wote, karibuni sana Dodoma kuja kushuhudia kazi ya Mheshimiwa Mbunge wenu anavyoendelea kuchakarika kuwatumikia, karibuni sana.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini ambao ni viongozi wa wafanyabiashara wa madini kutoka Jijini Arusha, sijui kama wako hapa? Haya hatujawaona.

Wengine ni wageni wa Dkt. Kiruswa ambao ni wafanyakazi 19 kutoka shule ya *Meloc Academy* kutoka Longido, Jijini Arusha, karibuni sana wageni kutoka Longido. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watano wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni wafanyakazi kutoka *Rostam Car Dealers* kutoka Jijini Dar es salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 40 wa Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos ambao ni Madiwani na Watendaji wa Manispaa ya Magharibi “A” kutoka Zanzibar, simameni kwanza, wakiongozwa na Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo Ndugu Choum Shuwari Machano. *(Makofi)*

Pia wako na Katibu wake anayemsaidia kazi vizuri Bi. Lucy Edward. Tunawashukuru sana kwa kufika Bungeni kuja kuona mwakilishi wenu kazi anayofanya hapa, ahsante sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Veronica Kasambala na Ndugu Elizabeth Kasimila. *(Makofi)*

Kundi la pili, ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza, ni wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini cha Jijini Dodoma, karibuni sana kwenye Bunge lenu kuja kujifunza shughuli zinavyotekelezwa hapa. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wanachama 35 wa Skauti ambao ni vijana wa kike kutoka mikoa mbalimbali Tanzania, wakiongozwa na Katibu wao Ndugu Wintapa Lwila, karibuni sana Skauti. *(Makofi)*

Kundi lingine ni mwandishi wa makala za kuelimisha jamii Ndugu Abedinego Ibrahimu Salila. *(Makofi)*

Mgeni wa mwisho ni Ndugu Prisca William Nsanyiwa kutoka Makoko, Manispaa ya Musoma, karibu sana Mama Prisca kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Tunaendela na uchangiaji.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022

**na**

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2022

**MWENYEKITI:** Namwita sasa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na

Usalama Mheshimiwa Vita Kawawa kwa ajili ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Kamati.

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kwanza taarifa hii yote iingizwe katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha Februari, 2022 na Januari, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; awali ya yote kwa niaba ya Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa namna ya pekee, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha hali ya mahusiano ya kimataifa kwa kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na diplomasia ya uchumi; pamoja na kuunda Tume ya kuangalia jinsi ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa namna walivyojitoa kikamilifu na kutekeleza majukumu yao kwa moyo ari na weledi na hivyo kuwezesha Kamati kukamilisha majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Aidha, masuala yanayoainishwa kwenye Taarifa hii ni yale tu ambayo Kamati inaona kuwa utekelezaji wake unahitaji juhudi zaidi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa inayowasilishwa imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu Majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa;

(ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na

(iv) Sehemu ya Nne inahitimisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati ni kama zilivyowasilishwa katika sehemu ya kwanza ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati; yanaonekana katika sehemu pia ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati; Hali ya Ulinzi na Usalama Nchini. Katika kipindi ambacho taarifa hii inatolewa Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Umma na Utawala Bora; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ajili ya kupokea taarifa ya hali ya ulinzi na usalama. Taarifa hizo kwa pamoja na mambo mengine zilibainisha hali ya usalama wa

nchi, hali ya ulinzi wa mipaka pamoja na matukio yanayohatarisha ulinzi na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi wa Kamati wa taarifa hizo pamoja na tathmini ya hali halisi, naomba nilijulishe Bunge lako Tukufu kuwa, kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama ni shwari na kwamba kuna amani, usalama na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikakati ya Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kwa Vitendo; katika kipindi ambacho taarifa hii inawasilishwa, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Mikakati ya Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi bado haujawa na ufanisi wa kutosha kwani unakabiliwa na changamoto kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana kwa ushirikiano wa kimkakati na mahususi wenye malengo maalum baina ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara nyingine za Sekta ya Uchumi katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Hali hiyo inapunguza tija na ufanisi katika kufikia malengo ya diplomasia ya uchumi;

(ii) Kutokuwepo kwa utaratibu maalum wa kuandikisha *diaspora* na hivyo nchi kukosa takwimu sahihi za *diaspora*. Changamoto hii inaathiri upatikanaji takwimu halisi za mchango wa *diaspora* na mipango ya baadaye ya Taifa;

(iii) Diplomasia ya uchumi haieleweki ipasavyo miongoni mwa watendaji wa Serikali hususan wa ngazi ya mikoa na wilaya. Hali hii husababisha wafanyabishara na wawekezeji kutohudumiwa ipasavyo na kwa ufanisi;

(iv) Ushirikishwaji usiotosheleza wa wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. Hali hiyo inapunguza wigo wa manufaa ya diplomasia ya uchumi.

(v) Usafirishaji wa wanyama hai kama ng'ombe, mbuzi na kondoo kuhesabiwa kama sehemu ya mafanikio ya diplomasia ya uchumi ilihali utaratibu huo unaathiri ajira na thamani ya mauzo nje. Mathalani, hadi kufikia Oktoba, 2022 wanyama hai kama ng'ombe, mbuzi na kondoo takribani 4,000 walisafirishwa kwenda Bara la Asia na kuhesabiwa kuwa mafanikio. Hata hivyo, hali hii inazuia faida inayoweza kupatikana kutokana na kuongeza thamani ya bidhaa zinazotokana na wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Vyama Mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda; kama ilivyoelezwa awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Januari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda ambavyo ni *EALA, SADC-PF, CPA* na *IPU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Bunge limewakilishwa ipasavyo katika vyombo mbalimbali na uanachama katika vyombo hivyo, umekuwa na manufaa yanayoendana na mahitaji ya Kibunge na Taifa. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuendeleza ushirikiano kati ya Wawakilishi hao na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtiririko Usioridhisha wa Fedha za Miradi ya Maendeleo; uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za maendeleo. Taarifa zilizowasilishwa zilionesha kuwa baadhi ya Wizara zimepata fedha chini ya 35% na nyingine hazikupata fedha za miradi ya maendeleo kabisa. Taarifa ya kina kuhusu upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo umefafanuliwa kwa kina katika Sehemu ya Pili ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa; uchambuzi wa Kamati wa Mwezi Oktoba, 2022 kuhusu hali ya upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa ulibaini kuwa, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* ilisajili watu 23,630,813 hadi kufikia mwezi Novemba, 2022 ikiwa ni asilimia 68 ya lengo la watu milioni 34,080,610 waliokusudiwa kusajiliwa ifikapo mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilibaini kuwa kati ya idadi ya watu 23,406,360 waliosajiliwa, ni watu 19,634,720 ambao wamepata namba za utambulisho na ilikuwa imegawa vitambulisho 10,230,710.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea bado idadi ya vitambulisho vinavyozalishwa ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi. Aidha, uchambuzi wa kamati ulibaini kuwa zipo changamoto mbalimbali zinazochelewesha uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa mwenyekiti, Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali Zao; katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao katika kipindi cha Mwezi Julai hadi Disemba, 2022. Taarifa hizo, pamoja na mambo mengine

zilianisha hali ya uhalifu nchini na matukio yanayohatarisha hali ya usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa kwa kipindi cha Mwezi Oktoba hadi Desemba, 2022 makosa dhidi ya binadamu yaliyoripotiwa yalikuwa 3,092. Hilo ni ongezeko la makosa 516 sawa na asilimia 20 ikilinganishwa na makosa 2,576 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki kwa Mwaka 2020/2021. Ongezeko hilo litumike kama ishara ya mahitaji ya juhudi za kudhibiti makosa dhidi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajali za Barabarani; kwa kipindi cha Oktoba - Disemba, 2022; matukio ya ajali yaliyosababisha vifo katika kipindi hicho ni 281 ikilinganishwa na matukio 273 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Hili ni ongezeko la makosa nane, sawa na asilimia 2.9. Aidha, Katika kipindi hicho idadi ya watu waliokufa kutokana na ajali ni 382 ikilinganishwa na idadi ya watu 367 waliokufa kwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Hili ni ongezeko la watu 15 sawa na asilimia 4.1

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulionesha kuwa ajali za barabarani zimekuwa zikichangiwa na:-

(i) Uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya doria katika barabara kuu, taa za kuongozea magari, upungufu wa *speed radar touch,* upungufu wa kamera na vipima ulevi;

(ii) Kukosekana kwa utashi wa kisiasa kwa baadhi ya wanasiasa na hivyo kuingilia utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani. Mathalani, kuwazuia Askari kuwakamata bodaboda au bajaji wanapofanya uvunjifu wa Sheria;

(iii) Ubovu wa baadhi ya barabara, hali ambayo wakati mwingine husababisha ajali;

(iv) Hulka za kibinadamu kuamini kuwa ajali hazizuiliki na hivyo kuendesha pasipo kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani; na

(v) Kuwa na madereva wengi wasio na sifa ya udereva. Hali hii inasababishwa na mfumo uliopo wa utoaji leseni za udereva kutoa mwanya kwa watu wasio na sifa ya kuwa dereva kupata leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa katika siku za karibuni kumeibuka wimbi la magari ya watu/taasisi binafsi na za umma, kufungwa ving'ora kinyume na utaratibu ilihali wakiwa hawana uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya magari yenye ving'ora. Hali hiyo inahatarisha usalama kwa watumiaji wengine wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msongamano wa Wafungwa katika Magereza; uchambuzi wa kamati kwa kipindi cha kuanzia Julai - Desemba, 2022 ulibaini kuwa, bado kuna msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani ambapo jumla ya mahabusu na wafungwa magerezani ni 32,146 ikiwa ni sawa na asilimia 7.5, zaidi ya uwezo wa Magereza yaliyopo kwa sasa wa kuwahifadhi wafungwa na mahabusu 29,902.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa hali hii imeendelea kuchangiwa na:-

(i) Uchache wa Magereza nchini ikilinganishwa na idadi ya Wafungwa;Utegemezi wa adhabu za kifungo gerezani;

(ii) Kutotumika ipasavyo kwa mpango wa *Parole*; na

(iii) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kukaa magerezani kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali inafanya juhudi mbalimbali kukabiliana na msongamano wa wafungwa; Kamati ina maoni kwamba maazimio yaliyotolewa na Bunge katika Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022 kuhusu msongamano wa wafungwa, yanahitaji kufanyiwa kazi inavyostahili

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Wahamiaji Haramu Nchini; Kamati ilipata wasaa wa kupokea na kujadili taarifa kuhusu wahamiaji haramu nchini; ambapo taarifa ya Wizara ilionesha kuwa kwa kipindi cha Septemba - Desemba, 2022 Jumla ya wahamiaji haramu 7,493 walikamatwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa katika kipindi cha Septemba hadi Desemba, 2022, katika Magereza mbalimbali nchini kulikuwa na wafungwa na mahabusu wahamiaji haramu wapatao 3,108. Idadi hiyo imeongezeka kwa asilimia 93 ikilinganishwa na wahamiaji haramu 1,608 waliokuwepo Magerezani katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Uwepo wa wahamiaji haramu magerezani, unaigharimu Serikali kiasi cha wastani wa shilingi 15,540,000 kwa siku katika kuwapatia huduma mbalimbali za msingi. Ikiwa hali itabakia kama ilivyo kwa wafungwa/mahabusu hao waliopo magerezani, Serikali inatumia shilingi bilioni 5.67 kwa mwaka kuwatunza wafungwa/mahabusu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utendaji kazi wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji; katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Jeshi hilo limeendelea kutekeleza majukumu yake likiwa na

changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji kazi wake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Uchache wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji Nchini. Kwa sasa Jeshi hili lina jumla ya vituo 80 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya vituo 177 vinavyohitajika nchini;

(ii) Uhaba wa magari ya kuzima moto na uokozi. Kwa sasa Jeshi lina magari ya kuzima moto 76 ikilinganishwa na mahitaji ya magari 237 na magari ya uokozi yapo manne ikilinganishwa na mahitaji ya magari 35. Aidha, magari ya kubebea wagonjwa yapo mawili ikilinganishwa na mahitaji ya magari 169. Magari ya ngazi *(turntable ladder)* lipo moja ikilinganishwa na mahitaji ya magari tisa;

(iii) Upungufu wa *fire hydrants* katika maeneo mengi ya mijini na uchakavu wa vyanzo vilivyopo. Katika *fire hydrants* 2,339 zilizopo nchini 1,638 ni nzima na 701 zinahitaji matengenezo;

(iv) Upungufu wa Askari wa Uokozi Majini *(Divers)* ambao wapo 16 nchi nzima wakati mahitaji ni Askari 435;

(v) Ujenzi holela wa nyumba na miundombinu katika maeneo mengi ya mijini hali ambayo husababisha kutofikika kwa urahisi wakati wa dharura za kuzima moto na uokoaji; na

(vi) Wananchi kukosa elimu juu ya namna bora ya kuchukua tahadhari na kukabiliana na majanga ya moto na majanga mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipokea na kujadili utendaji kazi kwa Jeshi la Uhamiaji na Jeshi la Magereza ambapo ilibaini kuwa majeshi haya yanatekeleza majukumu yao yakiwa yanakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Changamoto hizo zimefafanuliwa kwa kina katika Sehemu ya Pili ya Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kukosekana kwa Alama za Mipaka ya Nchi; Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu Hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na kubaini changamoto za kukosekana kwa alama za mipaka *(beacons)*. Hali hiyo husababisha wananchi kutoka nchi tunazopakana nazo kuendesha shughuli haramu za kiuchumi. Mathalani, wafugaji kufanya shughuli za ufugaji katika maeneo ya mipaka ambayo hayaruhusiwi kisheria. Aidha, kukosekana kwa alama hizo husababisha wananchi hao kuingia nchini kwa utetezi kuwa hakuna alama za mipaka na hivyo kushindwa kutambua kuwa wameingia nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa Rasmi za Bunge zinaonesha kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu na Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kushughulikia suala hili. Hata hivyo, suala hili halijashughulikiwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubovu wa Barabara za Usalama Mipakani; ubovu huu umeendelea kusababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka yetu kwa nyakati zote. Katika baadhi ya maeneo Vyombo vya Ulinzi na Usalama vinapata changamoto ya kufika kutokana na ubovu wa barabara. Hali hiyo si nzuri kwa usalama katika maeneo ya mipakani na nchi kwa ujumla. Taarifa Rasmi za Bunge zinaonesha kuwa tangu Bunge la Kumi, Kamati hii imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutatua changamoto hii. Hata hivyo, suala hili bado halijatekelezwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Sita wa Bunge; Wakati wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za Kamati katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Mwezi Februari,

2022, Kamati ilipendekeza mambo mbalimbali kwa Wizara inazozisimamia na Bunge likapitisha mapendekezo hayo kuwa Maazimio. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilikuwa na Maazimio mawili (2) ambapo Azimio moja limetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na Azimio lingine halijatekelezwa kabisa. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa na Maazimio tisa ambapo Maazimio matatu yametekelezwa kwa ukamilifu, Maazimio matatu yametekelezwa kwa sehemu na Maazimio matatu hayajatekelezwa kabisa. Hivyo, kwa ujumla kasi ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge sio ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Mapendekezo. Baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo: -

(a) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa kimataifa.

(i) Kukosekana kwa ushirikiano wa kimkakati na mahususi wenye malengo maalum baina ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara nyingine za sekta ya uchumi katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kunapunguza tija na ufanisi katika kufikia malengo ya diplomasia ya chumi;

(ii) Kutokuwepo kwa utaratibu maalum wa kuandikisha *diaspora* kunasababisha nchi kukosa takwimu sahihi za *diaspora*. Changamoto hii inaathiri upatikanaji takwimu halisi za mchango wa *diaspora* na mipango ya baadaye ya nchi kuhusu *diaspora*;

(iii) Kutokueleweka ipasavyo kwa diplomasia ya uchumi nchini na hasa katika ngazi ya Mikoa na Wilaya kunasababisha wafanyabishara na wawekezeji kutohudumiwa ipasavyo na kwa ufanisi;

(iv) Ushirikishwaji usiotosheleza wa wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi unapunguza wigo wa manufaa ya diplomasia ya uchumi. Hivyo, ni vema Serikali ikaongeza mawanda ya ushirikishwaji wa wadau katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi;

(v) Usafirishaji wa wanyama hai kama ng'ombe, mbuzi na kondoo badala ya mazao yatokanayo na wanyama hao unasababisha kupotea kwa faida inayoweza kupatikana kwa kuongeza thamani ya bidhaa zinazotokana na wanyama hao.

(vi) Pamoja na nia ya dhati ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Balozi za Tanzania, kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kumeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi;

(vii) Ili kuweza kufikia malengo ya uanzishwaji wa Jumuiya za Kikanda ni muhimu Nchi Wanachama zingazingatia ipasavyo masharti ya Mkataba wa Jumuiya. Hivyo, ni vema Tanzania ikaendelea kushawishi nchi wanachama kuzingatia inavyostahili masharti ya mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya;

(viii) Wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu upatikanaji wa masoko ya bidhaa mbalimbali katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hali hii inasababisha wananchi kutonufaika ipasavyo na fursa za kiuchumo ikiwemo masoko ya bidhaa katika Jumuiya hizo.

(b) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

(i) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi *(beacons)* kunachangia uvamizi wa shughuli za binadamu na

shughuli haramu za kiuchumi katika maeneo hayo jambo ambalo si zuri kwa ulinzi na usalama wa nchi;

(ii) Ubovu wa barabara za usalama mipakani unasababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(i) Mwitikio mdogo wa wananchi juu ya utoaji wa taarifa za wahalifu imekuwa sababu mojawapo ya uhalifu kuendelea kufanyika katika Jamiii. Ikiwa Jamii itakuwa na mwamko wa kutoa taarifa kuhusu uhalifu kwa wakati itasaidia uhalifu kudhibitiwa mapema.

(ii) Wahalifu wengi waliokamatwa kuhusianana vikundi vya panya - *road* ni vijana wa umri wa miaka kati ya 13 hadi 30. Huku baadhi yao wakiwa bado ni wanafunzi wa sekondari. Hii inaashiria vijana hao kuwa na tamaa na ukosefu wa maadili, hali ambayo siyo afya kwa Taifa na kizazi kijacho.

(iii) Ongezeko la wahamiaji haramu kwa kiasi kikubwa linachangia msongamano wa Wafungwa Magerezani pamoja na Serikali kutumia fedha nyingi za walipa kodi kuwatunza wahamiaji haramu.

(iv) Uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya doria, taa za barabarani, tochi, kamera na vipima ulevi umekuwa ukichangia Jeshi la Polisi kushindwa kudhibiti ajali za barabarani.

(v) Baadhi ya magari ya Serikali na watu binafsi kuwa na ving’ora kinyume na utaratibu ilhali madereva wa magari hayo hawana uwelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya

ving'ora barabarani inahatarisha usalama wa watumiaji wengine wa barabara.

(vi) Upungufu wa Askari wa Uokozi Majini *(Divers)* unasababisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata changamoto wakati wa utekelezaji wa majukumu yake katika maeneo yenye bahari, maziwa na mito.

(vii) Kitendo cha baadhi ya madereva kupata leseni huku wakiwa hawana sifa na vigezo vya kuwa madereva, huchangia ajali za barabarani kutokana na madereva hao kutojua taratibu za barabarani ikiwemo Sheria ya Usalama Barabarani.

(viii) Wananchi katika maeneo mengi wameshindwa kukabiliana na majanga ya moto kutokana na kukosa elimu ya kukabiliana na kudhibiti majanga ya moto. Hivyo ni vema Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liendelee na mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya kukabiliana na majanga ya moto.

(ix) Uhaba wa vifaa na vitendea kazi kwa majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekuwa ni changamoto ya muda mrefu ambayo inaathiri utendaji kazi wa majeshi haya na pia kuathiri usalama wa raia na mali zao. Ucheleweshwaji wa fedha za Maendeleo kwa Fungu 14 na Fungu 29 kunaathiri utekelezaji wa miradi muhimu ya majeshi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza Maoni ya Kamati, naomba sasa kutoa Mapendekezo kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikakati ya Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kwa vitendo. Mpango wa Kunufaika na Fursa za Kiuchumi:-

Kwa kuwa, moja za faida za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mtangamano wa Kikanda ni wananchi wa nchi wanachama kunufaika na fursa mbalimbali ikiwemo za kiuchumi ili kupata tija iliyokusudiwa;

Na kwa kuwa, kwa sasa nchi yetu haina mpango mkakati unaoainisha fursa mbalimbali zilizopo na namna wananchi wanavyoweza kunufaika na fursa hizo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mkakati unaotekelezeka utakaoainisha fursa za kiuchumi na namna Watanzania watakavyonufaika na fursa hizo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za kikanda.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi:-

Kwa kuwa, ili nchi iweze kunufaika na Diplomasia ya Uchumi ipasavyo, ni muhimu wawekezaji wakahudumiwa kimkakati kwa kuzingatia vigezo katika kufikia malengo ya uwekezaji unaolengwa kufanyika katika ngazi zote kuanzia Wizara, kwenye Taasisi zinazohusika na uwekezaji pamoja na ngazi ya Mkoa na Wilaya;

Na kwa kuwa, utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi hauleweki vema nchini na hasa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ambapo ndiyo wawekezaji na wafanyabiashara wengi huwekeza, viongozi wa maeneo hayo hawana uelewa kuhusu Diplomasia ya Uchumi na hivyo kuathiri biashara za uwekezaji;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mkakati wa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi nchini ikiwemo ngazi ya Mkoa na Wilaya ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara na wawekezaji wanapokwenda katika

maeneo hayo wanahudumiwa kimkakati ili kupata tija iliyokusudiwa;

(c) Ushirikiano wa Kimkakati Baina ya Wizara Zinazohusika na Sekta za Uchumi:-

Kwa kuwa, ili nchi iendelee katika uwekezaji kupitia Diplomasia ya Uchumi ni muhimu Wizara za Sekta za Uchumi zikawa na ushirikiano wa kimkakati ili kufikia malengo tarajiwa;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa ushirikiano wa kimkakati baina ya Wizara za Sekta ya Uchumi kwa namna moja ama nyingine kunaathiri uwekezaji na biashara nchini na hivyo kuinyima nchi fursa ya kunufaika ipasavyo na Diplomasia ya Uchumi;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango wa ushirikiano wa kimkakati baina ya Wizara zinazohusika na Sekta ya Uchumi ili kuwa na utaratibu mzuri wa pamoja katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi.

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, Usarishaji wa Wanyama Hai:-

Kwa kuwa, usafirishaji wa wanyama hai kwenda nje ya nchi unapeleka ajira nje ya nchi sambamba na mapato ambayo yangeweza kubaki nchini; *(Makofi)*

Na kwa kuwa, usafirishaji wa nyama na mazao yatokanayo na wanyama badala ya wanyama hai utaongeza ajira nchini pamoja na mapato sambamba na kuongeza thamani ya bidhaa;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mazingira yatakayowezesha kusafirisha nyama nje ya nchi na kuachana na utaratibu wa kusafirisha wanyama hai ili kuongeza thamani ya bidhaa, kuongeza mapato zaidi pamoja na kuongeza wigo wa ajira nchini. *(Makofi)*

(e) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Uendelezaji wa Viwanja vya Balozi za Tanzania:-

Kwa kuwa, bajeti inayotengwa kila mwaka ni ndogo na haitoshi kujenga jengo moja la ubalozi pamoja na jengo la kitega uchumi;

Na kwa kuwa kushirikisha sekta binafsi na za umma katika ujenzi wa majengo ya balozi na kitega uchumi kutarahisisha upatikanaji wa fedha za ujenzi na hivyo ujenzi kukamilika kwa wakati;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, kabla ya kuanza utekelezaji wa mpango huo, Serikali ihakikishe kuwa inayo hati ya viwanja na vibali vyenye kuruhusu eneo husika kutumika kama Ofisi ya Ubalozi na matumizi ya kibiashara, kuwa na mpango kazi wa mradi na kuwa na mkakati wa kimasoko baada ya kukamilika ujenzi.

(f) Ukosefu wa Alama za Mipakani:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa alama za mipakani umekuwa ukisababisha wananchi wa nchi jirani kuvuka mpaka na kuingia nchini na kufanya shughuli za kibinadamu na shughuli nyingine haramu za kiuchumi.

Kwa kuwa, hali hiyo inachangia ugumu katika kudhibiti mipaka, na hivyo kuhatarisha usalama wa nchi;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kuweka alama za mipaka.

(g) Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubovu wa Barabara za Usalama Mipakani:-

Kwa kuwa barabara nyingi za kiusalama ni mbovu, na hali hiyo inasababisha vyombo vya ulinzi na usalama kukabiliwa na changamoto katika kudhibiti mipaka;

Na kwa kuwa changamoto ya ubovu wa barabara za usalama mipakani isipotatuliwa udhibiti wa mipaka utakuwa siyo wa uhakika;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itenge fedha za ujenzi wa barabara za usalama mipakani katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili kumaliza changamoto hiyo.

(h) Mheshimiwa Mwenyekiti, Usalama wa Raia na Mali zao:-

Kwa kuwa, mwitikio mdogo wa wananchi juu ya utoaji wa taarifa za wahalifu imekuwa sababu mojawapo ya uhalifu kuendelea kufanyika katika jamii;

Na kwa kuwa jamii ikiwa na mwamko wa kutoa taarifa kuhusu uhalifu kwa wakati itapelekea vitendo vya kihalifu kudhibitiwa mapema;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kutoa elimu ya kimkakati kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutoa taarifa za uhalifu kwa wakati ikiwa ni sehemu ya jamii kuchukua hatua dhidi ya uhalifu pamoja na umuhimu wa kuwa na ulinzi shirikishi katika makazi kama sehemu ya kukabiliana na uhalifu.

(i) Ukosefu wa Maadili kwa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahalifu wengi waliokamatwa na Jeshi la Polisi kuhusiana na vikundi vya panya - *road* ni vijana wenye umri wa miaka 13 hadi 30:-

Na kwa kuwa miongoni mwa vijana hao waliokamatwa ni wanafunzi wa Shule za Sekondari, hali hii inayoashiria ukosefu wa maadili kwa vijana wa umri huo; na ikiwa hatua hazitachukuliwa mapema Taifa litakuwa na vijana wasio na maadili;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kwa kushirikiana na Viongozi wa Dini pamoja na wadau mbalimbali iandae mpango mahsusi wa kuwaelimisha vijana kuanzia ngazi ya familia juu ya umuhimu wa maadili na kuepuka kufanya uhalifu ili kuwa na Taifa lenye nidhamu.

(j) Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhaba wa Vitendea Kazi;

Kwa kuwa, uhaba wa vitendea kazi kwa majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekuwa ni changamoto ya muda mrefu;

Na kwa kuwa, uhaba huo husababisha majeshi hayo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanishi na hivyo kuathiri usalama wa raia;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuyawezesha majeshi chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa vitendea kazi kwa kuzingatia mahitaji halisi na kwa wakati. *(Makofi)*

(k) Mheshimiwa Mwenyekiti, Upungufu wa Askari wa Uokozi Majini. Nchi yetu inazungukwa kwa kiasi kikubwa na bahari, mito, mabwawa na maziwa. Hivyo, ni muhimu kuwa na Askari wa Uokozi Majini na vitendea kazi vyake kwa mujibu wa mahitaji ili kukabiliana ipasavyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nenda ukahitimishe muda wako umekwisha, kengele ya pili imeshapigwa.

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mkakati wa muda mrefu wa kutoa mafunzo ya uokozi majini kwa askari wengi zaidi pamoja na ununuzi wa vifaa vya uokozi na kuzingatia mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa liipokee nakujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI, 2022- JANUARI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[*Inatolewa Chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

## SEHEMU YA KWANZA

### MAELEZO YA JUMLA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote kwa niaba ya Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama.

Aidha, kwa namna ya pekee nampongeza Mhe. Rais kwa kuimarisha hali ya mahusiano ya kimataifa kwa kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na Diplomasia ya Uchumi; pamoja na kuunda Tume ya kuangalia jinsi ya kuboresha Taasisi za Haki Jinai.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020; naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii ya Mwaka ni ya pili katika kipindi cha kwanza cha uhai wa Kamati katika Bunge la Kumi na Mbili. Kwa muktadha huu, naomba niwashukuru Wajumbe

ambao kwa kipindi chote tangu kuundwa kwake, wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wajumbe hao ni: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Vincent Paul Mbogo,Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Janeth Mauris Masaburi, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Cosato David Chumi, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - | Mjumbe; na |
| 21. | Mhe. Ally Mohamed Kassinge, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Aidha, masuala yanayoainishwa kwenye Taarifa hii ni yale tu ambayo Kamati inaona kuwa utekelezaji wake unahitaji juhudi zaidi kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa inayowasilishwa imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo: -

i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu Majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa;

ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;

iii) Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na

iv) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

**1.1 Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi; na kwamba Serikali inawajibika kwa Wananchi kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati hii inatekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge ambalo, kwa niaba ya Wananchi, ndio linaisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake kama Ibara ya 63 (2) (3) inavyoeleza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 6(3) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1) (2) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati Tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara Tatu (3) kama ifuatavyo:-

i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

ii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na

iii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati hii ni: -

i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

ii) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara zilizoainishwa hapo juu, Kamati hii ina majukumu matano (5) ya nyongeza yaliyoainishwa kwenye Kanuni ya 7(2) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni: -

i) Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;

ii) Kufuatilia mwenendo na hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;

iii) Kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;

iv) Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwananchama; na

v) Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

**1.2 Njia na Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati;**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na

matakwa ya Kanuni ya 136 (3) na (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2021/2022 na 2022/2023. Njia zilizotumika ni:-

i) Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;

ii) Vikao na Wajumbe wa Mabunge ya Kikanda pamoja na Wawakilishi katika Vyama vya Kibunge kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu yao;

iii) Ziara za kukagua utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;

iv) Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023;

v) Kutoa taarifa maalumu ya ushauri kwa Serikali juu ya masuala ya utekelezaji ambayo yanahitaji kurekebishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 135 (17); na

vi) Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Serikali na Taasisi zake.

### 1.3 Shughuli zilizotekelezwa

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2022 – hadi Januari, 2023 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo:-

### 1.3.1 Mafunzo na Semina mbalimbali

**Mheshimiwa Spika,** mafunzo yalitolewa katika kipindi kinachotolewa Taarifa ili kupata ufahamu, kujenga uelewa, kupata uzoefu na mbinu zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati na sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Mafunzo na Semina zilizotolewa yalihusu:-

i) Chanzo cha migogoro katika Jamii pamoja na umuhimu wa kutatua migogoro hiyo;

ii) Mchakato na masuala muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa Sera ya Ulinzi;

iii) Maudhui ya Sheria ya Parole na utaratibu wake katika kupunguza msongamano wa Wafungwa Magerezani;

iv) Utaratibu wa kushughulikia Bajeti ya Sekta ya ulinzi; uzoefu wa Mabunge mengine namna yanavyoshughulikia bajeti ya Sekta ya Ulinzi;

v) Mbinu na Stadi za uchambuzi wa Sheria za Kimataifa, Itifaki na Mikataba ya Kimataifa;

vi) Udhibiti wa ajali za barabarani na utaratibu wa fidia baada ya ajali; na

vii) Utekelezaji wa mkataba wa African Free Trade *Continental Area* pamoja na namna Tanzania inavyoweza kunufaika nao.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikiri kuwa mafunzo na semina hizo kwa kiasi kikubwa yamewajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hususan katika masuala yanayohusu bajeti katika sekta ya ulinzi, utungaji wa sera, utatuzi wa migogoro, ulinzi wa amani, Uchambuzi wa Mikataba ya Kimataifa na itifaki na Maudhui

ya Sheria ya Parole na utaratibu wake pamoja na ulinzi wa amani.

### 1.3.2 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

**Mheshimiwa Spika**, kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Wizara ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1)(d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake. Lengo la kupokea na kujadili taarifa hizo ilikuwa ni kulisaidia Bunge katika utekelezaji wa jukumu lake la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Matokeo ya shughuli hizo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

### 1.3.3 Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Matokeo ya shughuli hii yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Bajeti wa Mwezi Aprili hadi Juni, 2022.

### 1.3.4 Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Shughuli Mbalimbali za Wizara

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Masharti ya Kifungu cha 7(1)(d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za

Bunge, katika kipindi cha Mwezi Oktoba, 2022, Kamati ilitembelea moja ya mitandao ya Barabara kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokea Dodoma - Manyara hadi Namanga Mkoani Arusha. Aidha, Kamati pia ilitembelea miradi ya ujenzi wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya za Chamwino na Dodoma na kukagua ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Uhamiaji unaoendelea katika eneo la NCC Link Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa miradi iliyotembelewa yaliwasilishwa Serikalini. Hata hivyo, masuala ambayo Kamati inaona yanahitaji utekelezaji zaidi, yanafafanuliwa katika sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

### 1.3.5 Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi;

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Taarifa ya matokeo ya shughuli hiyo iliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Bajeti Mwezi Aprili na Juni 2022.[1]

### 1.3.6 Kushughulikia Hoja ya kuridhia Mkataba

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 7 (1) (b) cha Nyongeza ya Nnane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati ilishughulikia Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa nchi Huru za Afrika (OAU) ya Kuzuia na

[1] Taarifa Rasmi za Majadiliano ya Bunge ya tarehe 05 Mei, tarehe 19 Mei na tarehe 31 Mei, 2022.

Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 *(Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism of 2004)*. Kamati ilichambua kwa kina Itifaki hiyo na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake.[2]

### 1.3.7 Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (2) cha Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati pia ina jukumu ya Kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika; pamoja na taarifa za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti hayo, katika kipindi ambacho taarifa hii inatolewa, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Jukwaa la Kibunge la SADC (SADC PF) pamoja na vyama vya kibunge vya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA). Taarifa hizo zimefanyiwa uchambuzi na matokeo yake yamebainishwa katika taarifa hii.

### 1.3.8 Kufuatilia Mwenendo na Hali ya Mtangamano wa Jumumuiya ya Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa kuhusu Mwenendo wa hali ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

---

[2] Taarifa Rasmi ya Majadiliano Bungeni ya tarehe 19 Septemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Februari 2022 hadi Januari, 2023, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki. Maudhui ya taarifa hiyo yameiwezesha Kamati kuwa na msingi wa maoni na mapendekezo kuhusu ushirikiano na mtangamano huo.

### 1.3.9 Kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Mwezi Januari, 2023, Kamati ilikutana na Wizara inazozisimamia kwa lengo la kupokea taarifa mbalimbali. Miongoni mwa taarifa zilizopokelewa ilihusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa 6 uliofanyika Mwezi Februari, 2022. Lengo lilikuwa ni kupata taarifa ili kufanya tathmini kwa kiasi gani Serikali inatekeleza Maazimio ya Bunge kwa maslahi mapana ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati yanaonekana katika sehemu ya Pili ya taarifa iliyowasilishwa mezani.

## SEHEMU YA PILI

## UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.0 MAELEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, sasa naomba kutoa taarifa ya matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala mbalimbali yaliyobainika wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyoelezwa hapo awali, masuala yanayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili

kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa.

### 2.1 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Kamati inahusu masuala ambayo Kamati imebaini wakati inapitia na kujadili taarifa zilizowasilishwa na Wizara husika. Aidha, sehemu hii pia inabainisha changamoto mbalimbali ambazo Kamati imeziona kutokana na uchambuzi iliyoufanya.

### 2.2 Hali ya Ulinzi na Usalama wa Nchi

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi ambacho taarifa hii inatolewa, Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ajili ya kupokea taarifa ya hali ya ulinzi na usalama. Taarifa hizo pamoja na mambo mengine, zilibainisha hali ya usalama wa nchi, hali ya ulinzi wa mipaka pamoja na matukio yanayohatarisha ulinzi na usalama wa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa Kamati wa taarifa hizo pamoja na tathmini ya hali halisi, naomba nilijulishe Bunge lako tukufu kuwa, kwa ujuma hali ya ulinzi na usalama ni shwari na kwamba kuna amani, usalama na utulivu.

#### 2.2.1 Mikakati ya Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kwa Vitendo

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi ambacho taarifa hii inawasilishwa, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Mikakati ya Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi bado haujawa na ufanisi wa kutosha kwani unakabiliwa na changamoto kama ifuatavyo; -

i) Kukosekana kwa ushirikiano wa kimkakati na mahususi wenye malengo maalumu baina ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara nyingine za Sekta ya Uchumi katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Hali hiyo inapunguza tija na ufanisi katika kufikia malengo ya Diplomasia ya Uchumi;

ii) Kutokuwepo kwa utaratibu maalumu wa kuandikisha Diaspora na hivyo nchi kukosa takwimu sahihi za Diaspora. Changamoto hii inaathiri upatikanaji takwimu halisi za mchango wa Diaspora na mipango ya badaye ya Taifa;

iii) Diplomasia ya Uchumi haieleweki ipasavyo miongoni mwa watendaji wa Serikali husuani wa ngazi ya Mikoa na Wilaya. Hali hii husababisha wafanyabishara na wawekezeji kutohudumiwa ipasavyo na kwa ufanisi;

iv) Ushirikishwaji usiotosheleza wa wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi. Hali hiyo inapunguza wigo wa manufaa ya Diplomasia ya Uchumi.

v) Usafirishaji wa wanyama hai kama Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo kuhesabiwa kama sehemu ya mafanikio ilihali utaratibu huo unaathiri ajira na thamani ya mauzo nje. Mathalani, hadi kufikia Oktoba, 2022 wanyama hai kama Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo takribani 4000 walisafirishwa kwenda Bara la Asia na kuhesabiwa kuwa mafanikio. Hata hivyo, hali hii inazuia faida inayoweza kupatikana kutokana na kuongeza thamani ya bidhaa zinazotokana na wanyama hao.

### 2.2.2 Mpango wa Uendelezaji wa Majengo na Viwanja vya Balozi za Tanzania

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa zilizochambuliwa, Kamati ilibaini kuwa Tanzania inamiliki jumla ya majengo 108 kwenye Balozi zetu katika nchi mbalimbali. Kati ya majengo hayo; majengo 52 sawa na asilimia 48 yana hali nzuri, majengo 47 sawa na asilimia 44 yanahitaji ukarabati mkubwa na majengo 9 sawa na asilimia 8 yamechakaa kwa kiwango cha kuathiri hadhi na sifa ya Tanzania iliyonayo nje ya nchi. Takwimu hizo zinaonesha kuwa asilimia 52 ya majengo yote hayapo katika hali nzuri na hayaleti taswira nzuri katika nchi yetu. Vilevile, Tanzania inamiliki viwanja 11 vilivyopo katika maeneo muhimu kwenye nchi mbali mbali ambavyo havijaendelezwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, katika kutekeleza mpango wa kuendeleza viwanja vya Balozi za Tanzania nje ya nchi pamoja na ukarabati, Wizara imekamilisha zoezi la usanifu wa majengo 14. Aidha, Wizara inaendelea na utekelezaji wa miradi 5 yenye majengo 6 katika balozi 5 kwa kutangaza zabuni na kuwapata wakandarasi wa kutekeleza miradi hiyo. Miradi hiyo ni; Ujenzi wa Jengo la Ghorofa 17 la Ubalozi na Kitega Uchumi Kinshasa, Ujenzi wa majengo pacha ya Ghorofa 22 kwa ajili ya Ofisi za Balozi na Kitega Uchumi Nairobi, Ujenzi wa Jengo la Ubalozi na Makazi Muscat, Ujenzi wa Jengo la Ghorofa 8 la Ubalozi na Kitega Uchumi Moroni; Ukarabati wa jengo la zamani la ubalozi wa Tanzania Washington.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, kutokana na hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kutokuwa mzuri, Wizara tayari imekwishaanza mazungumzo na Taasisi za Umma na binafsi ili ziweze kushirikiana kwa ubia katika ujenzi wa majengo katika Balozi zetu. Taasisi ambazo zimeanza mazungumzo na Wizara ni NSSF, Benki ya CRDB na NMB.

**Mheshimiwa Spika**, hatua zilizochukuliwa na Wizara za kuanza majadiliano na Taasisi za Umma na binafsi ni utekelezaji wa maelekezo ya Kamati. Hii inatokana na ukweli kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Balozi na Majengo ya Kitega Uchumi licha ya kwamba hazipelekwi kama zilivyoidhinishwa, pia ni kidogo na kwamba ili kumaliza ujenzi wa jengo moja itachukua zaidi ya miaka 15.

Hivyo, ujenzi wa Ofisi za Balozi kwa ushirikiano wa Taasisi binafsi na za umma utasaidia utekelezaji wa miradi hiyo kwenda kwa kasi na hivyo kupata tija inayokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, ni matarajio ya Kamati kuwa majadiliano hayo yatafikia makubaliano yenye tija kwa pande zote mbili.

### 2.2.3 Hali ya Ushirikiano wa kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa kuhusu hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuwa hali ya ushirikiano wa kikanda na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni nzuri.

Aidha, mbali ya kwamba hali ya ushirikiano ni nzuri bado zipo changamoto mbalimbali ambazo zisiposhughulikiwa zinaweza kuathiri hali ya ushirikiano na mtangamano wa Jumuiya hii. Changamoto hizo ni pamoja na;-

i) Kasi ndogo ya Sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya kimataifa;

ii) Uelewa mdogo wa Wananchi kuhusiana na fursa zitokanazo na Mtangamano wa Kikanda;

iii) Baadhi ya nchi kuendelea kuweka tozo za ndani au kodi za ndani kwenye bidhaa zinazozalishwa katika Jumuiya kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani kinyume na makubaliano yaliyopo;

iv) Kuwepo kwa vikwazo mbalimbali visivyo vya kiushuru miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vikwazo hivyo vinaathiri biashara baina ya nchi wanachama;

v) Migogoro ya ndani ya kisiasa kwa baadhi ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, na

vi) Tofauti za kisiasa baina ya nchi wanachama; hali ambayo inapunguza ushirikiano katika Jumuiya.

### 2.2.4 Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Vyama Mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda

**Mheshimwa Spika**, kama ilivyoelezwa awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda.

**Mheshimwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha Januari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda kama ifuatavyo; -

i) Taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA);

ii) Taarifa za wawakilishi wa Bunge katika Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika (SADC-PF);

iii) Taarifa za wawakilishi wa Bunge katika Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA); na

iv) Taarifa za wawakilishi wa Bunge katika Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Bunge limewakilishwa ipasavyo katika vyombo mbalimbali na uanachama katika vyombo hivyo, umekuwa na manufaa yanayoendana na mahitaji ya Kibunge na Taifa. Hata hivyo kuna umuhimu wa kuendeleza ushirikiano kati ya wawakilishi hao na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**2.3 Mtiririko Usioridhisha wa Fedha za Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** mtiririko wa fedha za maendeleo umeendelea kuwa changamoto katika Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati. Mtiririko huo wa fedha ni kama unavyobainishwa hapa chini;-

**2.3.1 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (Fungu 34)**

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya Kamati inaonesha kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni miongoni mwa Wizara ambazo hazipewi fedha za miradi ya maendeleo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Mathalani, katika kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi 2021/2022 Wizara ilitengewa jumla ya **Shilingi 48,506,699,800.** Kati ya fedha hizo kiasi kilichopokelewa ni **Shilingi 9,654,529,520.00** sawa na **asilimia 19** ya fedha zilizoidhinishwa katika kipindi cha miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika,** hali hii ya kutopelekwa kwa fedha za maendeleo imeendelea pia katika kipindi hiki cha nusu Mwaka wa Fedha 2022/2023. Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2022, inaonesha kuwa hakuna

fedha ya miradi ya maendeleo iliyopokelewa. Hali hii inaathiri mipango ya ukarabati na uendelezaji wa ujenzi wa Ofisi za Kibalozi na Majengo ya Vitega Uchumi pamoja na makazi ya watumishi.

### 2.3.2 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2022 na kubaini kuwa; Fungu 51 - Wizara, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Fungu 28 - Jeshi la Polisi na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji ndiyo pekee yalikuwa yamepokea fedha za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo; Wizara imepokea **Shilingi 39,684,581** sawa na **asilimia 3**, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imepokea **Shilingi 13,585,690,025.95** sawa na **asilimia 21**, Fungu 28 limepokea **Shilingi 95,660,000** sawa na **asilimia 0.29** na Fungu 93 limepokea **Shilingi 3,544,249,191.93** sawa na **asilimia 29** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, kati ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu 51 - Wizara ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba salama tatu (3) za wahanga wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar pamoja na ununuzi wa magari mawili.

Aidha, kwa Upande wa Fungu 28 - Jeshi la Polisi, Kamati ilibaini kuwa fedha zilizotolewa ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo Maafisa wa Polisi Kata/Shehia katika kutekeleza muundo wa Ushirikishwaji wa jamii pamoja na kutoa mafunzo kwa Maafisa wa Polisi Kitengo cha Habari ili kuboresha utoaji wa taarifa za kazi za Polisi.

Kwa upande wa Fungu 93 fedha hizo zinalenga kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo; ununuzi wa magari 30 pamoja

na Ukamilishaji wa ujenzi Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi, Mtwara na Geita.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Fungu 29: Jeshi la Magereza liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 21,369,600,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia Desemba, 2022 hakukuwa na fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa mieadi ya maendeleo.

Aidha, kwa upande wa Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, liliidhinishiwa **Shilingi 9,930,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo hadi kufikia Disemba, 2022 hakukuwa na fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kutokutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa Mafungu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kunaathiri mpango wa utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

### 2.3.3 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 230,333,171,000.00** kwa mafungu yake yote matatu ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2022 Wizara hii ilikuwa imepokea fedha za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo;-

(i) Fungu 38 - Ngome hadi kufikia mwezi Disemba 2022, lilikuwa limepokea kiasi cha **Shilingi 10,000,000,000.00** sawa na **asilimia 17.74** ya bajeti iliyoidhinishwa.

(ii) Fungu **39 - JKT** halikuwa limepokea kiasi chochote cha fedha; na

(iii) Fungu 57 - Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 52,912,641,003.19** sawa na **asilimia 33.07** ya fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge.

**2.4Upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati wa Mwezi Oktoba, 2022 kuhusu hali ya upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa ulibaini kuwa, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ilisajili watu Milioni 23,630,813 hadi kufikia Mwezi Novemba, 2022 ikiwa ni asilimia 68 ya lengo la watu Milioni 34,080,610 waliokusudiwa kusajiliwa ifikapo Mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilibaini kuwa kati ya idadi ya watu Milioni 23,406,360 waliosajiliwa, ni watu Milioni19,634,720 ambao wamepata namba za utambulisho ikiwa ni sawa na asilimia 84 ya watu waliosajiliwa. Aidha, Kamati ilihoji idadi ya vitambulisho vilivyotolewa kulingana na Namba hizo za usajili tangu mradi huu ulipoanza mwaka 2012 na kubaini kuwa vitambulisho Milioni 11,055,315 vilizalishwa ikiwa ni sawa na asilimia 56 ya Namba za Usajili zilizopo. Aidha, kati ya vitambulisho vilivyozalishwa, NIDA ilikuwa imegawa vitambulisho 10,230,710.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea bado idadi ya vitambulisho vinavyozalishwa ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Aidha, zipo changamoto mbalimbali zinazochelewesha uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa. Kutokana na ukweli kuwa kwa sasa huduma nyingi zimeunganishwa na kitambulisho cha Taifa, Kamati ililipa suala hili uzito wa kipekee na hivyo ilitoa ushauri maalum kuhusu hatua za kuchukua ili kuboresha upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushauri uliotolewa utashughulikiwa na kwamba juhudi kuhusu suala hili zitaripotiwa mara wa mara kwenye Kamati.

### 2.5 Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao katika kipindi cha Mwezi Julai hadi Disemba, 2022. Taarifa hizo, pamoja na mambo mengine zilianisha hali ya uhalifu nchini na matukio yanayohatarisha hali ya usalama wa raia na mali zao. Miongoni mwa uhalifu uliohatarisha usalama wa raia na mali zao katika kipindi tajwa ni uhalifu unaofanywa na vikundi vya panyaroad katika mikoa ya Dar es salaam na Pwani.

**Mheshimiwa Spika,** nafurahi kutoa taarifa kuwa kazi nzuri iliyofanywa na Jeshi la Polisi imewezesha kudhibiti uhalifu uliokuwa ukifanywa na vikundi vya panyaroad na kuendelea kudhibiti uhalifu wa silaha.

Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa ni wajibu wa Jeshi la Polisi kuhakikisha kuwa uhalifu wa aina yoyote unadhibitiwa ipasavyo na kutojirudia tena nchini.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati pia ulibaini kuwa kwa kipindi cha Mwezi Oktoba hadi Desemba, 2022 makosa dhidi ya binadamu yaliyoripotiwa yalikuwa **3,092** hilo ni ongezeko la makosa **516** sawa na **asilimia 20** ikilinganishwa na makosa **2,576** yaliyoripotiwa katika kipindi kama hichi kwa Mwaka 2021. Ongezeko hilo litumike kama ishara ya mahitaji ya juhudi za kudhibiti makosa dhidi ya binadamu.

### 2.6 Ajali za Barabarani

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Oktoba - Disemba, 2022; matukio ya ajali yaliyosababisha vifo katika kipindi hicho ni **281** ikilinganishwa na matukio **273** yaliyoripotiwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Hili ni ongezeko la makosa **8,** sawa na asilimia **2.9.** Aidha, Katika kipindi hicho idadi ya, watu waliokufa kutokana na ajali ni **382** ikilinganishwa na idadi ya watu **367** waliokufa kwa kipindi kama hicho Mwaka 2021. Hili ni ongezeko la watu **15** sawa na asilimia **4.1.**

**Mheshimiwa spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulionesha kuwa ajali za barabarani zimekuwa zikichangiwa na;-

i) Baadhi ya Askari wa Usalama Barabarani kujihusisha na rushwa na hivyo kushindwa kutimiza wajibu wao katika kushughulikia makosa ya barabarani;

ii) Uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya doria katika barabara kuu, taa za kuongozea magari, upungufu wa *speed radar touch,* upungufu wa kamera na vipima ulevi;

iii) Kukosekana kwa utashi wa kisiasa kwa baadhi ya wanasiasa na hivyo kuingilia utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani. Mathalani, kuwazuia Askari kuwakamata bodaboda au bajaji wanapofanya uvunjifu wa Sheria;

iv) Ubovu wa baadhi ya barabara hali ambayo wakati mwingine husababisha ajali;

v) Hulka za kibinadamu kuamini kuwa ajali hazizuiliki na hivyo kuendesha pasipo kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani; na

vi) Kuwa na madereva wengi wasio na sifa ya udereva. Hali hii inasababishwa na mfumo uliopo wa utoaji leseni za udereva kutoa mwanya kwa watu wasio na sifa ya kuwa dereva kupata leseni.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa katika siku za karibuni kumeibuka wimbi la magari ya watu/taasisi binafsi na za umma, kufungwa ving'ora kinyume na utaratibu ilihali wakiwa hawana uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya magari yenye ving'ora. Hali hiyo inahatarisha usalama kwa watumiaji wengine wa barabara.

## 2.7 Msongamano wa Wafungwa katika Magereza

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Magereza kwa kipindi cha kuanzia Julai - Desemba, 2022 na kubaini kuwa, bado kuna Msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Magerezani ambapo jumla ya Mahabusu na Wafungwa Magerezani ni **32,146** ikiwa ni sawa na **asilimia 7.5** zaidi ya uwezo wa Magereza yaliyopo kwa sasa wa kuwahifadhi Wafungwa na Mahabusu **29,902.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa hali hii imeendelea kuchangiwa na;-

i) Uchache wa Magereza nchini ikilinganishwa na idadi ya Wafungwa;

ii) Utegemezi wa adhabu za kifungo gerezani;

iii) Kutotumika ipasavyo kwa mpango wa Parole; na

iv) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kukaa magerezani kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Serikali inafanya juhudi mbalimbali kukabiliana na msongamano wa Wafungwa; Kamati ina maoni kwamba maazimio yaliyotolewa na Bunge katika Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022 kuhusu msongamano wa Wafungwa, yanahitaji kufanyiwa kazi inavyostahili.

## 2.8 Hali ya Wahamiaji Haramu Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata wasaa wa kupokea na kujadili taarifa kuhusu wahamiaji haramu nchini; ambapo taarifa ya Wizara ilionesha kuwa kwa kipindi cha Septemba - Desemba, 2022 Jumla ya wahamiaji haramu **7,493** walikamatwa katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulibaini kuwa katika kipindi cha Septemba hadi Desemba, 2022, katika Magereza mbalimbali nchini kulikuwa na Wafungwa na Mahabusu wahamiaji haramu wapatao **3,108.** Idadi hiyo imeongezeka kwa **asilimia 93** ikilinganishwa na wahamiaji haramu **1,608** waliokuwepo magerezani katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Uwepo wa wahamiaji haramu magerezani, unaigharimu Serikali kiasi cha wastani wa **Shilingi 15,540,000 kwa siku** katika kuwapatia huduma mbalimbali za msingi. Ikiwa hali itabakia kama ilivyo kwa wafungwa/mahabusu hao waliopo magerezani, Serikali inatumia Shilingi **Bilioni 5.67**[3] kwa mwaka kuwatunza wafungwa/mahabusu hao.

**Mheshimiwa Spika**, Kiasi hicho cha fedha kinachotumika kuwatunza wafungwa/mahabusu hao kingeweza kununua **madawati 81,030** kwa kila dawati kugharimu **Shilingi 70,000.00,** Kwa msingi huo kuna haja ya Serikali kuepuka kutumia gharama kuwatunza wafungwa/mahabusu haramu na kuzielekeza kwenye miradi ya maendeleo.

### 2.9 Utendaji kazi wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati iipokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Jeshi hilo limeendelea kutekeleza majukumu yake likiwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji kazi wake. Changamoto hizo ni pamoja na;-

i) Uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji nchini. Kwa sasa Jeshi hili lina jumla ya vituo 80 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya vituo 177 vinavyohitajika nchini;

ii) Uhaba wa magari ya kuzima moto na uokozi. Kwa sasa Jeshi lina magari ya kuzima moto 76 ikilinganishwa na

[3] Gharama ya kumhudumia Mfungwa/mahabusu mmoja ni shilingi 2500 kwa siku.

mahitaji ya magari 237 na magari ya uokozi yapo 4 ikilinganishwa na mahitaji ya magari 35. Aidha, magari ya kubebea wagonjwa yapo 2 ikilinganishwa na mahitaji ya magari 169. Magari ya ngazi *(turntable ladder)* lipo 1 ikilinganishwa na mahitaji ya magari 9;

iii) Upungufu wa *fire hydrants* katika maeneo mengi ya mijini na uchakavu wa vyanzo vilivyopo. Katika *fire hydrants* 2,339 zilizopo nchini 1,638 ni nzima na 701 zinahitaji matengenezo;

iv) Upungufu wa Askari wa Uokozi Majini *(Divers)* ambapo waliopo kwa sasa ni Askari 16 nchi nzima wakati mahitaji ni Askari 435;

v) Ujenzi holela wa nyumba na miundombinu katika maeneo mengi ya mijini hali ambayo husababisha kutofikika kwa urahisi wakati wa dharura za kuzima moto na uokoaji; na

vi) Wananchi kukosa elimu juu ya namna bora ya kuchukua tahadhari na kukabiliana na majanga ya moto na majanga mengine.

**2.10 Utendaji kazi wa Jeshi la Magereza**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi ambacho taarifa hii inatolewa, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za tendaji kazi wa Jeshi la Magereza. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Jeshi hilo linatekeleza majukumu likiwa linakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri utandaji kazi wa kila siku. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Migogogoro ya ardhi na wakati mwingine ardhi ya Jeshi kutwaliwa na Serikali kutokana na Jeshi la Magereza kutokuwa na Hati ya Umiliki. Juhudi za upimaji zinakwama kutokana na Jeshi kutokupatiwa fedha kwa ajili ya shughuli hiyo;

ii) Uhaba wa Magari ya Viongozi na ya kusafirishia mahabusu kwenda mahakamani; mathalan, kwa sasa Jeshi lina magari 390 ikilinganishwa na mahitaji ya magari 800;

iii) Upungufu wa nyumba za watumishi Idadi ya nyumba zilizopo ni 5,199 ikilinganishwa na idadi ya maafisa na Askari 12,888 waliopo; na

iv) Mabadiliko ya tabianchi huathiri shughuli za urekebishaji katika uzalishaji wa mazao ya kilimo.

**2.11 Utendaji kazi wa Jeshi la Uhamiaji**

**Mheshimwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati iipokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Jeshi la Uhamiaji. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Jeshi hilo linatekeleza majukumu yake likiwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utendaji kazi wake. Changamoto hizo ni pamoja na;

i) Uwepo wa wahamiaji haramu na usafirishaji haramu wa binadamu; Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazokabiliwa na tatizo la wahamiaji haramu.

ii) Upungufu wa majengo ya ofisi na nyumba za kuishi watumishi. Mahitaji ya ofisi ni **majengo 159** wakati majengo ya ofisi yaliyopo **ni 57** sawa na **asilimia 35** na hivyo kuwepo **upungufu wa ofisi 102.**

Kwa upande wa nyumba za makazi mahitaji ni nyumba 4,228 lakini nyumba **zilizopo ni 454** sawa na **asilimia 10**. Hivyo kuwepo upungufu wa **nyumba 3,774**.

iii) Uwepo wa madeni yenye jumla ya kiasi cha **Shilingi 2,716,668,696.36.** Kiasi hicho kinajumuisha madai ya watumishi, wazabuni, wakandarasi na watoa huduma.

### 2.12 Kukosekana kwa Alama za Mipaka ya Nchi *(Beacons);*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu Hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na kubaini changamoto ya kukosekana kwa alama za mipaka *(beacons)*. Hali hiyo husababisha wananchi kutoka nchi tunazopakana nazo kuendesha shughuli haramu za kiuchumi. Mathalani, wafugaji kufanya shughuli za ufugaji katika maeneo ya Mipaka ambayo hayaruhusiwi kisheria. Aidha, kukosekana kwa alama hizo husababisha wananchi hao kuingia nchini kwa utetezi kuwa hakuna alama za mipaka na hivyo kushindwa kutambua kuwa wameingia nchi nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa rasmi za Bunge zinaonesha kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu na Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kushughulikia suala hili. Hata hivyo, suala hili halijashughulikiwa kwa ukamilifu wake.

### 2.13 Ubovu wa Barabara za Usalama Mipakani

**Mheshimiwa Spika**, Ubovu wa barabara za usalama mipakani umeendelea kusababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka yetu kwa nyakati zote. Katika baadhi ya maeneo vyombo vya ulinzi na usalama vinapata changamoto ya kufika kutokana na ubovu wa barabara. Hali hiyo si nzuri kwa usalama katika maeneo ya mipakani na nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa rasmi za Bunge zinaonesha kuwa tangu Bunge la Kumi, Kamati hii imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutatua changamoto hii. Hata hivyo, suala hili bado halijatekelezwa kwa ukamilifu wake.

## 2.14 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Sita wa Bunge;

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli za Kamati katika Mkutano wa 6 wa Bunge, Mwezi Februari, 2022, Kamati ilipendekeza mambo mbalimbali kwa Wizara inazozisimamia na Bunge likapitisha mapendekezo hayo kuwa Maazimio. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilikuwa na Maazimio mawili (2) ambapo Azimio moja limetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na Azimio lingine halijatekelezwa kabisa. Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilikuwa na Maazimio 9; ambapo Maazimio matatu yametekelezwa kwa ukamilifu, Maazimio matatu yametekelezwa kwa sehemu na Maazimio matatu hayajatekelezwa kabisa. Hivyo, kwa ujumla kasi ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge sio ya kuridhisha.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo: -

#### 3.1.1 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

i) Kukosekana kwa ushirikiano wa kimkakati na mahususi wenye malengo maalumu baina ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara nyingine za sekta ya uchumi katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kunapunguza tija na ufanisi katika kufikia malengo ya diplomasia ya chumi;

ii) Kutokuwepo kwa utaratibu maalumu wa kuandikisha Diaspora kunasababisha nchi kukosa takwimu sahihi za Diaspora. Changamoto hii inaathiri upatikanaji takwimu

halisi za mchango wa Diaspora na mipango ya badae ya nchi kuhusu Diaspora;

iii) Kutokueleweka ipasavyo kwa Diplomasia ya Uchumi nchini na hasa katika ngazi ya Mikoa na Wilaya kunasababisha wafanyabishara na wawekezeji kutohudumiwa ipasavyo na kwa ufanisi;

iv) Ushirikishwaji usiotosheleza wa wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi unapunguza wigo wa manufaa ya Diplomasia ya Uchumi. Hivyo, ni vema Serikali ikaongeza mawanda ya ushirikishwaji wa wadau katika utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi;

v) Usafirishaji wa wanyama hai kama Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo badala ya mazao yatokanayo na wanyama hao unasababisha kupotea kwa faida inayoweza kupatikana kwa kuongeza thamani ya bidhaa zinazotokana na wanyama hao.

vi) Pamoja na nia ya dhati ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Balozi za Tanzania, kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kumeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi;

vii) Ili kuweza kufikia malengo ya uanzishwaji wa Jumuiya za Kikanda ni muhimu nchi wanachama zingazingatia ipasavyo masharti ya Mkataba wa Jumuiya. Hivyo, ni vema Tanzania ikaendelea kushawishi nchi wanachama kuzingatia inavyostahili masharti ya mkataba wa uanzishishwaji wa Jumuiya;

viii) Wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu upatikanaji wa masoko ya bidhaa mbalimbali katika nchi

za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hali hii inasababisha wananchi kutonufaika ipasavyo na fursa za kiuchumo ikiwemo masoko ya bidhaa katika Jumuiya.

### 3.1.2 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

i) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi *(beacons)* kunachangia uvamizi wa shughuli za binadamu na shughuli haramu za kiuchumi katika maeneo hayo jambo ambalo si zuri kwa ulinzi na usalama wa nchi;

ii) Ubovu wa barabara za usalama mipakani unasababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka ya nchi.

### 3.1.3 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

(i) Mwitikio mdogo wa wananchi juu ya utoaji wa taarifa za wahalifu imekuwa sababu moja wapo ya uhalifu kuendelea kufanyika katika Jamiii. Ikiwa Jamii itakuwa na mwamko wa kutoa taarifa kuhusu uhalifu kwa wakati itasaidia uhalifu kudhibitiwa mapema;

(ii) Wahalifu wengi waliokamatwa kuhusianana vikundi vya panyaroad ni vijana wa umri wa miaka kati ya 13 hadi 30. Huku baadhi yao wakiwa bado wanafunzi wa Sekondari. Hii inaashiria vijana hao kuwa na tamaa na Ukosefu wa maadili; hali ambayo sio afya kwa Taifa na kizazi kijacho;

(iii) Ongezeko la wahamiaji haramu kwa kiasi kikubwa linachangia msongamano wa Wafungwa Magerezani pamoja na Serikali kutumia fedha nyingi za walipa kodi kuwatunza wahamiaji haramu;

(iv) Uhaba wa vitendea kazi kama vile; magari ya doria, taa za barabarani, tochi, kamera na vipima ulevi umekuwa ukichangia Jeshi la Polisi kushindwa kudhibiti ajali za barabarani;

(v) Baadhi ya magari ya Serikali na watu binafsi kuwa na ving'ora kinyume na utaratibu ilihali Madereva wa magari hayo hawana uwelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya ving'ora barabarani inahatarisha usalama wa watumiaji wengine wa barabara;

(vi) Upungufu wa Askari wa Uokozi Majini (Divers) unasababisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupata changamoto wakati wa utekelezaji wa majukumu yake katika maeneo yenye Bahari, Maziwa na Mito;

(vii) Kitendo cha baadhi ya madereva kupata leseni huku wakiwa hawana sifa na vigezo vya kuwa madereva huchangia ajali za barabarani kutokana na madereva hao kutojua taratibu za barabarani ikiwemo Sheria ya usalama Barabarani;

(viii) Wananchi katika maeneo mengi wameshindwa kukabiliana na majanga ya moto kutokana na kukosa elimu ya kukabiliana na kudhibiti majanga ya moto. Hivyo ni vema Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liendelee na mkakati wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya kukabiliana na majanga ya moto.

(ix) Uhaba wa vifaa na vitendea kazi kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekuwa ni changamoto ya muda mrefu ambayo inaathiri utendaji kazi wa Majeshi haya na pia kuathiri usalama wa raia na mali zao; na

(x) Ucheleweshwaji wa fedha za Maendeleo kwa Fungu 14 na Fungu 29 kunaathiri utekelezaji wa miradi muhimu ya Majeshi hayo.

### 3.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza Maoni ya Kamati, naomba sasa kutoa Mapendekezo kama ifuatavyo;-

### 3.2.1 Mikakati ya Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi kwa Vitendo

### A. Mpango wa Kunufaika na Fursa za Kiuchumi

**KWA KUWA,** moja za faida za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mtangamano wa Kikanda ni Wananchi wa nchi wanachama kunufaika na fursa mbalimbali ikiwemo za kiuchumi ili kupata tija iliyokusudiwa;

**NA KWA KUWA,** kwa sasa nchi yetu haina mpango mkakati unaoainisha fursa mbalimbali zilizopo na namna wananchi wanavyoweza kunufaika na fursa hizo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mkakati unaotekelezeka utakaoainisha fursa za kiuchumi na namna Watanzania watakavyonufaika na fursa hizo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za kikanda.

### B. Mpango wa Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi

**KWA KUWA**, ili nchi iweze kunufaika na Diplomasia ya Uchumi ipasavyo ni muhimu wawekezaji wakahudumiwa kimkakati kwa kuzingatia vigezo katika kufikia malengo ya uwekezaji unaolengwa kufanyika katika ngazi zote kuanzia Wizarani, kwenye Taasisi zinazohusika na uwekezaji pamoja na ngazi ya Mkoa na Wilaya;

**NA KWA KUWA**, Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi hauleweki vema nchini na hasa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ambapo ndiyo wawekezaji na wafanyabiashara wengi huwekeza. Viongozi wa maeneo hayo hawana uelewa kuhusu Diplomasia ya Uchumi na hivyo kuathiri biashara na uwekezaji;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mkakati wa utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi nchini ikiwemo ngazi ya Mkoa na Wilaya ili kuhakikisha kuwa wafanyabiashara na wawekezaji wanapokwenda katika maeneo hayo wanahudumiwa kimkakati ili kupata tija iliyokusudiwa.

**C. Ushirikiano wa Kimkakati Baina ya Wizara Zinazohusika na Sekta za Uchumi**

**KWA KUWA,** ili nchi iendelee katika uwekezaji kupitia Diplomasia ya Uchumi ni muhimu Wizara za Sekta za Uchumi zikawa na ushirikiano wa kimkakati ili kufikia malengo tarajiwa;

**NA KWA KUWA**, Kukosekana kwa ushirikiano wa kimkakati baina ya Wizara za Sekta ya Uchumi kwa namna moja ama nyingine kunaathiri uwekezaji na biashara nchini na hivyo kuinyima nchi fursa ya kunufaika ipasavyo na Diplomasia ya Uchumi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango wa ushirikiano wa kimkakati baina ya Wizara zinazohusika na Sekta ya Uchumi ili kuwa na uratibu mzuri wa pamoja katika kutekeleza Diplomasia ya Uchumi.

**D. Usarishaji wa Wanyama Hai**

**KWA KUWA,** usafirishaji wa wanyama hai kwenda nje ya nchi unapeleka ajira nje ya nchi sambamba na mapato ambayo yangeweza kubaki nchini;

**NA KWA KUWA,** usafirishaji wa nyama na mazao yatokanayo na wanyama badala ya wanyama hai utaongeza ajira nchini pamoja na mapato sambamba na kuongeza thamani ya bidhaa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mazingira yatakayowezesha kusafirisha nyama nje ya nchi na kuachana na utaratibu wa kusafirisha wanyama hai ili kuongeza thamani ya bidhaa, kuongeza mapato zaidi pamoja na kuongeza wigo wa ajira nchini.

### 3.2.2 Mpango wa Uendelezaji wa Viwanja vya Balozi za Tanzania

**KWA KUWA**, bajeti inayotengwa kila mwaka ni ndogo na haitoshi kujenga jengo moja la ubalozi pamoja na jengo la kitega uchumi;

**NA KWA KUWA** kushirikisha sekta binafsi na za umma katika ujenzi wa majengo ya balozi na kitega uchumi kutarahisisha upatikanaji wa fedha za ujenzi na hivyo ujenzi kukamilika kwa wakati;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, kabla ya kuanza utekelezaji wa mpango huo Serikali ihakikishe kuwa inayo hati ya kiwanja na vibali vyenye kuruhusu eneo husika kutumika kama ofisi ya ubalozi na matumizi ya kibiashara, kuwa na mpango kazi wa mradi na kuwa na mkakati wa kimasoko baada ya kukamilika ujenzi.

### 3.2.3 Ukosefu wa Alama za Mipaka na Ubovu wa Barabara za Usalama Mipakani

#### A. Ukosefu wa Alama za Mipaka

**KWA KUWA** ukosefu wa alama za mipakani umekuwa ukisababisha wananchi wa nchi jirani kuvuka mpaka na kuingia nchini na kufanya shughuli za kibinadamu na shughuli nyingine haramu za kiuchumi;

**NA KWA KUWA** hali hiyo inachangia ugumu katika kudhibiti mipaka; na hivyo kuhatarisha usalama wa nchi;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kuweka alama za mipaka.

**B. Ubovu wa Barabara za Usalama Mipakani**

**KWA KUWA** barabara nyingi za kiusalama ni mbovu na hali hiyo inasababisha vyombo vya ulinzi na usalama kukabiliwa na changamoto katika kudhibiti mipaka;

**NA KWA KUWA** changamoto ya ubovu wa barabara za usalama mipakani isipotatuliwa udhibiti wa mipaka utakuwa si wa uhakika;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itenge fedha za ujenzi wa barabara za usalama mipakani katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ili kumaliza changamoto hiyo.

**3.2.4 Usalama wa Raia na Mali zao**

**A. Mwitikio Mdogo wa Wananchi Juu ya Utoaji Taarifa za Uhalifu**

**KWA KUWA**, Mwitikio mdogo wa Wananchi juu ya utoaji wa taarifa za wahalifu imekuwa sababu moja wapo ya uhalifu kuendelea kufanyika katika Jamiii;

**NA KWA KUWA** jamii ikiwa na mwamko wa kutoa taarifa kuhusu uhalifu kwa wakati itapelekea vitendo vya kihalifu kudhibitiwa mapema;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kutoa elimu ya kimkakati kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutoa taarifa za uhalifu kwa wakati ikiwa ni sehemu ya jamii kuchukua hatua dhidi ya uhalifu pamoja na umuhimu wa

kuwa na ulinzi shirikishi katika makazi kama sehemu ya kukabiliana na uhalifu.

**B. Ukosefu wa Maadili kwa Jamii**

**KWA KUWA,** Wahalifu wengi waliokamatwa na Jeshi la Polisi kuhusiana na vikundi vya *panyaroad* ni vijana wenye umri wa miaka 13 hadi 30;

**NA KWA KUWA** miongoni mwa vijana waliokamatwa ni wanafunzi wa Shule za Sekondari, hali hii inaashiria Ukosefu wa maadili kwa vijana wa umri huo. Na ikiwa hatua hazitachukuliwa mapema Taifa litakuwa na vijana wasio na maadili,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kwa kushirikiana na Viongozi wa Dini pamoja na wadau mbalimbali iandae mpango mahsusi wa kuwaelimisha vijana kuanzia ngazi ya Familia juu ya umuhimu wa maadili na kuepuka kufanya uhalifu ili kuwa na Taifa lenye nidhamu.

**C. Uhaba wa Vitendea Kazi**

**KWA KUWA**, Uhaba wa vitendea kazi kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekuwa ni changamoto ya muda mrefu;

**NA KWA KUWA,** uhaba huo husababisha Majeshi hayo kushindwa kutekeelеza majukumu yao kwa ufanishi na hivyo kuathiri usalama wa raia na mali zao;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuyawezesha Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Nani ya Nchi vitendea kazi kwa kuzingatia mahitaji halisi na kwa wakati.

**D. Upungufu wa Askari wa uokozi majini *(Divers)***

**KWA KUWA**, nchi yetu inazungukwa kwa kiasi kikubwa na Bahari, Mito, Mabwawa na Maziwa. Hivyo, ni muhimu kuwa na Askari wa Uokozi majini na vitendea kazi vyake kwa mujibu wa mahitaji ili kukabiliana ipasavyo na ajali za majini;

**NA KWA KUWA**, kwa sasa, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linakabiliwa na upungufu wa Askari na vitendea kazi vya uokozi majini hali inayoathiri ufanisi wa Jeshi hilo katika maeneo yenye Mito, Maziwa, Mabwawa na Bahari;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mkakati wa muda mrefu wa kutoa mafunzo ya uokozi majini *(divers)* kwa Askari wengi zaidi pamoja na ununuzi wa vifaa vya uokozi kwa kuzingatia mahitaji halisi.

**3.2.5 Ajali za Barabarani**
**A. Utoaji Leseni za Udereva kwa Wasiokidhi Vigezo**

**KWA KUWA,** mfumo wa sasa wa utoaji leseni za udereva unatoa mwanya kwa baadhi wa madereva ambao hawana sifa wala vigezo kupata leseni;

**NA KWA KUWA** hali hii huchangia ajali za barabarani kutokana na kuwa na madereva wasio na sifa za kuendesha vyombo vya moto;

**KWA HIYO BASI**; Bunge linaazimia kwamba, Serikali ianze mchakato wa kuutazama upya mfumo uliopo wa utoaji leseni za udereva ili kuwa na mfumo imara ambao utatoa fursa kwa madereva pekee waliokidhi vigezo kupata leseni.

### B. Ufungwaji wa Ving'ora Kinyume na Utaratibu

**KWA KUWA**, katika siku za karibuni baadhi ya magari ya Serikali na binafsi yamefungwa ving'ora kinyume na utaratibu;

**NA KWA KUWA**, Madereva wa magari hayo hawana uwelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya magari yenye ving'ora na hivyo kuendesha pasipo tahadhari na kuhatarisha usalama wa watumiaji wengine wa barabara;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, kudhibiti matumizi holela ya ving'ora kwenya magari na kuhakikisha kuwa ving'ora hivyo vinafungwa kwenye magari yanayostahili.

### C. Uendeshaji Mbovu na Usiofuata Sheria kwa Madereva wa Bodaboda

**KWA KUWA**, uendeshaji mbovu na usiofuata Sheria za Usalama wa Barabarani unafanywa na madereva bodaboda umekuwa moja ya chanzo cha ajali za barabarani;

**NA KWA KUWA**, Wanasiasa wamekuwa wakiingilia Jeshi la Polisi katika kusimamia Sheria ya Usalama Barabarani dhidi ya waendesha boda boda, jambo linaloweza kusababisha vijana wengi ambao ni madereva wa boda boda kupata ulemavu wa kudumu na wengine kupoteza maisha kutokana na ajali. Aidha, Kamati inatoa rai kwa wanasiasa kuacha kuliingilia Jeshi hilo kwani kwa kufanya hivyo kunasababisha vijana wengi wa madereva bodaboda kupoteza maisha kutokana na ajali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali iendelee kudhibiti uendeshaji mbovu wa madereva bodaboda kwa kusimamia ipasavyo Sheria ya Usalama Barabarani.

### 3.2.6 Suala la Wahamiaji Haramu

**KWA KUWA**, suala la wahamiaji haramu nchini ni miongoni mwa sababu zinazochangia msongamano wa wafungwa magerezani;

**NA KWA KUWA,** Serikali inatumia fedha nyingi za walipa kodi kuwatunza wafungwa na mahabusu wahamiaji haramu;

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba, Serikali pamoja na Mamlaka zake kuja na mpango mkakati wa muda mrefu na unaotekelezeka utakao hakikisha kwamba, nchi yetu haindelei kuwa na wahamaiji haramu.

### 3.2.7 Mapendekezo ya Jumla

**KWA KUWA,** Bunge linapotoa Maazimio kuhusu jambo mahsusi, linafanya hivyo ili kuhakikisha tija iliyokusudiwa inafikiwa kwa ustawi wa nchi yetu;

**NA KWA KUWA,** tathmini ya Kamati inaonesha Serikali imetekeleza sehemu tu ya maazimio ya Bunge; na hivyo kusasababisha jambo ambalo limeazimiwa kubakia kama lilivyo au kuwa na athari zaidi kwa ustawi wa nchi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa maazimio yote yaliyotolewa na Bunge.

**KWA KUWA,** Maazimio ya Bunge yanatolewa kwa niaba ya wananchi,

**NA KWA KUWA,** Maazimio hayo yanalenga kutatua changamoto zilizobainika na kwamba, kuripoti utekelezaji wake mara kwa mara kutapelekea maazimio hayo kutekelezwa kwa ufanisi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Wizara zote zinazohusika na utekelezaji wa maazimio yote ya Bunge ziwasilishwe kwa Katibu wa Bunge Taarifa za Utekelezaji wake katika kila robo ya Mwaka wa Fedha.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2022 hadi Februari, 2023. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 136 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Eng. Hamad Masauni, (Mb), pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Jumanne Sagini (Mb) kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi ambacho Kamati imefanya kazi nao.

Vilevile, namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Dkt. Stagomena Laurence Tax (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe.

Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge

kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili, Makatibu wa Kamati Ndg. Omary Magwinza, Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

…………………………
Vita R. Kawawa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

06 Februari, 2023

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa taarifa yako.

Namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, aje asome taarifa yake.

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka kuhusu Utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti katika kipindi cha Januari, 2022 hadi Januari, 2023. Aidha, taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka kuanzia mwezi Julai hadi Desemba, 2022 na mwelekeo hadi mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yetu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tisa kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ulifanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Nyongeza ya Nane, fasili ya 9, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari, 2022 hadi Januari, 2023, shughuli zilizotekelezwa na Kamati ni kama zinavyoonekana kwenye Taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati, naomba nitoe taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati wa kutekeleza majukumu yake. Masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tathmini ya utekelezaji wa mwaka wa fedha 2021/2022 inajumuisha mwenendo wa

viashiria mbalimbali vya uchumi wa jumla. Kwa muhtasari mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni mfumuko wa bei. Katika mwaka 2021/2022 Mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni deni la Serikali. Hadi Juni, 2022, deni la Serikali lilikuwa Shilingi bilioni 71,559.0, sawa na ongezeko la asilimia 11.4 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 64,272.3 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa Shilingi bilioni 47,519.2 na deni la ndani lilikuwa Shilingi bilioni 24,039.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mwenendo wa Mapato na Matumizi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilikusudia kukusanya na kutumia kiasi cha Shilingi trilioni 37.99. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani yalikuwa Shilingi trilioni 25.69, misaada ni Shilingi trilioni 1.14 inayojumuisha misaada ya kibajeti, misaada ya maendeleo pamoja na mifuko ya kisekta. Mikopo nafuu ilikuwa ni Shilingi trilioni 3.13, mikopo ya kibiashara kutoka nje ilikuwa ni Shilingi trilioni 3.05 na mikopo ya kibiashara kutoka ndani ilikuwa ni Shilingi trilioni 4.99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufika tarehe 30 Juni, 2022 Serikali ilikusanya na kutumia kiasi cha Shilingi trilioni 36.92 sawa na ufanisi wa asilimia 97.2. Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wa kusimamia upatikanaji mzuri wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hakika Mheshimiwa Rais anatekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya Awamu ya Sita ya "Kazi Iendelee". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala yaliyobainika kwenye Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022 ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022; kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Juni, 2020, Bunge lilijadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/2022 – 2025/2026 wenye dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya masuala yaliyobainika katika tathmini ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2021/2022 ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya mapendekezo ya mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024; Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi trilioni 43.29 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 4.36 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2022/2023 ya Shilingi trilioni 41.48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja mahsusi za Kamati za Bunge za Kisekta; katika Bunge la Bajeti la mwaka 2022, Kamati ilipokea jumla ya hoja mahsusi 10 zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi. Hoja hizo zilihusu nyongeza ya fedha katika mafungu mbalimbali, pamoja na mabadiliko ya sheria na sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Wenyeviti wa Kamati pamoja na Serikali. Baada ya mashauriano, Kamati iliwasilisha mapendekezo yake katika Kamati ya Uongozi, na Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika na matokeo ya mashauriano hayo yaliwasilishwa Bungeni kupitia taarifa ya Kamati. Hoja zilizofanyiwa kazi na Serikali ni kama zinavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la ziara za Kamati. Katika kipindi cha Januari, 2022 hadi Januari, 2023, kwa nyakati tofauti, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mtwara, Tanga, Manyara na Kilimanjaro pamoja na nchi ya Uturuki na Umoja wa Falme za Kiarabu. Malengo ya ziara hizo Serikali ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka (tarehe 1 Julai hadi 30 Desemba, 2022); katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 41.48. Kati ya fedha hizo jumla ya Shilingi trilioni 26.47 zilitarajiwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 15.01 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya shilingi trilioni 19.46 sawa na asilimia 46.9 ya lengo la kukusanya na kutumia shilingi trilioni 41.48. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 12.29 zilitumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 7.17 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua hii ya utekelezaji kwa sababu mwenendo huu unaonesha kwamba utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 unaweza kufikia asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya mapato ya ndani pamoja na mwenendo wa matumizi ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi kuhusu Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka 2022/2023 ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo wa *ECF* kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)* ni mkopo uliotolewa katika dirisha la *Extended Credit Facility (ECF)* ambapo Tanzania ilipata Dola za Marekani bilioni 1,046, sawa na shilingi trilioni 2.4. Mkopo huo utatolewa kwa awamu saba katika kipindi cha miezi 40 kuanzia Julai, 2022 hadi Julai, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa makubaliano, kwa mwaka wa kwanza 2022/2023, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ni Shilingi bilioni 760 ambayo itatolewa kwa awamu mbili kwa mwaka. Aidha, mkopo huu ni wa pili baada ya ule wa *Rapid Credit Facility (RCF)* maarufu kama mkopo wa UVIKO – 19. Mgao wa fedha za awamu ya kwanza za *ECF* wa jumla ya Shilingi bilioni 349.829 ulitolewa mwezi Agosti, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yaliyobainika katika uchambuzi wa Utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kupitia mkopo huu ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Kamati ya Mwaka, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bajeti kwa Mwaka 2022; Mafanikio katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti; Kamati inapenda kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza maazimio ya

Kamati kikamilifu kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Mapendekezo ya Jumla: Maafisa Ugani kutekeleza majukumu yao ya Msingi; Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kwamba Maafisa Ugani wanatoa huduma za ugani kikamilifu. Hatua hii ni pamoja na kugawa jumla ya pikipiki 2000 kwa ajili ya Maafisa Ugani. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba pikipiki hizo hazijaweza kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kutokana na kukosa mafuta na Maafisa Ugani kukosa vitendea kazi kama vile vifaa vya kupimia afya ya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, imebainika kwamba Maafisa Ugani wengi wamekuwa wakipewa majukumu mengine kama vile Watendaji wa Kata na Vijiji na hivyo kuacha majukumu yao ya msingi ya kutoa huduma ya ugani. Kamati inaishauri Serikali kwanza kuhakikisha Maafisa Ugani wanafanya majukumu yao ya msingi ya ugani na pili ni kuhakikisha kwamba wanapatiwa mafuta na vitendea kazi ili watekeleze majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kuhusu Deni la Serikali na Deni la Taifa. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mawazo tofauti kuhusu Deni la Serikali na Deni la Taifa na hivyo kuleta upotoshaji, mkanganyiko na taharuki kwenye jamii. Watu wengi bado hawana uelewa juu ya utofauti kati ya Deni la Serikali na Deni la Taifa na jinsi deni la Serikali linavyolipwa. Mfano, imefika mahali baadhi ya wanasiasa wanawatisha wananchi kwamba kila mmoja atatakiwa kulipa kiasi fulani cha fedha ili kulipa Deni la Serikali jambo ambalo siyo la kweli. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Wizara ya Elimu kuandaa mada ambayo itakuwa ni lazima kwa wanafunzi wa Sekondari, Vyuo vya Ufundi na Vyuo Vikuu kufundishwa kuhusu Deni la Serikali na Deni la Taifa. Hali hii

ikiachwa kama ilivyo hivi sasa wananchi wengi watapotoshwa na wanasiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara kwa mfumo wa Uhandisi, Usanifu, Manunuzi, Ujenzi na Utafutaji wa Fedha *(EPC+F)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi alilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba baadhi ya barabara katika mwaka huu wa fedha zitajengwa kwa kasi kwa kutumia mfumo wa *EPC+F*. Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na kubaini kwamba matumizi ya mfumo huo hayatakuwa na matokeo ya haraka kama ilivyokusudiwa kwa sababu kuu mbili. Moja mwenye mamlaka ya kukopa kwa niaba ya Serikali ni Waziri wa Fedha na Mipango kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali Sura ya 134 na pili ujenzi wa namna hii una athari ya moja kwa moja kwenye Deni la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kwamba kuliko kutumia mfumo huu ambao utachukua muda na utakuwa na gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya barabara. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi michache ya barabara na kuikamilisha kwa wakati pamoja na kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa barabara ili kuokoa fedha za matengenezo. Endapo itaonekana kukopa ni lazima basi ni vyema mikopo iwe yenye masharti nafuu ili itekeleze miradi ya barabara za kimkakati ambazo zina tija kwa Taifa kuliko kutumia mfumo huu ambao unaweza kuathiri deni la Serikali kwa namna ambayo linaweza isihimilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya misamaha ya kodi mbalimbali zinazotumiwa na Serikali ili kuchochea maendeleo. Serikali kupitia Bunge imekuwa ikifanya marekebisho mbalimbali ya Sheria za kodi ili kutoa misamaha ya kodi. Malengo ya kutoa misamaha hii ni kuleta unafuu kwa wanachi, kuchochea ukuaji wa sekta binafsi mbalimbali, kukuza sekta binafsi pamoja na kuchochea maendeleo ya viwanda na uwekezaji nchini, ikiwa ni pamoja na kusaidia miradi mikubwa ya kimaendeleo. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba baadhi ya misamaha ama inatumika vibaya au haifikii malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya malengo ya misamaha ya kikodi iliyotolewa endapo inafikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo mahususi. Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iandae mpango wa uhitaji wa rasilimali watu kwa ajili ya maendeleo ya uchumi.

Kwa kuwa, Serikali haina mpango wa Taifa unaoonesha mahitaji ya rasilimali watu kwa Taifa, ambao ungekuwa nyenzo ya mgao wa Mikopo ya Elimu ya Juu;

Na kwa kuwa, hivi sasa Serikali inatumia wastani wa Shilingi Billioni 573 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu, mpango huo utaiwezesha Serikali kuwa na kanzi data ya mahitaji ya taaluma ili kuwe na ulinganifu wa wataalam wanaohitajika kulingana na kasi ya ukuaji wa uchumi, vilevile, mpango huu utaiwezesha Serikali kuelekeza fedha zaidi kwenye taaluma zinazohitajika katika vyuo vya kati na vya juu;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango wa uhitaji wa rasilimali watu ili taaluma zinazozalishwa katika Vyuo Vikuu na vya kati ziendane na maendeleo yetu ya uchumi na ndiyo uwe nyenzo kuu ya kugawanya fedha za mkopo wa Elimu ya Juu. Hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa kujiajiri wao wenyewe ili kuondokana na wahitimu kuwa na taaluma ambazo hazina masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)

Kwa kuwa, Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa wapo wa aina mbili. Wapo wanaojiunga kwa mujibu wa sheria na wapo wanaojiunga kwa kujitolea. Changamoto kubwa iliyopo ni kukosekana kwa ajira baada ya kumaliza muda wao wa miaka mitatu hasa hawa ambao wako katika kundi la kujitolea;

Na kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara zake kama vile Wizara ya Kilimo inataka kuanzisha mchakato wa kuwapatia mitaji na mashamba vijana mbalimbali ili kujikwamua kimaisha na hatimae kuchechemua uchumi. Aidha, kampuni ya SUMA JKT huajiri wafanyakazi kila mwaka kwa kutoa tangazo hadi kwa wale ambao hawapo makambini;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia masuala yafuatayo: -

(i) Wizara ya Kilimo kuanza na vijana ambao wako katika makambi mbalimbali ya jeshi kwa kujitolea,
(ii) SUMA JKT wanapotangaza ajira za Walinzi waanze kwanza na vijana waliopo katika makambi ya Jeshi wenye sifa stahiki ambao wanakaribia kumaliza mikataba na endapo hawatoshi basi watafutwe na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itasaidia kuondoa changamoto ya ajira kwa vijana wanaoenda jeshini kwa kujitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifumo ya TEHAMA ya kukusanyia mapato kutosomana.

Kwa kuwa, bado kuna changamoto ya kutosomana kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Taasisi pamoja na Wizara kama vile *TPA* na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Kutosomana kwa mifumo kumesababisha kupotea kwa mapato ya Serikali na Ukaguzi wa Kodi (*Tax Audit)* kuwa mgumu;

Na kwa kuwa, Serikali imekuwa ikiendelea kujenga mifumo mbalimbali bila kuihuisha ili isomane na hivyo bado changamoto ya upotevu wa mapato ya Serikali inaendelea kuwepo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia masuala yafuatayo:-

(i) Serikali kufanya uchambuzi wa mifumo yote ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato ili kuihuisha pamoja na kuiunganisha ili isomane. Hatua hii itapunguza upotevu wa mapato ya Serikali; na

(ii) Serikali kutenga jumla ya Shilingi Billioni 560 kwa ajili ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ili wahuishe mifumo yao na kuiunganisha kwa ajili ya kukusanya mapato ya Serikali kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo wa asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana wa Watu Wenye Ulemavu.

Kwa kuwa, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 inaitaka kila Halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake

ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

Na kwa kuwa, suala hili ni takwa la kisheria, Kamati imebaini kuwepo na masuala yafuatayo yanayokiuka sheria;

(i) Kuna Halmashauri zimekuwa zikijumuisha deni la kutotenga asilimia 10 kwa mwaka wa fedha uliopita kwenye asilimia 10 ya mikopo ya mwaka husika ili ama zionekane zimevuka lengo au zionekane zimefikia lengo tofauti na sheria inavyotaka; na

(ii) Halmashauri zingine zimekuwa zinatoa chini ya kiwango cha asilimia 10 ya mapato ghafi. Mfano wa Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Kibaha asilimia Tatu, Halmashauri za Wilaya ya Morogoro, Chato, Bukombe, Masasi na Nkasi zilichangia asilimia Tano.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia Halmashauri zote kufuata utaratibu wa kisheria uliopo katika kutenga asilimia 10 ya mkopo kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, hatua zichukuliwe kwa zile Halmashauri ambazo hazitafikia lengo ilihali zimekusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi la Taifa - *TANAPA* kuongezewa hifadhi.

Kwa kuwa, mwaka 2019 Serikali iliongezea Shirika la Hifadhi la Taifa *(TANAPA)* hifadhi mpya Sita na hivyo kufanya idadi ya hifadhi zinazosimamiwa na *TANAPA* kuwa 22. Vilevile, *TANAPA* iliongezewa Ofisi za Kanda Nne, Vituo vitano vya Malikale na Ofisi Unganishi. Pamoja na ongezeko hilo la majukumu mapya bajeti ya uendeshaji ya Mamlaka ilibaki ile ile;

Na kwa kuwa, hatua hii imeathiri utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa sababu ya ukomo wa bajeti ambao umekuwa hauendani na ongezeko la majukumu ya Shirika. Mfano, bajeti ya uendeshaji kwa mwaka 2019/2020 ilikuwa ni Shilingi Bilioni 105, katika mwaka huo huo eneo la usimamizi liliongezeka kutoka kilometa za mraba 47,471 hadi kufikia kilomita za mraba 104,578.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, pamoja na ongezeko hilo, bajeti ya uendeshaji wa Shirika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebakia ile ile sawa na iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambacho ni kiasi cha Shilingi Bilioni 105 ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 222 na Fedha za Maendeleo kiasi cha Shilingi Bilioni 120 kwa mwaka;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia katika bajeti ya mwaka 2023/2024, *TANAPA* kuongezewa kiasi cha fedha shilingi bilioni 170. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 100 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni 70 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hatua hii itawezesha *TANAPA* kukidhi mahitaji ya msingi. Hatua hii siyo tu itawezesha TANAPA kutekeleza shughuli zake lakini vilevile tunaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Royal Tour katika kuongeza utalii na kuvutia wawekezaji nchini katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura *(Contingency Fund)*.

Kwa kuwa, Sheria ya Bajeti sura ya 439 katika vifungu vya 35, 36, 37, 38 na 39 inaelezea kuhusu umuhimu wa Serikali kuwa na Mfuko wa Dharura *(Contingency Fund)* pamoja na utaratibu wa matumizi ya fedha katika Mfuko huo;

Na kwa kuwa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Kifungu Namba 140 (1a-b) na (2)

imesisitiza juu ya uanzishwaji wa mfuko wa dharura pamoja na taratibu za uendeshaji wa mfuko huo;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ianzishe Mfuko wa Dharura na kutenga fedha kama sheria inavyoelekeza kwa ajili ya kukabiliana na dharura zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali.

Kwa kuwa, katika kipindi cha Julai hadi Juni 2022, Serikali ilikusanya jumla ya Shilingi Trilioni 36.92 kutoka vyanzo vyote sawa na asilimia 97.2 ya bajeti nzima ya Serikali;

Na kwa kuwa, Katika mwaka wa fedha 2021/2022 hamisho la fedha ndani ya mafungu *(Reallocation Within Votes)* kwa Mafungu mengi ya Serikali limezidi asilimia Saba kinyume na Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015. Aidha, kati ya Mafungu 86 yaliyofanyiwa uhamisho wa fedha, Mafungu 50 yalizidi asilimia Saba likiwemo Fungu Namba 46 ambalo uhamisho wake ni asilimia 63.33 ya bajeti iliyotengwa. Hali hii inamaanisha kwamba matumizi hayaakisi mapato yaliyopangwa - Kiambatisho B;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe uhamisho wa fedha kati ya mafungu na ndani ya mafungu unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti na kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuiwezesha Kampuni ya Taifa ya Mbolea *(Tanzania Fertilizer Company – TFC)*.

Kwa kuwa, mahitaji ya mwaka ya mbolea ni tani 698,260, mbolea ambayo inapatikana nchini kwa ajili ya matumizi ni tani 480,848 sawa na upungufu wa tani 217,412, hivyo kuna wakulima wengi wanakosa mbolea za kupandia

na kukuzia kutokana na uhaba. Aidha, uzalishaji wa ndani wa mbolea ni asilimia Sita tu ya mahitaji yote;

Na kwa kuwa, Serikali imetenga Shilingi Bilioni 160 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea kwa wakulima wote nchini. Vilevile Serikali ilianzisha Kampuni ya Mbolea Tanzania mwaka 1968 yenye madhumuni ya kuzalisha, kuhifadhi na kusambaza aina zote za mbolea. Pamoja na kuagiza, kununua, kuuza ndani na nje ya nchi bidhaa za mbolea aina zote zinazozalishwa na kampuni au watengenezaji wengine;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali iiwezeshe Kampuni ya Taifa ya Mbolea kwa mtaji wa Shilingi Bilioni 60 ili iweze kununua mbolea toka kwa wazalishaji moja kwa moja kuliko ilivyo sasa, ambapo kampuni hii inalazimika kununua mbolea kutoka kwa mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kurejesha Tume ya Taifa ya Mipango.

Kwa kuwa, Tume ya Taifa ya Mipango katika nchi yoyote ndiyo chombo kikuu cha kupanga maendeleo na kuratibu masuala yote yanayohusu mipango ya nchi na uzoefu unaonesha ili Taifa liendelee ni lazima liwe na Tume ya Mipango. Mfano, mataifa ya Asia yamefanikiwa kimaendeleo kwa kuwa na Tume za Mipango thabiti;

Na kwa kuwa, Serikali ipo katika mchakato wa kuirejesha Tume ya Taifa ya Mipango;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba pamoja na dhamira ya Serikali ya kuirejesha Tume ya Taifa ya Mipango, Serikali irejeshe Sheria ya Tume ya Mipango "*Planning Commission Act (Cap 314)*" kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 kama ilivyoondolewa kupitia Sheria hiyo ya Mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kipaumbele ya sekta ya anga.

Kwa kuwa, Serikali imewekeza katika Sekta ya anga ikiwa ni pamoja na ununuzi wa takribani ndege 11 kupitia Shirika la Ndege la Taifa ili kuvutia uwekezaji na utalii. Aidha, ili juhudi hizi zizae matunda yanayotarajiwa lazima ziende sanjari na kuwa na miundombinu wezeshi katika viwanja vyetu vya ndege. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* ambayo ndiyo yenye jukumu la kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege nchini inakabiliwa na changamoto kubwa ya kibajeti;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa miundombinu muhimu kunasababisha ndege za *ATCL* kulazimika kupaki inapofika muda wa usiku kutokana na sababu mbalimbali. Mathalani kukosekana kwa taa katika viwanja vya ndege na kukosekana kwa mifumo muhimu pamoja na minara ya kuongozea ndege. Hali hii inasababishwa na kukosekana kwa fedha za kutosha katika kugharamia miradi ya maendeleo hasa za uendelezaji wa viwanja vya ndege;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* kuongezewa bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 ya jumla ya Shilingi 45,559,857,841, kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria shilingi 20,280,465,539;
(ii) Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza Shilingi 7,224,737,722;
(iii) Usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha Shilingi 7,083,654,580;
(iv) Ujenzi wa Jengo la Kuongoza Ndege *(Control Tower)* na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba Shilingi 2,220,000,000;

(v) Ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara Shilingi 7,251,000,000; na
(vi) Ununuzi wa mtambo wa Zimamoto kwa Kiwanja cha Ndege cha Arusha Shilingi Bilioni 1,500,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio na changamoto za utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya Kamati, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia mgawanyo wa fedha za mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa wa Shilingi Trilioni 2.4 pamoja na utekelezaji wa miradi kupitia mkopo huo;
(ii) Kufanya mdahalo wa Bunge zima kuhusu masuala ya uchumi pamoja na kujadili mapendekezo ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023;
(iii) Kamati ilishauri Serikali na ikakubali kuanzisha utaratibu wa utozaji wa kodi wa kijiditali;
(iv) Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuongeza fedha za Maendeleo kwenye Fungu 45 la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Fungu 23 Mhasibu Mkuu wa Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023;
(v) Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuanzisha mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Manunuzi Sura ya 410;
(vi) Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuiongezea Wizara ya Kilimo bajeti hadi kufikia kiasi cha Shilingi Bilioni 954 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023;
(vii) Kamati iliharakisha mchakato wa kufanya marejeo ya mikataba 39 ya miradi ya umeme vijijini inayotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* baada ya kukwama kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika utekelezaji wa majukumu ya kamati. Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Kamati ilikabiliana na changamoto zifuatazo:-

(a) Changamoto ya Kanuni ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Muswada wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Kanuni ya 93(2) inaelekeza Muswada wa Sheria unapaswa kumfikia Katibu wa Bunge katika muda usiopungua siku 21 kabla ya Muswada huo kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza isipokuwa kwa Muswada uliowasilishwa kwa hati ya dharura. Uzoefu unaonesha kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha haujawahi kutekeleza matakwa hayo ya kikanuni kwa zaidi ya miaka minne. Hivyo, kusababisha Kamati kuwa na kipindi kifupi cha kuchambua, kujadili na kushauri mapendekezo ya Muswada huo kabla haujawa Sheria. Kamati inashauri kwamba, Serikali itekeleze matakwa ya Kanuni ili Kamati iweze kutekeleza shughuli yake kikamilifu.

(b) Changamoto ya muda wa uwasilishaji wa taarifa ya Kamati, taarifa kuhusu Hali ya Uchumi, Mpango na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 69(c) ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020 inaelekeza kwamba Mwenyekiti anayewasilisha maoni ya Kamati atayawasilisha kwa muda usiozidi dakika 30. Kutokana na ukubwa wa Taarifa ya Kamati kuhusu Hali ya Uchumi, Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka husika, muda wa dakika 30 hautoshi kwa Kamati kuwasilisha maoni yake kikamilifu. Kamati inapendekeza ni vyema Kanuni hii ikafanyiwa marekebisho ili kuongeza muda kutoka dakika 30 ilivyo hivi sasa hadi dakika 60 wakati wa usomaji wa taarifa hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Naomba nihitimishe kwa kumshukuru kwanza Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson,

Mbunge, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, Naibu Spika kwa miongozo yao ambayo wamekuwa wakiipatia Kamati na hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge, kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakitoa kwa Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Dkt. Natu Mwamba Katibu Mkuu, ambao walishirikiana sana na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Omari Kigua, Mbunge, Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, ninawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambao umesaidia katika kuhakikisha kwamba Kamati inasimamia Serikali ipasavyo, naomba majina yao yaingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya Uongozi thabiti wa Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* - Katibu wa Bunge, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Ndugu Maombi Kakozi, Ndugu Wilfred Akasi, Ndugu Lilian Masabala na Ndugu Trifina Tanzania pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Fadhati Kamote kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo katika Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba shughuli za Kamati zinafanyika kama zilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa hii na hatimae kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2022 HADI MWEZI JANUARI, 2023 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA, JULAI - DESEMBA 2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

**SEHEMU YA KWANZA**
**MAELEZO YA JUMLA**

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka kuhusu Utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti katika kipindi cha Januari 2022 hadi Januari 2023. Aidha, Taarifa hii inatoa Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka kuanzia mwezi Julai hadi Desemba 2022 na mwelekeo hadi Mwezi Juni, 2023.

### 1.1. *Muundo wa Taarifa*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Tisa (9) kama ifuatavyo: -

i. Sehemu ya Kwanza ni Maelezo ya Jumla kuhusu Majukumu na Shughuli Zinazotekelezwa na Kamati;
ii. Sehemu ya Pili ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2021/2022;
iii. Sehemu ya Tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha Nusu Mwaka kuanzia Mwezi Julai hadi Desemba 2022 na Mwelekeo hadi Mwezi Juni, 2023
iv. Sehemu ya Nne ni Tathmini ya Mkopo wa *Extended Credit Facility* (ECF) kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF);
v. Sehemu ya Tano ni Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ya Mwaka 2022;
vi. Sehemu ya Sita ni Maoni na Mapendekezo ya Jumla;
vii. Sehemu ya Saba ni Maoni na Mapendekezo Mahsusi;
viii. Sehemu ya Nane ni Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati; na
ix. Sehemu ya Tisa ni Hitimisho.

### 1.2. *Majukumu ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ulifanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Nyongeza ya Nane, Fasili ya 9, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 97(2) na 136 (3) (5) (8) na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 kuhusu kukutana, kushirikisha Wadau kwenye shughuli za Kamati na uzingatiaji wa Bajeti ya

Serikali iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na 2022/2023, machapisho mbalimbali ya Taasisi za Kimataifa kama vile Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB) pamoja na tafiti mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

### 1.3. *Shughuli za Kamati Zilizotekelezwa*

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari, 2022 hadi Januari, 2023 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022;
b) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2021/2022;
c) Kupitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

d) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2022/2023 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;
e) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo pamoja na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2022/2023;
f) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti za Mifuko ya Mahakama, Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; pamoja na kuidhinisha Bajeti ya Mifuko hiyo kwa Mwaka wa fedha 2022/2023;

g) Kuchambua na kushauri kuhusu Mapendekezo ya mabadiliko ya sheria mbalimbali kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2022 (The Finance Bill, 2022);
h) Kupitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Mwaka 2023/2024;
i) Kuchambua Taarifa za utekelezaji na utendaji kutoka kwenye Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo;
j) Kuchambua Taarifa ya utendaji kazi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2022/2023;
k) Kushiriki mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwaongezea uwezo wajumbe wa Kamati katika nyanja za kodi, fedha, uchumi, uwekezaji, ujenzi wa miundombinu, pamoja na mifumo mbalimbali ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato;
l) Kukutana na wadau mbalimbali ili kupokea maoni, mapendekezo na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria za kodi na zisizo za kodi zinazoathiri Sekta binafsi. Baadhi ya Wadau waliokutana na Kamati ni wafuatao: - Jumuiya ya wazalishaji viwandani (CTI), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Kampuni ya Ferrotch Africa Ltd, Tanzania Hunting Operators Association (TAHOA), Tanzania Tour Operators Association (TATOA), Tanzania Air Operators, Tanzania Sports Betting Association, Taasisi ya Wafanyabiashara wa Mafuta rejareja Tanzania (TAPSOA), Baraza la Kilimo Tanzania (ACT), Wasafirishaji (Transpoters), Broadcasting – DSTV, Tanzania Association of Oil Marketing Companies (TAOMAC) pamoja na Taasisi, Wakala, Mamlaka na Mashirika mbalimbali ya Umma, Azam Media, Tanzania Mobile Network Operators Association (TAMNOA), Research on Poverty Alleviation (REPOA), Taasisi ya Wajibu;

m) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu vyanzo vipya vya Mapato ili kupunguza utegemezi wa kibajeti;

n) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa mwaka 2022/2023 kwa ajili ya kuishauri Serikali;

o) Kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Taasisi mbalimbali pamoja na miradi ya Kimkakati. Miradi iliyotembelewa ni kama ifuatayo; Mitambo ya Kuzalisha Umeme ya Kinyerezi I na Kinyerezi II, Uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga, Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), Ujenzi wa Madarasa, barabara, mageti ya Utalii na Mitambo iliyonunuliwa kupitia fedha za Mkopo za UVIKO-19 za IMF, Kiwanda cha Saruji cha Twiga, Benjamini Mkapa Special Economic Zone, na Mitambo ya kuzalisha umeme ya Songas kwa kutumia gesi iliyopo Ubungo.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0. UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati wa kutekeleza majukumu yake. Masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

### 2.1. *Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022*

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 inajumuisha mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi wa jumla. Kwa muhtasari mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi vimetathminiwa kama ifuatavyo: -

### 2.1.1. Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2021 Pato la Taifa lilikua kwa **asilimia 4.9** ukilinganisha na ukuaji wa **asilimia 4.8** mwaka 2020. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na uwekezaji wa kimkakati hususan katika ujenzi wa miundombinu ya Nishati, Maji, Afya, Elimu, Ujenzi wa barabara, Reli na viwanja vya ndege, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu na makaa ya mawe. Vilevile, katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka 2022 ukuaji wa Pato la Taifa ulilingana na ukuaji wa kipindi kama hicho mwaka 2021 wa asilimia 5.2. Hatua hii ni ya kupongeza kwa sababu ukuaji wa uchumi haukukua kwa asilimia hasi pamoja na kwamba kasi hii ya ukuaji ni ndogo, ukilinganisha na miaka kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO - 19. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuchochea uzalishaji na uwekezaji katika Sekta za uzalishaji kama vile Utalii, Kilimo, Madini, Usafirishaji na Huduma ili kuongeza uzalishaji na kukuza Pato la Taifa na hatimaye ukuaji wa uchumi urudi tena kwenye wastani wa **asilimia 7** kwa mwaka.

### 2.1.2. Mfumuko wa Bei

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Mfumuko wa bei ulifikia wastani wa **asilimia 4.0** ikilinganishwa na **asilimia 3.3** katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021. Pamoja na kuongezeka kwa kiwango hicho bado mfumuko huu uko ndani ya lengo la muda wa kati wa **asilimia 5.0** Serikali iliyojiwekea na ndani ya lengo la wigo wa wastani wa **asilimia 8.0** uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), na Jumuiya ya Maendeleo

Kusini mwa Afrika (SADC) la kati ya **asilimia 3.0** hadi **asilimia 7.0**.

**Mheshimiwa Spika,** kuongezeka kwa kiwango cha mfumuko wa bei kilitokana na kupanda kwa bei za vyakula kutokana na mahitaji makubwa kutoka nchi za jirani ambazo zilikuwa na uhaba wa chakula. Ikumbukwe kwamba katika Kapu la bidhaa linalotumika kupima mfumuko wa bei (CPI), chakula na vinywaji visivyo na kilevi inachukua uzito wa **asilimia 28.2**, kati ya makundi 13 ya bidhaa za msingi (core inflation). Aidha, ongezeko la bei ya mafuta kwenye soko la Dunia lililosababisha ongezeko kwenye gharama za usafirishaji ambalo pia lilichochea ongezeko la bei za vyakula. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na pia kuvutia uwekezaji zaidi kwenye uzalishaji wa bidhaa za msingi za viwandani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa nchini kama vile chuma, mafuta ya kula, na sukari ya viwandani

**Jedwali Na 1: Fahirisi ya Mfumuko wa Bei wa Taifa**

| Na. | Kundi Kuu | Uzito % | Desemba ,2021 | Desemba, 2022 | Asilimia kwa mwezi 1 | Asilimia kwa miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Chakula na vinywaji visivyo na kilevi | 28.2 | 105.90 | 116.15 | 2 | 9.7 |
| 2. | Sigara na vinywaji vyenye kilevi | 1.9 | 102.85 | 103.72 | 0.1 | 0.8 |
| 3. | Nguo na | 10.8 | 105.65 | 108.39 | 0.6 | 2.6 |

| Na. | Kundi Kuu | Uzito % | Desemba ,2021 | Desemba, 2022 | Asilimia kwa mwezi 1 | Asilimia kwa miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Viatu | | | | | |
| 4. | Nyumba , Maji, Umeme, Gasi na mafuta | 15.1 | 105.14 | 107.93 | 0.3 | 2.7 |
| 5. | Samani, vyombo vya nyumbani na matenge nezo | 7.9 | 104.36 | 108.18 | 0.2 | 3.7 |
| 6. | Afya | 2.5 | 103.39 | 105.11 | 0.2 | 1.7 |
| 7. | Usafiri | 14.1 | 105.33 | 110.70 | 0.2 | 5.1 |
| 8. | Mawasiliano | 5.4 | 102.42 | 103.72 | 0.2 | 1.3 |
| 9. | Utamaduni, Sanaa na Michezo | 1.6 | 102.65 | 104.73 | 0.1 | 2.0 |
| 10. | Elimu | 2.0 | 101.16 | 101.90 | 0.0 | 0.7 |
| 11. | Huduma ya Hoteli na Migahawa | 6.6 | 105.71 | 108.60 | 0.2 | 2.7 |
| 12. | Huduma za Kifedha na Bima | 2.1 | 100.36 | 100.22 | 0.1 | -0.1 |
| 13. | Ulinzi | 2.1 | 103.38 | 106.01 | 0.3 | 2.5 |
| **JUMLA** | | **100** | **104.92** | **110.01** | **0.8** | **4.8** |
| **MAKUNDI MENGINE** | | | | | | |
| 1. | Fahirisi ya Msingi | 73.9 | 105.25 | 1107.87 | 0.2 | 2.5 |
| 2. | Fahirisi ya bidhaa zisizo za msingi | 26.1 | 104.00 | 116.08 | 2.3 | 11.6 |

| Na. | Kundi Kuu | Uzito % | Desemba ,2021 | Desemba, 2022 | Asilimia kwa mwezi 1 | Asilimia kwa miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Mafuta | 5.7 | 104.96 | 113.20 | 1.1 | 7.9 |
| 4. | Fahirisi ya Huduma | 37.2 | 104.03 | 106.61 | 0.1 | 2.5 |
| 5. | Fahirisi ya Bidhaa | 62.8 | 105.46 | 112.02 | 1.2 | 6.2 |
| 6. | Huduma za Elimu na Bidhaa visaidizi vya Elimu | 4.1 | 103.36 | 104.92 | 0.0 | 0.5 |
| 7. | Chakula kutoa vinywaji | 71.82 | 104.54 | 107.60 | 0.3 | 2.9 |

***Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu***

### 2.1.3. Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

**Mheshimiwa Spika,** thamani ya shilingi ya Tanzania katika mwaka 2021/2022 ilipungua dhidi ya dola ya Marekani kwa kiwango cha wastani wa **asilimia 0.16** na kufikia wastani wa **Shilingi 2,313.96** kwa dola moja ya Marekani kutoka **Shilingi 2,310.18** kwa mwaka 2020/2021. Utulivu huu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ulitokana na utekelezaji mzuri wa Sera za fedha na bajeti, mfumuko mdogo wa bei na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Ili kuimarisha thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, Serikali lazima iwekeze kwenye Sekta zinazoweza kuongeza mauzo ya nje ili kupata fedha za kigeni. Kamati inaishauri Serikali kuongeza

uwekezaji katika Sekta za Kilimo, Utalii, Mifugo pamoja na Madini ili kufikia dhamira hiyo.

### 2.1.4. Akiba ya Fedha za Kigeni

**Mheshimiwa Spika,** Akiba ya fedha za kigeni ilifikia **Dola za Marekani milioni 5,110.3** Juni, 2022 kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.6. Akiba hii imeshuka ukilinganisha na **Dola za Marekani milioni 5,209.8** katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021. Kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni kunaathiri mfumuko wa bei nchini. Aidha, njia pekee na ya uhakika ya kuimarisha akiba yetu ya fedha za kigeni ni kuongeza mauzo nje ya nchi. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka akiba ya fedha za kigeni kwa kutumia dhahabu ambayo thamani yake haibadiliki sana kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi. Vilevile, Serikali iendelee kuimarisha uhusiano na Wabia wa Maendeleo pamoja na Mashirika ya Kimataifa ya Fedha kwa sababu fedha za mikopo na misaada zinasaidia kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.

### 2.1.5. Deni la Serikali

**Mheshimiwa Spika,** hadi Juni, 2022, Deni la Serikali lilikuwa **Shilingi bilioni 71,559.0**, sawa na ongezeko la **asilimia 11.4** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 64,272.3** kipindi kama hicho mwaka 2021. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa **Shilingi bilioni 47,519.2** na deni la ndani lilikuwa **Shilingi bilioni 24,039.8**. Ongezeko hilo la deni lilitokana na kupokelewa kwa mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo Ujenzi wa miundombinu ya barabara, Reli, Viwanja vya ndege, Umeme, Elimu na Afya pamoja na kutolewa kwa hatifungani

maalumu yenye thamani ya **Shilingi trilioni 2.18** kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi (PSSSF) linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuweka ukomo kwenye kiashiria cha uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani. Hivi sasa ulipaji wa deni kwa kutumia mapato ya ndani ikijumuisha mikopo ya ndani ya kudumisha deni (Roll Over) ni **asilimia 30.36**. Vilevile, Serikali iendelee kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake pamoja na miradi ya maendeleo.

**2.1.6. Mwenendo wa Mapato na Matumizi**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali ilikusudia kukusanya na kutumia kiasi cha **Shilingi trilioni 37.99**. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani yalikuwa **Shilingi trilioni 25.69**, misaada ni **Shilingi trilioni 1.14** inayojumuisha misaada ya kibajeti, misaada ya maendeleo pamoja na mifuko ya kisekta. Mikopo nafuu ilikuwa ni **Shilingi trilioni 3.13**, mikopo ya kibiashara kutoka nje ilikuwa ni **Shilingi trilioni 3.05** na mikopo ya kibiashara kutoka ndani ilikuwa ni **Shilingi trilioni 4.99**.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufika tarehe 30 Juni 2022 Serikali ilikusanya na kutumia kiasi cha **Shilingi trilioni 36.92** sawa na **asilimia 97.2** ya lengo iliyojiwekea. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 22.73** ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi trilioni 15.26** ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu

Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wa kusimamia upatikanaji mzuri wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hakika Mheshimiwa Rais anatekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya Awamu ya sita ya "Kazi Iendelee".

**Jedwali Na. 2. Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 Shilingi Bilioni**

| MAPATO/MATUMIZI | BAJETI | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Mapato ya Ndani** | **25,691.7** | **24,395.6** | **95.0** |
| Mapato ya Kodi (TRA) | 20,283.4 | 20,029.3 | 98.7 |
| Mapato Yasiyo ya Kodi (TRA) | 1,494.7 | 902.0 | 60.3 |
| Mapato Yasiyo ya Kodi | 3,049.8 | 2,574.8 | 84.4 |
| Mapato ya Halmashauri | 863.9 | 889.5 | 103.0 |
| **Misaada** | **1,138.1** | **708.5** | **62.3** |
| Misaada ya Kibajeti | **-** | **103.2** | |
| Misaada ya Maendeleo | 915.5 | 519.3 | 56.7 |
| Mifuko ya Kisekta | 222.6 | 86.0 | 38.6 |
| **Mikopo Nafuu** | **3,128.5** | **4,116.8** | **131.6** |
| Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 1,310.7 | 1,291.7 | 98.6 |
| Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo | 1,770.0 | 2,818.3 | 159.2 |
| Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | 47.8 | 6.8 | 14.2 |
| **Mikopo ya Kibiashara Kutoka Nje** | **3,045.1** | **1,809.5** | **59.4** |
| **Mikopo ya Kibiashara Kutoka Ndani** | **4,989.1** | **5,894.4** | **118.1** |
| Mikopo ya Kugharamia Miradi | 1,838.8 | 2,850.0 | 155.0 |
| Mikopo ya Kulipa Mtaji Deni la Ndani | 3,150.3 | 3,044.4 | 96.6 |
| **JUMLA YA MAPATO** | **37,992.5** | **36,924.8** | **97.2** |
| | | | |

| MAPATO/MATUMIZI | BAJETI | HALISI | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida** | **22,732.8** | **22,561.5** | **99.2** |
| Mishahara | 8,136.5 | 8,087.4 | 99.4 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali (Deni) | 8,756.8 | 8,756.8 | 100.0 |
| Matumizi Mengineyo & CFS | 5,839.5 | 5,717.3 | 97.9 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **15,259.7** | **14,654.3** | **96.0** |
| Miradi ya Fedha za Ndani | 11,591.1 | 11554.6 | 99.7 |
| Miradi ya Fedha za Nje | 3,668.6 | 3,099.7 | 84.5 |
| **JUMLA YA MATUMIZI** | **37,992.5** | **37,215.8** | **98.0** |

***Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango***

### 2.1.7. Masuala Yaliyobainika kwenye Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/22, Kamati ilibaini kasoro zifuatazo: -

#### i. Ukusanyaji wa mapato

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani kwa **asilimia 95** ya lengo la kukusanya **Shilingi trilioni 25.69**, hali hiyo ilichangiwa zaidi na ufanisi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kuongeza mapato ya kodi hadi **asilimia 98.7**. Hata hivyo, Kamati inaamini kwamba Mamlaka ina uwezo mkubwa zaidi katika kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya mapato ya ndani kumesababishwa na:-

a) Baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu kutokutumia mashine za kielektroniki za kutolea stakabadhi (Electronic Fiscal Device Receipt-EFD) wakati wanapofanya mauzo;

b) Baadhi ya Halmashauri kutowasilisha benki fedha zilizokusanywa kupitia mashine za POS *(Point of Sales);*
c) Baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kukwepa ulipaji kodi pamoja na kuwepo kwenye kanzi data ya walipa kodi. Mfano walipa kodi waliosajiliwa ni **milioni 4** lakini wanaolipa kodi ni **milioni 2** tu na hivyo kuikosesha Serikali mapato yake stahiki;
d) Mamlaka ya mapato kushindwa kukusanya malimbikizo ya madeni ya kodi za nyuma kutoka kwa walipa kodi. Mfano kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2021 ilibaini kwamba kuna ongezeko la madeni yasiyokusanywa kwa **asilimia 94.6** kutoka **Shilingi trilioni 3.86** hadi **Shilingi trilioni 7.54** mwaka 2019/2020 na 2020/2021 mtawalia.
e) Baadhi ya wafanyabiashara bado hawajajiunga na mfumo wa Marejesho ya Kodi kwa Njia ya Kieletroniki *(Electronic Filing- E-Filling)*
f) Serikali pia imekuwa inapoteza mapato kwenye mafuta ambayo yanakuwa hayajabainishwa matumizi yake kama ni kwa ajili ya kusafirishwa nje au kwa ajili ya matumizi ya ndani;
g) Baadhi ya makampuni ya Serikali kutowasilisha kodi zao za Makampuni kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini endapo Serikali itazifanyia kazi changamoto hizi tutaweza kujiendesha na hata kupunguza utegemezi wa fedha za washirika wa maendeleo. Hivyo, kuna haja ya Serikali kuimarisha mifumo ya udhibiti na usimamizi wa mapato yake ili kuwezesha Serikali kupata mapato stahiki. Aidha, Serikali iimarishe vitengo vyote vya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuziba mianya ya upotevu wa mapato.

**ii. Ukusanyaji wa Mapato yaliyoko chini ya Msajili wa Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/22 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusanya jumla ya **Shilingi bilioni 850.28** kati ya makadirio ya kukusanya **Shilingi bilioni 777.01** sawa na ufanisi wa **asilimia 109.** Ufanisi huu ulichangiwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na utendaji mzuri wa Taasisi zinazochangia **asilimia 15** ya mapato ghafi kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na ufuatiliaji makini wa Ofisi ya Msajili wa hazina .

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ufanisi huu kunachangamoto ya kisheria ambapo Sheria haijaweka hatua za kisheria zinazotakiwa kuchukuliwa dhidi ya Taasisi na Mashirika ambayo huchelewesha uwasilishajiwa gawio na mapato mengine yanayokusanywa na Ofisi ya Msajili kwa wakati. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuleta marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu) Sura 370 ili kuweka kifungu mahsusi kinachotoa adhabu kwa kutozingatia matakwa ya Sheria katika uwasilishaji wa michango, gawio na ziada ili kuleta uwajibikaji.

**Jedwali Na. 3. Makusanyo kwa Mwaka 2021/2022**

| Na. | Mapato yasiyo ya kodi | Bajeti ya Mwaka | Makusanyo | Ufanisi (%) |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Gawio | 372,882,603,001 | 357,528,737,004.51 | **96** |
| **2.** | Michango ya Asilimia 15 | 298,775,479,691 | 324,025,703,627.12 | **108** |
| **3.** | Mawasiliano ya TTMS | 10,984,639,397 | 9,481,254,946.67 | **86** |
| **4.** | Marejesho ya Mikopo na Riba | 1,570,074,540 | 54,227,849,370 | **3454** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **5.** | Mawasilisho Mengineyo | 93,782,962,532 | 105,017,840,361.84 | **112** |
| **JUMLA** | | **777,995,759,161** | **850,281,385,310.14** | **109** |

***Chanzo: Ofisi ys Msajili wa Hazina***

### iii. Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji miradi ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 jumla ya **Shilingi trilioni 14.65** zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 96** ya lengo la **Shilingi trilioni 15.26.** Utolewaji huu wa fedha kwa kiasi kikubwa umeenda kwenye miradi mikubwa ya kimkakati. Miradi midogo haikamiliki kwa wakati kutokana na suala la ongezeko la gharama linalotokana na mabadiliko ya gharama (variations) katika utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza miradi michache na kuikamilisha kwa wakati kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haikamiliki kwa wakati. Jambo hili linaongeza gharama kubwa kwa Serikali. Ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi hii, Serikali inaweza kugawanya miradi katika ngazi ya Wilaya hadi Mikoa na hasa ile ambayo inaweza kukamilika kwa mwaka mmoja wa fedha. Mfano miradi ya ujenzi wa Zahanati, vituo vya afya, miradi midogo ya maji na miradi ya barabara vijijini. Hali hii itasaidia kuondoa ongezeko la gharama ya miradi kwa Serikali.

### iv. Mikopo ya kibiashara kutoka nje

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 Serikali iliweza kukopa katika soko la nje kiasi cha **Shilingi trilioni 1.81** sawa na ufanisi wa

**asilimia 59.4** ya lengo la **Shilingi trilioni 3.05.** Kutofikiwa kwa lengo kumesababishwa na kutokupatikana kwa mikopo hiyo kwa wakati na masharti magumu yanayoambatana na mikopo hiyo. Kamati imebaini kwamba Serikali ilifidia kukosekana kwa mikopo ya nje kwa kutumia mikopo ya kibiashara katika soko la ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ambayo ilizidi kiwango tarajiwa kwa zaidi ya **asilimia 55**. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilipanga kukopa kutoka vyanzo vya ndani **Shilingi trilioni 1.84** lakini ilikopa **Shilingi trilioni 2.85.** Hatua hii ina madhara kwa uchumi wetu kwa sababu inazinyima fursa sekta binafsi kupata mikopo. Ni wazi kwamba, Taasisi za fedha zinakuwa na utayari zaidi wa kuikopesha Serikali kuliko sekta binafsi. Hivyo, Kamati inaishuri Serikali kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework – DCF) kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za wahisani na mikopo yenye masharti nafuu ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Utekelezaji wa mwongozo huu utasaidia upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo nafuu ili kupunguza mikopo ya kibiashara yenye masharti magumu na riba za juu.

### 2.2. *Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo Juni, 2020. Bunge lilijadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/2022 – 2025/2026 wenye Dhima ya Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango ulikuwa na maeneo makuu matano ya vipaumbele ambavyo ni: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.

### 2.2.1. Baadhi ya masuala yaliyobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2021/2022

#### 2.2.1.1. kuwepo kwa Miradi ya muda mrefu ambayo hatikelezwi kama ilivyopendekezwa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kwamba Serikali imekuwa na miradi mingi ya kimkakati ambayo utekelekezaji wake unasuasua. Miradi iliyochambuliwa ni Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas - LNG) – Lindi; Mradi wa Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Mradi wa Chuma – Liganga; Mradi wa Bandari ya Bagamoyo, Mradi wa Engaruka Magadi soda, Mradi wa Mabwawa Makubwa ya umwagiliaji Farkwa na Kidunda, Mradi wa Reli ya Mbamba Bay – Mchuchuma - Liganga hadi Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokutekeleza miradi hii hivi sasa kunaweza kuwa na athari kuu mbili. Moja ni gharama ya kutekeleza miradi hii siku zijazo inaweza kuwa kubwa kuliko hivi sasa na Pili ni rasilimali tulizonazo hivi sasa mfano LNG zinaweza zisiwe na matumizi kutokana na mabadiliko ya teknolojia na maendeleo ya kiuchumi. Kamati iliishauri Serikali ianze kuitekeleza miradi hii haraka iwezekanavyo kwa sababu miradi hii haitegemei Bajeti ya Serikali na ina manufaa makubwa kwa

Taifa. Ili kuepuka athari za baadaye za uchambuzi wa mikataba ufanywe kwa umakini.

**2.2.1.2. Miradi ya Barabara ya miaka mingi kutokutekelezwa kikamilifu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa barabara 38 zenye jumla ya Kilomita 8,575.29 zilizopo kwenye hatua mbalimbali na kubaini mambo yafuatayo: Kwanza, kuna barabara ambazo zina miaka zaidi ya 10 katika hatua ya upembuzi yakinifu na uchambuzi wa kina na hazijaanza kujengwa. Pili, kuna baadhi ya barabara zimejengwa kilomita chache na ujenzi haujaendelea kwa kipindi cha muda mrefu. Aidha, Barabara mpya zinaendelea kuibuliwa ilihali barabara za zamani hazijakamilika. Hatua hii inasababisha ongezeko la gharama ya riba kwa Serikali inayotokana na kutolipa wakandarasi kwa wakati kwa sharti la uhakiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kukamilisha ujenzi wa barabara zilizoainishwa kwenye Mpango na kuharakisha malipo ya wakandarasi pindi hati za malipo (certificates) zinapowasilishwa. Aidha, endapo itabidi Serikali ifanye uhakiki usizidi siku 20 za kazi. Hatua hizi zitasaidia kupunguza hasara inayotokana na riba.

**2.2.1.3. Ushirikishwaji hafifu wa Sekta Binafsi katika kutekeleza Mpango**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Sekta binafsi ni injini ya kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, ushirikishwaji wake katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo si wa

kuridhisha. Sekta binafsi nchini bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i. Uwepo wa Mamlaka nyingi za udhibiti zinazosimamia shughuli za sekta binafsi;
ii. Uwepo wa riba za juu na ugumu katika upatikanaji wa mikopo pamoja na ucheleweshaji wa utoaji wa maamuzi;
iii. Uwepo wa leseni, tozo na ada nyingi kwenye biashara moja; na
iv. Urasimu katika kupata vibali vya kazi na ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kwamba bado Serikali haijatekeleza ipasavyo Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini (Blueprint) ambayo inaaminika ni mwarobaini wa kutatua changamoto hizi. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini ili kutatua changamoto za wafanyabiashara nchini.

### 2.2.1.4. Utekelezaji wa Vipaumbele

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kwamba Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022 vilikuwa vingi kuliko uwezo wa kifedha wa Serikali. Aidha, kumekuwa na kurudiwa rudiwa kwa baadhi ya vipaumbele ambavyo havitekelezwi mfano, mradi wa Liganga na Mchuchuma na Kiwanda cha kuchakata Gesi Asilia. Kamati inaishauri Serikali kuweka vipaumbele vichache inavyoweza kuvitekeleza kwa ufanisi kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha za maendeleo kila mwaka.

**2.3.** ***Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (The Finance Bill, 2022)***

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 127 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kamati iliwasilisha Bungeni Taarifa ya maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (The Finance Bill, 2022).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia kifungu kwa kifungu pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na baadaye ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kupendekeza marekebisho katika Muswada. Sheria zilizowasilishwa na kufanyiwa kazi katika Muswada huo zilikuwa ni thelathini na nane (38), Kamati ilizichambua na baada ya mashauriano, Serikali ilikubali kuondoa sheria tatu kutokana na sababu mbalimbali. Sheria zilizoondolewa ni sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) Sura ya 172, Sheria ya Halmashauri (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na Sheria ya Utalii Sura ya 65. Hivyo, Kamati ilichambua na kupitisha sheria zifuatavyo: -

i. Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura ya 156;
ii. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;
iii. Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213;
iv. Sheria ya Korosho, Sura ya 203;
v. Sheria ya Makampuni, Sura 212 (The Companies Act, (Cap.212)
vi. Sheria ya Hakimiliki, Sura ya 218;
vii. Sheria ya Tasinia ya Maziwa, Sura ya 262;
viii. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
ix. Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta, Sura 306
x. Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414;

xi. Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa nje ya Nchi, Sura ya 196;
xii. Sheria ya Mbolea, Sura ya 378;
xiii. Sheria ya Magari ya Kigeni, Sura ya 84;
xiv. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
xv. Sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada, Sura ya 134;
xvi. Sheria ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi, Sura ya 120;
xvii. Sheria ya kodi ya Mapato, Sura ya 332;
xviii. Sheria ya Bima, Sura ya 394;
xix. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;
xx. Sheria ya Udhibiti wa Usafirishaji wa Nchi Kavu, Sura ya 413;
xxi. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya), Sura ya 290;
xxii. Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
xxiii. Sheria ya Madini, Sura ya 123;
xxiv. Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura ya 437;
xxv. Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura ya 297;
xxvi. Sheria ya Bandari, Sura ya 166;
xxvii. Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38;
xxviii. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
xxix. Sheria ya Uwakala wa Meli, Sura 415;
xxx. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
xxxi. Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408;
xxxii. Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318;
xxxiii. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
xxxiv. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na
xxxv. Sheria ya Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Sheria hizi umefafanuliwa kwa kina kwenye uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji

wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 kwa kipindi cha nusu mwaka.

## 2.4. *Tathmini ya Mapendekezo ya Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2023/2024*

**Mheshimiwa Spika,** mwezi Novemba, 2022 Serikali iliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/2024 kama Sheria ya Bajeti inavyoelekeza. Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadiliana na Serikali kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo na Mpango huo. Kimsingi, Mwongozo huo umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 43.29** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 4.36** ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2022/2023 ya **Shilingi trilioni 41.48**. Mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa **Shilingi trilioni 31.03** sawa na **asilimia 71.7** ya bajeti yote, Kati ya fedha hizo mapato ya kodi ni **Shilingi trilioni 26.37,** mapato yasiyo ya kodi **Shilingi trilioni 3.51** na mapato ya Halmashauri **Shilingi trilioni 1.14**. Aidha, kiasi cha **Shilingi trilioni 4.51** zinatarajiwa kutoka kwenye misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuziba nakisi ya bajeti. Kamati iliishauri Serikali kuhusu masuala yafuatayo: -

### 2.4.1. Kutotabirika kwa Sera za Kodi

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya mara kwa mara ya sheria za kodi ni moja ya changamoto kubwa inayowakabili wawekezaji na wafanyabiashara nchini na hivyo kusababisha kutotabirika kwa sera za fedha na kodi. Hali hii, husababisha wawekezaji kutokufanya uwekezaji wa muda

mrefu na wenye tija. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kalenda ya mabadiliko ya kodi ambayo itaweka muda maalum wa kufanya mabadiliko ya sheria na viwango mbalimbali vya fedha na kodi badala ya utaratibu wa sasa ambao mabadiliko ya kodi hufanyika takribani kila mwaka.

### 2.4.2. Uratibu wa Shughuli za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini uwepo wa changamoto katika uratibu wa shughuli za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfano, katika uunganishaji wa umeme vijijini, Wakala wa umeme vijijini (REA) haunganishi miundombinu ya umeme katika Taasisi zote za Umma zilizoko katika eneo husika; Wizara ya kilimo kutafuta vijana kwa ajili ya kuendeleza mashamba makubwa na wakati huohuo kuna vijana waliojitolea JKT hawana shughuli za kuwaingizia kipato; Aidha, Kamati ilibaini kwamba Taasisi moja ya umma kukwamisha Taasisi nyingine ya umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo mfano, Wakala wa Misitu (TFS) kuzuia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kupitisha miundombinu ya umeme mpaka walipie njia. Pamoja na uwepo wa *Dash Board* ya uratibu wa Shughuli za Serikali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu bado tatizo hili limeendelea kuwepo kwa sababu baadhi ya Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali zinafanya kazi kwenye mfumo wa vihenge (silos). Kamati inaishauri Serikali katika miradi yake yote kuanzisha utaratibu wa kushirikisha Wizara, Idara na Taasisi zote zinazoguswa na mradi unaotekelezwa na Wizara, Idara na Taasisi husika.

### 2.4.3. Barabara zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kujenga barabara inayounganisha mipaka ya Tanzania na nchi ya Kenya kupitia Wilaya za Mkinga – Lushoto mkoa wa Tanga hadi Same - Holili katika mkoa wa Kilimanjaro. Hatua hii itasaidia uwepo wa njia

rasmi ya kufikia mipaka hiyo na hivyo kuondoa changamoto ya biashara ya magendo na kuongeza mapato ya Serikali.

## 2.5. *Hoja Mahsusi za Kamati za Bunge za Kisekta*

**Mheshimiwa Spika,** katika Bunge la Bajeti la mwaka 2022, Kamati ilipokea jumla ya hoja mahsusi 10 zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara na Taasisi. Hoja hizo zilihusu nyongeza ya fedha katika mafungu mbalimbali, pamoja na mabadiliko ya sheria na sera. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilikutana na Wenyeviti wa Kamati pamoja na Serikali. Baada ya mashauriano Kamati iliwasilisha mapendekezo yake katika Kamati ya Uongozi, na Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika na matokeo ya mashauriano hayo yaliwasilishwa Bungeni kupitia Taarifa ya Kamati.

### 2.5.1. Hoja zilizofanyiwa Kazi na Serikali

#### 2.5.1.1. Fungu 45: Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea hoja kuhusu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuongezewa Bajeti ya **Shilingi bilioni 10.8** ili kukidhi mahitaji ya kaguzi. Kutokana na ukomo wa Bajeti Serikali ilikubali kuliongezea Fungu hilo **Shilingi bilioni 5** pungufu kwa **Shilingi bilioni 5.8** ukilinganisha na maombi. Fedha hizo zilihitajika kwaajili ya kujenga mifumo ya ukaguzi na kununua magari kwa ajili ya ukaguzi wa ufanisi. Baada ya majadiliano Kamati ilipendekeza fungu hili liongezewe jumla ya **Shilingi bilioni 3.9** kwa ajili ya matumizi yafuatayo: -

i. Kiasi cha **Shilingi bilioni 2.5** kwa ajili ya kujenga na kuimarisha mifumo ya ukaguzi na usimamizi; na
ii. **Shilingi bilioni 1.4** kwa ajili ya kununua magari ya shughuli za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imetekeleza ahadi yake ya kuiongezea Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali bajeti ya jumla ya **Shilingi bilioni 3.9** kupitia utaratbu wa uhamisho kati ya mafungu mwezi Januari 2023.

**2.5.1.2. Kupunguza Ushuru wa Forodha kwa Mafuta ghafi ya Michikichi kutoka Nje**

**Mheshimiwa Spika,** kulikuwa na changamoto ya kuongezeka kwa bei ya Mafuta ya Kula yanayotokana na zao la Michikichi "*Palm Oil*". Ili kuleta unafuu wa bei katika mafuta hayo, Kamati iliishauri Serikali kufanya mabadiliko katika Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Mwaka 2004 (East African Community Customs Management Act, 2004). Lengo ni kupunguza kiwango cha ushuru wa forodha katika uingizaji wa mafuta ghafi ya mchikichi "*Crude palm Oil*" na ambayo yamechujwa kwa kiwango cha kati "*Semi rifined*" na yaliyochujwa "*refined*" ili mafuta ya kula yapatikane kwa bei nafuu. Kamati ilishauri masuala yafuatayo:-

i. Kuangalia uwezekano wa kutoza kwa kiwango cha asilimia sifuri Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mafuta yaliyochujwa walau mara mbili "*Double refined*" yanayotokana na mbegu za pamba, mchikichi na alizeti yanayozalishwa ndani ili yaweze kushindana katika soko; na

ii. Kuweka mikakati ya muda mrefu ya kuhakikisha kwamba mafuta ya kula yanazalishwa ndani kwa wingi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 na kusamehe VAT kwa kipindi cha mwaka mmoja, kwenye mafuta yaliyochujwa walau mara mbili "Double Refined" na yanayotokana na mbegu zilizozalishwa hapa nchini kama vile pamba, alizeti na michikichi. Hatua hii, imesababisha bei ya mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi (double refined) imepungua kwa wastani wa shilingi 23,000 kwa lita tano kutoka shilingi 35,000 hadi 37,000 iliyokuwa inatozwa hapo awali na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**2.5.1.3. Usuluhishi wa Kesi na migogoro ya Kodi**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi tarehe 31 Disemba, 2021 kesi zenye thamani ya **Shilingi trilioni 5.18** zilikuwa kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB), Mahakama ya Rufaa ya Mapato ya Kodi (TRAT) na Mahakama ya Rufaa (CA). Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 (The Tax Adimistration Act Cap 438) kifungu cha 51(5), Mlipa kodi yeyote kabla ya rufaa yoyote ya kodi kusikilizwa lazima alipe moja ya tatu ya kodi yote aliyofanyiwa makadirio au alipe kodi yote isiyobishaniwa. Hivyo, kuendelea kuwa na kiwango kikubwa cha kesi katika Bodi na Mahakama za Rufani ambapo suala hili huwa na pande mbili. Moja ni Serikali kuchelewa kukusanya mapato yake kwa kesi ambazo itashinda na pili ni kuendelea kushikilia fedha za wafanyabiashara ambao kimsingi hawana hatia. Kamati inapendekeza kwamba, Serikali kuanzisha Mkakati

maalum wa kumaliza mashtaka katika Bodi na Mahakama za Rufaa za Kodi ili Serikali ipate mapato yake stahiki na wafanyabiashara warejeshewe fedha zao endapo wanastahii.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Desemba 2022, TRAB imesikiliza mashauri 317 na kiasi kinachobishaniwa ni **Shilingi bilioni 675.73**. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya mashauri 625 ya kiasi kinachobishaniwa cha **Shilingi trilioni 3.74** na **Dola za Marekani milioni 3.48** hayakusikilizwa. Vilevile, TRAB imepanga kuendelea kusikiliza mashauri kwa mpango maalum "special sessions" ambapo Mwezi Februari na Machi 2023 itasikiliza mashauri mbalimbali katika mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Morogoro, Pwani na Mtwara na Aprili hadi Juni 2023 itasikiliza mashauri katika mikoa ya Dar es Salaam, Musoma, Manyara, Iringa, Katavi, Songwe, Mbeya na Njombe.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Desemba 2022, TRAT ilikuwa na mashauri 171 ambayo hayajasikilizwa kutokana na muda wa uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Wenyeviti watatu (3) kufikia ukomo. Kiasi kinachobishaniwa katika mashauri hayo ni **Shilingi bilioni 480.44** na **Dola za Marekani milioni 2.93.** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuharakisha usuluhishi wa migogoro ya kodi ili Serikali ipate kodi yake na wafanyabiashara warejeshewe fedha zao ambazo zinashikiliwa na Serikali.

**2.5.1.4. Kuboresha kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit Unit)**

**Mheshimiwa Spika,** Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ni muhimu kwa sababu ukaguzi wake hufanyika mara kwa mara "*real* time *audit*" hata hivyo

kitengo hiki kimekuwa hakina nguvu kwa sababu ya muundo wake na utendaji kazi wake. Baadhi ya Changamoto zinazokikabili kitengo hiki ni pamoja na:-

i. Kitengo kinawasilisha Taarifa yake kwenye Kamati ya ukaguzi ambayo ina wajumbe 5, watatu kutoka Taasisi husika na wawili kutoka nje ambao wote wanateuliwa na Afisa Masuuli wa fungu husika. Taratibu za kimataifa zinahitaji walau wajumbe watatu watoke nje ya fungu au Taasisi husika; na
ii. Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kipo chini ya Afisa Masuuli na kinapata Bajeti chini ya fungu husika hivyo inaondoa uhuru wa ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipendekeza kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili kuleta tija kwenye Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Maeneo yanayopendekezwa kufanyiwa mabadiliko ni kama ifuatavyo:-

i. Kuwafanya wakaguzi wa ndani wawajibike kwa Mkaguzi Mkuu wa ndani;
ii. Kamati ya Ukaguzi kubadilisha idadi ya wajumbe watatu watoke nje na wawili watoke ndani;
iii. Sheria hiyo itoe mwanya kwa Mkaguzi wa Ndani endapo itatokea hajakubaliana na majibu ya Menejimenti aruhusiwe kuwasilisha Taarifa yake kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani moja kwa moja kwa hatua zaidi; na
iv. Inashauriwa kwamba Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani iwe na fungu lake ili iwe na uhuru wa kukagua na kutoa maoni.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Sheria ya Fedha zimefanyiwa marekebisho mwaka 2022/2023 na

kuchapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 478K. Kanuni hizo zimeanza kutumika rasmi Julai 01, 2022 ambapo wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi watatu watatoka nje ya Taasisi ikiwemo Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, Kanuzi hizo zinaelekeza Wakuu wa Vitengo vya Ukaguzi kuwasilisha moja kwa moja taarifa zao kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali iwapo Maafisa Masuuli hawatatoa majibu ama Kamati za Ukaguzi hazijakaa kujadili Taarifa katika muda uliopangwa kisheria. Vilevile, Serikali imetekeleza mapendekezo ya Kamati kwa kuanzisha Fungu 006 ambalo litakuwa ni mahsusi kwa ajili ya Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali.

**2.5.1.5. Ujenzi wa Ofisi za Wabunge**

**Mheshimiwa Spika,** Utaratibu unaotumika hivi sasa wa kuwapatia Ofisi Wabunge majimboni bado una changamoto zifuatazo kwa Waheshimiwa wabunge :-

i. Baadhi ya maeneo ya Halmashauri hayana vyumba vya kuwapa Wabunge ili wavitumie kama Ofisi zao;
ii. Baadhi ya Ofisi wanazopatiwa Wabunge haziendani na hadhi zao; na
iii. Maeneo wanayopewa Ofisi ama ni mbali na wananchi au hayafikiki kwa urahisi.
iv.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI imefanya tathmini ya wapi hasa panafaa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge na ni mamlaka ipi inatakiwa kusimamia ujenzi wa Ofisi hizo na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo. **Asilimia 71** ya waliohojiwa, walipendekeza kuwa Ofisi hizo zijengwe katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya; **asilimia 21** walipendekeza Ofisi za Wabunge zijengwe kwenye Ofisi za

Wakurugenzi wa Halmashauri; **asilimia 5** walipendekeza Ofisi hizo ziwe zinajitegemea; na **asilimia 3** walipendekeza Ofisi hizo zijengwe katika Majimbo husika. Matokeo hayo yalitokana na sababu zifuatazo, upatikanaji wa huduma kwa urahisi, kupunguza gharama pamoja na ukaribu kwa ajili ya kutatua changamoto kwa kushirikiana na Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya. Aidha, kuhusu usimamizi wa ujenzi wa ofisi za wabunge, **asilimia 28** ya wahojiwa walipendekeza ujenzi usimamiwe na Ofisi ya Waziri Mkuu, **asilimia 23** wamependekeza ujenzi usimamiwe na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, **asilimia 7** imependekeza ujenzi usimamiwe na Bunge na **asilimia 42** hawakutoa maoni katika eneo hili.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kabla ya kufanya uamuzi wowote kuwahoji wabunge wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu wao ndio wahusika**.**

### 2.5.1.6. Utekelezaji wa Miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini

**Mheshimiwa Spika,** miradi ya umeme vijijini ilikuwa inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Kukosekana kwa vifaa kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi; na
ii. Kupanda kwa bei ya vifaa vya umeme tofauti na bei ambazo zilikuwa kwenye mikataba na hivyo kusababisha wakandarasi kushindwa kutekeleza Miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kwamba tayari Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijiji *(REA)* ilimuandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili atoe ushauri wa kitaalamu na kuruhusu mabadiliko yafanyike katika Mikataba ya umeme.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliweza kutekeleza maagizo ya Bunge kwa kupitia mikataba yote 39 ya Mradi wa Kupeleka

Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (R3R2) ambapo baada ya kupitia upya gharama za vifaa (Nyaya na Mashine Umba), jumla ya **Shilingi bilioni 78.29** ziliongezeka bila Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Gharama zilizoongezeka zilikuwa bado zipo ndani ya bajeti ya mradi kwani jumla ya gharama za mikataba iliyosainiwa ilikuwa ni **Shilingi trilioni 1.22.** Hata hivyo, baada ya uhakiki wa kina ambao hufanyika wakati wakandarasi wanaanza kazi, gharama ya mradi ilishuka hadi **Shilingi trilioni 1.08**. Upungufu huo umetokana na kupungua kwa urefu wa njia za Umeme wa Msongo wa kati kutoka kilomita 28,297 hadi kilomita 23,424. Hii ina maana kwamba baada ya uhakiki wa kina, gharama halisi za utekelezaji wa mradi zilipungua kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 140.** Gharama zote hizo ni pamoja na VAT.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa maana hiyo, baada ya kufanya mapitio ya gharama za vifaa, jumla ya gharama ya mradi kwa mikataba yote 39 ni **Shilingi trilioni 1.18** (pamoja na VAT) ambayo ipo ndani ya bajeti ya mradi hivyo Serikali haikulazimika kutafuta pesa za ziada.

### 2.5.1.7. Maslahi ya Madiwani

**Mheshimiwa Spika,** kulingana na Tangazo la Serikali Na. 47 la tarehe 20, Novemba, 2020 idadi ya Kata katika Mikoa yote 26 Tanzania Bara ilikuwa 3,956 katika Halmashauri 184. Madiwani waliopo ni 5,327 ambapo Madiwani 3,953 ni wakuchaguliwa na Madiwani 1,374 ni wa Viti Maalum walioteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kufuatia Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** tangazo la Serikali la Mgawanyo wa Maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 537 la tarehe19 Julai, 2019 idadi ya Vijiji katika Mikoa yote 26 Tanzania Bara katika Halmashauri 184 ni 12,318. Vilevile, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Mgawanyo wa Maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji)

Na. 536 la tarehe 19 Julai, 2019 idadi ya Mitaa ni 4,263. Mitaa na vijiji ina jumla ya Wenyeviti 16,581 walichaguliwa ambapo Wenyeviti wa Vijiji ni 12,318 na Wenyeviti Mitaa ni 4,263. Viongozi hawa pamoja na kufanya majukumu mbali hawana mishahara na badala yake huishi kwa kulipwa posho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipendekeza masuala yafuatayo: -

i. Serikali kufanya mapitio ya stahili za Waheshimiwa Madiwani na wenyeviti wa mitaa na vijiji; na
ii. Kuangalia uwezekano wa kufuta Waraka Na. 1 wa mwaka 2015 wa Katibu Mkuu Kiongozi ili kutotambua Udiwani kama kazi. Hatua hii itaruhusu Watanzania walio na kazi kugombea na kuwa madiwani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kwamba kwa sasa posho za kila mwezi za waheshimiwa Madiwani zilinalipwa na Hazina, hii imesaidia waheshimiwa Madiwani kupata posho hizo kwa wakati hasa kwa zile Halmashauri zenye uwezo mdogo wa makusanyo. Pamoja na hilo bado posho za madaraka zinaendelea kulipwa na Halmashauri zenyewe. Hata hivyo, Serikali inaendelea kufanya mapitio ya stahili za waheshimiwa madiwani ikiwemo kuangalia uwezo wa Halmashauri katika ulipaji wa posho za madaraka ili kuona uwezekano wa kuongeza posho hizo. Pamoja na hilo, Serikali inafanya tathmini ya uwezo wa ukusanyaji wa mapato katika ngazi za vijiji ili kubaini vijiji vyenye uwezo mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ambayo yanaweza kutumika kulipa baadhi ya stahili hizo. Hivyo, tathmini hiyo ikikamilika, utatolewa mwongozo wa namna bora ya utekelezaji wake.

### 2.5.1.8. Ufuatiliaji na Tathmini

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2020/2021 Ofisi ya Rais -

TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 7.56** kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Miradi, Programu na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 4.31** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 3.25** ni fedha za nje. Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi kwa kipindi cha miaka mitatu ni **Shilingi bilioni 4.12** sawa na **asilimia 54.48** ya bajeti yote katika kipindi hicho ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 3.80** na fedha za nje ni **Shilingi milioni 319.34**.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Serikali za Mitaa kutumia wastani wa **asilimia 25** hadi **30** wa Bajeti yote ya maendeleo na kawaida bado kiwango kinachotengwa kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini hakitoshelezi. Mathalani, katika kipindi cha Miaka mitatu kwa wastani zinatengwa **Shilingi bilioni 2.52** kiasi hiki hakiendani na mahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kupendekeza masuala yafuatayo: -

i. Kuandaa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini;
ii. Kuandaa sheria kuhusu Ufuatiliaji na Tathmini itakayobainisha majukumu ya kila muhusika katika zoezi la Ufuatiliaji na Tathmini;
iii. Kutenga kila mwaka walau **Shilingi bilioni 10** kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini; na
iv. Kuhuisha Mifumo yote ya Ufuatiliaji na Tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, Serikali inaendelea kukusanya maoni kutoka kwa wadau ambayo yatatumika kuandaa Taarifa za Utafiti wa Kizio (Baseline Study). Hadi Desemba 2022, ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau umekamilika, hususan Wizara, Taasisi za Umma, Bunge, Vyuo, Taasisi za Utafiti pamoja na Wadau wa Maendeleo (DPs). Ukusanyasaji wa maoni kutoka Tawala za

Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa unatarajiwa kukamilika Februari 2023. Kukamilika kwa Taarifa za Utafiti wa Kizio (Baseline Study) utajenga msingi wa maandalizi ya Sera. Aidha, kutungwa kwa Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini kutategemea matokeo ya maandalizi ya Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo.

**2.5.1.9. Kutwaa Maeneo yaliyozunguka Ofisi ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** eneo la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limezungukwa na Taasisi za Umma kama vile GPSA, Maghala ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Hotel ya FiftySix, Soko la Mama Rehema Nchimbi, Maghala yanayomilikiwa na Kampuni ya ALKO, Jengo la mazoezi yaani GYM na Chuo cha Biashara (CBE). Maeneo hayo yote hayako chini ya umiliki wa Ofisi ya Bunge hivyo, kuwa hatarishi kwa usalama wa Bunge lenyewe na Viongozi ambao hutembelea Bunge kwenye matukio makubwa ya kitaifa. Matukio hayo ni kama vile Rais kulihutubia Bunge, Bajeti Kuu ya Serikali na Kuapishwa kwa Wabunge na Spika. Kwa kuwa, maeneo hayo si mali ya Bunge yanahitaji kulipiwa fidia kabla ya Bunge kuyamiliki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kufanya mchakato wa kutafuta maeneo kwa ajili ya Taasisi za Umma zinazozunguka eneo la Bunge na Pili, kulipa fidia kwa watu binafsi waliopo katika maeneo yanayozunguka Ofisi ya Bunge ili waachie maeneo yao. Aidha, ilishauriwa kutenga fedha za maendeleo kupitia mafungu ya Taasisi husika ili iwe fidia kwa mali ambazo zitaachwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, suala hili limepewa umuhimu wa kipekee kwa lengo la kuimarisha usalama wa maeneo yanayozunguka eneo la Bunge, hivyo imeundwa Timu ya pamoja ya Wataalam chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo imeshirikisha wadau wote muhimu wakiwemo Wataalam kutoka Ofisi ya Bunge na

Taasisi za Umma zenye umiliki wa maeneo yanayokusudiwa kutwaliwa. Timu hiyo imekwisha fanya majadiliano na Taasisi ambazo maeneo yao yamepangwa kutwaliwa hasa ikizingatiwa kuwa walikwishaanza mikakati ya uendelezaji wa maeneo yao. Timu hiyo imekamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa kwenye Mamlaka zinazohusika kwa ajili ya maamuzi.

### 2.5.1.10. Kalenda ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 124(2) cha Ushuru wa Bidhaa Sura ya 145 kinamruhusu Waziri wa Fedha na Mipango kufanya mabadiliko ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha mfumuko wa bei. Wadau kutoka sekta binafsi wanaiomba Serikali kutobadili viwango vya ushuru wa bidhaa vilivyopo ili Sekta ya vinywaji isitetereke kutokana na mfumuko wa bei uliopo hivi sasa. Aidha, Serikali inashauriwa kuweka utaratibu wa kalenda ya mabadiliko ya kodi ili sera za kikodi nchini ziwe zinatabirika na kuvutia wawekezaji zaidi " *Fiscal Stability*".

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishauri masuala yafuatayo;

i. Kuanzisha utaratibu wa kalenda ya Kodi kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na
ii. Kuangalia uwezekano wa kuendelea na viwango vya ushuru wa bidhaa kama vilivyo hivi sasa ili kuleta uendelevu "*stability*" kwenye Sekta ya vinywaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imeendelea na viwango vilivyopo vya Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli ikiwa ni pamoja na vinywaji. Hatua hii inalenga kuleta *stability* kwenye Sekta hiyo, kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta ya viwanda, kulinda na kukuza ajira na mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa.

## 2.6. *Ziara za Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari 2022 hadi Januari, 2023, kwa nyakati tofauti, Kamati ilifanya ziara katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mtwara, Tanga, Manyara na Kilimanjaro pamoja na nchi ya Uturuki na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Ziara hizo zilikuwa na lengo la: -

i. Kukagua shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati;
ii. Kutembelea Mitambo ya Kuzalisha Umeme ya Kinyerezi one na Kinyerezi two pamoja na mitambo ya Kuzalisha Umeme wa Gesi Ubungo;
iii. Kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR kipande cha Dar es Salaam-Soga (Chalinze);
iv. Kutembelea Kiwanda cha Saruji cha Wazo Hill pamoja na eneo la EPZA la Benjamin Mkapa – Mabibo Dar es Salaam;
v. Kutembelea Kiwanda cha Nguo cha NIDA Textile;
vi. Kutembelea kiwanda cha Viuwadudu Kibaha;
vii. Kutembelea na kukagua Miundombinu ya kupokelea mafuta katika bandari za Mtwara, Tanga na Dar es Salaam, pamoja na bomba la mafuta TAZAMA, KOJ na sehemu ya kuhifadhi mafuta -TIPER;
viii. Kutembelea eneo la Chongoleani la Mradi wa bomba la mafuta la Afrika Mashariki (EACOP);
ix. kutembelea na kukagua utekelezaji wa fedha za Uviko -19 katika jiji la Arusha, Manyara na Kilimanjaro; na
x. Kupata uzoefu wa nchi zingine kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, uchumi na ukusanyaji wa mapato.

### 2.6.1. Masuala muhimu yaliyojitekeleza

**Mheshimiwa Spika,** kwa muhtasari naomba niwasilishe masuala muhimu yaliyobainika wakati wa ziara za Kamati kama ifuatavyo: -

### a) Miundombinu ya Mafuta

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea miundombinu ya kupokelea mafuta iliyopo bandari ya Mtwara, Tanga na Dar es salaam na kubaini masuala yafuatayo: -

i. Wateja wa mikoa ya kusini pamoja na ile ya kaskazini wamekuwa wanaenda kuchukua mafuta Dar-es-salaam hivyo kupelekea kusiwe na biashara ya mafuta katika mikoa ya Mtwara na Tanga. Hali hii husababisha uwepo wa mafuta kwa wingi katika maeneo hayo na kukosekana mahali pakuhifadhia mafuta mapya;
ii. Kutokana na ukosefu wa sehemu ya kuhifadhia mafuta, muagizaji hulazimika kulipa *demurrage fee* kutokana na meli kukaa baharini muda mrefu;
iii. Mafuta yanayotakiwa kushushwa Mtwara kulazimika kushushwa Dar-es-salaam kutokana na kiwango kinachotakiwa kupelekwa Mtwara kutokuwa na faida kibiashara (Economically Feasible) hali hii husababisha bei ya mafuta Mtwara kuwa kubwa pindi yanaposafirishwa kwenda bandari ya Mtwara kutoka bandari ya Dar es Salaam;
iv. Kutokuwepo kwa kituo cha kujaza mafuta baharini *bunkering facility*. Kituo hiki kitasaidia kutoa huduma na kujaza meli mafuta baharini. Kwa upande wa Afrika Mashariki kituo hiki hivi sasa kipo kimoja tu katika Bandari ya Mombasa; na
v. Kuna changamoto ya uwezo mdogo wa matanki ya kuhifadhia mafuta nchini na hivyo kusababisha

meli kuchukua muda mrefu kusubiri nafasi ipatikane kwa ajili ya kushusha mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali iwekeze kwenye kujenga *bunkering facility* ambayo imeonekana ni kitu cha muhimu hasa kutokana na suala la utafutaji wa mafuta na gesi (*exploration)* katika ukanda wa kusini mwa Tanzania. Vilevile, Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha makampuni ya mafuta yaliyopo katika Mikoa ya kusini na kaskazini yanachukua mafuta katika Bandari za karibu na maeneo hayo. Aidha, Serikali ilishauriwa kwamba ili kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa Meli za Mafuta kushusha ni kuongeza eneo la kuhifadhia mafuta ili kuepusha gharama za ziada.

**b) Kiwanda cha Saruji cha Twiga Cement - Wazo Hill**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kwamba uzalishaji wa saruji katika kiwanda hicho umeongezeka. Hata hivyo, kinakabiliwa na changamoto kuu tatu. Kwanza, wananchi kuvamia ardhi ambayo ina malighafi za kiwanda; Pili, bei kubwa ya gesi ambayo inatumika kama nishati katika kuchakata saruji na Tatu, ni uingizwaji wa saruji kutoka nchi za jirani kwa mikoa ya pembezoni. Kwa kuwa, masuala yote haya yanahitaji hatua za kisera na kisheria, Kamati iliyawasilisha katika Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hatua zaidi.

**c) Mamlaka ya Eneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea eneo huru la Mauzo Nje la Benjamin Mkapa (Benjamin Mkapa Special Economic Zone). Katika eneo hilo Kamati ilitembelea kiwanda cha nguo na kiwanda cha kuzalisha kadi za simu pamoja na Kadi za Benki. Kamati ilibaini kwamba EPZA inaweza kuwa na mchango mkubwa sana katika maendeleo ya viwanda na

mauzo nje ya nchi endapo italipa fidia na kuendeleza maeneo mengi zaidi nchini. Aidha, Kamati iliiagiza EPZA kuwasilisha mahitaji ya fedha Bungeni ili kuona uwezekano wa kuendeleza maeneo yake. Vilevile, Serikali ilishauriwa kuondoa kodi ya ardhi katika maeneo yote ya *Special Economic Zone* (SEZ) ili kupunguza gharama za maeneo hayo.

**d) Kiwanda cha Nguo cha NIDA Textile Mills**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya ziara ndani ya viwanda vya nguo vya Nida ilibaini masuala yafuatayo: -

i. Viwanda hivi vinakabiliwa na tatizo kubwa la uingizwaji wa bidhaa za nguo kwa njia ya magendo kutoka nchi za nje ambazo huua soko na kuikosesha Serikali mapato yake;
ii. Uhaba wa malighafi za pamba kipindi ambacho sio cha msimu, na hivyo kuagiza pamba nje ya nchi ambayo huongeza gharama za Uzalishaji;
iii. Tatizo la riba za juu za Mikopo kutoka kwa mabenki ya Kibishara linaathiri mtaji wa Viwanda vya NIDA kwa asilimia kubwa; na
iv. Kupungua kwa viwanda vya uzalishaji wa nguo na nyuzi toka viwanda 33 hadi viwanda 6.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kupitia Wizara ya kilimo kuhakikisha kwamba pamba inapatikana kwa mwaka mzima na si katika kipindi cha msimu pekee. Vilevile, Serikali idhibiti bidhaa za magendo zinazoingizwa na hivyo kuathiri soko la ndani.

**e) Kiwanda cha Viuwadudu (Tanzania Biotech Products Limited)**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kutembelea Kiwanda hiki ilibaini kwamba changamoto kubwa inayokikumba Kiwanda hiki ni ufinyu wa bajeti ya utafiti na ya kulipia ithibati.

Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za kutosha ili kiwanda hiki kiweze kujiendesha kwa faida kama ilivyokusudiwa.

## 2.7. *Mafunzo kwa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka mmoja, Kamati ilipata mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwajengea uwezo na ujuzi wajumbe ili waweze kutekeleza majukumu yao. Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na Programmu za Miradi ya LSP II na PFMRP zilishiriki katika kutoa mafunzo hayo. baadhi ya mafunzo ambayo Kamati ilishiriki ni kama ifuatavyo: -

i. Mfumo wa ulipaji Serikalini (MUSE);
ii. Utendaji kazi wa mfumo wa Mahakama pamoja na kutembelea jengo jipya la Makao Makuu ya Mahakama Dodoma;
iii. Miongozo ya Ofisi ya Msajili wa Hazina inayohusu usimamizi wa Mashirika ya Umma;
iv. Mfumo wa Engineering, Procurement, Construction-Financing (EPC+F);
v. Uhimilivu wa deni la Serikali pamoja na faida na hasara za kutumia mfumo wa EPC+F katika ujenzi wa barabara nchini;
vi. Benki kuu ya Tanzania kuhusu utendaji kazi wa Credit Refrence Bureau, Mwenendo wa soko la dhamana za Serikali baada ya Benki kuu ya Tanzania kushusha viwango vya riba;
vii. Mizania ya Benki Kuu;
viii. Sekta ya mafuta na gesi yaliyotolewa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC);
ix. Mfumo wa uagizaji wa Mafuta wa Pamoja (Petroleum Bulk Procurement System) kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), faida na hasara zake;

x. Namna Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inadhibiti bei na usambazaji wa mafuta ya petroli nchini;
xi. Usimamizi na usalama wa mifumo ya Serikali pamoja na utekelezaji wa sera ya Taifa ya TEHAMA;
xii. Uhimilivu wa Deni la Taifa na Viashiria vyake;
xiii. Namna ya kuchambua na kuzitumia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali;
xiv. Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani (IAG)
xv. Ujenzi na uendelezaji wa miundombinu iliyotolewa na wakala wa barabara vijijini na Mijini (TARURA);
xvi. Mfumo wa manunuzi Serikali yaliyotolewa na TANEPS
xvii. Ununuzi wa magari Serikalini yaliyotolewa na GPSA

## SEHEMU YA TATU

### 3.0. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu Mwaka (TAREHE 1Julai hadi TAREHE 30 Desemba 2022)

### *3.1. Sura ya Bajeti na utekelezaji hadi Desemba, 2022*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha Sheria ya Bajeti Sura 439 ya mwaka 2015, Serikali iliwasilisha mbele ya Kamati Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya nusu mwaka. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 41.48**. kati ya fedha hizo jumla ya **Shilingi trilioni 26.47** zilitarajiwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi tilioni 15.01** kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya **Shilingi trilioni 19.46** sawa na **asilimia 46.9** ya lengo la kukusanya na kutumia **shilingi trilioni 41.48.** Kati ya fedha hizo **shilingi trilioni 12.29** zilitumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi**

**trilioni 7.17** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua hii ya utekelezaji kwa sababu mwenendo huu unaonyesha kwamba utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 unaweza kufikia **asilimia 95.**

### 3.1.1. Makusanyo ya Mapato ya Ndani

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 Serikali iliweza kukusanya mapato ya ndani na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa jumla ya **Shilingi trilioni 13.40** sawa na **asilimia 47.8** ya makadirio ya kukusanya na kutumia **Shilingi trilioni 28.02**. Hatua hii ni ya kupongeza kwa sababu inaonesha kwamba makusanyo ya mapato yanatarajiwa kufikia **asilimia 96** ya matarajio.

**Jedwali Na. 4. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (Bilioni)**

| Na | Chanzo | Bajeti (2022/23) | Utekelezaji Nusu Mwaka (2022/23) | Asilimia %ya bajeti |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Kodi | 23,652.8 | 11,676.9 | 49.37 |
| 2. | Mapato ya Halmashauri | 1,012.3 | 458.6 | 45.30 |
| 3. | Mapato yasiyo ya kodi | 3,352.8 | 1,264.8 | 37.72 |
| 4. | Misaada na Mikopo kutoka nje | 4,648.6 | 3,014.6 | 64.85 |
| 5. | Mikopo ya ndani | 2,480.2 | 823.8 | 33.22 |
| 6. | Mikopo ya ndani roll over | 3,300 | 1,671.5 | 50.65 |
| 7. | Mikopo ya masharti ya | 3,034 | 552.2 | 18.2 |

| Na | Chanzo | Bajeti (2022/23) | Utekelezaji Nusu Mwaka (2022/23) | Asilimia %ya bajeti |
|---|---|---|---|---|
| | kibiashara | | | |
| | **Jumla** | **41,480.58** | **19,462.4** | **47** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

3.1.2. **Ukusanyaji wa Mapato chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina katika Kipindi cha Nusu Mwaka 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha nusu mwaka hadi kufikia Desemba, 2022 Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusanya jumla ya **Shilingi bilioni 424.32** ikiwa ni sawa na **asilimia 46** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 931.93** katika kipindi hicho. Kwa mwenendo huu ni dhahiri kuwa Ofisi ya Msajili itaweza kufikia makusanyo kwa **asilimia 92 – 100**. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia vyanzo bunifu ili kupata mitaji kwa ajili ya Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo yanachangamoto za kimtaji. Vyanzo hivyo ni kama kujiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar-es-salaam na kuruhusu watanzania kushiriki katika uwekezaji. Vilevile, Kamati inaitaka Ofisi ya Msajili kuendelea kusimamia ufanisi na utendaji kazi wa Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na Kampuni ili kuimarisha makusanyo ya mapato yaliyoko katika sheria ya msajili wa hazina.

**Jedwali Na. 5. Makusanyo kwa Kipindi cha Nusu Mwaka Hadi Desemba, 2022**

| Na. | Mapato yasiyo ya kodi | Bajeti ya Mwaka | Makusanyo Nusu Mwaka | Ufanisi Nusu Mwaka (%) |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Gawio | 470, 516,968,799 | 68,125,080,540.50 | **14%** |
| **2.** | Michango ya Asilimia 15 | 297,501,732,004 | 105,297,462,734.57 | **35%** |
| **3.** | Mawasiliano ya TTMS | 10,000,000,000 | 5,397,017,999.13 | **54%** |
| **4.** | Marejesho ya Mikopo na Riba | 34,152,351, 670 | 18,008,611,875 | **53%** |
| **5.** | Mawasilisho Mengineyo | 119,754,960,160 | 227,493,531,119.06 | **190%** |
| **JUMLA** | | **931,926,013,633** | **424,321,704,268.26** | **46%** |

***Chanzo: Ofisi ya Msajili wa Hazina***

### 3.1.3. Mwenendo wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 Serikali imetoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya **Shilingi trilioni 19.46** sawa na **asilimia 91.7** ya makadirio ya **Shilingi trilioni 21.22** ya nusu mwaka. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 4.48** zilitumika kwa ajili ya mishahara, **Shilingi trilioni 4.26** kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali, **Shilingi trilioni 3.55** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi trilioni 7.17** zilitumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Serikali katika kipindi husika ililipa marejesho mbalimbali ya kodi (tax refunds) yenye thamani ya **Shilingi bilioni 590.3** ikiwa ni ufanisi wa **asilimia 165.8** ya malengo ya kulipa

**Shilingi bilioni 356** katika kipindi husika. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambayo inaenda kurejesha mitaji na imani kwa wahusika waliokuwa wanaidai Serikali kwa kipindi kirefu.

***3.2. Utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 kwa Kipindi cha Nusu Mwaka 2022/2023.***

**Mheshimiwa Spika,** mwaka 2022 Serikali ilifanya marekebisho katika sheria 35 kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022. Mabadiliko hayo yalifanyika kwa malengo ya kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini (MKUMBI), uboreshaji wa mfumo wa kodi ili kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na kutoa msamaha kwa maeneo muhimu ili kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali za uchumi. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2022 maboresho hayo yalikuwa yamekusanya jumla ya **Shilingi trilioni 1.19** sawa na **asilimia 43.8** ya kukusanya **Shilingi trilioni 2.71** likiwa ni lengo la mwaka.

***3.3. Uchambuzi Kuhusu Bajeti ya Serikali katika kipindi cha Nusu Mwaka 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika,** malengo ya ukusanyaji wa mapato haukufikiwa kutokana na sababu mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. Kutokuwa na mifumo ya ukusanyaji wa kodi ya biashara mtandao: Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022, ukusanyaji wa kodi hii haukuweza kuanza kutokana na matengenezo ya kimfumo yaliyokuwa yanaendelea. Mfumo huu una lengo la kuwatambua, kuwasajili na kukusanya kodi kutoka kwa makampuni na wadau wengine wote wanaojihusisha na biashara mtandao;

ii. Kupungua kwa thamani ya uingizaji wa bidhaa: Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kurejesha kodi ya ongezeko la thamani kwenye simu janja, vishikwambi na modemu. Hatua hiyo ilisababisha kupungua kwa idadi ya simu janja na vishikwambi vilivyoingizwa nchini kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2022. Hivyo, thamani ya uagizaji wa mizigo ya simu janja na vishikwambi imepungua kutoka **Shilingi bilioni 201.70** hadi **Shilingi bilioni 92.50;**

iii. Serikali haikuweza kukusanya kodi ya mapato ya **asilimia 2** kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma wa kidijitali wa kigeni: Hii ilitokana na kutokukamilika kwa mfumo unaosimamia usajili, uwasilishaji wa ritani na ulipaji kodi kwa watoa huduma za kidijitali wa kigeni. Mfumo huo kwa sasa umekamilika na umeanza kutumika kuanzia Januari, 2023;

iv. Kupungua kwa uingizaji wa bidhaa za sukari kutoka nje ya nchi: katika marekebisho yaliyofanywa na Serikali ni pamoja na kutoza ushuru wa bidhaa wa shilingi 500 kwa kilo moja ya bidhaa ya sukari (sugar confectionery) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na zinazozalishwa hapa nchini. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 marekebisho haya yaliongeza mapato ya Serikali kwa **Shilingi trilioni 4.04** ikilinganishwa na lengo la **Shilingi trilioni 17.02** sawa na **asilimia 33.7** tu. Ufanisi huu umetokana na kupungua kwa uingizaji wa bidhaa za sukari kutoka nje kutoka kilo milioni 34 hadi kilo milioni 8.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, mara kwa mara Serikali hupendekeza chanzo cha mapato bila kuwa na uhakika na utayari wa namna ya ukusanyaji wake na hivyo, kuathiri utekelezaji wa bajeti. Hii inaleta matokeo hasi katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Kutokana na changamoto hii Serikali ina nakisi ya **Shilingi trilioni 3.67** ambazo zingetokana na vyanzo hivyo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inapopendekeza vyanzo vya mapato inapaswa iwe imejiandaa katika utekelezaji wake.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0. TATHMINI KUHUSU MKOPO WA *EXTENDED CREDIT FACILITY* (ECF) KUTOKA SHIRIKA LA FEDHA LA KIMATAIFA (IMF) wa DOLA ZA MAREKANI BILIONI 1,046

**Mheshimiwa Spika,** Mkopo wa ECF ni mkopo uliotolewa kupitia dirisha *la Extended Credit Facility* (ECF) ambapoTanzania ilipata **Dola za Marekani bilioni 1,046**, sawa na **Shilingi trilioni 2.4**. Mkopo huo utatolewa kwa awamu saba (7) katika kipindi cha miezi 40 kuanzia Julai 2022 hadi Julai 2025. Kwa mujibu wa makubaliano, kwa mwaka wa kwanza 2022/2023, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge ni **Shilingi bilioni 760** ambayo itatolewa kwa awamu mbili kwa mwaka. Aidha, mkopo huu ni wa pili baada ya ule wa Rapid Credit Facility (RCF) maarufu kama mkopo wa UVIKO – 19.

**Mheshimiwa Spika,** mgao wa fedha za awamu ya kwanza za ECF wa jumla ya **Shilingi bilioni 349.829** ulitolewa mwezi Agosti 2022. Kiwango hiki ndicho kitakachokuwa kinatolewa kwa kila awamu katika awamu saba (7) kutegemeana na mabadiliko ya thamani ya shilingi ambapo jumla itakuwa **Shilingi trilioni 2.45.** Aidha, mgao wa awamu ya pili kwa mwaka 2022/2023 utatolewa mwezi

Machi 2023 baada ya IMF kufanya tathmini ya utekelezaji wa makubaliano baina ya pande mbili. Fedha hizi ziligawanywa katika Sekta za Nishati, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Sekta ya huduma za Maendeleo ya Jamii (wamachinga) na Kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

### 4.1. *Lengo la Mkopo*

**Mheshimiwa Spika,** mkopo uliotolewa na IMF wa ECF kupitia Dirisha la Mfuko wa Kupunguza umasikini na kukuza Uchumi (Poverty Reduction and Growth Trust - PRGT) una lengo la kurekebisha matatizo ya urari kwa nchi zenye matatizo ya urari ya muda mrefu (Proctracted Balance of Payment Problem). Hivyo, lengo kuu la mkopo huu ni kuwekeza kwenye sekta za uzalishaji ambazo zinaweza kuongeza mauzo nje ya nchi na kupunguza uagizaji wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa nchini. Mkopo huu hautakuwa na riba na utakuwa na muda wa neema (Grace Period) wa miaka 5.5.

**Jedwali Na 6. Mgawanyo wa Fedha za Mkopo wa ECF kutoka IMF "000"**

| SEKTA | OC | DEV | JUMLA | OC % | DEV % | JUMLA % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mifugo | 10,279,568 | 29,720,432 | 40,000,000 | 25.7 | 74.3 | 100 |
| Uvuvi | 17,172,775 | 42,827,225 | 60,000,000 | 28.62 | 71.38 | 100 |
| Kilimo | 28,621,291 | 71,378,709 | 100,000,000 | 28.62 | 71.38 | 100 |
| REA | 73,400,000 | 26,600,000 | 100,000,000 | 73.4 | 26.6 | 100 |
| Nishati | 146,800,000 | 53,200,000 | 200,000,000 | 73.4 | 26.6 | 100 |
| Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 61,535,777 | 153,464,223 | 215,000,000 | 28.62 | 71.38 | 100 |
| Machinga | 13,235,500 | 31,764,500 | 45,000,000 | 41.67 | 58.33 | 100 |
| **JUMLA** | **351,044,911** | **408,955,089** | **760,000,000** | **46.19** | **53.81** | **100** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

### *4.2. Masuala yaliyobainika katika uchambuzi wa Utekelezaji wa Miradi inayotekelezwa kupitia mkopo huu.*

i. Utekelezaji wa miradi kupitia mkopo huu wa miezi 40 unaweza usifikiwe kwa sababu miradi mingi iliyopokea fedha bado iko kwenye mchakato wa manunuzi;

ii. Baadhi ya malengo hayatafikiwa kutokana na fedha za mkopo kuelekezwa kwenye maeneo ambayo hayaendani na malengo ya mkopo;

iii. Kuna mkanganyiko wa takwimu za fedha zilizopo kwenye miradi ya maendeleo ya ECF na zile zilizopo kwenye Kitabu cha miradi ya maendeleo Volume IV. Ambapo kwenye mgawanyo inaonesha fedha za ECF ni shilingi bilioni 760 wakati kwenye kitabu cha maendeleo inaonesha ni shilingi bilioni 648;

iv. Baadhi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa kupitia mkopo huu zinaweza zisiendelee miezi 40 ya mkopo kuisha mfano fedha za mkopo kutumika kufanyia mafunzo mfano. Shilingi milioni 800 zilizotengwa kutoa mafunzo kwa wakulima 120,000;

v. Kwa kuwa, moja ya sharti la mkopo ni kutoa fedha mara baada ya kujiridhisha na matumizi ya fedha zilizotolewa awamu iliyotangulia, kwa hali hii ya utekelezaji wake unaweza ukazidi miezi 40 kutokana na sheria ya manunuzi na usimamizi usioridhisha;

vi. Sheria ya Manunuzi inasababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi kutokana na mchakato mrefu wa manunuzi;

vii. kila fungu lililopokea fedha za ECF limetenga fedha ili zitumike kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini. Hata hivyo, bado hatuna Sera ya nchi ya kitaifa wala Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini. Kwa hali hiyo mkopo utakapokamilika tutarejea kwenye utaratibu wa kawaida ambapo Ufuatiliaji na Tathimini (M&E) haufanyiki kama inavyotakiwa;

viii. Baadhi ya Wizara zilizonufaika na mkopo hazikuweza kubainisha mwendelezo wa miradi inayotekelezwa kwa Fedha hizi mara baada ya miradi kuisha;

ix. Kucheleweshwa kwa misamaha ya kodi ya ongezeko la Thamani (VAT) na hivyo kusababisha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi mbalimbali; na

x. Kwa ile miradi ambayo inatekelezwa na Wizara katika Halmashauri na itahamishiwa katika Halmashauri husika baada ya miradi kukamilika. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuikabidhi Halmashauri miradi hiyo kwa ajili ya kuisimamia na kuiendesha.

**Mheshimiwa Spika,** endapo changamoto hizi hazitafanyiwa kazi mapema iwezekanavyo ni wazi kwamba hatutapata mgao unaofuata na lengo la mkopo huu halitafikiwa. Kama ambavyo Serikali ilitoa Mwongozo wa Manunuzi kwenye Mkopo wa Fedha za Ufadhili wa Kupambana na Ugonjwa wa UVIKO – 19 (Rapid Credit Facility – RCF) wa shilingi trilioni 1.3 ni vyema hatua hii ikachukuliwa kwenye mkopo huu.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0. UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE yaliyoTOKANA NA TAARIFA YA kamati ya MWAKA kuhusu utekelezaji wa majukumu ya KAMATI ya bajeti kwa mwaka 2022

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati ya mwaka 2022 ilikuwa na jumla ya mapendekezo 19 ambayo Bunge lako liliridhia yakawa maazimio ya Bunge. Maazimio hayo yalihusu utekelezaji wa Bajeti, Sheria na miradi ya maendeleo. Aidha, maazimio yalihusu maeneo ya kiuchumi, utozaji wa kodi, usimamizi wake pamoja na vyanzo vya mapato. Kamati imefanya uchambuzi wa

utekelezaji wa maazimio ya Bunge na kubaini masuala yafuatayo: -

### 5.1. *Mafanikio katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kupitia kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza maazimio yafuatayo ya kamati kikamilifu: -

i. Bunge liliazimia kwamba Bajeti ya Kilimo iongezwe kwa walau **Shilingi billioni 500**, Mhe Rais aliridhia na kuongeza Bajeti kwa takribani **Shilingi billioni 700** na hivyo kufanya bajeti ya Wizara ya Kilimo kuwa **Shilingi bilioni 954;**
ii. Kulikuwa na changamoto ya uhaba wa watumishi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania na hivyo kusababisha ukaguzi kutofanyika kila mwaka, Mhe Rais aliridhia kibali cha kuajili watumishi 2100. Zoezi la kuajiri watumishi wapya linaendelea hatua kwa hatua na hivi karibuni Mamlaka ya Mapato imepokea idadi ya watumishi 1548 na wengine zaidi ya 400 wako katika hatua ya usaili;
iii. Kulikuwa na azimio la kutunga sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Mhe. Rais alisikia na muswada uko katika hatua za maboresho ili uletwe tena Bungeni baada ya kuletwa mara ya kwanza; na
iv. Kulikuwa na Changamoto ya kutoishirikisha kamati ya Bunge ya Bajeti na Bunge kuhusu mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004. Kwa dhati naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, (Mb) kwa kuhakikisha kwamba katika mwaka 2022/2023 kamati ya Bajeti inashirikishwa kikamilifu na serikali

juu ya mapendekezo yake kabla ya kupelekwa kwenye jumuiya ya Afrika mashariki.

### 5.2. *Masuala yaliyobanika katika Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kupitia kamati ya Bajeti*

i. Kuna baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa na changamoto kwa miaka mingi lakini utekelezaji wake unaonyesha kwamba ama Serikali inafanya utafiti au iko katika ukusanyaji wa maoni ya wadau. Mfano changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya PPP pamoja na uhitaji wa Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini;
ii. Kuna changamoto katika kufanya maamuzi ya haraka na yenye manufaa kwa taifa mfano Utekelezaji wa MKUMBI sio wa kuridhisha na pili uanzishwaji wa Ofisi ya Mpokea Malalamiko ya Kodi "Tax Ombudsman" umekwama kutokana na kukosekana kwa kibali cha kuwahamishia watumishi katika Ofisi hiyo;
iii. Miradi ya muda mrefu haijatekelezwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali ili kutanzua vikwazo vya utekelezaji wa miradi hiyo ni kufanya vikao. Jambo hili haliwezi kutanzua utekelezaji wa miradi hii kwa sababu limekuwa ni tatizo la muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa kina wa Maazimio ya Bunge kupitia kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti umeambatishwa katika **kiambatisho A** kwa rejea. Kamati itaendelea kufuatilia utekelezaji wa maazimio yaliyobaki kila wakati ili kuhakikisha kwamba yote yanatekelezwa kikamilifu.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

### 6.1. *Mfumo wa utolewaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya changamoto ambayo kamati imebaini ni kwamba hakuna mfumo thabiti wa utolewaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Bungeni. Hali hii husababisha miradi ya maendeleo ya muda mrefu kutotekelezwa au kutekelezwa kwa kusua sua. Kamati inaishauri Serkali kuwa na Mfumo utakaokuwa unatunza Taarifa za Jina la mradi, muda wa utekelezaji, gharama za mradi na Jina la Kampuni, mkandarasi au mzabuni anaetoa huduma. Taarifa ya mfumo huo iwe inawasilisha Bungeni walau kila baada ya miezi 3 ili Bunge liisimamie Serikali kikamilifu.

### 6.2. *Maafisa Ugani kutekeleza majukumu yao ya Msingi*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuhakikisha kwamba maafisa ugani wanatoa huduma za ugani kikamilifu. Hatua hii ni pamoja na kugawa jumla ya piki piki 2000 kwa ajili ya maafisa ugani. Hata hivyo kamati imebaini kwamba pikipiki hizo hazijaweza kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa kutokana na kukosa mafuta na maafisa ugani kukosa vitendea kazi kama vile vifaa vya kupimia afya ya udongo. Aidha, imebainika kwamba maafisa ugani wengi wamekuwa wakipewa majukumu mengine kama vile watendaji wa kata na vijiji na hivyo kuacha majukumu yao ya msingi ya kutoa huduma ya ugani. Kamati inaishauri Serikali kwanza kuhakikisha maafisa ugani wanafanya majukumu yao ya msingi

ya ugani na pili ni kuhakikisha kwamba wanapatiwa mafuta na vitendea kazi ili watekeleze majukumu yao kikamilifu.

**6.3. *Elimu kuhusu Deni la Serikali na Deni la Taifa.***

**Mheshimiwa Spika**, Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mawazo tofauti tofauti kuhusu Deni la Serikali na Deni la Taifa na hivyo kuleta upotoshaji, mkanganyiko na taharuki kweny jamii. Watu wengi bado hawana uelewa juu ya utofauti kati ya Deni la Serikali na Deni la Taifa na jinsi deni la Serikali linavyolipwa. Mfano, imefika mahali baadhi ya wanasiasa wanawatisha wananchi kwamba kila mmoja atatakiwa kulipa kiasi fulani cha fedha ili kulipa Deni la Serikali jambo ambalo siyo la kweli. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Benki Kuu pamoja na Wizara ya Elimu kuandaa mada ambayo itakuwa ni lazima kwa Wanafunzi wa Sekondari, vyuo vya ufundi na Vyuo Vikuu kufundishwa kuhusu Deni la Serikali na Deni la Taifa. Hali ikiachwa kama ilivyo hivi sasa wananchi wengi watapotoshwa na wanasiasa.

**6.4. *Usambazaji wa Gesi Asilia***

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na ongezeko la bei katika nishati ya mafuta kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vita kati ya nchi ya Urusi na Ukraine ambayo imesababisha nishati hii kuwa adimu duniani. Kamati inatambua kwamba Serikali tayari ilishaanza utekelezaji wa mradi wa matumizi ya gesi asilia (LNG) ambao tayari umeanza kusambaza gesi hii katika maeneo machache ya Mkoa wa Dar es Salaam na katika magari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa gesi hii inasambazwa katika maeneo mengi ili kuwezesha wananchi kuanza kutumia gesi hiyo. Aidha, miundombinu ya usambazi iendelee kujengwa ili kuhakikisha kuwa watumiaji wanaongezeka na hivyo kupunguza utumiaji wa mafuta ambayo yanaagizwa kutoka nje kwa kutumia fedha za kigeni.

**6.5. *Ujenzi wa Barabara kwa Mfumo wa Uhandisi, Usanifu, Manunuzi, Ujenzi na Utafutaji wa Fedha* (EPC+F-Engineering Procurement Construction and Financing)**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23 Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi alilitaarifu Bunge lako kwamba baadhi ya barabara katika mwaka huu wa fedha zitajengwa kwa kasi kwa kutumia mfumo wa EPC+F. Kamati ya Bunge ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na kubaini kwamba matumizi ya mfumo huo hayatakuwa na matokeo ya haraka kama ilivyokusudiwa kwa sababu kuu mbili. Moja mwenye Mamlaka ya Kukopa kwa Niaba ya Serikali ni Waziri wa Fedha na Mipango kwa Mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali Sura ya 134 na pili ujenzi wa namna hii una athari ya moja kwa moja kwenye Deni la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwamba kuliko kutumia mfumo huu ambao utachukua muda na utakuwa na gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya barabara. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi michache ya barabara na kuikamilisha kwa wakati pamoja na kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa barabara ili

kuokoa fedha za matengenezo. Endapo itaonekana kukopa ni lazima basi ni vyema mikopo iwe yenye masharti nafuu ili itekeleze miradi ya barabara za kimkakati ambazo zina tija kwa Taifa. Kuliko kutumia mfumo huu ambao unaweza kuathiri deni la Serikali kwa namna ambayo linaweza isihimilike.

### 6.6. *Kurejea Mikataba ya Makubaliano ya Kutokutoza Kodi Mara Mbili (Double Taxation Agreement)*

**Mheshimiwa Spika,** Hadi hivi sasa Tanzania imesaini mikataba ya makubaliano ya kutokutoza kodi mara mbili (Double Taxation Agreement) 10. Mikataba mingi ilisainiwa kati ya miaka ya 1960 na 1990. Kamati inaishauri Serikali kufanya marejeo ya mikataba hiyo na kuangalia kama kuna haja ya kuendelea na mikataba hiyo kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi ukizingatia nyakati za sasa zimebadilika tofauti na za wakati ule hasa katika nyanja za ufanyaji biashara. Aidha, tuangalie uwezekano wa kuingia mikataba mingine ambayo itakuwa na manufaa kwa Taifa, kama ilivyofanya na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) mwezi Septemba, 2022.

### 6.7. *Matumizi ya Misamaha ya Kodi mbalimbali zilizotumiwa na Serikali ili kuchochea maendeleo*

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Bunge imekuwa ikifanya marekebisho mbalimbali ya Sheria za kodi ili kutoa misamha ya kodi. Malengo ya kutoa misamaha hii ni kuleta unafuu kwa wanachi, kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali, kukuza sekta binafsi pamoja na kuchochea maendeleo ya viwanda na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kusaidia miradi mikubwa ya maendeleo. Hata hivyo,

kamati imebaini baadhi ya misamaha ama inatumika vibaya au haifikii malengo yaliyokusudiwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimini ya malengo ya misamaha ya kikodi iliyotolewa endapo imefikia malengo yaliyokusudiwa.

**6.8. *Mfumo wa Usimamizi wa Mikopo ya asilimia 10 Ten Percent Loan Mangement Information System (TPLMS)***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua juhudi za Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Mikopo ya asilimia 10 unaoitwa *Ten Percent Loan Management Information System* (TPLMS) kwa lengo la kuboresha usimamizi na utoaji wa taarifa za shughuli zinazofanywa na vikundi. Pamoja na kwamba mfumo huo umeleta changamoto kwa watumiaji kama vile kutopatikana katika maeneo mbalimbali na baadhi ya walengwa wenye elimu ndogo kuhusu matumizi ya tehama kushindwa kuingia kwenye mfumo bado mfumo huu utakuwa na manufaa. Kamati imebaini kwamba changamoto kubwa ya marejesho ya mikopo ni shughuli zinazokopewa, uelewa mdogo wa wakopaji kuhusu uendeshaji wa biashara na matumizi ya mikopo yasiyokusudiwa. Aidha, imebainika mikopo hii inasimamiwa na afisa maendeleo ya jamii ambao hana taaluma yoyote kuhusiana na suala la mikopo.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo Kamati inaishauri Serikali kwanza kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na afisa mikopo na pili ni kutoa elimu na kuwashauri wakopaji ili kuwezesha kufanya marejesho. Uwepo wa mfumo hauwezi kuleta uhakika wa kufanyika kwa marejesho.

***6.9. Utengaji wa fedha za maendeleo kwenye Halmashauri***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kuna baadhi ya Halmashauri ambazo zimekuwa zikichangia chini ya **asilimia 10** ya kwa ajili ya mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Moja ya sababu zilizotajwa ilikuwa ni baadhi ya Halmshauri hizo kutokuwa na uwezo wa kuchangia **asilimia 40** ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayojumuisha **asilimia 10**. Hii imepelekea kuongezwa kundi la Halmshauri ambazo zina mapato ya chini ya **Shilingi bilioni 2** kuanza kuchangia **asilimia 20** badala ya **asilimia 40** ya Mapato ya Ndani kwa ajili ya Maendeleo katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/2024. Kutokana na changamoto hiyo Ofisi ya Rais TAMISEMI wameamua kuongeza kundi la Halmashauri ambazo zitachangia **asilimia 20** ya mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kuongeza kundi hili hakuondoi tatizo la msingi la Halmashauri kutotenga **asilimia 10** ambayo ni takwa la kisheria. Hivyo Kamati inaendelea kuisistizia Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe kuwa Halmashauri zote kulingana na kundi zilizopo zinachangia **asilimia 10** ya mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama Sheria inavyotaka. Aidha, Serikali ione haja ya kuziwezesha Halmshauri ambazo zina hali mbaya ya makusanyo na wakati huo huo zina fursa nyingi za kiuchumi ili nazo ziweze kujikwamua kiuchumi na kuongeza ukusanyaji wa mapato. Vilevile, Serikali ifanye tathmini fursa za kiuchumi kwa kila wilaya (economic district survey) na kuangalia ni uwekezaji

gani unatakiwa kwenye wilaya ipi ili kuongeza mapato.

## SEHEMU YA SABA

### 7.0. MAONI NA MAPENDEKEZO MAHUSUSI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati pamoja na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

**7.1.** ***Serikali iandae Mpango wa Uhitaji wa Rasilimali Watu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi.***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** Serikali haina mpango wa Taifa unao onyesha mahitaji ya rasilimali watu kwa Taifa ambao ungekuwa nyenzo ya mgawo wa Mikopo ya Elimu ya Juu.

**NA KWA KUWA,** hivi sasa Serikali inatumia wastani wa **Shilingi billioni 573** Kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu. Mpango huo utaiwezesha Serikali kuwa na kanzi data ya mahitaji ya Taaluma ili kuwe na ulinganifu wa wataalamu wanaohitajika kulingana na kasi ya ukuaji wa uchumi. Vilevile, mpango huu utaiwezesha Serikali kuelekeza fedha zaidi kwenye taaluma zinazohitajika katika vyuo vya kati na vya juu

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae Mpango wa Uhitaji wa Rasilimali watu ili taaluma zinazozalishwa katika vyuo vikuu na vya kati ziendane na maendeleo yetu ya uchumi na ndio uwe nyenzo kuu ya kugawanya fedha za mkopo wa Elimu ya Juu. Hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la

ajira kwa kujiajiri wao wenyewe ili kuondokana na wahitimu kuwa na taaluma ambazo hazina soko.

**7.2. *Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** Vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa JKT wapo wa aina 2. Wapo wanaojiunga kwa mujibu wa Sheria na wapo wanaojiunga kwa kujitolea. Changamoto kubwa iliyopo ni kukosekana kwa ajira mara baada ya kumaliza muda wao wa miaka mitatu hasa hawa ambao wako katika kundi la kujitolea.

**NA KWA KUWA,** Serikali kupitia Wizara zake kama Wizara ya Kilimo inataka kuanzisha mchakato wa kuwapatia mitaji na mashamba vijana mbalimbali ili kujikwamua kimaisha na hatimaye kuchechemua uchumi. Aidha, Kampuni ya Suma JKT huajiri wafanyakazi kila mwaka kwa kutoa Tangazo hadi kwa wale ambao hawapo makambini.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia masuala yafuatayo: -

(i) Kwanza ni kwa Wizara ya Kilimo kuanza na vijana ambao wako katika makambi mbalimbali ya jeshi kwa kujitolea;

(ii) SUMA JKT wanapotangaza ajira za walinzi waanze kwanza na Vijana waliopo katika makambi ya jeshi wenye sifa stahiki ambao wanakaribia kumaliza mikataba na endapo hawatoshi ndipo watafutwe wengine.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua hii itasaidia kuondoa changamoto ya ajira kwa vijana wanaoenda jeshini kwa kujitolea.

**7.3. *Mifumo ya TEHAMA ya kukusanyia mapato kutosomana***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** bado kuna changamoto ya kutosomana kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Mapato na Taasisi pamoja na Wizara kama vile TPA na Ofisi ya Rais Tamisemi. Kutosomana kwa mifumo kumesababisha kupotea kwa mapato ya Serikali na Ukaguzi wa Kodi (Tax Audit) kuwa mgumu.

**NA KWA KUWA**, Serikali imekuwa ikiendelea kujenga mifumo mbalimbali bila kuihuisha ili isomane na hivyo bado changamoto ya upotevu wa mapato ya Serikali inaendelea kuwepo.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia masuala yafuatayo;

(i) Serikali kufanya uchambuzi wa mifumo yote ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato ili kuihuisha pamoja na kuiunganisha ili isomane. Hatua hii itapunguza upotevu wa mapato ya Serikali; na
(ii) Serikali kutenga jumla ya **Shilingi billioni 560** kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili wahuishe mifumo yao na kuiunganisha kwa ajili ya kukusanya mapato ya Serikali kikamilifu.

**7.4. *Mkopo wa Asilimia 10 kwa Wanawake, Vijana wa Watu Wenye Ulemavu.***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 inaitaka kila Halmashauri kutenga **asilimia 10** ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**NA KWA KUWA,** suala hili ni takwa la kisheria Kamati imebaini kuwepo na masuala yafuatayo yanayokiuka sheria:

i. Kuna Halmashauri zimekuwa zikijumuisha deni la kutotenga **asilimia 10** kwa mwaka wa fedha uliopita kwenye **asilimia 10** ya mikopo ya mwaka husika ili ama zionekane zimevuka lengo au zionekane zimefikia lengo tofauti na sheria inavyotaka; na
ii. Halmashauri nyingine zimekuwa zinatoa chini ya kiwango cha asilimia 10 ya mapato ghafi, Mfano wa Halmashauri hizo ni Halmashauri ya Kibaha asilimia 3, Halmashauri za Wilaya ya Morogoro, Chato, Bukombe, Masasi na Nkasi zilichangia asilimia 5.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia Halmashauri zote kufuata utaratibu wa kisheria uliopo katika kutenga **asilimia 10** ya mkopo kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, hatua zichukuliwe kwa zile Halmashauri ambazo hazitafikia lengo hali ikiwa imekusanya mapato.

**7.5. *Shirika la Hifadhi la Taifa - TANAPA Kuongezewa Hifadhi***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** mwaka 2019 Serikali iliongezea Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) hifadhi mpya 6 na hivyo kufanya idadi ya hifadhi zinazosimamiwa na TANAPA kuwa 22. Vilevile, TANAPA iliongezewa Ofisi za Kanda 4, Vituo 5 vya Malikale na Ofisi Unganishi. Pamoja na ongezeko hilo la majukumu mapya bajeti ya uendeshaji ya Mamlaka ilibaki ile ile.

**NA KWA KUWA** hatua hii imeathiri utekelezaji wa majukumu ya Shirika kwa sababu ya ukomo wa bajeti ambao umekuwa hauendani na ongezeko la majukumu ya Shirika. Mfano bajeti ya uendeshaji kwa mwaka 2019/2020 ilikuwa ni **Shilingi bilioni 105** katika mwaka huo huo eneo la usimamizi liliongezeka kutoka kilometa za mraba 47,471 hadi kufikia kilomita za mraba 104,578. Aidha, pamoja na ongezeko hilo, bajeti ya uendeshaji wa Shirika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebakia sawa na iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambacho ni kiasi cha **Shilingi bilioni 105** ukilinganisha na mahitaji halisi ya fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 222** na Fedha za Maendeleo kiasi cha **Shilingi bilioni 120** kwa mwaka.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia TANAPA kuongezewa kiasi cha fedha **Shilingi bilioni 170** katika bajeti ya mwaka 2023/2024**.** Kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 100** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 70** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hatua hii itawezesha TANAPA kukidhi mahitaji ya msingi. Hatua hii sio tu itawezessha TANAPA kutekeleza shughuli zake lakini vilevile tunaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia *Royal Tour* katika kuongeza utalii na kuvutia wawekezaji nchini katika sekta hiyo.

### *7.6. Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura (Contigency Fund)*

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** Sheria ya Bajeti sura ya 439 katika vifungu vya 35, 36,37,38 na 39 inaelezea kuhusu umuhimu wa Serikali kuwa na mfuko wa dharura (Contigency fund) pamoja na utaratibu wa matumizi ya fedha katika Mfuko huo.

**NA KWA KUWA,** Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kifungu namba 140 (1a-b) na (2) imesisitiza juu ya uanzishwaji wa mfuko wa dharura pamoja na taratibu za uendeshaji wa mfuko huo.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali ianzishe mfuko wa dharura na kutenga fedha kama sheria inavyoelekeza kwa ajili ya kukabiliana na dharura zitakazojitokeza.

**7.7. *Usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA,** katika kipindi cha Julai hadi Juni 2022, Serikali ilikusanya jumla ya **Shilingi trilioni 36.92** kutoka vyanzo vyote sawa na **asilimia 97.2** ya bajeti nzima ya Serikali.

**NA KWA KUWA,** Katika mwaka wa fedha 2021/2022 hamisho la fedha ndani ya fungu (Reallocation Within Votes) kwa mafungu mengi ya Serikali limezidi **asilimia 7** kinyume na Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015. Aidha, kati ya mafungu 86 yaliyofanyiwa uhamisho wa fedha mafungu 50 yalizidi **asilimia 7** likiwemo fungu namba 46 ambalo uhamisho wake ni **asilimia 63.33** ya Bajeti iliyotengwa. Hali hii inamaanisha kwamba matumizi haya akisi mapato yaliyopangwa (tazama **kiambatisho B)**.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe uhamisho wa fedha kati ya mafungu na ndani ya mafungu unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti na kanuni zake.

**7.8.** ***Kuiwezesha Kampuni ya Taifa ya Mbolea (Tanzania Fertilizer Company – TFC)***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** mahitaji ya mwaka ya mbolea ni tani 698,260 mbolea ambayo inapatikana nchini kwa ajili ya matumizi ni tani 480,848 sawa na upungufu wa tani 217,412 hivyo kuna wakulima wengi wanakosa mbolea za kupandia na kukuzia kutokana na uhaba. Aidha, uzalishaji wa ndani wa mbolea ni **asilimia 6** tu ya mahitaji yote.

**NA KWA KUWA** Serikali imetenga **Shilingi bilioni 150** kwa ajili ya ruzuku ya mbolea kwa wakulima wote nchini. Vilevile Serikali ilianzisha Kampuni ya Mbolea Tanzania (Tanzania Fertilizer Company – TFC) mwaka, 1968 yenye madhumuni ya Kuzalisha, kuhifadhi na kusambaza aina zote za mbolea; pamoja na Kuagiza, kununua, kuuza ndani na nje ya nchi bidhaa za mbolea aina zote zinazozalishwa na kampuni au Watengenezaji wengine.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali iiwezeshe Kampuni ya Taifa ya Mbolea (TFC) kwa mtaji wa **Shilingi bilioni 60** ili iweze kununua mbolea toka kwa wazalishaji moja kwa moja kuliko hali ilivyo sasa, ambapo Kampuni hii inalazimika kununua mbolea toka kwa mawakala.

**7.9.** ***Kurejesha Tume ya Taifa ya Mipango (Planning Commission)***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Tume ya Taifa ya Mipango katika nchi yoyote ndio chombo kikuu cha kupanga maendeleo na kuratibu masuala yote yanayohusu mipango ya nchi na uzoefu unaonesha ili Taifa liendelee ni lazima liwe na Tume ya Mipango.

Mfano Mataifa ya Asia (Asian Tigers) yamefanikiwa kimaendeleo kwa kuwa na Tume za Mipango thabiti.

**Mheshimiwa Spika, NA KWA KUWA** Serikali ipo katika mchakato wa kuirejesha Tume ya Taifa ya Mipango.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba pamoja na dhamira ya Serikali ya kuirejesha Tume ya Taifa ya Mipango, Serikali irejesha Sheria ya Tume ya Mipango "Planning Commission Act (Cap 314)" kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 kama ilivyoondolewa kupitia Sheria hiyo ya Mwaka 2018 wakati ikiendelea na mchakato mwingine.

**7.10. *Nyongeza ya Fedha kwa Ajili ya Kutekeleza Miradi ya Kipaumbele ya Sekta ya Anga***

**Mheshimiwa Spika, KWA KUWA** Serikali imewekeza katika Sekta ya anga ikiwa ni pamoja na ununuzi wa takribani ndege 11 kupitia Shirika la Ndege la Taifa (ATCL) ili kuvutia kuvutia uwekezaji na watalii. Aidha, ili juhudi hizi zizae matunda yaliyotarajiwa lazima ziende sanjari na kuwa na miundombinu wezeshi katika viwanja vyetu vya ndege. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) ambayo ndio yenye jukumu la kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya Ndege nchini inakabiliwa na changamoto kubwa ya kibajeti.

**NA KWA KUWA**, Kukosekana kwa miundombinu muhimu kunasababisha ndege za ATCL kulazimika kupaki inapofika muda wa usiku kutokana na sababu mbalimbali. Mathalani kukosekana kwa taa katika viwanja vya ndege na kukosekana kwa mifumo muhimu pamoja na minara ya kuongozea ndege (Control Tower). Hali hii inasababishwa na

kukosekana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo hasa za uendelezaji wa viwanja vya ndege.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kuongezewa bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024 ya jumla ya **Shilingi bilioni 45,559,857,841**, kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria **Shilingi bilioni 20,280,465,539**;
(ii) Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la Abiria na Miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza **Shilingi bilioni 7,224,737,722;**
(iii) Usimikaji wa Mfumo wa Taa za Kuongozea Ndege (AGL System) katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha **Shilingi bilioni 7,083,654,580;**
(iv) Ujenzi wa Jengo la Kuongoza Ndege (Control Tower) na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba **Shilingi bilioni 2,220,000,000;**
(v) Ujenzi wa Jengo la Abiria na Miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara **Shilingi bilioni 7,251,000,000**; na
(vi) Ununuzi wa Mtambo wa Zimamaoto kwa Kiwanja cha Ndege cha Arusha **Shilingi bilioni 1,500,000,000**.

## SEHEMU YA NANE

## 8.0. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 8.1. *Mafanikio katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipata mafanikio yafuatayo; -

(i) Kupokea, kujadili na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria mbalimbali za kodi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 iliyokuwa na jumla ya Sheria 38;
(ii) Kupitia mgawanyo wa fedha za mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa wa **Shilingi trilioni 2.4** (Extended Credit Facility – ECF) pamoja na utekelezaji wa miradi kupitia mkopo huo;
(iii) Kufanya mdahalo wa Bunge zima kuhusu masuala ya uchumi pamoja na kujadili mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya mwaka wa fedha 2022/2023;
(iv) Kamati ilishauri Serikali na ilikubali kuanzisha utaratibu wa utozaji wa kodi wa kijiditali;
(v) Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuongeza fedha za Maendeleo kwenye fungu 45 la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na fungu 23 Mhasibu Mkuu wa Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023;
(vi) Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuanzisha mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Manunuzi Sura ya 410;
(vii) Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuiongezea Wizara ya Kilimo bajeti hadi kufikia kiasi cha **Shilingi bilioni 954** katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023;
(viii) Kamati iliishauri Serikali na ikakubali kuanzisha mchakato wa utwaaji wa maeneo yanayolizunguka Bunge la Tanzania;
(ix) Kamati iliishauri Serikali kuhusu mapendekezo juu ya mabadiliko ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 (East Africa Customs Management Act - ECMA);
(x) Kamati iliharakisha mchakato wa kufanya marejeo ya mikataba 39 ya miradi ya umeme vijijini

inayotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) baada ya kukwama kwa muda mrefu;

(xi) Kusimamia utekelezaji wa miradi kupitia mifuko iliyozingirwa (Ring Fenced Fund), Mfuko wa Maendeleo ya Reli, Mfuko wa Maendeleo ya Barabara, Mfuko wa Maji, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) na Mfuko wa Maendeleo ya Umeme Vijijini;

(xii) Kuwasilisha Bungeni jumla ya Taarifa sita. Taarifa hizo ni kama ifuatavyo:

a) Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka unaoishia 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023;

b) Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Mfuko wa Bunge, Mahakama na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mifuko hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023

c) Taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2021, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23;

d) Taarifa kuhusu Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2022 (The Finance Bill, 2022);

e) Taarifa kuhusu Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Fedha Na. 13 wa mwaka 2022; na

f) Taarifa kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2023/2024;

(xiii) Kamati ilifanikiwa kupokea jumla ya Taarifa 64 ambapo ilizijadili na kuzichambua na kuzitolea mapendekezo mbalimbali;

(xiv) Kamati ilifanikiwa kukutana na Wizara za Serikali zaidi ya 15, Mamlaka zaidi ya 13, Taasisi zaidi ya 12 pamoja na Kampuni zaidi ya 4 za Serikali ili kupitia, kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri katika masuala mbalimbali; na

(xv) Kamati ilifanikiwa kukutana na wadau zaidi ya 33 kutoka Sekta binafsi na Taasisi za utafiti na kupokea, kujadili na kusikiliza Maoni na Mapendekezo mbalimbali kuhusu masuala ya kodi na Sera za fedha.

### 8.2. *Changamoto katika Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali, Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatazo: -

### 8.2.1. Changamoto ya Kanuni ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Muswada wa Sheria ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Kanuni ya 93(2) inaelekeza Muswada wa Sheria unapaswa kumfikia Katibu wa Bunge katika muda usiopungua siku ishirini na moja kabla ya Muswada huo kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza isipokuwa kwa Muswada uliowasilishwa kwa hati ya dharura. Uzoefu unaonesha kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha haujawahi kutekeleza matakwa hayo ya kikanuni kwa zaidi ya miaka 4. Hivyo, husababisha Kamati kuwa na kipindi kifupi cha kuchambua, kujadili na kushauri mapendekezo ya Muswada huo

kabla haujawa Sheria. Kamati inashauri kwamba, Serikali itekeleze matakwa ya Kanuni ili Kamati iweze kutekeleza shughuli yake kikamilifu.

**8.2.2. Changamoto ya Muda wa uwasilishaji wa Taarifa ya Kamati, Taarifa kuhusu Hali ya Uchumi, Mpango na Bajeti ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 69(c) ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020 inaelekeza kwamba Mwenyekiti anayewasilisha maoni ya Kamati atayawasilisha kwa muda usiozidi dakika thelathini. Kutokana na ukubwa wa Taarifa ya Kamati kuhusu Hali ya Uchumi, Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka husika, muda wa dakika thelathini hautoshi kwa Kamati kuwasilisha maoni yake kikamilifu. Kamati inapendekeza ni vyema Kanuni hii ikafanyiwa marekebisho ili kuongeza muda kutoka dakika thelathini ilivyo hivi sasa hadi dakika sitini wakati wa usomaji wa Taarifa hii.

**8.2.3. Ucheleweshwaji wa Taarifa kutoka Serikalini**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni 136(8) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imejiwekea utaratibu wa kuzitaka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kuwasilisha Taarifa zake Ofisi ya Bunge si chini ya siku tatu kabla ya kikao husika. Pamoja na utaratibu huo kumekuwa na changamoto ya uwasilishaji wa Taarifa mbele ya Kamati, hivyo kupelekea Kamati kushindwa kuchambua na kuishauri Serikali kikamilifu. Kamati inashauri kwamba ni vyema Serikali ikafuata utaratibu wa kuwasilisha Taarifa siku tatu kabla ya kikao

husika ili kuiwezesha Kamati kupata muda wa kutosha wa kuchambua na kushauri juu ya Taarifa hizo.

**8.2.4. Tofauti ya Takwimu baina ya Wizara na Taasisi za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kwamba kuna tofauti ya takwimu zinazowasilishwa kati ya Wizara na Taasisi za Serikali. Mfano, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliwasilisha Taarifa kuhusu idadi ya vijiji vilivyopata Umeme ni 10,312 badala ya 9,787 kama ilivyowasilishwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA). Kamati inashauri Serikali kuwa na mfumo unaotoa Taarifa sahihi ili kuondoa mkanganyiko wa tofauti ya takwimu katika eneo linalofanana.

**SEHEMU YA TISA**

**9.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru kwanza wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mb Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkiipatia Kamati na hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mb kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakitoa kwa Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Dkt. Natu Mwamba Katibu Mkuu ambao walishirikiana na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** pia napenda kumshukuru Mhe. Omari Kigua, Mb na Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambao umesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inasimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifauatavyo: -

1. Daniel Baran Sillo, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb
4. Mhe. Issa Jummanne Mtemvu, Mb
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
9. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
10. Mhe. Shally Josepha Raymomd, Mb
11. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
12. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb
13. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb
15. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
16. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
17. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb
18. Mhe. Abbas Gulam Tarimba, Mb
19. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb
20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb
21. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb
22. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya Uongozi thabiti wa Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* Katibu wa

Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Emmanuel Rhobi, Makatibu wa Kamati Ndg. Maombi Kakozi, Ndg. Wilfred Akasi, Ndg. Lilian Masabala na Ndg. Trifina Tanzania pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Fadhati Kamote kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo katika Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba shughuli za Kamati zinafanyika kama zilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Daniel Baran Sillo, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
06 Februari, 2023

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa taarifa yako. Sasa tunaanza uchangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza kabisa atakuwa ni Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo na baadae Mheshimiwa Esther Nocholas Matiko na Mheshimiwa Felista Deogratius Njau. Tuanze na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu kuhusu taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1972, aliyekuwa Mfalme wa Dubai wakati huo, Sheikh Rashid Bin Maktoum, alikuwa na ndoto ya kujenga bandari kubwa sana katika ukanda ule wa Ghuba ya Uajemi na Mashariki ya Kati kwa ujumla lakini kwa bahati mbaya washauri wake kutoka Uingereza walimwambia hapana mradi huu hautakuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya washauri wake kutoka Uingereza walimwambia hapana mradi huu hautakuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi. Sheikh Maktoum alikataa alisema hapana sikubaliani na ushauri huu. Hata kama mradi huu hautakuwa maslahi ya kiuchumi nitautekeleza kwa sababu ninaamini wajukuu na watoto wangu hawataweza kuutekeleza mradi huu miaka mingi ijayo kwa sababu gharama zake zitakuwa zimepanda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajifunza nini? Tunachojifunza ni kwamba, tukitaka kupiga hatua ya maendeleo ya haraka kama Taifa tunapaswa kuwa na viongozi, na ninaposema viongozi sina maana ya viongozi wa kitaifa nina maana ya Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa; tunahitaji kuwa na viongozi wa aina gani? tunahitaji mambo mawili. Kwanza tunahitaji viongozi wenye maono makubwa, wanaozingatia maslahi ya kizazi kinachokuja kuliko kizazi cha sasa. Pili tunahitaji viongozi wenye ujasiri wa kufanya maamuzi magumu kwa sababu kutakuwa na watu maamuzi hayo wanayatilia shaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nayasema haya; kwa zaidi ya miaka 15 tumekuwa tukizungumza utekelezaji wa mipango ya utekelezaji wa miradi mikuu miwili, mradi wa makaa ya mawe na chuma kule Liganga na Mchuchuma pamoja na mradi wa kusindika gesi asilia kule Lindi. Kwa bahati mbaya katika kipindi cha miaka 15 mpaka leo miradi hii haijatekelezwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, nadhani kama miradi hii ingetekelezwa miaka 15 iliyopita, Taifa letu lingepata maslahi makubwa sana ya kiuchumi, na nitayataja. Kwanza gharama za miradi hii zingekuwa chini sana kuliko ilivyo leo, pili tungetekeleza mradi wa gesi asilia miaka 15 iliyopita leo tungenufaika na soko kuu sana linalotokana na uhaba wa gesi asilia duniani unaotokana na vita vya Ukraine na Urusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tungetekeleza mradi wa gesi asilia miaka 15 iliyopita leo tungepata gesi nyingi sana inayotumika katika kuendesha mitambo na magari na hatimaye kupunguza uagiziaji wa mafuta kutoka nje. Lakini kwa upande wa chuma leo tungekuwa na chuma cha kutosha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa reli ya kati. Hivi sasa Taifa letu linatumia kiasi kikubwa sana za fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza chuma kinachohitajika katika ujenzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tungetekeleza miradi miaka 15 iliyopita ingetusaidia sana kwa sababu naamini miaka mitano mpaka 10 inayokuja mahitaji ya gesi asilia duniani yatakuwa yamepungua sana, kwa maana hiyo gesi asilia haitakuwa na faida kubwa kwa Taifa letu. Kwa nini nasema hivyo? Hivi sasa mjasiriamali mkuu sana duniani anayeitwa Elon Musk ameshaanza uzalishaji wa magari yanayotumia umeme. Jambo hilo likifanyika kwa kiwango kikubwa gesi haitakuwa na matumizi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mataifa mbalimbali tayari yameshaanza utafiti hivi sasa wa namna ya kutumia gesi ya hydrogen kama chanzo kikuu cha nishati. Jambo hilo likifanyika gesi asilia ya Tanzania haitakuwa na maslahi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa ushauri wa mwanadamu anayeaminika kuwa mtu mwenye busara kubwa sana kupata kutokea hapa duniani Mfalme Suleiman. Mfalme Suleiman aliwahi kusema maneno haya, na sisi kama viongozi tunapaswa kuyazingatia; akasema hakuna wakati mzuri wa kutekeleza mambo makubwa na muhimu kwa wanadamu kuliko sasa hivi. Tusisubiri muda unaokuja kwa sababu huo muda utakaokuja hatuna uhakika kwamba kila kitu kitakuwa sawa. Lakini, mwisho hatujui Mwenyezi Mungu amepanga lini na nini, kesho na kesho kutwa, kwa hiyo tunapaswa kutekeleza leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali tunapaswa kufanya kila linalowezekana sisi kama Taifa tuitekeleze miradi hii sasa kwa sababu hatujui kitakachotokea baada ya miaka mitano au kumi ijayo, linalowezekana leo lisingoje kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo aweze kuchangia.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anayoifanya, amekuwa kinara kwa matendo kukuza diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kuhusu diplomasia ya uchumi kwa wananchi bado iko chini, hakuna uelewa, kuanzia wizarani, mikoani, wilayani mpaka vijijini, hasa maeneo ya mipaka ambako wafanyabiashara wengi hawajapewa elimu kuhusu diplomasi ya uchumi, kwahiyo bado wanafanya shughuli zao za kiuchumi kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukuza diplomasia ya uchumi, Wizara ya Kilimo, Viwanda na Biashara, Wizara ya Ulinzi pamoja na Maliasili lazima viwe *coordinated* pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Wizara ya Kilimo ina mpango wa kuanza hizi *block farming* ambazo zinaenda kuanzishwa nchi nzima, ndio mwanzo pekee ambao tunahangaika vijana hawana ajira. Wale vijana wanaotoka JKT kwa sababu watakuwa tayari wameshajifunza kilimo, kufanya kazi kwa bidii, wakishatoka JKT wapelekwe kwenye hizi *block farming* ambazo zinaanzishwa na Wizara ya Kilimo. Na hii Wizara ifanye tathmini kwa yale mazao ambayo yana soko. kwa mfano kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini waje waanzishe *block* za kulima mahindi kwa sababu tayari wananchi wana uelewa wa uzalishaji wa mahindi. Waje na *block* za kuanzisha ngano, soya, alizeti pamoja na Ukanda wa Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika wafanye utafiti kuanza hizi *block* hata kilimo cha miwa. Na kwenye hizo *block* waanzishe kutengeneza viwanda vidogo vodogo ambazo block wakishatoa mazao yao tusiuze mazao ghafi, tuweke mashine, viwanda ili ziweze ku-*process* tuuze nje mazao yanye thamani kamili, tusiuze mazao ambayo yamelimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hizo *block farming* ifike mahali tupangiwe taratibu na kanuni, hizi *block farming* ziwe *connected* na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya watu wakitoka JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi Mheshimiwa Rais atazipeleka kwenye *block farming,* ukishazipeleka kule watapelekewa raia ambao hawana utaalamu na hivyo hizi *block farming* zitageuka kama ndiyo sehemu ya kujifunzia. Kwa hiyo JKT waunganishwe na hizi *block farming* ili waende kuwa wasimamizi wa hizi *block farming,* kwa sababu fedha nyingi zitaenda, wataenda kuanza kujifunza kulima. Lakini zikiunganishwa na Jeshi la Ulinzi tutapata mazao, mashine zitapelekwa viwanda vidogo vidogo wananchi wa kule wakiungana na wanajeshi kazi itafanyika vizuri kwa bidii. Wizara ya Viwanda na Biashara itafute masoko. Kwa hiyo hizi *block farming* zitengenezwe kulingana na aina ya masoko ya mazao yanayohitajika na nchi jirani ili kukuza diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa imeongelea kuhusu mipaka. Ukitaka kutazama kwa undani kabisa Wabunge wengi wamelalamika uzalendo unapungua na tukiona nchi jirani kuna changamoto ya uhalifu hasa maeneo ya *buffer zone*. Maeneo ya mipakani kuna uhalifu unaojirudiarudia. Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Ardhi watengewe bajeti ili waweze kwenda kuimarisha miundombinu ya kuweka bicon kwenye mipaka na barabara zile za kiuchumi pamoja na za kiulinzi ili vyombo vyetu vya ulinzi vinapofanya kazi ya ulinzi mawasiliano yaweze kufika kwa urahisi, kwa sababu wahalifu wengi wanakaa maeneo ya *buffer zone* maeneo ambayo ndiyo vichaka vya uhalifu unaoendelea, hasa katika maeneo yale ambayo shughuli za kiuchumi zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wafanyabiashara wafanye vizuri maeneo ya mipaka Wizara ya Ardhi pamoja na Miundombinu watenge na waainishe barabara za kiuchumi, *beacon* ziwekwe ili mambo yaende vizuri. Kwa sababu hizi wizara; kwanza nizipongeze kwanza, zinafanya kazi kubwa mno; Wizara ya Ulinzi, vyombo vya ulinzi vyote kwa pamoja amani na utulivu tulionao Tanzania ni kwa sababu haya majeshi yetu, Jeshi la Polisi, vyombo vya ulinzi vinafanya kazi

usiku kucha; na hata sisi wenyewe Bungeni tunakaa kwa usalama kwa sababu ya vyombo vya ulinzi vinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu anaendelea kutoa ajira kwenye hivi vyombo ili viendelee kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje na Usalama hizi wizara bado zina bajeti finyu sana. Nashauri Wizara ya Fedha itenge bajeti ili iweze kuipatia hivi vyombo vya ulinzi pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Sehemu kubwa ina changamoto kubwa sana. Mheshimiwa Rais anahangaika huko nje kutafuta masoko lakini ukiangalia hata makazi ya balozi pamoja na ofisi zetu huko nje, pamoja na viwanja vingi havijaboreshwa. Muonekano wa kuvutia diplomasia ya uchumi pamoja na watalii ianze kuonekana nje. Kwa hiyo wizara hii ipewe fedha ili iweze kujenga miundombinu mizuri na kuweza kutangaza Tanzania nje kwa muonekano wa viwanja vyetu pamoja na ofisi.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilitengewa takribani bilioni 48.5; lakini mpaka tunafikia sasa katika kipindii chote cha miaka 5 wizara hii ilikabidhiwa bilioni tisa tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo unaipokea taarifa.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili. Hii Wizara ya Mambo ya Nje haijapata fedha kwa muda mrefu, imesahaulika. Kamati ilienda Ethiopia tukakuta kuna viwanja ambavyo bado havijajengwa, Kamati ikaomba miadi na Mheshimiwa Rais wa Ethiopia, Mheshimiwa Rais kwa kuheshimu diplomasia na nchi yetu akaahirisha safari zake akakutana na Kamati. Akaturuhusu na akatuhakikishia viwanja hivyo ambavyo vingeweza kuchukuliwa virejeshwe na akashauri pajengwe ubalozi mzuri ambao utarudisha mahusiano kati ya Tanzania na Ethiopia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo kwa mchango wako lakini kwa kuzingatia muda. Nilimwita Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko wakati huo Mheshimiwa Felister Deogratius Njau ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru dakika tano ni chache lakini nitajitahidi kuweza kuchangia nitakachoweza. Kwanza kabisa napongeza maoni ya Kamati zote mbili na hasa Kamati yangu ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kuhusu kwenye mwenendo wa ukusanyaji wa mapato. Ni dhahiri kwamba kwa malengo ambayo wamejiwekea Serikali wanafikia asilimia 95 mpaka 96, kwa maana ya trilioni 24, mpaka 25. Lakini kiuhalisia kama tukiweza kudhibiti mianya yote ya upotevu wa mapato kama tukiweza ku-*exhaust* rasilimali tulizonazo kama nchi tuna uwezo wa kukusanya hata zaidi ya trilioni 40 na kuwa sio tegemezi kwa washirika wa maendeleo tuna uwezo huo na nitaenda kubainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia changamoto ambazo zimeainishwa kwenye taarifa yetu ambazo zinapelekea upotevu wa kodi. Mathalani tuna hizi mashine za *EFD;* ni kweli kabisa tafiti zikifanyika kwa kina, na mimi mwenyewe nina ushahidi na nimeshasema mara kadhaa kwenye kamati; wafanyabiashara wana hizi *EFD* machine lakini *in real sense* hawazitumii, *at a time*. Ukienda wanakwambia ni mboovu, wakati mwingine ukienda unamkuta mfanyakazi anakwambia bosi amefungia. Kwa hiyo hizi zote zinasababisha upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tunaelezwa kwamba pamoja na kwamba walipa kodi ni wachache sana kwa Taifa letu tunaambiwa wako milioni nne, lakini kati ya hao milioni nne wanaolipa kodi ni milioni mbili tu. Sasa kama ni hao milioni mbili wanalipa tunafika hizi trilioni 24 mpaka 25. Tukiziba mianya yote ya upotevu wa fedha hata hiyoo trilioni 40 niliyosema ni chache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo pia linapoteza haya mapato. Taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2021 imeonesha kabisa kwamba kuna malimbikizo makubwa sana ya madeni ya kodi ambayo hayakusanywi. Inaonesha mwaka 2019/2020 madeni ambayo yalikuwa hayajakusanywa ni trilioni 3.86 ilivyokuja 2020/2021 yakaongezeka kwa asilimia 96 na kufikia trilioni 7.54. Haya maseni kama yangekuwa yamekusanywa yangeweza kuongezeka sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto nyingi kubwa, tungekusanya haya mapato ya trilioni 7.5 mathalani yakaenda kwenye mfuko wa barabara ambao unahitaji trilioni 2.4 tu kuhakikisha wanaimarisha miundombinu ya barabara, kwa maana ya *TANROADS* na *TARURA*. Leo mvua zikinyesha hapapitiki, vijijini si mijini. Trioni 2.4 tu ukizichomoa kwenye hizo trilioni 7.5 ambazo *CAG* ameziainisha, hapa kama yangekusanywa kwa wakati hayo madeni ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu yangeweza kujenga barabara ambazo kwenye utekelezaji wa mpango inaonyesha kuna barabara za zaidi ya miaka 10 ziko kwenye upembuzi yakinifu na uchambuzi zingine zimejengwa kilomita kadhaa na kutelekezwa. Tukiweza kufanya kwa uadilifu makusanyo haya tunaweza kujenga Taifa

Mheshimiwa Mwenyekiti. Lakini ukichukua trilioni mbili tu ukapeleka kwenye sekta ya afya ambapo kwa sera ya afya tunataka kila kijiji kiwe na zahanati na kila kata iwe na kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikopa tu alichokisema Mheshimiwa Kakunda juzi milioni 100 inajenga zahanati nzuri tu katika trilioni 2 hizi uchukue milioni 800 tu upeleke kwenye zahanati utajengewa zahanati 8000. Zahanati 8000 unapeleka zahanati 7000 vijijini na zahanati 1,000 unapeleka kwenye mitaaunakuwa umetatua pakubwa sana kati ya vijiji 12,000 kulinganisha na ambayo tuko nayo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua trilioni 1.2 ambayo inabaki ukapeleka kwenye vituo vya afya una uwezo wa kujenga vituo vya afya 2,400 katika kata 3,900 tulizonazo. Ukiangalia sasa hivi nii chache sana zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nishati walikuja kwenye bajeti wakasema kwa bajeti ambayo tunawatengea sasa hivi itawachukua takribani miaka 18 kuweza kupeleka mradi wa *REA* kwenye vitongoji na vijiji; kwa bajeti ambayo ni ya trilioni sita tu iliyoko mbele. Ukichukua tu trilioni 3.14 kutoka kwenye hizi ambazo zimeachwa kukusanywa kwa muda wote huu tunaweza kupunguza kwa *gap* kubwa sana na wananchi wakapata umeme wa *REA* na wakakuza uchumi, wakazidisha usalama kwenye maeneo yetu na kuongeza kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunashindwa kutekeleza haya? Kamati imeeleza vyema, kwamba *TRA* au Serikali ihakikishe inakuwa na mifumo thabiti ya kudhibiti upotevu wa mapato unaofanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine wafanyakazi tulionao wanahitajika 8,000 wako 6,000. Juzi Kamati ya Bajeti ilitembelea Uturuki. Kule *TRA* yao wana wafanyakazi 28,000. Leo tungekuwa na wafanyakazi toshelezi hapa tuka-*invest* kwenye rasilimaliwatu hawa watu ambao wana *EFD* hawazitumii, hawa watu wanaokwepa kulipa kodi ambao wako kwenye kanzidata wangeweza kulipa kodi, tuajiri walao tufike 8,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuajiri wa kudumu na wengine wa kimkataba, tufanye kama *piloting* tu. Hebu tuweke kuna watu wengi wamesoma mambo ya kodi tuwaajiri kwa mkataba wa miaka miwili au mitatu tuone mapato yatakusanyika mara ngapi. Tukifanya hivi tunapoteza mapato wakati tungewekeza kwenye rasilimaliwatu tungeweza kukusanya fedha nyingi na kupeleka kwenye maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri sana Serikali, na niliombe hata Bunge lako hili liazimie, katika vipaumbele vyetu walau tuwezeshe *TRA* wawe na wafanyakazi wa kutosha, wawe na mifumo imara ya kuweza kugundua huu upotevu wa fedha. Pia tunaambiwa kuna wafanyabiashara wengine ambao bado hawajaunganishwa kwenye mfumo wa kidigitali wa kufanya marejesho ya kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri sana Serikali na niliombe hata Bunge lako hili liazimie katika vipaumbele vyetu walau tuwezeshe *TRA* wawe na wafanyakazi wa kutosha, wawe na mifumo imara ya kuweza kugundua huu upotevu wa fedha. Pia tunaambiwa kuna wafanyabiashara wengine ambao bado hawajaunganishwa kwenye mfumo wa

kidigitali wa kufanya marejesho ya kikodi. Sasa kama ujamuunganisha ni *definitely* Mapato yanapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania ambao wanafikika huko chini maskini kabisa lakini unakuta wanabanwa wanalipa vikodi vidogo vidogo ndiyo tunaweza kufanya hivyo, wakati tuna mianya mikubwa tunaipoteza ambayo tungekusanya nakuweza kulisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mfumuko wa bei kwa haraka sana. Ukiangalia mfumuko wa bei kwenye kapu la bidhaa linalotumika kupima mfumuko wa bei. Vyakula na vinywaji visivyo na kilevi vinauzika takribani asilimia 28.2, usafiri na wenyewe una asilimia 15 pale, nyumba, gesti na nini vina asilimia 14 hivyo ndiyo vimebeba uzito mkubwa. Ukiangalia Januari, 2022 na leo Januari, 2023 nilijaribu tu kupita kwenye masoko kuangalia. Mfano, mwaka 2022 maharage yalikuwa kilo shilingi 2,000 lakini leo ni shilingi 3,600 na kuna mengine mpaka shilingi 5,000 inategemea na *category.* Ukija kwenye mchele ulikuwa shilingi 1,500 mpaka shilingi 1,800 mpaka shilingi 2,000, leo ni shilingi 3,600 mpaka shilingi 4,000 inategemea pia na *category.* Ukija kwenye sembe ndiyo kabisa ime-*shoot* pakubwa sana. Ukienda kwenye ngano kilo 25 ilikuwa shilingi 27,000 leo ni shilingi 45,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ni magumu sana, Watanzania *purchase power* yetu iko chini sana. Leo ukitembea mtaani ukakuta watu wana *depression,* wana afya ya akili, *one of the reasons* ni hii, hebu tujitahidi tuone ni jinsi gani tunaweza tukafanya tufanye *standardizations* ya bei hizi kwa Watanzania. Mtanzania wa kawaida hawezi aka-*afford,* mimi mwenyewe tu hapa *at a time* nikipewa *bill* naona hela nyingi sana, asikwambie mtu Mtanzania maskini wakule kijijini, anaumia sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua umenivumilia muda ni mchache, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. Nilimwita Mheshimiwa Felista Deogratius Njau wakati huo wafuatao wanajiandaa; Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis pamoja na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwa uchache kulingana na dakika zilizoko mbele yangu. Kwanza kabisa nipongeze Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa ya kutukuka na ya kizalendo wanayoifanya katika Taifa letu. Natangulia kupongeza kwa sababu vyombo hivi havina bajeti ya kutosha lakini kazi wanayoifanya ni kubwa sana. Nafikiri wangekuwa wanafanya kazi ambayo haina mashiko tusingekuwa tuko salama leo. Kwa heshima hii nawapa kwa sababu wanafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda moja kwa moja kwenye Bajeti ya Maendeleo. Tumesikia maoni ya Kamati, nami naungana nayo asilimia 100, lakini kwa masikitiko yangu makubwa, tumeangalia Ngome fungu namba 28 wamepokea asilimia 17.74 tu. Kwenye hii Jeshi letu liko hoi bin taabani, lakini wajibu wake ni mkubwa mno kulingana na bajeti ambayo wameipokea. Tunaelekea Bunge la Bajeti na hawa watu hawajapokea hata robo ya bajeti yao, ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua JKT ni eneo ambalo kila mtu anaangalia baada ya Taifa letu kuonekana kwamba ajira imekuwa ni duni kwenye Taifa letu, vijana hawana ajira hata awe na kitu gani, lakini nafasi ya ajira kwenye Taifa letu ni ndogo, wako mtaani, wana fani zao, lakini hawaajiriki mahali popote, hawawezi kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekimbilia kwenye chaka la Vyombo vya Ulinzi na Usalama ambao wameonesha kuajiri

vijana wengi kwenye Taifa letu. Hii siyo siri ni lazima tuseme ili tuone ni wapi palipotoboka? Eneo kubwa zaidi ni JKT ambao kimsingi mpaka sasa hivi vijana wetu wako huko kwenye mafunzo kwa maaana ya uzalendo lakini baadaye wataingia kwenye ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT pesa walizoomba jana za bajeti mpaka leo naongea hapa wamepata asilimia sifuri, *the shame*. Asilimia sifuri, tukajiuliza maswali kwamba hawa watu huenda vigezo hawajatimiza wakaja kwenye Kamati, tukawahoji wakasema na *certificate* walishapeleka, kuna nini kinaendelea kwenye Jeshi letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawezi kulia wakasikika au kusema popote kutokana na *ethics* za kazi zao, lakini sisi kama Taifa tunalionaje Jeshi hili ambalo linalinda ulinzi, mali zetu, uraia na watu wetu, wamepata asilimia sifuri? Mwaka jana walikuja hapa wakaleta Miradi yao ya Maendeleo wanayotaka itengewe fedha, Chita ambapo kuna Kilimo wameweka hekari 12,000, tukiamua kuhudumia eneo lile hata mfumuko wa bei utapungua. Tunafikiria nini kuhusu Taifa kama Vyombo vya Ulinzi na Usalama hatuwezi kuviangalia, hatuwezi kuvitengea bajeti kwa manufaa ya Taifa letu. Mama yetu kipenzi anazunguka kutafuta pesa huku na kule, nia yake ya dhati ni kulisaidia Taifa, Taifa linasaidikaje kama usalama wa nchi unakuwa tete? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia hili naona kuna la kufanya. Juzi Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alikuwa hapa akasema fedha hazigawiwi tu kama peremende, ni lazima kuwe na utaratibu umefuatwa, utaratibu umefuatwa fedha ziko wapi? Akamjibu Mheshimiwa Bashe, hapa akamwambia kwa kuwa wewe hujatimiza vigezo fedha zimejaa, zilizojaa zielekee kwenye Vyombo vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda naelekea maeneo yetu ya Jeshi la Magereza. Kwenye nchi yetu, kwenye Taifa Jeshi la Magereza mpaka sasa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakuongeza dakika moja maana muda wako umekwisha.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshazidiwa…

**MWENYEKITI:** Malizia sasa.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa Magereza ni watu 29,902, leo tuna watu 321,146. Tuliojaza kule siyo Watanzania, wako wahamiaji haramu 3,809 wako pale. Tuliomba tukasema kuwa kuna mkakati wa ziada wa kuwaondoa wahamiaji haramu, wahamiaji wale kwa siku wanatumia Sh.15,540,000, kwa mwaka wanatumia billion 5.6, bajeti ambayo tungeipeleka kwenye vituo vya afya, tukaipeleka kwenye madawati, tungepata madawati 81,000. Tungepeleka kwenye nyumba za Walimu tungepata nyumba za Walimu 62,200. Leo tunalia lakini watu wako *picnic,* wale wahamiaji haramu pale hatuwezi kuwapeleka shambani wakalime. Kwanza wako *weak* na wanafurahia kwa sababu wamepumzika, sisi tunapumzisha watu, wanakula pesa za Mama yetu, anakwenda kuzitafuta Ughaibuni, tuwe na uchun gu na pesa hizi za Rais wetu anatafuta Ugaibuni ili watoto wake wale. Nauliza swali, kiko wapi cha kumpikia mgeni wenyeji kulala na njaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na utaratibu wa vyombo vya sheria wawaondoshe watu hawa, tayari Jeshi la Uhamiaji wamechukua hatua, wameanza kutoa *Visa* rejea, nawapongeza sana. Hoja hii ilikuwa ya kwangu mwaka jana, wameanza, lakini walioko ndani waondoshwe waende kwao tubaki sisi tubanane humu humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, tunakushukuru kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Kwanza sina budi kuzipongeza Kamati zote zilivyowasilishwa hapo, zimewasilisha vizuri. Vilevile nipongeze na Vikosi vyetu vya Ulinzi ambavyo vinafanya kazi nzuri ya kulinda raia wake waliyokuwepo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee Magereza kuhusiana na *parole*. *Parole* ilikuwa nia yake kupunguza msongamano uliokuwepo Magerezani. Sheria ni nzuri, lakini wanashindwa kufikia mwisho na kwa nini wanashindwa kufikia mwisho na magereza yetu yanakuwa na msongamano wa wafungwa? Ni kwa sababu Bodi inakaa inaangalia, inafanya tathmini inamwona huyu raia alivyo anastahiki kuwa huru, lakini raia yule hawezi kuwa huru kwa sababu sheria inazungumza kwamba lazima mhusika wa kesi ile aliyomshtaki yule mtu aridhike na yeye, kwa sababu yeye ndiye aliyemshtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili wa ubinadamu mtu ameshakaa Gerezani muda mrefu, Bodi wameunda kisheria na huyu mtu ameshaangaliwa anafaa kutoka, anachukuliwa mtu wa mtaani kwa sababu ndiye aliyemshtaki anakuwa mtu yule ana roho mbaya, siku nyingine anaichukia familia ya yule mtu anakataa, akikataa hawezi kutoka. Sasa hii sheria inafanya kazi gani? Hii sheria wailete tuibadishe au mhusika anayekuwa na ile kesi Bodi wanapokaa wamwalike, ili kama kuna hoja zitoke kule, hawawezi kumfanya yule mtu anakubali mwenzie atoke kutokana na hoja zilizokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hii sheria haijaletwa, ikafanyiwa marekebisho kipengele baada ya kipengele, msongamano wawafungwa Magerezani utakuwa unaendelea. Hili lingine nataka nilizungumze kwamba hivi sasa Bodi ya *Parole* haina Mwenyekiti na pia si mbaya mkaliangalia na hilo ikapata Mwenyekiti, Bodi ikaweza kutimia na ikafanya kazi kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja na hii diplomasia ya kiuchumi. Diplomasia ya Kiuchumi kwa Tanzania itatusaidia sana, lakini tuishinikize Wizara ile Sera ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje itoke, kwa sababu ile sera ndiyo itazidi kuiboresha hii diplomasia ya kiuchumi kwa sababu kuna mambo mengi humo yanataka kuangaliwa. Tunataka kuangalia *the diaspora,* tunataka kuangalia Wawekezaji wetu watafanya kazi vipi? Tunataka kuona Wizara za Kisekta ambazo nazo zinataka kuchangia ingawa Wizara inasema wanashirikiana na Wizara za Kisekta, lakini mwamko hatuoni. Watakapotoa sera kutakuwa na kanuni, wataweza kuzibana hata hizi Wizara za Kisekta ziweze kufanya kazi na zikiweza kufanya kazi tutajua kwamba hii Sheria itaweza kufanya kazi na diplomasia ya kiuchumi itaweza kunyanyuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bila kuwepo sera na kanuni na elimu mikoa yetu haitoweza kufanya kazi kwa sababu jambo lolote literemke chini kwenye mikoa na wilaya lakini hawajui kinachoendelea na hawajui kinachoendelea kwa sababu sera bado haijajipanua, ingawa Wizara wanasema kwamba iko njiani wakati wowote itatolewa. Tungeomba itoke tupate na kanuni ili iweze kufanya kazi na hizi shughuli za kidiplomasia za kiuchumi, tuweze kufanya wafanyabiashara, wawekezaji, wakulima wajue mipaka yao vipi watafanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika hili la wahamiaji haramu nchini. Hili kweli suala zito, hili suala pia tunaongeza msongamano Magereza kwa sababu watu wanatoka nchi

nje anaingia ndani Tanzania, anazamia, anakuja tuseme kaja kisheria au kaja kinyume na kisheria, anazamia humu, wanawakamata wanawapeleka Magerezani Serikali ndiyo inaingia gharama, lakini kuna mtazamo Wizara ya Mambo ya Ndani ambao wanauangalia kwamba wanataka wafanye sasa hivi wanaingia kama wameingia kisheria, wanawagongea wapite waende zao itakuwa nzuri au hawakuja kisheria wanaambiwa arejee tena kwao lakini hapa Tanzania asikae kutuongezea msongamano Magerezani, kuwalisha Magerezani, mtu kakaa akiondoka kama alikuja na lilishe duni anaondoka ametengemaa hapa Tanzania. Sasa hata na hilo tunaona liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naweza kuzungumzia kidogo tu fedha za maendeleo. Jamani Wizara ya Fedha vioneni vikosi, fedha ya maendeleo hamuwatilii na barua za kuomba wanakuleteeni na barua wakileta, hii tunaingia *quarter* ya mwisho, kesho kutwa *quarter* ya mwisho, unampa pesa mwisho aifanye nini? Wakati ilikuwa kuna *quarter* ya kwanza, ya pili, ya tatu, hata yale malengo yalikuwa kayapangia hayawezi kufanikiwa. Sasa hebu watazameni jamani, kwani Vikosi vimekosa nini Hata hamuwapi? Naomba hili suala jamani tuliangalie, Vikosi wanatusaidia, wanatulinda na ndiyo watu wetu wa karibu katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu wakati huo wafuatao wanajindaa, Mheshimiwa Condester Michael Sichwale, Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye moja ya hoja iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Bajeti. Nikitambua mimi

ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, naona nichangie katika kipengele kimoja tu kwenye ukurasa wa 50 wa ripoti ya Mwenyekiti au ripoti yetu kwenye eneo la mikopo hii ambayo sisi kama nchi tunaifurahia jinsi gani Rais wetu anaipambania. Kabla ya kufanya hivyo, nitumie nafasi hii sana kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoendelea kufanya kazi kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mikopo ambayo imezungumzwa katika ripoti yetu kuna huu mkopo wa *(ECF-Extended Credit Facility)* kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa *IFM* wa Dola za Kimarekani Bilioni 1.04 au sawa na Shilingi za Kitanzania Trilioni 2.4. Kuna shida, Kamati inasema ina shaka juu ya malengo kama yanafikiwa, labda niwapitishe lengo kubwa kwenye mkopo huu wa trilioni 2.4 ambalo ni dirisha la pili na niwakumbushe ni dirisha la pili ambao tumepata, tofauti na lile dirisha la kwanza ambalo tulipata zile *(RCF - Rapid Credit Facility)* au UVIKO 19 hizi fedha ni *2.4 trillion*. Fedha hizi tulizichukua kwa sababu ya lengo, lengo kubwa lilikuwa ni kupunguza urali kwa ujumla, urali wa nchi yetu katika yale ambayo tunaweza badala ya ku-*import,* tukaweza kuzalisha ndani na tofauti na hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kinachotokea ni changamoto kubwa sana. Ukiangalia ufanisi wa Mkopo huu mpaka sasa mkopo huu umetolewa mwezi Agosti ambao unatakiwa katika masharti yake utatolewa kwa awamu saba kwa vipindi vya miezi arobaini, lakini mpaka sasa ambapo ni dirisha linakuja mwezi wa Tatu mwakani kwa maana ya baada ya tathmini, lakini taasisi zote hizo ambazo zimepewa au maeneo yote ya kipaumbele matano, eneo la kilimo, uvuvi, nishati maji, nishati umeme, bado hakuna hata moja lililofika asilimia 30. Hii ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunategemea Shilingi bilioni 760, tunaambiwa kwenye Kamati ndiyo tunatarajia tupewe ndani ya mwaka mmoja na tumepewa

kwa awamu mbili; ya kwanza shilingi bilioni 349, sasa hivi tulitarajia kabla hao Wazungu hawajaja kutufanyia tathmini ili watupe *second tranche,* maana yake tulitakiwa tufike hata asilimia 60 au 70 sasa tuko chini ya asilimia 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakutajia kwa uchache. Eneo la kilimo, *ECF* kilimo, wametumia asilimia 28. Yaani fedha waliyopangiwa ni shilingi bilioni 40 wamepata shilingi bilioni 11; eneo la uvuvi, Fungu 64 katika bajeti ya shilingi bilioni 60 wamepata shilingi bilioni 1.1, yaani asilimia 1.9. Eneo lingine kama kilimo katika vipaumbele vitano wamefanya vitatu tu na vyote chini ya asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuonesha nini? Kama tumewapa kilimo eneo la umwagiliaji katika Fungu 5, shilingi bilioni 215, wamepewa chini ya shilingi bilioni 42. Sasa tunataka kujiuliza, hawa jamaa wakija kutufanyia tathmini ili tupate *second tranche* tutaweza kufanikiwa? Swali lingine unajiuliza, hivi mama anavyoenda kupata haya madirisha, anaenda anakutananayo kwa bahati mbaya au tayari wataalamu mnakua mnasema tunahitaji jambo fulani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani hela inapatikana ndiyo mnaanza kujipanga katika ofisi zenu. Maana kama nchi lazima tujue sasa, shida ni nani? Shida ni nyie wasimamizi, makamisaa wetu katika Wizara? Shida ni nini? Manunuzi? Shida ni nini? Kwa nini hatusogei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe kwa haraka, inawezekana hii ni tabia. Tunaambiwa palikuwa na dirisha la kwanza la *RCF* au *UVICO 19,* tuliambiwa mambo mengi sana. Nami nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Watanzania wanajua ni ile shilingi bilioni 600 na kitu ambayo ilienda kujengea madarasa 15,000 yakiwepo 12,000 na 3,000 ya shikizi. Mambo mazuri yalionekana pale, lakini hela nyingine ziko wapi? Mambo mengine ni yapi? Tunaona moja moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa, nataka niwakumbushe; na ndiyo maana hatutekelezi hii mikopo tunayopewa. Tuliambiwa tungeweza kuwa; hela iliyoenda afya Shilingi milioni 263, tena afya kwa upande wa Wizara, nyingine zilienda TAMISEMI, lakini lengo lake lilikuwa ni kununuliwa magari 503. Yako wapi? Ndani ya magari hayo; *Land Cruiser Hard Top* 262, *basic ambulance* 373, *advance ambulance* 20, ziko wapi? Ndiyo maana nazungumzia malengo ya mikopo yetu, ni kweli toka mwezi Juni, 2022 tuliambiwa yangeanza kuja magari hapa *ambulance,* mpaka leo hakuna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dirisha la pili hili tunaendeleanalo. Changamoto za utendaji kazi chini ya asilimia 30. Rais wetu, mama yetu, ataenda atakutana na dirisha la tatu, mtamwingiza chaka tena achukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe. Tuna shida kama Taifa. Katika bajeti zetu za Serikali za kila mwaka, bajeti ya 2022/2023 ni ya shilingi bilioni 41 tumesema hapa, lakini fedha za maendeleo zinazowekwa ni takribani shilingi trilioni 15.1. Kama shilingi trilioni 15.1 tunaendelea kufurahia Shilingi trilioni 1.3, *RCF* tunafurahia shilingi trilioni 2.4 tena tunazifurahia, na ni kweli, ni vizuri na tunazifuatilia, kwa nini hatufuatilii shilingi trilioni 15 zile za maendeleo katika kila mwaka, kwanini hatuzifuatilii? Katika kipindi cha miaka mitano, maana yake ni zaidi ya shilingi trilioni 60. Kama nchi tumeziweka katika maendeleo, lakini hakuna *follow up. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko shida. Tumesema hapa kwenye Kamati, shida ya Sheria ya *M&E,* tuliomba sera ije hapa tutunge sheria ya *monitoring and evaluation* ingeweza kutusaidia kama nchi kuweza kufuatilia fedha zetu nyingi zinazoshuka chini. Leo shida yetu tunafurahia mikopo, nami naifurahia, mama yangu anaitafuta, lakini zile hela zetu

tunazoziweka katika maendeleo, zetu wenyewe Shilingi milioni 14 hadi 15 mbona hatuzifuatilii na zinapotea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tungeweza kuweka *ring fence* kwenye hela fulani tukawapelekea *TARURA* wenye kilometa 144,000 mtandao wa barabara. Wote hapa tunajua, tuna barabara za vumbi tunatamani ziwe changarawe au lami, kwa nini tusipeleke fedha nyingi tukazitolee macho kwenye barabara zetu za ndani za *TARURA? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Taifa, lazima tujitathmini sana. Mikopo tunaitaka, lakini vilevile na fedha zetu za ndani za maendeleo tuzitolee macho kwa kutungiwa sheria. Ije hapa sera, tutunge sheria ya *monitoring and evaluation* ili tusimamie fedha zetu zote zinazoshuka chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, tunakushukuru kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe aweze kuchangia.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Kwanza niseme naunga mkono hoja zote za Kamati ambazo zimewasilishwa Mezani; Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaelekeza mchango wangu kwenye Wizara ya Mambo ya Nje. Hapa nataka kuchangia kwenye diplomasia ya uchumi. Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akiwasilisha hoja yake, alisema kwamba tunapotaka kutekeleza diplomasia ya uchumi kwenye Wilaya zetu, hususan kwenye Halmashauri pamoja na tawala za mikoa, watendaji wetu wa Serikali hawana uelewa kuhusiana na diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii naona ni kwa sababu, zipo hata jumuiya za kikanda ambazo sisi ni wanachama huko, kumekuwa na utaratibu wa Serikali kutokurudi kutupa taarifa ya jumuiya hizo. Kwamba, kwa wakati huo malengo yale ambayo sisi tulijiunga kwenye hizo jumuiya, mpaka sasa hivi tunaendelea kunufaika na nini; na mpaka sasa hivi nini kinapaswa kuboreshwa? Wachukue maoni ya wadau? Tunapoongelea diplomasia ya uchumi ni pamoja na hizo jumuiya ambazo ndiyo zinatufanya tuwe washirika pamoja na wenzetu tunapotaka kutekeleza hiyo diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kurejea kidogo kutoka kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwenye Sura ya 7, Ukurasa wa 182, ule ukurasa wa 184 inapoongelea diplomasia ya uchumi, nitasoma kipengele kimoja tu. Kinasema kwamba, "Kulinda uchumi na maslahi mapana ya Taifa kwa kutumia jiografia ya nchi kimkakati na ushawishi wa kihistoria, hususan kwenye ukanda wa Kusini."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi katika miaka mitano ambayo tunatekeleza, inapoongelea kwenye suala la mambo ya diplomasia ya uchumi inatambua kwamba ni lazima tutumie hizi jumuiya za kikanda, lakini na historia zetu za kiuchumi huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka kuongelea sana sana kwenye hii jumuiya. Mwaka 1996 tulikuwepo kwenye *COMESA,* mwaka 2000 tukajitoa kwenye *COMESA*. Swali ambalo nataka kujiuliza hapa, sasa hivi ni miaka 20 imepita toka sisi tujitoe kwenye umoja huu ambao ulikuwa unaunganisha nchi za Kusini mwa Afrika pamoja na nchi ambazo ziko Mashariki ya Afrika. Ziko baadhi ya nchi ambazo ziko kwenye *SADC,* lakini haziko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini nchi hizi zinapatikana *COMESA* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, nchi kama Misri na Ethipia; hivi kwa mfano, unamuachaje Misri awe ni mshirika wako katika kutekeleza diplomasia ya uchumi, ikiwa Misri mwenyewe ndiye anatujengea Bwawa la Mwalimu Nyerere? *Egypt* wao ndio wanatujengea Bwawa la Mwalimu Nyerere? Je, zipo fursa ngapi za kiuchumi ambazo sisi tulipaswa tupate kutoka kwenye nchi ya Misri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Misri ndio watu ambao tunawauzia bidhaa za ngozi. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba, Serikali haijawahi kuja na ripoti miaka 23 iliyopita, sisi tulivyojitoa *COMESA* kipindi kile kwamba, labda ada ilikuwa kubwa, tulikuwa tunalinda bandari zetu kwamba tungekuwa wanachama, watu wangepitisha mizigo yao bure; tulikuwa tunalinda viwanda vyetu vya ndani, lakini sasa hivi zama zimebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajitoa *COMESA* mwaka 2000 tuchukulie *process* zilianza mwaka 1999, tayari tulikuwa tuko karne ya 20, sasa hivi tunaongelea kuanzia mwaka 2000 na sasa hivi tuko karne ya 21 teknolojia imebadilika, mambo ya uchumi yamebadilika na uongozi umebadilika. Tumetoka kipindi kile akiwa Rais ni Hayati Mheshimiwa Mkapa, sasa hivi tuko na Mama Samia ambaye yeye ni mwanadiplomasia wa kwanza. Je, hatuoni tunaendelea kumpa kazi ya ziada ya kwenda kuanza kuongea na watu wa Misri na watu wa Ethiopia ili tukaenao mezani, tukubaliane baadhi ya mambo wakati tunayo *platform* ambayo ni *COMESA* ingetusaidia kuweza kushirikiana na wenzetu kuwa pamoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nauliza swali la msingi hapo juzi, Serikali walijibu kwamba, kwa sababu tuko *EAC* na tuko *SADC* hatuoni umuhimu wa sisi kuwepo tena *COMESA*. Sidhani kama hili ni sawa kwa sababu, hizi nchi ambazo ziko *East African Community* na hizi nchi ambazo ziko *SADC* na hizi

ambazo ziko *COMESA* peke yake haziko kwenye nchi zote hizi mbili, tunazikuta wapi tukitaka kushirikiana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tanataka kuweka umoja wa Afrika ili tuwe na sehemu moja ya kufanya biashara; je, tunapotaka kutekeleza haya, kama tunayo *platform* ambayo sasa hivi inaweza ikatuunganisha na nchi zaidi ya 20 na sisi tukawa huko ni wanachama, wafanyabiashara wetu wakanufaika, wafanyabiashara wetu wakasaidika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naona ipo haja Serikali iwe inakaa inatuletea ripoti. Hata sasa hivi tuko *East African Community,* lakini bado ziko changamoto nyingi sana ambazo wafanyabiashara wetu wanaendelea kupitia. Tuko *SADC* sasa hivi, lakini kulifikia soko la Congo tu pamoja na kwamba, Congo ni mwanachama mwenzetu kwenye *SADC,* lakini tunapata changamoto nyingi. Wakati mwingine unakutana na wafanyabiashara mpaka wanashauri kwamba labda tungekuwepo *COMESA* ingetusaidia kupunguza hizi changamoto kwa sababu, lengo la *COMESA* lilikuwa ni kuwepo na ushirika wa kiuchumi, kuwepo na soko moja ili kuondoa hizo changamoto za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naona kwamba, Serikali iende ikafanye tathmini itujie na majibu, katika miaka 23 ambayo tunayo mpaka tulipofikia sasa hivi, ipo haja ya sisi kurudi *COMESA*. Hata kama hawataona haja ya kurudi *COMESA,* waje watusaidie kuainisha tutambue. Pia takwimu hizo zitusaidie kwenda kule kwenye Halmashauri zetu na kwenye mikoa yetu kwa wananchi wa kawaida ambao tunataka watekeleze diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea mambo haya ya jumuiya, imeonekana diplomasia ya uchumi ni ya watu wa kaliba fulani, waliosoma tu, watu ambao wako juu, wakati watekelezaji wakubwa ni wakulima, wananchi wa kawaida.

Wangefahamishwa haya mambo, yamkini wangejua kwamba, kama nchi yetu iko *SADC* tunanufaika na vitu gani? Kama nchi yetu iko kwenye umoja wa Afrika Mashariki tunanufaika na vitu gani? Wananchi hawana uelewa kabisa katika mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea, hapo tunaposema tuendelee kufanya tathamini zetu na Serikali iwe inatuletea taarifa kutoka kwenye jumuiya tulizonazo, mfano mzuri unaweza ukaona kwamba, unapoenda kwenye ule ukanda wa Ziwa tanganyika tumejenga bandari zaidi ya tano. Kuna Bandari ya Katanga, Bandari ya Kipili, Bandari ya Kabwe, na Bandari mpya ya Karema. Tulipokuwa tunauliza swali hapa, ni namna gani Serikali itatusaidia kuondoa changamoto ambazo tunazipata kupitia Zambia kuingia nchi ya Congo? Serikali ilikuwa inatujibu kwamba, tumeshajenga bandari na ni mkakati ambao utatufanya sisi tuingie *DRC* moja kwa moja bila kupitia nchi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tuna uelewa kidogo, mimi nikamfuata Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi nikamwambia Mheshimiwa Waziri majibu haya ambayo mnatupa, nafikiri Serikali haijafanya tathmini. Uende wewe na timu yako ukatembelee zile bandari ambazo zimejengwa kwenye Ziwa Tanganyika na uende upande wa pili ambao ni wa Congo, ili ukaone kama jambo hilo linatekelezeka ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipoenda, amekuja kutupa taarifa. Unagundua kabisa kwamba ni kitu ambacho hakitafanyika mwaka huu wala hakitafanyika mwakani ili sisi tuweze kupitia Ziwa Tanganyika kuweza kufika Congo, *especially,* kufika Lubumbashi ambayo ndiyo miongoni mwa majimbo ambayo yanafanya vizuri sana kibiashara ambapo hata sisi Watanzania wengi wana-*target* kupeleka mazao yao huko. Ni kitu ambacho sio cha sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wao kwa kwenda kufanya tathmini, na kufanya takwimu ikatusaidia wao kuja na njia mbadala wajue tukitaka kuingia Congo kuna namna ambavyo hatuwezi kuikimbia Zambia. Aidha, sisi turudi *COMESA* ili kurahisisha kuondokana na hizo changamoto au kutafuta njia nyingine mbadala namna gani sisi tuisaidie nchi ya Congo kujenga barabara kwao ili tuweze kupita kutoka Ziwa Tanganyika kwenda moja kwa moja. Hayo yote yamefahamikaje? ni baada ya viongozi wetu wa Serikali kwenda kufanya tathmini na kuleta ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo mambo ya kuendelea kukaa. Kama tulishajitoa *COMESA* sasa hivi tuko wakati mwingine, vita ya uchumi ni kubwa, kila mtu analiangalia soko la Congo. Nasi kwa kutumia soko la Congo tu peke yake linaweza likatuongezea mapato kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester Sichalwe. Nilimwita Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami napongeza Kamati zote mbili, nami ni Mjumbe wa Kamati ya NUU. Hili ninalolisema mara zote nimelisema na sitaacha kulisema kwamba, Mheshimiwa Rais, kama mwanadiplomasia namba moja, ameendelea kuitendea haki nafasi yake, ameendelea kufanya ziara, ameendelea kutafuta wawekezaji, ameendelea kufanya shughuli zote ambazo zinathibitisha kwamba Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ni mwanadiplomasia namba moja katika Taifa letu. Hizi shughuli anazozifanya zitakuwa na thamani na manufaa kwa Taifa letu kama kutakuwa na *connection* na kama kutakuwa na

*link* kati ya shughuli ambazo zinaratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara nyingine za kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa yetu, mojawapo ya jambo ambalo limejitokeza ni kukosekana kwa mkakati maalum wa kiushirikiano kati ya Wizara ya Mambo ya Nje katika kutekeleza diplomasia ya uchumi na Wizara nyingine za kisekta. Ni kweli kwamba ushirikiano upo, lakini tunachokitaka ni ushirikiano wa kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitatoa mfano. Kwa takribani miaka minne, na bahati nzuri Waziri wa Kilimo yuko hapa; Wizara ya Mambo ya Nje imekuwa ikiratibu vijana takribani 100 kwenda nchini Israel kujifunza masuala ya kilimo kwa muda wa miezi 11. Hapa ninalo tangazo la 2019 ambalo limeandikwa, "Tangazo la Mafunzo ya Kilimo Nchini Israel." Tangazo hili linaalika vijana waliomaliza *SUA* waende Israel wakajifunze kilimo kwa muda wa miezi 11. Sasa wakisharudi wale vijana ni wa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale vijana sio tena wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Wale ni vijana wa Kilimo; lakini mpaka hapa tunavyozungumza sijui kama Wizara hata ina takwimu vijana hawa ni wangapi *in total* na wako wapi? *As far as I know, majority* wamerudi. Sana sana *the best they can do,* wanajiajiri katika biashara ya boda boda. Sasa tumewapeleka vijana miezi 11 wamejifunza *very advanced skills* za mambo ya kilimo, lakini kwa sababu hakuna mkakati mahususi wa kuonesha hiyo *link,* Wizara ya Mambo ya Nje imeshatimiza wajibu wao, lakini wale ambao wangepaswa kuwalea wanakuwa hawajatimiza lile ambalo lingekuwa ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri. Katika maazimio ya Kamati ya Bajeti, maoni na mapendekezo mahususi, ukurasa wa 68, imeeleza ya kwamba, katika huu mpango ambao Mheshimiwa Bashe anakujanao wa *block farming*

Serikali ianze na vijana wa *JKT.* Naomba kulishawishi Bunge lako, kama sehemu ya hayo maazimio ambayo kwa namna moja au nyingine yatakuja kulisaidia Taifa letu kukabiliana na mfumuko wa bei, hususan katika kipengele cha mafuta ya kula. Katika bajeti iliyopita, katika Muswada wa fedha, tulisema hapa tumetoa ahueni kwa waagizaji wa mafuta, lakini tuwe *honest* katika nafsi zetu, je, mafuta ya kula yamepungua bei kutokana na hilo punguzo ambalo tumewapa waingizaji wa mafuta? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli tukiwa wakweli wa nafsi, hakuna punguzo ambalo linamfikia mlaji, isipokuwa ni manufaa wanayojinufaisha wafanyabiashara wakubwa wanaoagiza mafuta hayo. Kwa sababu hiyo, nashawishi Bunge lako, tuongeze azimio kwamba, katika hii hoja mahususi ambayo wenzetu wa bajeti wamesema, tuseme kwamba, Bunge liazimie tuwape kazi na nyenzo wenzetu wa JKT na SUMA-JKT ya kuhakikisha kwamba Taifa hili ndani ya miaka miwili, litajitosheleza kwa mafuta ya kula na litaweza kusafirisha mafuta ya kula kwenda nje. *That is the only way* ya kuhakikisha tunakabilana na mfumuko wa bei katika baadhi ya vitu ambavyo tunaweza tukazalisha hapa nchini. Vinginevyo tutabaki na taarifa za *UVICO,* na taarifa za vita ya Ukraine na Urusi. Lazima tuje na mikakati, tubuni namna ambayo tutaondokana na shida hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tumesema kwamba, lazima tu-*link*. Kuna hawa vijana wa JKT, hawa waliotoka Israel wangeweza kuwa ndio wasaidizi wao katika hiyo *block farming.* Katika ku-*link,* nakushukuru wewe unatoka Mufindi, sisi tunazalisha mazao ya kilimo. Katika diplomasia ya uchumi tunasema kwamba, pawepo na mkakati kwamba hii elimu ifike mpaka kule chini. Sisi watu wetu wa Mafinga, Mufindi, Iringa, Kilolo na Njombe waweze ku-*access* masoko ya mbao, milunda na mazao ya misitu kwenye soko la Congo. Waweze ku-*access* soko la nafaka kwenye soko la Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri bashe shahidi, wale Bodi ya Mazao Mchanganyiko walipeleka kule mazao yamekaa miezi mitatu yanashindwa kuingia kwa sababu tu kumekosa *link* kuwashirikisha watu wa mambo ya nje kushirikiana na Kilimo na Viwanda na Biashara kujua je, soko la Congo limekaaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe soko la Congo kule Lubumbashi ni lazima ushirikiane na wale *tycoon* ujue wanapita njia gani ndio uweze ku *access* lile soko, sasa kama hakuna hiyo *link* tutabaki tu tunalaumiana, hivyo itoshe tu kusema kwamba tunahitaji kuwa na *link* kati ya diplomasia yetu ya uchumi, uzalishaji wetu na Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze umetusomea hapo tangazo, nimeona kutakuwa na Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itakuwa ni mojawapo ya *link* nzuri sana kwa sababu bila viwanda, bila mazao huwezi kuwa na Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhitimisho niende kwenye suala la *NIDA* kwa haraka sana, pamoja na maazimio ya jumla. Katika suala la *NIDA* kwenye taarifa yetu tumesema ya kwamba *NIDA* inafanya kazi nzuri *so far* inafanya kazi nzuri, lakini wananchi wanataka vitambulisho. Mpaka hapa tunapozungumza *NIDA* wanafanya kazi mbili utambuzi, usajili na kutoa vitambulisho. Mpaka sasa wameshatambua wananchi takribani milioni 23 kati ya wananchi milioni 34 mpaka kufikia 2025/2026 wanaenda vizuri kwa sababu ni asilimia 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hao waliotambuliwa ambao ni milioni 23 ni milioni 19 sawa na asilimia 84 tayari wana ile namba ya *NIDA*, lakini wenye vitambulisho ni milioni 10 tu sawa na asilimia 56. Maana yake kila watu 100, 56 wana kitambulisho cha NIDA 44 hawana kitambulisho cha NIDA.

Kwa hiyo, pale Serikali inayo wajibu wa kuisaidia *NIDA* kama ni Fedha au namna nyingine isaidie ili mwananchi apate kitambulisho, kwa sababu baadhi ya huduma zinataka siyo uwe na namba bali uwe na kitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maazimio ya jumla naomba kuhitimisha ipasavyo tuzisaidie Wizara hizi za Fedha, kwa sababu tumeona utekelezaji wa maazimio na tumesema kwamba Bunge linapoazimia siyo Mheshimiwa Chumi au Siyo Mwenyekiti wala siyo Mheshimiwa Vita Kawawa, sisi tunaazimia kwa niaba ya Wananchi. Kwa hiyo, matarajio yetu ni kwamba yale tunayoyaazimia ni kutatua changamoto na kero za wananchi, sasa yasipotekelezwa maazimio, maana yake ni kwamba hatujatatua na kupunguza kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ushauri wangu kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha pamoja na changamoto za kibajeti tuhakikishe kwamba yale tunayoazimia ambayo yanahitaji fedha kuyatekeleza basi wenzetu wapewe fedha. Kwa kuhitimisha Wizara ya Mambo ya Nje tu kwa mfano, kwa miaka mitano walitakiwa wapewe bilioni 48 za kuweza kujenga majengo na kuyaboresha ambayo majengo haya tungeweza kuyapangisha yangetupa mapato lakini mpaka ninavyozungumza ndani ya miaka mitano wamepewa tu bajeti ambayo haizidi asilimia 19. Kwa hiyo, katika kutekeleza maazimio ambayo yanahitaji fedha wenzetu wa fedha wajitahidi kutoa fedha ili tutekeleze, tupunguze kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja zote, Mungu atubariki wote, abariki wananchi wa Mafinga na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato David Chumi kwa mchango wako. Wachangiaji wetu wa Mwisho

atakuwa ni Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira na Mheshimiwa Abbas Gulam Tarimba.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii, nami mchango wangu utajielekeza katika taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kutambua rasilimali watu tuliyonayo katika Diaspora, tumeona hivi karibuni ameendelea kutoa nafasi mbalimbali za uteuzi kwa Watanzania wenzetu ambao walikuwa wanafanya kazi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo nipongeze Kamati kwa kutambua umuhimu wa Diaspora pia kwa kutambua kwamba bado hatuna mfumo sahihi wa kutambua wenzetu wa Diaspora lakini kuweza kuwafungamanisha katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea mwaka 2021 mwezi Juni nilichangia katika mchango wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje hapa Bungeni ilikuwa ni Tarehe 01 Juni, 202, ambapo niliishauri Serikali, kwakuwa suala la uraia pacha lina changamoto mbalimbali na linagusa Katiba, tujielekeza katika suala la Hadhi Maalum ambalo litawezesha diaspora kupata kila kitu na kunufaika na kujishughulisha na shughuli zote za kiuchumi, kasoro maeneo mawili. kujishughulisha na masuala ya kisiasa pamoja na ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama. Nashukuru wakati ule tulipata jibu hapa hapa Bungeni kwamba Serikali inafanyia mapitio Sera ya Mambo ya Nje, ndani ya Sera ile itaweka suala la diaspora na sera ile itakuwa tayari Disemba 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni takribani miaka miwili toka Bunge la Bajeti 2021, mpaka leo hii bado Serikali haijaja hapa Bungeni kutueleza bayana ni lini itakamilisha mpango wa hadhi maalumu kwa ajili ya diaspora. Ninasema hivi kwa sababu mchango wa diaspora katika ukuaji wa uchumi kwa Taifa letu ni mkubwa sana. Kwa mwaka 2022 Kenya peke yake imepata dola bilioni nne kupitia Diaspora na imefikia mpaka Diaspora ndiyo wana mchango mkubwa zaidi kwa *foreign currency* katika nchi ya Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunahitaji rasilimali watu, tunahitaji rasilimali fedha, tunajaribu kukuza uchumi, tunao diaspora ambao wana taaluma kubwa, tunao diaspora ambao wana mitaji lakini kwa kuwa bado tunashindwa kutambua hadhi maalum na kukamilisha mchakato wake tunashindwa kunufaika na diaspora lakini na diaspora wanashindwa kunufaika na nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa muda mrefu katika safari zake za nje ya nchi na kila nchi anayokwenda anakutana na diaspora, ni mara kadhaa Mheshimiwa Rais amekuwa akiahidi diaspora kwamba suala la hadhi maalumu linafanyiwa kazi, sasa nashangaa sana kwa nini Wizara hii inakwamisha maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea Bungeni na kutueleza bayana suala la hadhi maalumu kwa ajili ya diaspora litakamilika lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha naomba sana nipate kauli ya Serikali ni lini itakamilisha mchakato wa wenzetu diaspora kupata hadhi maalum ili waweze kujishughulisha na shughuli za kiuchumi nasi kama Taifa tuweze kupata:

(i) Takwimu sahihi za diaspora,
(ii) Takwimu sahihi za mchango wanadiaspora kwenye ukuaji wa uchumi wetu,

(iii) Kuwatumia katika rasilimali watu pale ambapo tunahitaki taaluma zao,
(iv) Kuwatumia katika rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Wizara hii iunge mkono jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kufungua uchumi wetu kidiplomasia na isiwe sehemu ya mkwamo wa kufanikisha suala la hadhi maalumu kwa diaspora. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Abbas Gulam Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie nikiwa mchangiaji wa mwisho na ninajua mara nyingi mchangiaji wa mwisho hutampigia kengele utamuachia tu atiririke wee! mpaka amalize. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na ningependa nizungumzie masuala ambayo yamewasilishwa na Mwenyekiti wetu, haraka niseme naunga mkono hoja zote mbili kwamba mimi kwangu ni asilimia mia moja kwa mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mpenzi wa kusoma sana hizi *Journals* za mambo ya kiuchumi, hivi karibuni nikasoma jarida moja linaitwa *Africa can end poverty* wakiwa na maana kwamba Afrika inaweza ikaondokana na umaskini, pale nikavutiwa na andiko moja la Ndugu mmoja anaitwa Waly Wane huyu ni Daktari wa Uchumi katika taasisi moja inaitwa *Development Research Group*. Huyu aliandika akajiuliza swali *is Tanzania raising enough tax revenue?* Alikuwa anajiuliza yeye katika *thesis* aliyokuwa anaandika kwamba hivi Tanzania inakusanya kweli kwa uhakikia kodi inayotosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni andiko la siku nyingi kidogo la tarehe 4 Februari, 2013. Sasa katika kusoma kwangu nikasema ngoja nifananishe na hali halisi hapa kwetu. Nichukue kwanza nafasi kusema kweli ya kuipongeza Serikali kwa maana ya *TRA* kwa maana mwaka 2021/2022 mapato ya ndani Serikali imeweza kukusanya trilioni 24.35 dhidi ya lengo la trilioni 25.6 na hii ni sawa na asilimia 95 Kamati imetoa pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi na juhudi kubwa iliyofanywa hawa akina Ndugu Waly Wane swali lao bado halijajibiwa. Nimejaribu kuangalia pia mapato yetu na mienendo ya jinsi tunavyofanya mipango yetu swali la Waly Wane bado halijajibiwa. Sasa nikasema hebu niangalie Kamati imeliangalia vipi suala hili, kwa mujibu wa maelezo ya Kamati kama ilivyo katika *paragraph 2.1.7* kuanzia ukurasa wa kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui nilijibu hili swali ama Bunge litajibu lakini tusikilize Kamati inasema nini, na maneno haya aliyasema hata Mheshimiwa Esther, kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu hawatumii *machine* za *EFD*, maana yake ni kwamba kuna upotevu hatukusanyi, kumbe sasa swali la Ndugu Waly Wane tunaanza kuliona kwamba kweli alivyouliza ni kwamba kweli hatukusanyi inavyopasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie jambo la pili baadhi ya Halmashauri zetu haziwasilishi fedha benki, hizo fedha zinakwenda wapi kama haziwasilishwi benki maana yake zinapotea, hazikusanywi na Serikali maana yake jibu ni kwamba hatuzikusanyi Serikali haipati mapato yake. Hata ukija kwenye masuala ya fedha ambazo hazikusanywi kutokana na madeni ambayo yamelimbikizwa, hilo nalo ni suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye idadi ya watu ambao wameandikishwa walipa kodi, watu Milioni Nne ndiyo wako katika kanzi data, watu wanaolipa ni nusu yao maana yake hata Mheshimiwa Esther aliuliza je, kama hao wengine Milioni Mbili waliobaki wangekuwa wanalipa tungekuwa tunapata kiasi gani? Hilo nalo ni swali la Ndugu Waly Wane anauliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye masuala mengine ya watu wanao *file returns* - marejesho ya kodi kwa njia ya ki-*electronic*, wapo watu ambao wameonekana hawafanyi hivyo maana yake hatuzikusanyi fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *tax audit* ambazo zinachelewa, hili tumelisema hapa Bungeni, inachukua miaka mitatu, minne kwa *TRA* kwenda kufanya *tax audit,* fedha za Serikali zimekaa pale hatuzikusanyi, na hilo nalo ni suala vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kuanzishwa kwa Ofisi ya Msuluhishi wa Kodi ambapo pengine masuala ya Kikodi yasingekwenda *TRAB na TRAT* kule yangeweza kusuluhishwa lakini bado haijamalizika. Hata haya mashauri yaliko katika hizi mahakama za *TRAB* na *TRAT* hazina muda. Zinaweza zikakaa muda wote ule, hakuna *specific period* kwamba ikifika muda fulani mashauri yamalizike, Serikali ipate fedha zake au mfanyabiashara arudishiwe fedha zake. Haya ni mambo ambayo tungependa tuyaone kwamba ni *concern* kubwa kwamba ni vitu vinavyotugusa. Kwamba laiti kama vitu hivi vitafanyika kwamba ni dhahiri kabisa inaweza tukapata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie kule Mtaa wa Nyamwezi pale Dar Es Salaam, ambao umejaa maduka mengi sana. Pale wale Maafisa wa Kodi ambao wanasimia ile *block* wapo Maafisa Watano tu na mtaa ule mpaka wakiumaliza kuutembelea maana yake watahitaji hata

mwaka mzima. Yawezekana kuna wafanyabiashara wengine hata hawapitiwi kabisa kuweza kupeleka taarifa zo za kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ni kisema hivyo maana yake kilio cha kupatikana kwa wafanyakazi wa kutosha wa *TRA* bado kiko pale pale, tusipokuwa na wafanyakazi wa kutosha *TRA* hatuwezi tukakusanya ela. Najua Serikali imejitahidi sana kuongeza idadi ya Wafanyakazi wa *TRA* lakini hakika hiyo inaanifanya nifikirie jambo moja. Kule kwenye Kata zetu, kila *kata* kuna Afisa Maendeleo, kila kata kuna Afisa Ugani, Kuna Afisa Elimu tunashindwa nini kuweka kila kata Afisa wa kodi. Tunaona taabu ya nini tuanze na Dar es Salaam tuangalie yale maeneo ambayo yanashughuli za kiuchumi nyingi ili tuweze kuwakia wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais aliyepita Mheshimiwa Jakaya anasema maneno haya ni *very famous* anasema kama huwezi kuliwa huwezi kula, ukitaka kula lazima uliwe, sasa sisi tena hawali watu wabaya wanakula watu wetu, Watanzania wakiajiriwa watatusaidia kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,hili linanipeleka vilevile kwenye utaratibu mwingine, naomba Serikali iweke katika mitaala yake hata kuanzia *primary school*, somo la uzalendo na ulipaji wa kodi. Watu wetu wakue wakiwa wanajua umuhimu wa uzalendo na umuhimu wa kulipa kodi. Hii pia itatusaidia kwa sababu kama tunatafuta fedha za kutosha na huku tunajua fedha za kutosha zinatoka katika *private sectors*, *private sector* kwa maana ni biashara, leo kulikuwa na swali linaulizwa hapa linahusiana na *blueprint* tuko nchi ya 141 na hili nalisema sana mwisho nitapewa jina la *blueprint*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko 141 Serikali inaulizwa lini mtatuletea taarifa ya utekelezaji, majibu yanayoletwa hapa yaani saa nyingine tunaheshimu Serikali yetu lakini saa

nyingine unashangaa unaweza ukasema ni ya kisiasa mno! Tunataka taarifa zile za kufanya ufanyaji wa biashara Tanzania uwe mwepesi, watu waweze kutupatia kodi, sasa hilo pia nalo lina ugumu gani? Haya mambo mengine unayazungumza na mimi kwa sababu hili eneo la fedha ni la Ndugu yangu Mwigulu, najua ni mwananchi mwenzangu, yaani najizuia kwelikweli kutumia maneno mengine yasiyofaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tarimba nilikuongeza dakika kidogo lakini nadhani tumefika mwisho.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Haya ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa mchango wako.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji mchana ambapo tutaanza na Mheshimiwa Zahoro Mohamed Haji pamoja na Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Shally Raymond na wengine nitawataja baadae ili waweze kujiandaa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo naahirisha shughuli za Bunge mpaka jioni Saa Kumi na Moja.

*(Saa 7. 15 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, tunaendelea na Majdiliano. Nilimwita Mheshimiwa Zahoro Mohammed Haji, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, wakati huo Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Joseph Raymond wanajiandaa.

**MHE. ZAHORO MOHAMMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na naomba kwa sababu ya umuhimu wa muda na uchache wake nitachangia kwa ufupi, naamini kwamba Bunge linaweza likanielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nizishukuru Wizara zetu zote tatu kwa kufanya kazi kubwa na ngumu. Hata hivyo kwa sababu ya uzalendo wao leo tuko salama, tuna na amani na nchi yetu iko vizuri ndani na iko vizuri nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya NUU. Kamati hii kwa mujibu wa taratibu tulizojipangia, inasimamia Wizara tatu. Inasimamia Wizara ya Mambo ya Nje, inasimamia Wizara ya Mambo ya ndani lakini pia inasimamia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ukiichukua vizuri maana yake ni kwamba ni kamati inayosimamia mambo yote yanayohusu Jamhuri, nje na ndani. Sasa kazi zake ni nyingi lakini nitaomba nitaje majukumu yetu Matatu ili niweze kwenda kwenye hoja zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu la kwanza kama NUU ni kusimamia Bajeti za Wizara hizi tatu, jukumu la pili, ni kusikiliza taarifa zao za utekelezaji, jukumu la tatu ni kufuatilia kile ambacho wametutaarifu kwamba kimetekelezwa na jukumu la nne ni kuangalia miswada na mikataba mbalimbali ili tuweze kuleta kwenu kwa ajili ya *ratification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa haraka haraka Wizara tatu hizi, Wizara ya Mambo ya Nje ni Wizara ambayo ndiyo kioo chetu Duniani. Tunapimwa kwa mazuri na mabaya na wenzetu kwa kutumia chombo hiki tulichokiunda kinachoitwa Wizara ya Mambo ya Nje. Vile vile tunalinda mipaka yetu tunatumia Jeshi letu la Ulinzi na Kujenga Taifa kwa sababu hawa wanatulinda angani, ardhini, mipakani na

baharini. Maana yake ni vyombo ambavyo tumevipa majukumu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunayo Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo jukumu lake kubwa ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Hivi ndivyo vyombo vinavyotulinda kwa kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa maana hiyo mimi naomba niende moja kwa moja jinsi tulivyowapa majukumu au majukumu waliyopewa kwa mujibu wa Sheria na Katiba yetu. Hivi ni vyombo muhimu na hivi si vyombo vya biashara. Hivi ni vyombo vya ulinzi nje na ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa ili viweze kufanya kazi, maana yake sisi kama Bunge tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba vyombo hivi vinafanya kazi zake kwa mujibu wa mipango iliyopo kwenye Katiba na Sheria zetu. Kwa sababu bila ya kuwa na mipango na tukaiwezesha maana yake ni kwamba Wizara hizi haziwezi kufanya kazi kwa kuwa hizi si Wizara za Biashara. Tumeongeza tu jukumu, kwa mfano kwenye Wizara ya Ulinzi, kwamba wakati wa amani wafanye kazi ya kuzalisha. *Literary* Jeshi si kazi yake kuzalisha, tumeliongezea tu. Jeshi kazi yake ni kulinda mipaka yetu, *full stop*. Haya mengine tunapenda tu kwa sababu ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili hizi kazi zifanyike, hawa watu lazima tuwawezeshe. Sasa kinacho nisumbua mimi na ambacho Kamati yetu imekiona, ni ukweli kama vile tumezifanya hizi Wizara ni Wizara ambazo hazina kazi au majukumu yake si ya Muhimu. Mimi naomba niliombe Bunge letu kwamba likubali na tuiombe Serikali, na Serikali tuiombe si kwa sababu ya kujipendekeza au kuibembeleza, ni wajibu wa Serikali kuviwezesha vyombo hivi ili vifanye kazi. Kwa sababu hatuwezi kulinda mipaka kama hatuna nyenzo, na nyenzo hizo ni kuwezesha na kuhakikisha kwamba bajeti yao inafanyiwa kazi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, naomba nitaje tu haraka haraka. Wizara ya Mambo ya Nje, kwa miaka minne mfulululizo kuanzia mwaka 2017, 2018 mpaka kufikia mwaka 2021 bajeti yao kwa jumla walipata asilimia 19. Hili ni tatizo letu sisi Wabunge na si Serikali. Kwa sababu kuna *gap* hapa kati ya bajeti tunayopitisha na taarifa ya *review* inayofanyika. Kwa hiyo ningeomba hili sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara hii ina vifungu kama sita hivi. Ukifanya *average,* kwa sababu kuna mafungu mengine yamepata zero kwenye maendeleo mpaka tunavyozungumza Disemba au Januari hii. Hata hivyo ukifanya *average* kuanzia tulipo anza mpaka Januari hii *average* wamepata asilimia 8.8 ya bajeti yao ya mwaka. Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiyo ukienda kwenye Wizara ya Ulinzi ambayo nao wana mafungu matatu makubwa, ukifanya *average* wamepata asilimia 16.93. Ni chombo gani kinachoweza kutulinda tukaishi kwa amani kwa bajeti ya aina hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana Bunge hili tukubali na tuishauri Serikali, tena tuishauri kwa sauti kali, kwamba vyombo hivi ambavyo vimepewa jukumu la kutulinda bado havijatendewa haki kwa sababu tunadhani ni vyombo vya pili au vilitakiwa kuwa vya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba nishauri kwa sababu nikisoma hizi haitapendeza. Naomba nishauri haya yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, inawezekana wengi wetu sisi Wabunge humu hesabu si kazi tuliyoizoea wala hatujui. Inawezekana kazi zetu nyingine huko ambazo humu

hatuwezi kuzitaja. Sasa kwa sababu hatujui mambo ya kimahesabu mimi ningeomba Wizara, hasa Wizara ya Fedha, ikubali kukutana na Kamati ya NUU itufafanulie, kwa sababu sisi ndio tunaofuatilia maslahi ya vyombo hivi vitatu vikubwa, ili tuwe kwenye sahahni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ningeliomba Bunge, kwa sababu nimesema kule mwanzoni kuna *gap* kati ya kupitisha Bajeti na kuja kwenye *review*. Hapa katikati hapa kuna *gap*. Maana yake ni kwamba Serikali inatekeleza halafu sisi tunakuja kusikia kulichotekelezwa na ambacho hakikutekelezwa, hapa kati kati kuna *gap*. Kwa hiyo ningeomba sana kwamba ni lazima tuzibe hili *gap* ili Serikali ijue kwamba Wabunge ndio wawakilishi wa wananchi, wanayo haki ya kujua kilicho kusanywa na kuhakikisha kwamba kinakwenda kule ambako tulikokusudia ili tusisubiri *review* tukaambiwa kipi kimefanyika na kipi hakikufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya *interest* ya muda, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zahoro Mohammed Haji kwa Mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph George Kakunda aweze kuchangia.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Bajeti lakini nachukua nafasi hii kwanza kupongeza Kamati zote Mbili zilizowasilisha leo kwa kazi nzuri ambazo zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli jioni hii ningependa nishauri katika maeneo Manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni eneo la mitaji katika sekta ya kilimo. Kumekuwa na kiu ya muda mrefu hasakwa sekta binafsi ambazo zinahitaji zipate mitaji kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo, hasa vijijini. Tatizo kubwa kwa

nini wamekuwa hawapati mitaji wanayohitaji, ni kwa sababu Sheria zetu za Ardhi Sheria Namba 4 na Sheria Namba 5 zinazuia uwezekano wa watu kutumia kama dhamana vijijini kwa ajili ya kupata mitaji; hasa kutoka kwenye benki. Hii ni kwa sababu, ardhi haijapimwa. Hata hivyo hili nimekuwa naisema mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tupitishe Sheria ya Vijiji Namba 5 mwaka 1999, Mpango ulifuata ulikuwa ni mkakati wa kutekeleza Sheria za Ardhi ambao ulianza kutekelezwa Mwaka 2000. Hata hivyo Mpango ule au Mkakati ule ulikuwa na miaka mitano. Walikuwa wamesema kwamba ndani ya miaka mitano vijiji vyote vitakuwa na mipango ya matumizi ya ardhi. Hata hivyo hadi leo hii tunavyozungumza hapa vijiji ambayo vina mipango ya matumizi bora ya ardhi ni vijiji 2,310. Ina maana kuna vijiji 10,000 havina mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu katika Wilaya ya Sikonge vijiji ambavyo vina mipango ya matumizi bora ya ardhi ni vijiji tisa tu kati ya vijiji 71. Maana yake ni kwamba tumekuwa tunazuia uwezekano wa kupata mitaji kutoka kwenye sekta ya ardhi kwa sababu ya sheria zetu. Nilikuwa natoa wito kwa Serikali, naomba Serikali ije na mkakati maalumu wa aidha kupima vijiji vyote, kwa sababu wastani wa kupima kimoja ni milioni 15 hadi 20; kwanini wasipange wakapima vijiji vyote kwa awamu mbili au tatu wakamaliza ili kusudi watu wetu wawe wanapata mitaji kutoka kwenye sekta ya ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa kushauri ni mfuatano wa mipango kwenye sekta ya miundombinu. Sasa tunajenga *SGR,* tunajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere na naipongeza Serikali *SGR* ya Tanzania hata watu wa nje wakija wanaona Kiwango, yaani *standard* ya *SGR* ya Tanzania inaizidi kwa mbali kiwango cha *SGR* za nchi Jirani, kwa hiyo, hiyo naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mfuatano na hasa kwa sababu tunadhani kwamba mpaka ikifika mwaka 2030 tutakuwa tumemaliza vipande vyote vya *SGR*, kama Mungu atatuwezesha. Hiyo hiyo itakuwa ni muda mfupi wa kutumia kuliko walivyotumia wenzetu walivyokuwa wanajenga miaka ile ya wakati wa Ukoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano, ujenzi wa reli ya kwanza nchini hapa kutoka Tanga mpaka Arusha ulitumia muda wa miaka 36. Kwa maana ya kipande cha kutoka Tanga mpaka Moshi ni miaka 18 na Kipande cha Kutoka Moshi Mpaka Arusha ni Miaka 18. Hata hivyo kama tutaweza sisi kujenga *SGR* vipande vyote kwa muda wa miaka 13 au 15 itakuwa ni *achievement* ambayo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye mfuatano, wenzetu wakoloni katika utawala wao wa miaka 71 mfuatano wao ulikuwa unajulikana. Walianza na Tanga – Moshi – Arusha, wakaja Dar es salaam – Tabora – Kigoma, wakaja na Tabora – Mwanza, wakaja na kaliua – Mpanda halafu wakajenga vireli vya kuunganisha. Kilosa – Mikumi, Manyoni – Singida, Mtwara – Nachingwea, Ruo- - Chilungura hadi Masasi, Msagali – Kongwa, Murwazi hadi Ruvu kuunganisha Reli ya Kati na Reli ya Tanga; na hiyo ndiyo iliyokuwa ya Mwisho ya Tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa baadaye baada ya uhuru baadhi ya reli tulizing'oa kwa sababu mbalimbali; lakini wenzetu walikuwa na mfuatano mzuri. Hata hivyo kwenye mfuatano huo baada ya uhuru walikuwa wanataka kuendelea kujenga reli mbili. Kulikuwa na Reli kutoka Arusha – Ufyome - Mbulu Kupitia Kondoa hadi Dodoma. Je, kama wakoloni walikuwa na mpango huo je, sisi baada ya kupata uhuru tuliona kwamba haufai tukaamua kuuacha kabisa? au tuna mpango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kulikuwa na Reli nyingine ya kutoka Arusha kupita *Mount* Kilimajaro Magharibi mpaka Jado Kenya kwa ajili ya kuunganishe na ile Reli ya Kenya Kwenda Uganda, nayo hivyo hivyo baada ya Uuuru tuliiacha. Je, kwenye mipango ya sasa hivi tunaona kwamba hizo Reli bado hazifai au namna gani kwenye mfuatano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ni kuhusu Tume ya Mipango. Tume ya Mipango ni Tume muhimu sana kuwepo ndani ya Serikali. Tulifanya kosa kuiondoa. Sasa mimi naomba Serikali ije na mkakati mzuri wa namna gani Tume ya Mipango i-*operate* ndani ya nchi ili itusaidie kuratibu mipango yote na itusaidie kwenye eneo la ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kushauri Serikali ni kuhusu wakandarasi. Wakandarasi wetu tumekuwa hatuwapi jukumu la uwajibikaji kwenye viwango *(standards)*. Katika nchi nyingine kama Malaysia wana taasisi mbili ambazo zinasimamia kwa mfano barabara wana taasisi mbili tu. Taasisi ya kwanza ni taasisi ambayo inatafuta fedha za barabara. Hiyo taasisi ndiyo inayoingia Mkataba wa ujenzi. Halafu taasisi ya pili ni ile ambayo inasimamia viwango, *quality control.* Yaani anaingia Mkataba huku akienda huku anasimamiwa na *quality controller* ambaye anasaini naye mkataba mwingine unaitwa *quality covenant.* Kwa hiyo, yule Mkandarasi anakuwa amepewa wajibu wa kuhakikisha kwamba ile barabara anayoijenga *quality* ni wajibu wake. Akijenga *quality* mbaya yeye atalipa *in full.* Sasa sisi tumekuwa hatuwapi wajibu wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa napenda kushauri, wataalamu wetu wananisikia huko, wahakikishe kwamba waende hata Malaysia wakajifunze jamaa zetu wanavyofanya kule namna ya kusimamia ile *quality control* ili uwe wajibu wa Mkandarasi kuhakikisha kwamba ana-*deliver*

kitu ambacho kina kiwango kinachotakiwa kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashkuru sana, ahasante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, nilimwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE.** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza nizishukuru Kamati zote mbili. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nina mambo kama matatu ya kuchangia. Ningeomba nianze na jambo la *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Serikali ni kuwaibika kwa wananchi wake, sielewi ni kitu gani kinafanyika kwenye jambo la *NIDA* mimi sielewi mpaka leo. Tangu mwaka 2012 mpaka leo, miaka 11, vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* ni asilimia 30.08 tu ambayo imekamlilika. Kwa mujibu wa taarifa zilizoko hapa za Kamati, watu waliotegemewa kuandikishwa ni milioni 34,080,610 na walioandikishwa na kupewa vitambulisho vya namba yaani kwa maana ya kupewa namba ni milioni 19,634,720 maana yake ni kwamba watu milioni 14,445,000 mpaka leo haijulikana wana namba au wana nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo waliopata vitambulisho ni 10,230,710 na milioni 9,400,004 hawajapata, hiyo ni asilimia 30 kwa hesabu zilizoko hapa. Sasa mimi najiuliza; vitambulisho vya *NIDA* ndiyo maisha ya Watanzania sasa hivi. Yaani kila kitu leo ni *NIDA*. Uende benki, uende kila mahali. Sasa najiuliza, hivi *sustainability* ya Vitambulisho vya Taifa ni ipi sasa? Kama milioni 34 imeshindikana, je, tukisema watu umri wa miaka 18 mpaka 85 pengine milioni 50 vitatengenezwa vitambulisho vya Taifa kwa miaka mingapi?

Sasa nashindwa kuelewa hivi kitambulisho kimoja cha taifa ni bei gani? Ambayo inaweza kutosha tukasema tunatoa Bilioni 3 au Trilioni 3 tukamaliza tatizo lote la vitambulisho vya taifa kwa hawa watu 34?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kata zangu kwenye Kata ya Mgeta, Kata ya Zalama, Kata ya Mihigo, Kata ya Mihunyali, Kata ya Uhunyali na Kata ya Mang'uta, Nyamuswa hivyo vyote ni asilimia 25 tu wamepata vitambulisho. Kuna kata moja asilimia sijui tatu, hamna vitambulisho vya Taifa na wimbo umekuwepo, wimbo, wimbo, tutauimba mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanadai vitambulisho vya Taifa mpaka lini na taasisi zipo na fedha wanasema walishatoa zipo? Nataka kutoa ushauri kwa wale ambao tumeandikisha vitambulisho vya Taifa kwenye wilaya zetu na kwenye majimbo yetu…

**MBUNGE FULANI:** Taarifa

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa ushauri kwenye majimbo yetu kwamba Serikali sasa iangalie kila jimbo kwa kila halmashauri ambazo zimeandikisha vitambulisho vya Taifa, idadi kiasi gani, wajue kwamba ni kiasi gani cha vitambulisho vya Taifa ambavyo havijatoka, waende watoe huko huko vijulikane na bajeti ijayo au Bunge linalokuja tuambiwe sasa, hili suala la vitambulisho vya Taifa lina mwisho wake, ni lini litaisha sasa? Kwa sababu sasa imekuwa kesi hii? Hatuwezi kuwa na nchi ambayo ina vitu vidogo vidogo vinaathiri maisha ya watu, wanahangaika huko, tukubaliane sasa hii kazi inaisha lini? Nadhani maazimio yaje hapo watuambie hii kazi inaisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye jambo lingine la mfumko wa bei. Sijui kama tunadanganyana au tunaangalia Taifa. Kutokana na *covid 19*, nchi zote duniani uchumi wao ulishuka kuanzia asilimia mbili mpaka asilimia

saba na mfumko wa bei Nchi yetu ya Tanzania uko nafuu kidogo, sijui kama tunaangalia hili au tuna matatizo. Mfumko wa bei kwa Tanzania unalinganishwa na nani unaposema ni mkubwa? Kwa sababu uchumi ukishuka lazima kuwe na mambo kama hayo. Niseme tu kwwenye uchumi wa sasa kwa mfumko wa bei nchi yetu ni nafuu ukilinganisha na nchi zingine. Tunatazama leo hakuna mtu anadanganywa, lipo wazi hilo, hakuna haja ya kudanganyana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa hilo kwamba mfumko wa bei kwa nchi yetu mara nyingi tunasema ni vyakula, najua hali ikienda vizuri kama ninavyoiona kwenye maeneo mbalimbali kwenye halmashauri, vyakula vitakuwepo na bei ya vyakula itashuka, lakini kuna kitu nakiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Mchumi lakini Wachumi wako humu wataniambia hivi kama tuna ujenzi wa miradi mikubwa kama Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, Mradi wa Reli, Bandari, Vituo vya Afya, Hospitali na Barabara na miradi mingine mingi mikubwa. Kama tunayo miradi mikubwa inayochukua sementi kwa wingi sana, inayochukua nondo kwa wingi sana, inayochukua mabati kwa wingi sana, inayochukua misumari kwa wingi sana, hivi tunategemea mfumko wa bei kwa vifaa vya ujenzi utashuka? Hauwezi kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoona ni kwamba lazima sasa Serikali itengeneze mpango maalum wa viwanda ambavyo vinazalisha sementi kwa ajili ya miradi mikubwa na viwanda ambavyo vitabaki kwa wananchi vinginevyo kama ni hivyo, hivyo viwanda vitakufa vyote kwa sababu vina bei, hata miradi mikubwa ina bei kubwa au nafuu kuchukua kwa haraka zaidi watauzia kwenye miradi mikubwa, wananchi wataendelea kuhangaika na bei kubwa. Kwa hiyo, tuangalie ni viwanda gani vinazalisha kwa wingi na vizalishe kwenye kiwango kinachotakiwa ili wananchi wabaki na sementi na

miradi mikubwa ibaki na sementi. Kwa hiyo nafikiria kwamba kwa hilo naomba niishauri Serikali namna ya kufanya kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilizungumzie ni deni la Taifa. Ni kweli deni hili ni himilivu kama tunavyoambiwa, lakini ni himilivu mpaka lini? Ni nani atakuja kupata *burden* ya deni, ni lazima tujifunge mikanda kuona kama deni hilo linakua kwa kasi tuone namna ya kulipunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo Mchumi pia ila nataka nishauri kwenye eneo hilo, kwa mfano kama leo tunalipa madeni kwa bilioni tisa, halafu tukakopa deni la masharti nafuu, tukawa tunalipa kwa bilioni nne. Halafu ile hela tuliyokopa kwa masharti nafuu tukalipa lile ambalo lina masharti magumu halafu tukabaki na salio, labda kwa mwezi tukawa tunalipa bilioni nne badala ya kulipa bilioni tisa, kwani hapo Mheshimiwa Mwigulu wewe unaonaje hapo. Kwa nini tuwe na madeni makubwa kiasi hiki? Tuone madeni makubwa yenye masharti magumu, tukope madeni yenye masharti nafuu tulipe, yaani tulipe lile deni lenye masharti magumu tubaki na lenye masharti nafuu, ili tubaki na akiba ambayo tutafanya kazi nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, nilimwita Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, wakati huo Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Luhaga Mpina wanajiandaa.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kipekee namshukuru Mungu tuko hapa tunaongea mambo ya maendeleo ya nchi yetu. Nitamke rasmi kwamba ninaunga mkono hotuba zote za Kamati mbili hizo kamati ya NUU na Kamati ya Bajeti na nawapongeza sana Wenyeviti waliowasilisha hotuba hizo. Pia nawapongea

Wabunge wote kwa kuweza kuunga mkono na kuweza kuyazungumzia mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia mambo machache. Jambo la kwanza naomba nizungumzie kuhusu ile asilimia kumi ya mapato ambayo inatoka kwenye *local government* kwa ajili ya kuwawezesha wanawake asilimia nne, vijana asilimia nne na walemavu asilimia mbili. Makusanyo yalikuwa mazuri sana kipindi chote tunachozungumzia sasa, lakini kinachosikitisha ni kwamba hela ile yote haikugawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza hapa kuna kama bilioni 18 zilibaki Benki Kuu hazikuchukuliwa na hazikuchukuliwa kwa sababu gani? kwa sababu ambao wanastahili kupewa hawaku-*qualify* lakini *qualification* moja wapo ambayo iliwafanya wasipewe hela hizo ni pamoja na kutokuwa na vikundi rasmi vya kuchukua hela hiyo. Sasa shida yangu mimi mpaka nikaja kuizungumzia ni kwamba, je, tunapozungumzia vikundi viundwe, Serikali inasaidia nini kufanya hivyo vikundi vimeundwa na vikaweza ku-*access* hizo hela? Haina maana tuseme kwamba wanawake wamewezeshwa lakini hela ipo Benki Kuu, hela haitoki, basi hata wale wachangiaji hawakufanya jambo la maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali sasa iangalie kwamba kuna kila sababu ya kuweka elimu ya kuwawezesha hawa ambao wanatakiwa kuchukua hiyo hela yaani wanawake hao, vijana hao na hao walemavu kupata hiyo asilimia wanayotakiwa. Hii iko kote Tanzania nzima, lakini mbaya zaidi wachangiaji ambao ni halmashauri tofauti, wengine wamechangia asilimia pungufu. Bila kutamka ni halmashauri zipi lakini kuna waliochangia asilimia saba, wengine wakachangia asilimia tano. Ni nani hasa anayetakiwa kuweka msisitizo kwamba lazima iwe asilimia kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linashangaza na tuliliona kwenye Kamati ni ile kwamba unakuta sasa hela hiyo imeshatolewa na halmashauri, inakuwa kwenye *suspense,* lakini zinakuja shughuli za dharura au Mwenge unapita, ile hela asilimia kumi ambayo haijakopeshwa inapelekwa kwenye shughuli kama hiyo. Hili siyo jambo zuri, hili tunadanganywa, halijakaa vizuri kabisa, kwa nini hela hiyo ya watu hawa mlioona kwamba wao hawana *security* ya kukopa benki wanatakiwa kusaidiwa uchukue hiyo hela upeleke kwenye mwenge, siyo jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wanzangu Waheshimiwa Wabunge ambao pia ni Waheshimiwa Madiwani wasimamie jambo hili. Hela hiyo inatoka kwa ajili ya wanawake, vijana na walemavu iende kwenye shughuli hiyo. Tusikubali hata senti moja ikaenda kwenye shughuli ambayo siyo. Hil limetokea kwenye halmashauri nyingi, tumesomewa, tumeiona na kwa pamoja tuliona kwamba hilo jambo siyo zuri na pia lisiwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumekuwa tukilizungumza hapa kila kukicha na bado tunaliona ni tatizo japo lilizungumziwa katika changamoto ambazo tulitarajia zingetatuliwa kipindi kilichopita lakini zikatatuliwa kwa asilimia kidogo sana, ni mikopo ya wafanyakazi kuwa na *interest rate* inayolingana na mikopo ya wafanyabiashara. Hili jambo liko Tanzania tu na ni kwa nini iwe hivyo? Kama taasisi binafsi yakiwemo mabenki yanakopesha basi yatofautishe, *risk* zilizopo kuwakopesha wafanya kazi na *risk* zilizopo kuwakopesha wafanyabiashara. Hapo unakuta kwamba mikopo hii imewekewa *insurance*, lakini utakuta kwamba mfanyakazi ambaye mshahara unakatwa kabla hata hajapewa yeye mwenyewe kwenda kulipia mkopo wake anachajiwa *interest rate* inayolingana na na *commercial rate.* Tumewaomba sana Wizara ya Fedha isimamie jambo hilo wamesema watafanya miaka nenda rudi, sasa kwa nini wafanya kazi wawe shamba la bibi?

Haingii akilini, naomba sana hili jambo liangaliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ukiwa mfanyabiashara umebeba riski nyingi sana mpaka waje wakufuate kwako, wafuatilie, ni tofauti na mfanyakazi ambaye unaletewa na mwajiri kwamba bwana mshahara wake umeingia lipia hapo. Kwa hiyo naomba jambo hilo nalo niliweke wazi kwamba ni vyema kabisa ikaonekana kwamba hawa watu waangaliwe tofauti na mikopo ya wafanyakazi napendekeza na tuliona hivo iwe *single digit,* wala isifike kwenye kumi au kumi na, hamna sababu na kwa sababu inarejeshwa yote na pale ambapo anakufa, basi insurance inalipa. Naomba sana hilo tuliangalie na nadhani linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo niliona ni vyema nilizungumzie ni akiba ya fedha za kigeni. Ilipofikia mwaka jana Juni tulikuwa na Dola za Kimarekani milioni 510.3 ambayo ilikuwa pungufu kwa ilivyokuwa mwaka 2021 ambayo likuwa ni milioni 5,209.8. Kupungua kwa fedha za kigeni kunaathiri mfumko wa bei, kwa hiyo kama Kamati na mimi mwenyewe nasisitiza kwamba kuweka akiba ya *forex,* kutumia dhahabu ni kitu bora zaidi kwa sababu haibadilikibadiliki wakati ambapo thamani inabadilika. Kwa hiyo basi, napendekeza na nasisitiza tuwekeze hela zetu kwenye dhahabu na katika *forex reserve* yetu kwenye dhahabu. Hili jambo tuliliongea mwaka juzi, mwaka jana na tunaliongea mwaka huu, nataraji Serikali itatusikia, ione kwamba hilo pendekezo ni muhimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, wakati huo Mheshimiwa Luhaga Mpina anajiandaa.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Kamati hizi mbili, lakini kwa sababu ya ufinyu wa muda, nitachangia kwenye Kamati ya Bajeti peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna suala geni ninaliongea, ni masuala ambayo tumeshayaongea hapa kuanzia wakati mpango wa Serikali unaletwa, wakati wa bajeti tunayaongea na bado hayajapata majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kwenye kipengele 2:1:4 cha Taarifa ya Bajeti ambacho kinapatikana ukurasa wa 10 ambacho msemaji aliyetoka kuongea amekigusia au ndio amemalizia kinachohusiana na akiba ya fedha za kigeni, lakini nitaongelea pia au nitafungamanisha na kipengele 2:4:1 kilichopo ukurasa wa 25 kinachosema kutotabirika kwa Sera za Kodi na namna mambo haya yanavyoweza kusababisha biashara kudorora nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku mbili, tatu zilizopita kuna mchangiaji alisema humu kwamba kuna uhaba mkubwa wa fedha za kigeni hasa dola kwenye mabenki yetu. Wako wafanyabiashara na kuna Wabunge wafanyabiashara wamekwenda benki inachukulia hata wiki mbili kwa Dola laki moja na hili limeendelea na maeneo mengine unashawishiwa angalau mteja wako unayetaka kufanya naye biashara kwa Dola umshawishi aweze kuchukua fedha nyingine kama *Euro* na kadhalika. Sasa hatujapata majibu ya kutosha kwamba huu upungufu wa fedha za kigeni huku kwa wafanyabiashara unatokana na nini? Kwenye taarifa hapa inaonekana tuna fedha za kigeni za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naifunganisha na kipengele 2:4:1, kutokutabilika kwa Sera za Kodi. Nataka kusema kwamba siyo Sera za Kodi tu lakini ni sera za uendeshaji katika nchi hii. Tulifanya *operation* ya kuondoa *Bureau De Change,* tukafunga *Bureau De Change* na

kunyang'anya watu hela na nyaraka nyingine zilichukuliwa na tukasema kwamba sasa benki ndio zitafanya hiyo biashara na watu wakakubali, lakini kumekuwepo na utaratibu wa watu wachache kupewa leseni za *bureau de change.* Wako watu wengi wamekidhi vigezo vipya lakini hawapewi leseni za *bureau de change*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siko tena kule kwenye kuuliza warudishiwe leseni, kule nimeshaona kwamba haiwezekani kwamba warudishiwe fedha zao, lakini wako ambao aidha walikuwa katika lile kundi la mwanzo au wengine wapya wamekidhi vigezo vyote vilivyowekwa kwenye maandishi lakini hawajapata. Nina uhakika na ushahidi wa watu saba, wanapojibiwa kwamba *do not meet seat and proper test,* yaani unajibiwa hivyo tu, mtu ana hela, mtu anafanya biashara nyingine, mtu analipa kodi, mtu amewekeza kwenye maeneo kedekede, lakini kwenye *Bureau De Change* anajibiwa hivyo tu au wengine wanaambiwa wana *integrity issues,* haielezwi. Sasa sijaelewa ipo kwenye kanuni, ni utashi wa Wizara au ni utashi gani, lakini tunaleta usumbufu mkubwa, watu wanahangaika na hatujui twende kwa nani?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea kuchangia.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongelea suala la *Bureau De Change* nikiongelea Moshi Mjini na Arusha hatuongelei tu hawa wafanyabiashara wakubwa, tunaongalea *Porter and Tour Guider* aliyetoka porini au mlimani ameingia pale mjini saa kumi amelipwa *tip* yake kwa Dola anataka kubadilisha anunue nyama aende nyumbani hana mahali pa kubadilisha hiyo hela na ni kwa nini? Kwa sababu *Bureau De Change* zimezuiwa na benki hazifungui baada ya ule muda wa kawaida wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa Waziri atuambie, Serikali ituambie, kuna siri gani kwenye *issue* ya *Bureau De Change?* Kwa nini leseni wamepewa watu wachache? Watu wengine wanakwenda wanajibiwa kirahisi na hakuna majibu na watu wanateseka na dola hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa zaidi, *Bureau De Change* walikuwa wana-*change currency* mpaka 20, lakini kwenye mabenki wana-*change currency* chache sana, Kenyan *money* ni baadhi ya benki kama *KCB, Euro*, dola, *paund currency* nyingine hawabadilishi, lakini tunajua kwamba kuna watu wetu wanakwenda hija wanahitaji hela, kuna watu wetu wanakwenda Dubai, wanahitaji hela ya Dubai, kuna watu wetu wanakwenda South africa wanahitaji hela ya South Africa, lakini mabenki yamejikita kwenye *currency* chache. Kwa hiyo ningependa sana Serikali itoe wingu kwenye suala la *Bureau De Change* kwa sababu linasababisha hasara kubwa, linasababisha usumbufu kwa wananchi na linawasababisha wafanyabiashara kushindwa kufanya biashara zao kwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ningependa kuiongelea ni kipengele 2:1:2 ambacho kiko ukurasa wa saba, linalohusiana na mfumko wa bei. Nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hela anayotoa kwa ajili ya ku-*subsidi*ze mafuta. Nimeona taarifa juzi Wizara ya Kilimo nayo imesema italeta mahindi mtaani kwa Sh.700 kwa kilo. Kwa kweli hizo ni juhudi kubwa sana za Serikali, lakini ukiangalia kwenye jedwali lililoko hapa katika mfumko wa bei, jedwali namba moja kwenye Taarifa ya Bajeti, inaonyesha chakula ndio kimekwenda asilimia 9.7 kwenye mfumko na chakula siyo mahindi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunathamini sana mchango wa Serikali kupunguza hayo makali, lakini jicho zaidi litupiwe kwenye chakula, ni dhahiri kabisa *purchasing power* ya chakula Tanzania na Kenya zinatofautiana kwa sababu

uchumi wake ni mkubwa. Kenya wana *demand* kubwa kwa sababu chakula chao hakiendi kwenda kuliwa, kinaenda kulisha viwanda na wana-*export*. Kwa hiyo wanaweza kununua kwa bei kubwa, tukiachia uhuru asilimia mia moja watu wetu watakufa njaa, lazima kuwe na *control mechanism* ya kuhakikisha chakula kinapata bei nzuri kwa namna ambavyo Serikali itaona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunakushukuru Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Nilimwita Mheshimiwa Luhaga Mpina, wakati huo Mheshimiwa Subira Hamisi Mgalu na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo wanajiandaa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ili niweze kuchangia kwa hizi Kamati zote mbili Kamati ya Bajeti na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na nianze kwa kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati hizi kwa taarifa zao nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nivipongeze sana Vyombo vya Dola na Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri sana ambavyo vinaendelea kufanya hapa nchini. Pia niwapongeze kwa hili, ajira zinazotolewa sasa hivi za Polisi, Magereza, Zimamoto pamoja na Uhamiaji ambazo zimetolewa ajira nyingi kwa wingi, vijana wetu wengi waliokosa ajira sasa watapata ajira. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Serikali katika hili na najua sharti kubwa lilikuwa la vijana wale wa JKT na wengine wapo kwenye vikosi kule tunawatakia kila la kheri sana kwa ajili ya kwenda kulijenga Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba niunge mkono sana pendekezo la Kamati la kurejesha Tume ya Mipango ili

tuwe na *think tank* ya Taifa katika kugakikisha kwamba mipango yetu inakuwa iko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato, nilipokea taarifa za mapato ya *TRA* ya mwezi wa kumi na mbili, naamini kama sikosei takwimu zangu yalikuwa yamefikia shilingi trilioni 2.5. Nawapongeza sana kwa hatua hiyo. Moja ya sababu ilizungumzwa hapa kwamba ni baada ya wao kuwa wameajiri watumishi 1,500 wakaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge tulishauri hapa, Serikali imeenda kutimiza. Tulihoji, kwa nini watu waliokabidhiwa jukumu kubwa la ku-*service* deni la Taifa, waliokabidhiwa jukumu kubwa la kulipa mishahara halafu wawe na tatizo la upungufu wa watumishi? Tunawataka sasa waendelee hivyo hivyo, hata ule ushauri uliotolewa kwamba waajiri hata vijana wa mkataba, vijana wetu wengi waliosemea kodi na pia tunao vijana wengi wa JKT kwenye vikosi vya kijeshi ambao wanaweza kuungana na hizi timu kwenda kuhakikisha maeneo yote ambao tunaweza tukapoteza mapato kwenye mipaka yetu, kwenye maeneo ya maji, bandari bubu na maeneo yote ambayo kuna ukwepaji mkubwa wa kodi, waweze kwenda kudhibiti maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu akiba ya fedha za kigeni, wenzangu wamezungumza hapa. Ukweli ni kwamba fedha za kigeni zimeshuka kutoka Shilingi milioni 5,209.8 hadi Shilingi milioni 5,110.3. Hili ni anguko la mwaka mmoja. Kama tusipoziba ufa, tutajenga ukuta. Uchumi wetu hauwezi kuimarika kama fedha za kigeni zinadondoka kwa kiwango hicho. Tutahimili vipi kulipa deni la Taifa? Tutahimili vipi kuagiza bidhaa kutoka nje? Kama unavyosikia sasa hivi wafanyabiashara wameanza kulalamika hawapati Dola; lakini tutahimili vipi uwekezaji hapa nchini? Kama mikataba mingine tumeingia ya Dola, tutahimili vipi kuweza ku-*manage* mikataba hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha hizi za kigeni zitaendelea kupotea, maana yake *Tanzanian Shilling* itaendelea kupoteza thamani, itaadimika. Kama *Tanzanian Shilling* itaendelea kuadimika, lazima tutakuwa tumechochea mfumuko wa bei kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zipo mbili tu katika hili eneo. Moja, usimamizi hafifu wa Sera za Fedha na Bajeti ambayo ni *Monentary and Fiscal Policy* lakini pia na ile *Balance of Payment.* Sasa tuliposema hapa, Waziri wa Fedha akazungumza kwamba labda kazi tunayoiweza ni Uganga wa Kienyeji, lakini hizi ndizo takwaimu ambazo zimezalishwa na taasisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuchukue hizo hatua sasa za kuhakikisha kwamba tunaweka pendekezo lingine kali sana hapa kwa ajili ya ulinzi wa hizo fedha zetu za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya Serikali nje ya bajeti, Waziri wa Fedha siku hiyo alizungumza hapa kwamba Shilingi bilioni 246 zimetumika nje ya bajeti, lakini pia ruzuku ya mafuta, Shilingi bilioni 700, hizo fedha hazimo kwenye bajeti. Pia, akazungumza kwamba Shilingi bilioni 360 alizolipwa *SYMBION* kama *CAG* alivyosema siyo hizo, lakini pia hakutaja ni shilingi ngapi yeye anazozijua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea fedha hizi zote ambazo Serikali imetumia nje ya bajeti, ingekuwa imezipeleka kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kwenda kuangalia uhalali wake ili Kamati ya Bajeti ikubaliane nazo na kuzipitisha, lakini sasa hivi taarifa ya Kamati ya Bajeti haya yote hayamo. Maana yake Serikali imetumia fedha nje ya bajeti kinyume cha sheria, kinyume cha utaratibu na utaratibu unaofuata pale unajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Kamati ya bajeti wanatakiwa watusaidie. Kwanza tuweke azimio la kuitaka

Serikali ilete matumizi yote ambayo yamefanyika nje ya bajeti halafu sasa kuanzia hapo Bunge lako Tukufu hili liweze kuchukua hatua zinazostahili kwa Waziri wa Fedha aliyesabibisha mkwamo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la Serikali, ukweli kabisa nilitegemea Kamati ya Bajeti wangetuondoa kwenye mkwamo huu. Tulilalamika kwamba Deni la Serikali kwanini limeongezeka kwa kasi? Swali la pili, kwanini deni la Serikali inaonekana kwamba kuna madeni ambayo Serikali imeingia zaidi ya kiwango ambacho kimeidhinishwa na Bunge? Sasa tulitegemea leo Kamati ya Bajeti wangekuja na madeni yote. Wangekuja na jedwali linaloonesha Serikali imekopa fedha kiasi gani na kwa ajili ya miradi gani katika kipindi hiki tunachokizungumza, lakini kwa ulinganifu na zile takwimu zilizowasilishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Aprili, 2021 mpaka Juni, 2022 ongezeko la deni la Taifa limekua kwa Shilingi trilioni 10.83, lakini kipindi cha Mei na Juni, 2021 Serikali ilikopa zaidi ya Shilingi trilioni 3.9. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 na 2021/2022, deni la Taifa lilikuwa linakua kwa wastani wa 4% lakini kwa sasa hivi deni la Serikali linakua katika miaka hiyo miaka miwili,...

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, subiri taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**T A A R I F A**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Mpina, na kwa kuwa taarifa iliyoko hapa ni ya Kamati ya Bajeti ambayo pamoja na mambo mengine inashughulikia

masuala haya ya fedha; kama unavyojua Kamati yetu ilikuwa inashughulikia masuala ya Kero za Muungano na mpaka sasa taarifa yake haijawekwa hadharani na baadhi ya maeneo mengine yalikuwa yanahusiana na fedha na mpaka sasa nchi na Bunge halijatoa taarifa juu ya masuala yanayohusiana na fedha ambayo imeridhiwa katika Kamati ya Kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwanini Kamati hii ambayo ingetumia fursa hii kutupa picha halisi na Serikali iweze kutupa na kanuni zinazotumika katika kugawanya fedha nyingine za Muungano katika pande zote mbili zikiwemo fedha za UVIKO ambazo tulizipata hivi karibuni tujue kanuni ambayo inatumika ili tuweze kuishauri Serikali vizuri katika masuala haya ambayo ni lazima yalindwe kwa wivu wa hali ya juu na pande zote mbili za Muungano ziweze kuridhika maana ndiyo msingi wa umoja na mshikamano wa dhati katika nchi yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, unaipokea taarifa?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina unaipokea taarifa au hupokei?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa. Naomba unilindie muda wangu. Nimesema deni la Taifa lilikuwa likikua kwa wastani wa 4% lakini kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022 sasa linakua kwa 12.33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa, Kamati imesema katika jedwali Na. 2 lililowasilishwa na Kamati ya Bajeti, ukifanya hesabu pale inaonekana kwamba Serikali imekopa zaidi ya Shilingi bilioni 322 nje ya kiwango kilichoruhusiwa na Bunge. Ukiangalia pale kwenye jedwali, ni zaidi ya Shilingi

bilioni 322. Pia Serikali imeenda kukopa, iliidhinishiwa hapa na Bunge kwenda kukopa mikopo ya ndani kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya maendeleo Shilingi trilioni 1.84, lakini Serikali ikaenda kukopa Shilingi trilioni 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya Shilingi trilioni moja. Maamuzi hayo yanasababisha sekta zetu za fedha za ndani zisiweze kupata mikopo. Pia inachochea kuongezeka kwa riba. Kama inasababisha kuongezeka kwa riba, lazima utegemee kuna mfumuko mkubwa wa bei tunaouandaa. Ndiyo maana nasema, usimamizi hafifu wa Sera za Fedha na Bajeti *(Monetary and Fiscal Policy)* katika nchi yetu sasa hivi umetamalaki sana. Naamini kwamba kuna shida katika utekelezaji wa Wizara ya Fedha kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana tunaposimama hapa Bungeni na mbele ya Bunge lako Tukufu, Mbunge unaambiwa kwamba wewe hujui uchumi, Mbunge eti wewe unaweza kuchangia tu kuhusu uganga wa kienyeji na kwamba mchumi ni mmoja tu katika nchi hii. Aliyesoma uchumi ni Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba peke yake ndio anayeujua uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanasemwa kwenye Bunge lako. Ni muhimu sana kusikiliza haya ambayo tunachangia.

*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye mfumuko wa bei ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina muda wako umeisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

**MWENYEKITI:** Nakuongeza dakika moja kwa ajili ya kuhitimisha hoja yako.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea, katakata ya umeme na ruzuku ya mafuta. Maeneo haya ni nyeti sana ambayo yame-*attract* sana mfumuko wa bei hapa nchini. Naomba jambo moja, wafanyabiashara wetu wote ambao wanadai leo malimbikizo ya mbolea ni Shilingi ngapi? Mbolea ya ruzuku iliyosambazwa mpaka sasa hivi kwa wananchi wetu ni tani ngapi? Kwanini Serikali imeshindwa kulipa fedha hizo na kusababisha wananchi wetu waendelee kuteseka na suala la mbolea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini kilichopelekea usumbufu mkubwa huu wa mbolea nchini ilhali Waziri wa Kilimo aliahidi hapa Bungeni kwamba *he is ready to bear any cost.* Akasema ruzuku inayokuja sasa hivi haitaibiwa, ruzuku inayokuja sasa hivi haitachakachuliwa, ruzuku inayokuja sasa hivi hatuwezi kuuziwa mbolea bandia, wananchi wetu mbolea yao haiwezi ikatoroshwa na wananchi watapata mbolea kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake leo wananchi wanapata mbolea kwa shida kubwa, wengine wanafia kwenye foleni, wengine wameshindwa kulima ambako tunategemea pia kilimo kitaanguza kutokana na maamuzi hayo tuliyoyafanya. Sasa Serikali ifanye jambo moja, suala hili la mbolea liletwe hapa Bungeni kwa ukubwa wake tulijadili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la katakata ya umeme ambayo haina utaratibu liletwe hapa Bungeni tulijadili kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 71(1)(a), kama utaniruhusu nisome: "bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpina wakati anachangia, amesema Serikali imekopa Shilingi trilioni 360, lakini akasema Serikali imekopa kuzidi kiwango cha wigo uliowekwa na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya hayana uhakika, na nimwombe sana Mheshimiwa Mpina kama ameyasema kwa kujua au kwa kutokujua na kama hana uhakika ni vizuri akayafuta na asipoyafuta tutakwenda kanuni inayofuata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, Kanuni ya 71 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimesema Shilingi trilioni 360 katika mchango wangu, *Hansard* itasema, na kama nimesema Shilingi trilioni 360 katika mazungumzo yangu yoyote, basi hiyo nitakuwa labda

nimeteleza kusema. Ninachokisema ni hivi, takwimu zote ninazotumia hapa, hakuna takwimu ya Mpina. Nilisema, ukichukua jedwali liliowasilishwa na Kamati ya Bajeti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, nafikiri umeshajibu, kwamba kama umejibu Shilingi trilioni 360, ni *slipping of the tongue*. Kwa hiyo, tumekuelewa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haimo kwenye *discussion* zangu zote.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza. Kwa hiyo, tunasema tumekuelewa kama umetamka hivyo, kwa maana umeshafuta. Hoja yetu ni kwamba, kama ungesimamia kwamba ulimaanisha, tungekwenda kwenye *Hansard,* tukiikuta tungekwenda kanuni inayofuatia. Kwa hiyo, tumeshakuelewa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nahitimisha kwa kusema hiyo…

**MWENYEKITI:** Umeshahitimisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshahitimisha eh? Haya, 360 haipo popote…

**MWENYEKITI:** Haya tunaendelea. Nilimwita Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa jioni ya leo nami kuchangia taarifa za Kamati zetu mbili zilizowasilishwa. Naunga mkono Kamati zote na kupongeza kazi nzuri iliyofanywa. Mchango wangu utajielekeza kwenye Kamati yetu ya Bajeti ambayo mimi pia ni Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze alipomalizia Mheshimiwa Mpina wakati wa mchango wake akirejea jedwali Na. 2. Kwa kuwa mchango wake umekuwa ukijielekeza kuigusa Taarifa ya Kamati na Kamati nzima ya Bajeti, ninachotaka kusema ni kwamba ukiangalia jedwali Na. 2 kwenye Taarifa yetu ya Kamati ukurasa wa 10, Serikali kwa mwaka huu wa fedha ulioishia 2022 haikukopa zaidi, kwa sababu ilitarajiwa mapato na matumizi kuwa shilingi trilioni 37.99 na walifanikiwa kupata shilingi trilioni 36.924. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye mikopo ya kibiashara kutoka nje Serikali ilitarajia kukopa Shilingi trilioni tatu ikakopa Shilingi trilioni 1.8 ikaziba nakisi kwenye mikopo ya kibiashara ya ndani. Kwa hiyo, imefanya tu ku- *offset*. Kwa hiyo, hakukuwa na changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ni kuhusu matumizi nje ya bajeti. Sheria ya Bajeti ya Kifungu Na. 43 kinaipa mamlaka Serikali kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni, lakini kwa kuwa mwaka wa fedha unaendelea ndiyo kwanza miezi sita, ninaamini kama kuna matumizi yaliyofanywa nje ya vifungu vilivyoidhinishwa na Bunge, bado ipo fursa Bunge hili hili kufanya mchakato utakaowasilishwa na kujadiliwa. Kwa hiyo, hakuna dhambi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine utajielekeza kwenye masuala mazima ya mapato na matumizi ya Serikali. Kwanza naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo inaendelea vizuri kwenye makusanyo ya mapato. Tumeona namna gani Serikali ikijitahidi. Nataka niseme katika mapato ya ndani ambayo yalikusanywa kwenye mwaka wa fedha ulioshia Juni, 2022 zaidi ya Shilingi trilioni 24, kati ya trilioni 25, asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia dhamana inayotumika kulipia mishahara shilingi trilioni nane, kulipia deni la nje ambalo halijakopwa sasa shilingi trilioni nane, matumizi

mengineyo Shilingi trilioni tano, unaona kama Serikali isingefanya maarifa mengine, fedha kwenye miradi ya maendeleo isingewezekana. Ninaposimama hapa, naipongeza Serikali kwa kupeleka zaidi ya shilingi trilioni 11 kutoka kwenye mapato ya ndani shilingi trilioni 11.55 kati ya shilingi trilioni 11.59, asilimia 99 kwa mara ya kwanza kwenye miradi mbali mbali na tumeiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, kulikuwa na hoja hapa, kwa kuwa Serikali labda ililipa *SYMBION* shilingi bilioni 356 pengine imechangia mfumuko wa bei, sikatai. ila je, hizi shilingi trilioni 11 zinazoenda kuchochea miradi ya maendeleo zinazowafikia wakandarasi wa kawaida, zinazosababisha ajira wa mafundi mchundo, kwa akina mama ntilie, zina mchango gani? Ni wazi kwamba pamoja na changamoto ya mfumuko wa bei lakini kama Serikali isingepeleka fedha nyingi za kutosha kutekeleza shughuli mbalimbali, ninaamini hali ingekuwa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasimama kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na kupambana na mfumuko wa bei, lakini imejielekeza kutekeleza miradi na wananchi wetu kupitia hiyo miradi wanapata pesa ambazo wanaweza kununua bidhaa ambazo bei yake imepanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeona jitihada kupitia ruzuku ya mbolea. Wametenga shilingi bilioni 150, lakini mpaka sasa hivi shilingi bilioni 190 zimetumika. Napenda kuthibitisha, mimi nimeona Mkoa wa Pwani mbolea ya ruzuku wananchi wakiipata na wakifurahi na wakiipongeza Serikali. Hiyo yote ni kushusha bei. Leo wananchi wanapata mbolea kwa nusu ya bei iliyokuwepo, yote hii ni mikakati ya kushusha bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kufufua Kampuni ya Mbolea Tanzania na kuipatia mtaji ambayo

imenunua mbolea na imeanza kusambazwa tarehe 25. Maana yake hata wale wafanyabiashara, waingizaji wa mbolea nchini watakapoona bei imeshuka kwenye Kampuni ya Serikali watashusha bei wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali sasa, hebu waangalie kwenye muktadha mzima wa chakula, hawawezi kuiitumia Bodi ya Mazao Mchanganyiko, nao wakanunua vyakula wakauza ili iweze kuchochea ushindani na kuweza kupunguza bei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali kwa mpango huo na kwa ruzuku inayoendelea kwenye mafuta. Ninaona dhamira njema ya kushughulikia mfumuko wa bei nchini kutokana na kazi mbalimbali wanazofanya. Sambamba na hilo, katika mwaka wa fedha unaoendelea Serikali iliondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye malighafi ya mbegu zinazozalisha mafuta hapa nchini na faida yake tumeona. Sasa hivi mafuta ya kula ya lita tano yanayozalishwa hapa nchini ni shilingi 27,000/= kutoka shilingi 35,000/= au shilingi 45,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, kwa niaba ya wanawake, watumiaji wa mafuta ya kula kwa hatua hizo. Niendelee kuwatia moyo waendelee kupambana kubuni, na Wabunge ndio washauri wa Serikali, tuisimamie Serikali, lakini sisi tutakapokuwa wa mfano kukataa kwa sababu ambazo ziko wazi, dunia nzima inasema Vita vya Ukraine na Urusi vimesababisha hali ngumu ya uchumi, sisi nani tukatae? Dunia nzima inashuhudia ukame, nchi yetu haijapata mvua misimu miwili, chakula kimezalishwa kidogo, kwa nini tukatae sababu za namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali ijikite kwenye matumizi ya mkopo wa shilingi trilioni 2.4, huu unaoendelea sasa, kwenye sekta ya kilimo, sekta ya uvuvi, sekta ya nishati na sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tumetoa mapendekezo mengi lakini dhima ya mkopo huu ni kuwezesha, kuzalisha mazao kuongeza mauzo nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni. Kuzalisha mazao ambayo yangeweza kuzalishwa hapa nchini tuache kuagiza nje ya nchi. Kwa hiyo, niwaombe Wizara zinazohusika mpaka sasa kama tulivyosema kwenye Kamati, mkipambana na mkopo huu ambao hauna riba, una *grace period* ya miaka mitano na nimpongeze na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayofanya, inaweza ikasaidia kushusha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu kwa mchango wako, nilimwita Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, wakati huo Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge wanajiandaa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie Kamati zetu mbili zilizowasilisha hapa leo, Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati yetu ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia upande wa taarifa iliyowasilishwa na Kamati yetu ya Bajeti na hususan ukurasa wa 62 wa taarifa, kipengele kile cha 6.5. Kamati inazungumzia ujenzi wa barabara kwa mfumo wa uhandisi, usanifu, manunuzi, ujenzi na utafutaji wa fedha kwa maana ya *EPC+F*. Ninaishukuru sana Serikali kwamba katika mpango huu ipo barabara maarufu ya Handeni - Kibilashi - Kiteto - Kondoa - Singida ambayo nayo imebahatika kuingia humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na barabara hizi tunazozijenga, lipo jambo moja la ajabu sana tunalifanya

kama Taifa. Nchi yetu ina mtandao wa barabara wenye thamani inazofikia Shilingi Trilioni 21. Barabara za kitaifa zina kilometa 36,361 na zina thamani ya Shilingi Trilioni 18. Barabara zetu za Wilaya zina mtandao wa kilometa 143,881 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 2.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza pamoja na kuwa na *asset* hii kubwa ya kitaifa inayosaidia uchumi wetu, hatuifanyii matengenezo. Hivi sasa barabara zetu za kitaifa zile kubwa na ambazo ndiyo mrija wa uchumi wetu zinahitaji matengenezo yanayokaribia Shilingi Trilioni 2.4 na Serikali imekuwa ikija hapa inadai haina fedha hizo za kukarabati barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tusipoliangalia litakuja kutuingiza kwenye gharama kubwa na litakuja kufanya uchumi wetu udhoofu, wananchi wetu wasafiri kwa shida, mizigo isafiri kwa taabu, vilevile watu waliopo kwenye sekta ya uendeshaji ya usafirishaji wataendesha shughuli zao kwa gharama kubwa sana ya kununua vipuli kwa sababu ya barabara mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano, athari ambazo zinaweza zikapatikana tukichelewa kufanya matengenezo ya barabara kwa kadri ya wataalam wanavyoelekeza. Miaka kadhaaa iliyopita tuliacha kufanya matengenezo ya barabara karibia 13, tukaziacha tu mwaka wa 11, 12 nyingine mpaka mwaka wa 20 tukaziacha. Matengenezo yale yalikuwa yagharimu Shilingi Bilioni 250, hatukufanya. Tulivyokuja kufanya, tumekuja kufanya matengenezo hayo kwa Shilingi Trilioni 1.28, ndiyo kusema tulikula hasara ya Shilingi Trilioni Moja nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sielewi kwanini Serikali inajivuta vuta na sielewi kwanini Serikali inajizungusha zungusha kukarabati barabara zetu hizi za kitaifa ambazo nakwenda kuzitaja hapa ziingie kwenye *Hansard* kwa kumbukumbu.

Barabara ya Kibaha - Mlandizi, Chalinze - Ngerengere, Melela - Iyovu, Igawa -Uyole, Uyole - Songwe, Mlandizi - Chalinze, Same - Himo, Himo - Arusha, Rusahunga - Rusumo, Shelui – Malendi - Nzega kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Nyanguge – Mwanza – Mara - *Border,* Makutano - Sirari, Usagara-Mwanza, Mtwara – Mingoyo - Masasi, Madaba - Makambako, Songea -Madaba, Ipole - Miemba, Rungwa - Ipole, Nzega - Manonga, Mwanza -Shinyanga - Usagara, Uyole - Kasumulu, Kobelo - Nyakasanza, Songea -Peramiho, Mikumi - Kidatu, Lupilo - Mahende na Himo-Marangu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi ukikuta barabara ya chini ina umri wa miaka 17. Barabara yenye umri mkubwa katika hizi kuliko zote ina umri wa miaka 37. Kwa nini tunakuwa hivi? Yaani ni kweli kwamba hatuoni umuhimu kabisa wa kutafuta hii Shilingi Trilioni 2.4 tukafanya ukarabati wa barabara hizi? Mfuko wetu wa Bodi ya Barabara, kwa mwaka makusanyo yake ni kama Shilingi Trilioni moja. Vyanzo vyake vya mapato ni tozo za mafuta ambazo zina-*constitute* karibia asilimia 97 ya fedha zote wanazopata, tozo za magari ya kigeni na tozo za kuzidisha uzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vyanzo hivi havitatosha kukarabati barabara zetu na barabara ukiitengeneza leo ukaikarabati unaipa uhai mrefu mwingine wa kuishi. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali na kwenye maazimio yetu kama Bunge tuweke maazimio kwamba Serikali lazima ije hapa na mapendekezo siku zijazo ya vyanzo vipya vingine vya mapato kwa ajili ya Bodi ya Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Barabara wanafikiria kutumia *infrastructure bond* kama sehemu mpya, nakubaliana nao ni chanzo kizuri, wanataka kwenda kutoza, kuweka tozo kwenye gesi asilia, kwenye yale magari ambayo yanatumia gesi asilia, siyo jambo baya. Wanataka kutoza kwenye *toll bridge* na wanataka kutumia hizi njia ya *EPC+F.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba nilishukuru barabara ya Handeni – Kibilashi - Kiteto kwenda kwenye hii njia ya *EPC+F,* kuna haja kubwa kama nchi, huu mfumo tunaotaka kuuendea wa *EPC+F* tukaupitia upya. *EPC+F* ina-*implication* moja kwa moja kwenye Deni la Taifa. Kwa hiyo, ni vizuri Bunge lako likaambiwa, kwa mfano zile barabara Nane ambazo zimetajwa kwamba zinajengwa kwa *EPC+F* mpango huo umefikia wapi na *implication* yake itakuwaje? Watawezaje ku-*spread* hiyo? Kuliko tukawa tunakuja hapa kuwaaminisha wananchi barabara zinajengwa halafu hazijengwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, nakushukuru sana, nilitamani kushauri eneo hilo, matengenezo ya barabara, Shilingi Trilioni 2.4, Serikali itoe maelezo na iweke kwenye mikakati yake kuja hapa na vyanzo vipya kwa ajili ya Bodi yetu ya Mfuko wa Barabara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei aweze kuchangia.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru sana na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na Baraza lake la Mawaziri kwa namna ambavyo wameweza kutuletea mafanikio kwenye mazingira ambayo ni magumu sana, mazingira ambayo hata nchi zile ambazo zina chumi komavu hazijaweza kuyakabili inavyostahili na kwa hiyo mfumuko wa bei kwenye nchi hizo kubwa, nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei uko juu ya tarakimu mbili na hapa kwetu unaona bado mfumuko wa bei ni takribani asilimia Tano au ni asilimia 4.8 na pia tunaendelea kukua kwa asilimia ambayo ni kubwa kuliko maeneo mengine na tumeweza kui-*stabilize* vizuri kwa namna moja au nyingine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kitu ambacho ni lazima tujivunie sana kwamba Serikali imefanya mambo ambayo lazima tufurahi kwamba inajizatiti na imeweka mifumo ambayo pengine kama itakuwa endelevu, kwa sababu tunaweza tukasema kwamba tumefanikisha lakini bado kuna viashiria kuna *risk* ambazo bado ziko kwenye uchumi ambavyo vinaweza vikapelekea hali ikabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafurahisha pia kwamba malengo ya bajeti kwa mantiki ya matumizi na mapato yake yamefikia kwenye asilimia kwa wastani wa 95, ni nzuri yaani hatuja-*miss* sana malengo yetu. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na viongozi wengine wa Wizara niliseme hiyo ni jambo la kufurahisha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli suala la visababishi vya mtikisiko kwenye chumi nyingi siyo suala ambalo linakuwa ni la muda mfupi, siyo la mpito kwa sababu hivi vita vya Ukraine vinaonekana vinaendelea na vitaendelea, hatuoni upeo wake vitaisha lini. Kwa hiyo, siyo jambo tu la kusema kwamba tutapigana kwa mambo ya dharura kwa kufanya mambo ya dharura kwa kutoa ruzuku na kadhalika ni jambo ambalo lazima tuliangalie kwa mapana yake kwamba tuchukue hatua madhubuti ili kusema kweli tusipoteze muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turuhusu kwamba vitu vifanyike kwa namna ambayo inastahili na katika kufanya maamuzi yoyote ambayo tunajua kanuni moja ya kufanya maamuzi ni kutathmini kama lile jambo ni la mpito au kama litakaa, kama litakaa basi maamuzi unatakiwa kufanya ni maamuzi ya ku-*accommodate* ile na kuruhusu uchumi uanze kwenda kwa namna nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwa mfano kwa upande wa suala zima la mfumuko wa bei. Mimi najiuliza tunatumia vigezo gani kulalamika sana? Kwa sababu asilimia Tano sisi

tulioishi miaka ya kale hiyo, tulikuwa na mfumuko wa bei asilimia 30 tukaishi nao, yaani ukiwa na hela inaishia huko huko kabla hata hujaamka. Kwa hiyo, sasa kama kweli mfumuko wa bei tarakimu tunazopewa ni za uhalisia, mimi naamini kwamba pengine watu hawangelalamika kiasi hicho! Naamini kuna tatizo aidha katika hiyo takwimu tunayopewa, haijawa ya uhalisia kwa sababu kama mfumuko wa bei ya mahindi ingepanda zaidi mara mbili, asilimia Moja na Tano katika kipindi cha Septemba 2022, unachelea kusema pengine kuna kitu, mfumuko wa bei ungekuwa kidogo uko juu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme kuna jambo ambalo tulijue kwamba kuna ile *base,* ile *index* yenyewe ambayo inatakiwa iwe na *episode* za kupanda juu lakini baadae unaanza kui-*stabilize* kwenye *level* tofauti. Kiwango kile kinakuwa kimepanda halafu unai-*stabilize* kwenye *level* ile na *inflation* sasa inakuwa kwenye *level* nyingine kwa sababu ile *index* imepanda, lakini sisi hatuangalii hivyo vitu. Kuna *two things,* kuna kupanda ile *index* na yale mabadiliko ya ile *index from time to time*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba hiyo ya kupanda, hiyo *spike* inatakiwa kwenye *index* ni nzuri mara nyingine. Kwa mfano, bei, nashukuru sana Mheshimiwa Mwigulu alisema siku moja, alisema mahali pengine sijui ni hapa, lakini ukweli ni kwamba bei za mazao ya wakulima zilikuwa chini sana kwa miaka mingi, miaka kama 10 hivi. Bei za mazao ya mahindi, mazao yote ambayo tunasema ni ya vyakula, zimekaa kama maji yaliyotulia. Sasa kwenye hali ya uchumi ya namna ile watu hawapati hamasa kuongeza uzalishaji, *it doesn't work.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka mwaka huu nikizalisha, nipate faida kubwa, inanirudisha kule kwenye shamba niongeze kilimo. Sasa unapoongeza kilimo, bei itashuka kidogo halafu bado ikishuka kidogo maana yake ni kwamba

watu watasema sasa kuna *glut,* yaani mazao yamekuwa mengi kwa hiyo watu wanayapunguza kidogo kuzalisha, wanakimbizana na vitu vingine halafu kipindi cha mwaka unaokuja wanaona tena kwamba aah! mbona bei zimeanza kupanda kwa sababu mazao yameshuka? Kwa hiyo, inakwenda namna hiyo na *that is the only how you can make agriculture pay.* Kilimo hakitalipa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mazao ya *export,* utaona kwamba pia *exchange rate* imekuwa *stable* sana. Tumesahau kwamba *exchange rate* pia ni *instrument* ya kutuwezesha kuendesha huu uchumi. Ili kuongeza faida ya *exporters,* watu wanaouza nje na hao wanaozalisha mazao ya kahawa, katani na kadhalika ni lazima *exchange rate* iwe ina-*move* ili akiuza akipata dola moja kule kwenye bei ya dunia haibadiliki sana. Utakuja kupata dola moja, inabakia Shilingi 2,300 kwa miaka mitano, utakuwa wewe gharama zinapanda lakini wewe hupati chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima ifike mahali pia Serikali na Benki Kuu ione kwamba kuna umuhimu wa kuchochea *exports* kwa kuruhusu mabadiliko stahili kwenye *exchange rate,* siyo kuifanya tu ikae *forever.* Kwa sababu uzuri mmoja wa kufanya vile, ile haitakuathiri sana kwenye mambo ya ulipaji wa madeni kwa sababu *export* zipo kwenye dola ile ile na deni liko kwenye dola ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme napongeza kukopa ndani zaidi kama tungekuwa kwa mfano, hiyo sekta binafsi haikopi, aidha sekta binafsi haikopi kwa zile riba ziko juu. Kwa sababu Serikali ikikopa *actually* deni linakuwa na uhimilivu zaidi kwa sababu deni la ndani halina tatizo la uhimilivu, lina tatizo la kukusanya tu mapato kwa sababu ni *domestic revenue,* lakini lile la nje lina tatizo kwa sababu lazima u-*generate dollars,* kama haujauza *exports* hutapata dola za kulipa zile dola na utapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *issue* ni kwamba lazima tukubali kwamba *exports* lazima ziongezeke kwa sababu lile deni tunalo na lazima tutalilipa na tutalilipa kwa madafu. Madafu ukiwa nayo lazima uyabadilishe yawe dola. Kwa hiyo, ni lazima tukazane na hiyo na ninaamini mfumo mzima wa kusema tukimbizane na kilimo ni sawa, lakini pia tukimbizane mimi nafikiri katika vipaumbele tunavyo vingi, vipaumbele ambavyo lazima tuvikazanie sana ni utalii ambao unaleta haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kina *risk* nyingi bado, hata ukijenga mabwawa, itajengwa kwa miaka mingapi uweze kuhamisha? Itachukua muda. Nadhani utalii, madini, mifugo utaona sasa hivi tuna-*export* nyama kwa wingi, mifugo na uvuvi pamoja pengine na madini, madini nimeshataja lakini naamini kwamba kuna ambavyo vipo najua kwamba ukifanya vitapiga. Ukisema utafanya hata ukiongeza itachukua muda na ile *chances* za ku-*realize the potential* ambayo wewe unalenga ni *may be is fifty fifty*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo la mwisho ukiniruhusu ni kwamba kuna hii mikopo ambayo imetengwa kwenye dirisha lile la Shilingi Trilioni Moja ambayo imetolewa wanasema Benki Kuu iko tayari kutoa, kusema kweli hiyo siyo *realistic*. Ukweli ni kwamba Benki Kuu Kifungu cha 40 cha Sheria ya Benki Kuu hakiruhusu Benki Kuu ikopeshe mabenki zaidi kwa kipindi zaidi ya miezi mitatu, sasa kilimo gani kinalimwa kwa miezi mitatu, hakuna! Mkimkopesha mtu utaenda kuvuna mazao yale ili akulipe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna tatizo hapo ni kwamba ni dirisha ambalo ni zuri lakini mimi naamini kwamba, hata hivyo wamewekea masharti kwamba lazima Benki ipeleke dhamana za Serikali, lakini ambacho wangefanya ni kwamba wangesema benki ilete mikopo ambayo imetoa kwa sekta binafsi kwa riba chini ya asilimia 10, walete hiyo

*portfolio* halafu wa i–*refinance* wakifanya hivyo, benki ambazo hazina hata hii dhamana zitakopesha zitapeleka ile mikopo ita-*refinance* watapewa fedha wataendelea kukopesha sehemu nyingine watapewa kwa hiyo asilimia Tatu. Kwa hiyo, *that is the only realistic way, otherwise* mimi nafikiri kwamba ni ngumu sana kupata mabenki ambayo yatakopa na kukopesha kama inavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba muda umekwisha, naunga mkono hoja, mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako Mheshimiwa Daktari Charles Stephen Kimei. Nilimtaja Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, wakati huo Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge pamoja na Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Ulenge anajiandaa.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya mimi pia kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kuhusiana na bajeti kimsingi tunazungumzia uwezo wa Serikali kuhimili, namna bora ya kuendesha shughuli za Serikali kwa maana ya miradi ya maendeleo na miradi ya kawaida, haya yote yanategemea sana uwezo wa Serikali kukusanya kodi na kodi inatoka kwenye shughuli za uzalishaji, hakuna maajabu katika uchumi ni kuzalisha ndiko ambako kunapelekea Serikali kuwa na uwezo wa kuuza bidhaa, ndani na nje ya nchi, kuvutia fedha za kigeni na kugharamia shughuli za maendeleo. Ndiyo maana Waziri wa Fedha alipokuwa anatuletea Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/2023, alijikita na alijielekeza katika mpango ule na hali ya uchumi kwenye sekta za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona Serikali ikiweka msukumo katika sekta za uzalishaji katika kilimo, mifugo,

nishati lakini pia katika ujenzi wa miundombinu ambayo inaweza kwenda kutusaidia katika kuimarisha uchumi wetu. Kwa maana ya reli ya mwendokasi - *SGR*, mradi mkubwa wa uzalishaji umeme wa kule Mwalimu Nyerere, ununuzi wa ndege za *ATCL*, miradi ya elimu, afya, maji, *regrow* kwa maana ya utalii na maliasili lakini pia teknolojia ya TEHAMA pamoja na sanaa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni mikakati ya ndani, ni sera za ndani katika kuimarisha uchumi wetu. Lakini sera hizi za ndani hatuwezi kwenda ku-*achieve* kama sera za nje hazita–*complement* jitihada za ndani. Kimsingi naweza kuzungumza kwamba hakuna kitu kinachoitwa sera za nje, sera za nje ni mwendelezo tu wa sera za ndani, kitu gani tunakitaka ndani na tunapataje nje, katika hilo wataalamu wetu ama wanadiplomasia wetu wanapaswa kuainisha misingi ambayo inaweza ikajenga mahusiano na nchi nyingine, katika kushawishi, kutetea maslahi yetu ya ndani ili tu–*achieve goals* za ndani kupitia mahusiano yetu ya nje. Kwa hiyo, sera za nje ukitafsiri ni uwezo wetu wa kutafsiri mikakati yetu ya ndani na jinsi gani tunaweza tukapata ama tuka-*achieve* nje. Tukatafsiri dunia pana kwa rasilimali zake kuona zinatujibu vipi changamoto zetu za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wizara ya Mambo ya Nje ni muhimu sana katika utekelezaji wa sera za ndani na mikakati yetu ya ndani. Sera ya nje ni lazima ijibu mikakati na shida zetu za ndani. Kwa hiyo utakuta katika hili unaweza kuona kwamba sera ya asili ya nchi yetu ilikuwa kusimama na wale wanaoonewa, kusimama na wanyonge kwa sababu tulijua uhuru wetu ulikuwa hatarini kama nchi nyingine za jirani hazitakombolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sera yetu ya nje kwenda kuzikomboa nchi jirani ili tujiimarishe na tusimamie usalama wetu sisi wa ndani, na ndiyo maana ndugu zetu

walikwenda vitani kukomboa nchi nyingine ili kuhakikisha kwamba tunalinda uhuru wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo usimamizi thabiti wa kanuni hii na nyinginezo wakati wa uhuru ndizo ambazo ziliipa heshima kubwa nchi yetu kwa sababu tulisimama na wanyonge lakini katika kulinda uhuru wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Mambo ya Nje si Biblia wala Msahafu, si Amri Kumi za Mungu, zinapaswa kubadilika kulingana na wakati. Na ndiyo maana tunaona kwamba mabadiliko ya fikra, mwenendo na mitazamo siku zote inabadilisha pia hata mikakati ya ku-*achieve* mambo yetu ya ndani kupitia mahusiano yetu ya nje. Na ndiyo maana mwaka 2001 tulikuja na kitu kinaitwa diplomasia ya uchumi. Dhana na lengo la diplomasia ya uchumi ni kuhakikisha kuwa mbali na malengo ya kidiplomasia, mfano kiulinzi, tunajikita katika kujenga na kuimarisha mahusiano na nchi nyingine kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu. Na katika hilo tunaweza kuona kwamba katika miongo miwili iliyopita tuliweza kuimarisha sana mahusiano yetu na ndiyo maana tuliweza kuvutia wawekezaji wengi na watalii wengi walikuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijielekeza katika kitabu cha mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 207 unatuelekeza kwamba diplomasia ya nchi yetu haitafungamana na upande wowote. Lengo ni kushirirkiana na nchi yoyote ambayo ina mapenzi mema ambayo matarajio yao na matumaini yetu yanaweza kukutana. Katika msingi huo diplomasia ya uchumi wetu ni lazima iwezeshe Tanzania kuwa kitovu cha uchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki pia katika Bara la Afrika kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo ni lazima turudi kwenye misingi ya asili kusimama na wale wanaoonewa. Sasa hivi unaweza kuona vita imetamalaki katika maeneo mengi katika nchi ambazo zinaendelea. Kule wanaoonewa

ni nani? wanaoonewa ni wafanyabiashara wakubwa ambao wamewekewa vikwazo hafanyi biashara kwa sababu tu wamezaliwa katika nchi fulani ambayo wengine hawaitaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule anayeonewa ni nani? ni wataalamu na *researches* ambao hawana uhuru wa ku-*practice* utaalamu wao kwa sababu tu wamezaliwa katika eneo fulani la kijiografia. Katika misingi hiyo sisi ambao tunasimama na hao ambao ni *victim* wa mambo ambayo yanaendelea tunafaidika vipi. Tunapaswa kutumia *loop hole* hiyo kuwavutia hapa kuja kufanya shughuli zao za kiuchumi, Kama ni wafanyabiashara wa waje walete fedha hapa kwa sababu huko kwao hazina usalama. Kama wana utaalamu wa kilimo waje walime hapa. Kwa mfano nchi kama Ukraine inalima sana alizeti. Sasa hivi hawawezi kulima, wakulima hao hawalimi, wataalam wao hawafanyi kazi. Kwa nini tusiwaonyeshe kwamba hapa kuna fursa ya kuja ku-*achieve* kile ambacho walikuwa wanakifanya katika nchi zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mitaji mingi kule nje sasa hivi ambayo imefungwa hawawezi kufanya biashara kwa sababu ya vita. Sisi kama Tanzania tunawezaje kutumia *loop hole* hiyo ku-*attract* hao watu kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru mwaka jana tuliona dhamira ya dhati ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alipowaita mabalozi wote wa Tanzania ambao wanawakilisha nchi zetu nje, aliwaita pale Zanzibar na alikaa nao kwa siku kadhaa. Moja ya vitu ambavyo vilinivutia ni mwelekeo mpya wa diplomasia yetu ya uchumi ambao ndio ulikuwa msingi wa mkutano ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi ambayo walijadili, walizungumzia nafasi ya Tanzania katika uchumi wa kimataifa. Katika hili naomba nizungumze kitu kimoja. Balozi zetu zina nafasi kubwa sana ya kutusaidia ku-

*achieve* malengo yetu ya ndani. Lakini tunapaswa kuangalia ni jinsi gani ya kushirikisha sekta binafsi; kwa sababu hatuwezi ku-*achieve* haya yote ambayo tunayataka kama tunawafanya sekta binafsi kuwa *bystanders*, kuwa watazamaji. Katika msingi huu hata *diaspora* ni sehemu muhimu sana ya utekelezaji wa sera yetu ya nje kama tutawashirikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ambacho kinatokea sasa hivi? Tuna mashirika makubwa ambayo yanashirikiana na utalii. Kwa nini Wizara ya Mambo ya Nje isi-*recruit* watu kutoka sekta binafsi ambao ni wataalamu wa sekta husika ambao wanaweza wakavutia mitaji, wataalamu wa masoko na biashara wakaenda kuwa *stationed* kwenye balozi zetu? Si lazima walipwe mshahara na Serikali na wala si lazima walipwe mshahara na hazina, wanaweza wakawa *vetted* wakawa *attached* kwenye balozi zetu wakafanya kazi ya kuvutia mitaji, kuweka masoko, kuweka mikakati ya kuleta watalii na shughuli nyingine na wanadiplomasia wetu wakajikita katika shughuli za kidiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini shughuli za kitaalamu tukatengeneza utaratibu wa sekta binafsi na taasisi za Serikali kushiriki moja kwa moja na kukaa katika balozi zetu wakiwa wanatumikia nchi yetu katika maeneo ambayo wamebobea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote ambayo wenzangu wametangulia kuzungumza bado naweza kuzungumza kwamba Tanzania tumebarikiwa kwa jiografia yetu, tupo katika eneo zuri sana la kiukanda. Kwa mfano Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa hivi ina nchi takribani saba, pamoja na Sudan ya Kusini na Congo. jumuiya hii ina watu zaidi ya milioni 300. Hii inatupa uhakika wa soko kubwa la bidhaa zetu lakini inatupa eneo la mkakati la kufanya mahusiano na wawekezaji wa nje. Hii ni kwa sababu tuna soko la pamoja tuna ushuru wa pamoja na uhuru wa

wafanyabiashara wetu kuzunguka na mitaji yao katika eneo la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuona nia ya dhati ya Rais wetu, mama yetu Samia Suluhu Hassan. Yeye pekee alifanikiwa kuondoa vikwazo takribani 64 kati ya 68 katika biashara yetu na Kenya. Kuondoa vikwazo hivi kumepelekea ongezeko la biashara kutoka bilioni 800 mwaka 2020 mpaka trilioni 1.2 mwaka 2021. Sasa haya unaweza kuona ni jinsi gani Rais wetu ameweza kuondoa hivi vikwazo na taasisi za Serikali, kwa mfano Wizara ya Mambo ya Nje kupitia balozi zetu zinaweza zika-*compliment* jitihada hizi katika nchi nyingine. Huu ni mfano mmoja lakini…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. DENNIS L. LONDO:…** tuna mifano mingi ambayo tunaweza tukaitumia katika ku-*attract* wawekezaji na kuimarisha miradi yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo sasa namwita Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge aweze kuchangia.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi jioni hii ili niweze kuchangia hoja za kamati mbili; Kamati ya Bajeti na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nitajikita zaidi kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na

Usalama. Nikianza kwa kupongeza kwa dhati kabisa viongozi wa wanaoongoza Wizara zinazosimamiwa na Kamati yetu hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; nikianza na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, mama mchapakazi Mheshimiwa Tax pongezi sana kazi nzuri na kwenye kamati kwa kweli umeonesha ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Balozi Mbarouk Naibu Waziri ameonesha ushirikiano wa kutosha kwenye Kamati na yote ambayo tumeyaleta kwenye Bunge ni mchango wa pamoja kati ya sisi Wanakamati pamoja na viongozi wetu hawa wakisaidiana na watendaji wao. Lakini Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu wa Ulinzi Bashungwa naye ameonesha uwezo mkubwa sana. Nadhani katika historia ya nchi hii anaweza akawa labda ni Waziri wa pili kijana kuongoza Wizara hii nyeti na ameonesha kumudu. Nikupongeze sana ndugu yangu Bashungwa wewe pamoja na watendaji wako Wizara inakwenda vyema na sisi wanakamati hatuna shaka na wewe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kutekeleza majumu yao kiasi kwamba Watanzania tumeshazoea kuwa nchi yetu ni nchi shwari, nchi yetu ni nchi ya amani, nchi yetu ni nchi yenye mtangamano, haina shida yoyote mashaka yoyote ukilinganisha na baadhi ya nchi katika bara letu la Afrika au kwingineko duniani. Haya yote hayajafika hapa Tanzania kwa bahati nasibu isipokuwa ni kazi ya dhati kabisa inayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi mimi nitandoa kwa uchache sana katika maeneo machache ambayo yamelegalega katika wizara zetu mbili hizi; kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pia pamoja na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na maeneo haya kimsingi hayakulegalega kwa sababu ya utendaji usioridhisha wa Waziri au watendaji katika Wizara isipokuwa ni kwa kukosa ushirikiano miongoni mwa Wizara zingine ambazo zilipaswa zisaidie kuwezesha kazi za Wizara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kulikuwa nae neo la kulegalega kwa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kama ambavyo taarifa yetu imesema. Eneo hili limelegalega kwa sababu ya kukosekana kwa *coordination.* Nitoe ushauri kabisa katika Bunge hili, kwamba ili diplomasia ya uchumi iweze kutekelezwa ipasavyo lazima kuwe na utaratibu wa ku-*coordinate* miongoni mwa Wizara, kwa maana ya Wizara za Uzalishaji pamoja na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Wizara hiyo ya Mambo ya Nchi za Nje kumekuwa na kulegalega katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mfano katika balozi zetu kuna majengo 47 yanahitaji ukarabati mkubwa. Pia kuna majengo tisa yamechakaa, pia kuna majengo 11 hayako katika hali nzuri kabisa kiasi kwamba yanatweza hadhi ya nchi yetu Tanzania huko nchi za nje. Haya yote hayakufanywa kwa sababu ya uzembe katika wizara isipokuwa ni kwa sababu wizara haikuwezeshwa kutoa fedha za kutosha kwa wakati kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Januari 2023, wakati taarifa yetu sisi ndiyo tunaijadili kwenye Kamati yetu hakukuwa na fedha yoyote iliyopelekwa kutekeleza miradi hiyo. Huu ni msiba na ni si jambo ambalo linatakiwa watanzania au Wabunge tulitazame kwa mtazamo mwepesi mwepesi lazima tutazame kwa mtazamo mzito katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kukosekana hivyo jambo hili limeikumba pia Jeshi la Magereza. Bajeti ambayo tuliipitisha mwaka jana kwenye Jeshi la Magereza mwaka 2023 ni bilioni 21.369 lakini mpaka tunajadili taarifa ya Wizara ya kuanzia Julai 2022 mpaka Desemba 2022 hakuna fedha yoyote iliyopelekwa kwenye Jeshi letu la Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kufanya hivyo tafsiri yake ni tafsiri yake ni kwamba Jeshi la Magereza limeshindwa kutekeleza mipango yake ya usalama, mipango ya Ofisi za Magereza, mipango ya ujenzi au uanzishaji wa mashamba ya magereza pamoja na mpango wa kuboresha upatikanaji wa maji katikamagereza yetu. Hali hii si hali ambayo inaridhisha na inapendeza katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwamba haitoshi Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambayo fungu lake la fedha ni fungu 14, bajeti ambayo Bunge hili liliidhinisha ilikuwa ni shilingi bilioni 9 .93, lakini mpaka Julai Desemba hakuna fedha yoyote iliyopelekwa kwa ajili ya Jeshi la Uokoaji na Zimamoto. Huu ni msiba mkubwa. Inapotokea majanga ya moto au majanga mengine ambayo yanahitaji msaada wa jeshi hili Watanzania tumebaki tukiwa tunalaumu kuwa Zimamoto wameshindwa kufika kwa wakati, lakini kumbe ni kwa sababu hawajawezeshwa kupata vifaa vya kisasa kuweza kuokoa majanga kwa kipindi yanapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, lakini hapa nitagusia fungu moja tu ambalo ni Fungu 39 katika kamandi ile ya Jeshi la Kujenga Taifa. Kamandi ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa kipindi cha Julai mpaka Desemba hakuna hata senti tano ambayo imepelekwa kwenye Kamandi hii ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali ya kujiuliza ni kama ifuatavyo; kwa nini sasa Wizara hii inaitwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilhali hatuwezeshi JKT kufanya

majukumu yake? Kwa nini Jeshi limeweka Kamandi ya Jeshi la Kujenga Taifa ilhali hatuwezeshi JKT kufanya majukumu yake? Kwa nini kila mwaka tunachukua vijana ili waende JKT wakafanye *National Service* kule ilhali JKT haijawezeshwa kufanya yake? Huu ni msiba na kama ni msiba si jambo ambalo tunatakiwa tulijadili kwa wepesi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nitoe *assignment question* kwa Serikali; *is Tanzania, the United Republic a country or Nation state discuss. If it is a country, it is well and good to leave these armed forces without to incapacitate them. But if it is a National state should you, the Government please provide enough fund to the National Service, enough fund to armed forces, provide enough fund to the immigration forces in order for Tanzania to be a country a National state, United Republic and Sovereign State. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Haya naambiwa mmakonde huyo. Mchangiaji wetu anayefuata atakuwa ni Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge akifatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Innocent Bashungwa Waziri wa Ulinzi na baadaye atafatiwa Mheshimiwa Masauni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahasante sana kwa nafasi ya kuchangia ikiwa leo ni mara ya kwanza katika mwaka huu wa 2023; na sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye Enzi na Utukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ya kuchangia kwenye Kamati hizi mbili, na nitajikita kwenye Kamati ya Bajeti ambayo ina watu mahiri, makini na Bingwa kabisa. Napenda nitumie fursa hii kuwapongeza kwa kazi kubwa ambayo wanafanya na wanasikiliza kwa umakini

maoni ya wataalamu waliopo ndani ya Bunge hili na kuweza kuyafanyia kazi. Nawapongeza sana Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakwenda kuchangia kipengele cha 2.11 inayohusu Pato la Taifa. Kamati imeishauri Serikali kuweka mikakati ya kuchochea uzalishaji katika sekta za uzalishaji kama vile utalii, kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niishauri kamati kuongezea yafuatayo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuongeza Pato la Taifa tunafahamu mchango wa utalii katika Pato la Taifa. Na pato letu la Taifa walau lirudi pale kwenye asilimia saba kama ambavyo kama imesema. Tunafahamu Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ameshafanya kazi kubwa ya kulitangaza Taifa hili kwenye sekta nzima ya utalii. Lakini tusipokuwa makini kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais inaweza isilete matunda tarajiwa kama tusipoamua kuboresha viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wizara ya Mawasiliano imekwenda juu ya Mlima Kilimanjaro ikaweka mtandao kule. Tusifikiri tu wanaweza kupeleka yaliyo mazuri kwa wenzao kwamba bwana nipo juu ya Mlima Kilimanjaro njooni Tanzania kuna hivi lakini pia wanaweza wakapeleka yaliyo mabaya kama tusipoamua kuboresha viwanja vya ndege nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *International Civil Aviation Organization (ICAO) inazitaka* kila mamlaka za viwanja vya ndege kuwa na vyanzo vya mapato. Sisi Tanzania tumeweka *passenger service charge* ambayo n idola 40 kwa kila anayesafiri kwenda nje na shilingi 10,000 kwa kila ambaye anasafiri ndani ya nchi. Hela ambayo katika *low season* tunapata bilioni 40 na katika *high season* tunafika bilioni 55. Fedha hizi zinachukuliwa na *TRA* na mamlaka ya

viwanja vya ndege haiwezi kufanya lolote katika kuboresha viwanja vya ndege kwa sababu haina fedha ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini mamlaka inayosimamia viwanja vya ndege *(TCAA)* iweze kuwa na mapato lakini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege isiwe na mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini Mamlaka inayosimamia Viwanja vya Ndege *TCAA* iweze kuwa na mapato lakini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege isiwe na mapato? Kwa hiyo ili kuifanya kazi ya Mheshimwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kulitangaza Taifa hili kupitia *Royal Tour* kuwa endelevu, ni lazima tuiache Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iboreshe Viwanja vya Ndege kwa kuachiwa ile hela inayokusanywa kwa *passenger service charge* itumike na mamlaka ile na isiwe inang'ang'aniwa na *TRA,* wenyewe hawapati hata shilingi moja. Kwa mtindo huo hatuwezi kuifanya kazi nzuri ya *royal tour* kuwa kazi endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa taarifa iliyopo ni kwamba Kenya wanafuata Sheria hii ya *ICAO,* wanakusanya Viwanja vya Ndege wenyewe, Rwanda wanafanya hivyo, Malaysia wanafanya hivyo. Kwa hiyo nchi nyingi za jirani zenye viwanja vya ndege ambavyo ni bora wameweza kukusanya hizi fedha wenyewe na kuboresha miundombinu yao. Sasa Tanzania tuamue sasa kufanya juhudi za Mheshimiwa Rais za *Royal Tour* kuwa *sustainable* na kuleta tija inayotarajiwa kwa kuhakikisha tuna viwanja vya ndege vilivyo bora kwa kuiachia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege fedha ile ya *passenger service charge* ili waweze kufanya kazi yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekuwa tukishauri hapa kwamba Mamlaka ile iachiwe Wahandisi wa kuweza kufanya kazi zile za Kihandisi na suala hili limekuwa

linapotoshwa kidogo hapa kidogo Bungeni kwamba, Wahandisi waliopo *TANROADS* hawawezi kufanya kazi katika Viwanja Vya Ndege. *Issue* siyo suala la Uhandisi hapa, *issue* ni Mamlaka ambayo *TAA* imepewa. Mhandisi aliyekuwepo *TANROADS* yuleyule anaweza kufanya kazi Viwanja vya Ndege kulekule, *issue* ni *impact of the road* ndiyo ambayo inaangaliwa katika *design* tu pale, ndege inaposhuka *impact* yake ni nini na gari inapopita barabarani *impact* yake ni nini. Kwa taarifa tu iliyopo Wahandisi waliosimamia Viwanja vya Ndege ndiyo walewale walihamishwa wakapelekwa *TANROADS*. Kwa hiyo suala siyo *knowledge,* suala ni mamlaka iliyopewa *TAA,* warudishiwe Wahandisi wao ili waweze kufanya kazi ipasavyo kwa mujibu wa mamlaka iliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchangia kuhusiana na maoni mahususi ya Kamati ya Bajeti kipengele cha 7.1. Kamati imeishauri Serikali iandae mpango wa uhitaji wa rasilimali wa Taifa ili taaluma zinazozalishwa ziwe sawa na mahitaji ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Kamati katika kipengele hiki, lakini naomba kusema kwamba suala la taaluma yetu nchini haliwezi kuanza katika *level* ya juu wakati mwanafunzi anakwenda Chuo Kikuu, suala la taaluma, suala la rasilimali watu linapaswa kuanzia tangu mtoto akiwa tumboni kwa mama yake. Sasa Mheshimiwa Rais amefanya mpango mzuri wa lishe lakini tuhakikishe kunakuwa na afua endelevu. Kukosekana kwa afua endelevu kumesababisha akinamama wajawazito wanakosa damu ya kutosha na vilevile kuzaa uzao ambao hauna afya njema. Ndiyo hapo tunasema Taifa linakuwa na udumavu, udumavu umeshuka sasa hivi kwa asilimia 34, lakini hakika tunapaswa kushuka zaidi ili tuweze kuzalisha Taifa lenye watu wenye uwezo wa kubuni, uwezo wa kufikiri na uwezo wa kufundishika. Kwa hiyo kama Taifa tunapozungumzia suala la rasilimali watu ni lazima

tuwekeze nguvu huku chini mtoto anapokuwa tumboni na mtoto atakapozaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa iliyopo nikwamba Tanzania tunazalisha mabubu kila kukicha, kadri siku zinavyoendelea idadi ya mabubu inaongezeka. Mwaka 2018/2019 tulikuwa na mabubu 6,103 nchini, lakini ninavyozungumza sasa hivi mwaka 2023 tuna mabubu 8,503 nchini. Serikali inatoa fedha nyingi katika shule za mabubu hapa nchini kwa ajili ya kuwezesha chakula chao, kuwalipa Walimu wao, lakini jambo hili kama lingeangaliwa tangu mtoto anapozaliwa idadi hii ya mabubu isingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza fedha nyingi *unnecessarily,* Serikali sasa iamue, kila mtoto anapozaliwa apimwe usikivu. Haya mambo yanawezekana, kila Hospitali ya Wilaya kuwe na kifaa cha kupimia usikivu kwa mtoto anapozaliwa na kifaa kile huwezi amini hakihitaji mabillion ya fedha, kina-*range* kwenye shilingi milioni nani mpaka milioni 10 kipimo cha kupima usikivu, lakini kwenye hospitali zetu zote za wilaya vifaa vile havipo, ni nini tunatengeneza na ni rasilimali gani tunaitaka nchini? Kwa hiyo Serikali iamue ku-*save* hizi fedha zote ambazo zinapotea bure, iongeze nguvu katika vifaa vinavyoweza kupima usikivu mara mtoto anapozaliwa. Nchi za wenzetu zinafanya hivyo, lakini sisi tunaangalia tu macho yake ya njano, amelia kwa wakati, amegeuzwa miguu chini, anaonekana mtoto yuko salama, lazima tufanye *extra* kwa ajili ya kupata afya bora ya mtoto aliyezaliwa ili Taifa lipate rasilimali zilizo bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako Injinia Ulenge. Nilimwita Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa na naomba nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nataka nitumie nafasi hii kusema, tumesikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge na ushauri waliotupa katika baadhi ya maeneo na sisi kama Wizara tunachukua na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza mjadala umekuwa kwenye eneo la ushirikiano katika kutumia Taasisi za Majeshi na vilevile kutumia Vyombo vyetu vya Dola katika kushirikiana kwenye Sekta ya Kilimo. Nataka kuliambia Bunge lako Tukufu hivi karibuni nadhani siyo muda mrefu mtaona kwenye Vyombo vya Habari, Wizara ya Kilimo inasaini *MoU* na JKT kwa ajili ya maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, uzalishaji wa mbegu. Mbili, kwa ajili ya kutumia maeneo ambayo yanamilikiwa na Jeshi kwa ajili ya *strategic crop* mazao kama ya mafuta. Vilevile mbali na hapo jambo hili tulishalianza, namshukuru Waziri wa Ulinzi wa sasa na aliyemtangulia, mfano, mwaka huu wametuzalishia mbegu za alizeti tani 500, lakini vilevile mwaka huu tumesaini makubaliano na JKT Mgambo wanatuzalishia jumla ya eka 500 kwa ajili ya uzalishaji wa alizeti. Pia tunashirikiana na JKT Bulombora kwa ajili ya uzalishaji wa michikichi na sasa wameshaanza kusambaza miche ya michikichi itakayoweza kuzalisha jumla ya eneo la ekari 3,400. Kwa hiyo tumeshaanza mahusiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu na Kamati ya Mambo ya Nje, tumeanza ushirikiano mzuri sana na Wizara ya Mambo ya Nje na nimshukuru Waziri wa Mambo ya Nje, tumeshirikiana katika kufungua Soko la Parachichi China na sasa hivi tunashirikiana nao kwa ajili ya kuangalia namna gani tunaingia kwenye masoko ya *COMESA* hasa katika mazao ya tumbaku. Hivi karibuni pia tunashirikiana nao kwa ajili ya Mradi wa Maghala ambapo

kuna wawekezaji wako tayari kuja kuweka. Tunafanya kazi kwa karibu na Balozi zetu zote, ingawa matokeo yanaweza yasionekane kwa haraka, lakini tumeanza ushirikiano mzuri sana na wenzetu wa *Foreign*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliongelee ni hili eneo la mfumuko wa bei kwa ufupi tu. Serikali inachukua hatua na mpaka sasa tumeshapeleka vyakula katika halmashauri 47 katika mikoa 15 katika nchi yetu na maeneo ambayo tayari yameishaanza uzalishaji tumefunga vituo. Mfano, katika Wilaya ya Sengerema, maeneo ya Buchosa ambayo Wakulima wameshaanza kuvuna tumefunga vituo vya kuuza mazao kwa bei ya nafuu na tunaendelea mpaka sasa tumeshagawa tani 23,000, lakini vilevile tumeweka *allocations* ya jumla ya tani 40,000 ya mahindi ambayo tutaendelea kuiingiza sokoni na kuiuza kwa bei ya kati ya Sh.700 mpaka Sh.800 ili ku-*stabilize. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba na Bunge lako Tukufu lituelewe, hatuwezi kuondoa mfumuko wa bei kwa kuja na *shortcut*. Ni lazima tuongeze tija na ndiyo maana Serikali inawekeza kwenye maeneo ya umwagiliaji, inawekeza kwenye kutoa ruzuku za mbegu, tunatoa ruzuku ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niseme tu Mradi wa *Block Farm* wa vijana; tunao vijana ambao wanatoka JKT aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ulinzi alisha-*submit* majina ya vijana ambao katika *phase one* tunaanza nayo, tutawachukua hao vijana kwenda nao kwenye hii *project,* hatuwaachi vijana waliyopo JKT, lakini lazima miradi hii iende *parallel,* maeneo ya JKT wataendelea kuwa-*accommodate* vijana na sisi tunaya-*develop* kupitia Wizara ya Kilimo tutawa-*accommodate* vijana wote. Ni Mpango ndiyo tumeanza, kunaweza kukatokea marekebisho, tutaendelea kurekebisha wakati tunakwenda mbele. Hata hivyo, la msingi lazima vijana wamiliki ardhi ili

kuwafanya vijana wa nchi kuwaondoa kwenye kundi la watu wasio miliki ardhi na kuwaondoa kwenye hatari ya kuwa manamba katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie eneo la ruzuku ya mbolea. Cha kwanza niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge mfumo wetu wa ruzuku wa mbolea ni mfumo bora kuliko mifumo ambayo tumewahi kuwa nayo huko nyuma. Mfumo wetu wa ruzuku unamtambua mkulima na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, hofu ya kwamba tunaibiwa, kama tusingekuwa na Mfumo huu unaomtambua mletaji *agrodealer,* mkulima, hata mbolea ambazo zinatokea ubadhirifu tusingeweza kuzikamata. Niwahakikishie sitoingia kwenye *record* ya historia ya nchi kuwatia umaskini wakulima wa nchi hii kama baadhi ya watu walioingia kwenye *record* ya kuwatia umaskini wavuvi wa nchi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na ahsante sana kwa kuzingatia muda. Nilimwita Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukupongeza wewe kwa kutuongozea kikao vyema, lakini pia niungane na waliyochangia kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi kwa kazi nzuri ambayo mnafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza Wenyeviti kwa Mawasilisho mazuri, lakini kipekee nitumie nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Vita Kawawa, Makamu Mwenyekiti Vincent Mbogo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano mzuri na maoni, ushauri na maelekezo ambayo mnatupatia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la

Kujenga Taifa, tunawashukuru sana kwa ushirikiano huu. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango na yale ambayo Bunge litaazimia lakini pia maoni na ushauri ambao wametupatia tunaenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza mpendwa wetu Mheshimiwa Rais na Amir Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika michango ya leo na katika Bunge hili Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge wamempongeza kwa kazi nzuri ya kuimarisha diplomasia ya uchumi na diplomasia ya uchumi pamoja na diplomasia ya ulinzi ni vitu pacha. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais, kazi nzuri ambayo ameifanya ya kuhimarisha diplomasia ya uchumi, kazi hiyo hiyo nzuri imetuimarisha katika suala la diplomasia ya ulinzi. Kwa hiyo na hilo tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, kama wanavyofahamu majeshi yetu yanayo mahitaji makubwa, yapo mahitaji ya kisekta na katika hili niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri. Ukienda kwenye Vikosi na maeneo ya Majeshi yetu utakuta wanahitaji huduma ya maji, kwa hiyo itabidi tukae na Wizara ya Maji; Barabara wakati mwingine kwa shemeji yangu Angellah Kairuki upande wa *TARURA;* Mheshimiwa Profesa Mbarawa upande wa *TANROADS* na Sekta nyingi. Kwa hiyo niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuhudumia majeshi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja. Moja ya michango ya Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa ni ni kuhusu ajira kwa vijana wetu kupitia JKT. Ningependa kuwakumbusha kwamba, jukumu la kwanza na kubwa la JKT toka suala la kujiunga na JKT kwa mujibu wa sheria liliporudi mwaka 2013, yamekuwa masuala ya kuwajenga vijana kimaadili na kiuzalendo. Hata hivyo, kutokana na changamoto ya ajira nchini, Serikali imefanya kila aina ya

jitihada hata kupitia JKT, wale vijana ambao wanaenda kwenye mafunzo ama kwa mujibu wa sheria ama kwa kujitolea, jitihada za Serikali zinaendelea kufanyika kuhakikisha kwa kadri inavyowezekana vijana hawa wanapata ajira kupitia kwenye Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Takwimu za 2018, 2019 na 2020, vijana ambao wameenda JKT asilimia 45 wamepata ajira kwenye Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Serikali tunaendelea kuwa wabunifu hasahasa kwenye masuala ya mawanda upande Sekta za Uzalishaji ili kuhakikisha hata hii asilimia ambayo hawapati fursa kwenye Vyombo vya Ulinzi na Usalama, wanapata fursa kwenye maeneo mengine likiwemo suala ambalo Mheshimiwa Hussein Bashe, amelitaja *Memorandum of Understanding* kati ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Kilimo. Sasa hivi iko tayari na panapo majaliwa wiki ijayo tutaisaini ili kujikita zaidi kwenye *program* za Wizara za Kilimo, kwa mfano, kuna Skimu ya Umwagiliaji kule Chita. Kupitia skimu hii kwa Takwimu ambazo Mheshimiwa Waziri Bashe, amezisema kwa mfano uzalishaji wa mbegu za alizeti tani 500 zimefanyika kupitia *program* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuzalisha mbegu za mazao mbalimbali kwa mfano upande wa MAhindi tumezalisha tani 300 kupitia JKT, upande wa mpunga tumezalisha tani 468, upande wa mazao ya mafuta tumezalisha mbegu tani 206, lakini hata kwenye mazao ya chakula mahindi tumezalisha tani 3,876, Mpunga tani 1,276, hizi ni takwimu za mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kila sekta kuwa wabunifu katika kuhakikisha tunazalisha ajira milioni nane kama tulivyoahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025,

tutaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta kubuni mawanda ambayo yatasaidia vijana wengi kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunaliangalia ili kusaidia vijana kupata ajira ni kuangalia mitaala ambayo inafundishwa kwenye upande wa ufundi stadi na JKT. Kuangalia namna ya kupata *accreditation* ili vijana wanaopata ufundi stadi upande wa JKT iwe ni sawa na yule ambaye amehitimu *VETA* na Taasisi nyingine ambazo zinatoa *Vocational Training*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pia hivyo hivyo, kulikuwa na hoja ya uhitaji wa kuweka alama za mipaka pamoja na barabara za ulinzi; Waheshimiwa Mawaziri, Dada yangu Mheshimiwa Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi; Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi; pamoja na Mheshimiwa Mwigulu, Waziri wa Fedha, tumevichukua hivi, tutaendelea kushirikiana nao ili tuweze kuvitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Hamad Masauni, Waziri ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wakati huo Mheshimiwa Stergomena Tax, Waziri wa Mambo ya Nje pamoja na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango anajiandaa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru. Nianze kwa kuipongeza na kuishukuru sana Kamati yetu ya Mambo Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Vita Kawawa na Wajumbe wote kwa ushirikiano mzuri ambao wanaendelea kutupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona leo umesoma mabadiliko ya Waheshimiwa Wabunge kwenye Kamati, matarajio yangu Wajumbe wa Kamati hii wataendelea kuomba kubakia hapa kwa sababu tutawa-*miss* sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie mambo kama matatu mpaka manne kwa harakaharaka. La kwanza ni suala ambalo Waheshimiwa Wabunge, wengi wamelizungumzia kuhusu changamoto ya msongamano wa Wafungwa Magerezani na Mahabusu, ambapo mbali na maoni ya Waheshimiwa Wabunge lakini hata Kamati na yenyewe kwenye taarifa yake ililizungumza hili. Walieleza sababu nyingi ambazo zinaweza kusababisha jambo hili, moja katika mambo ambayo Kamati ilizungumzia ni jinsi ambavyo tuna upungufu wa Magereza nchini lakini wakaeleza vilevile masuala ya kutotumika ipasavyo kwa huduma hizi za *Parole* pamoja na wategemezi wa adhabu za kifungo kwa maana ya kutokutumia zile adhabu mbadala na nyingine ni hoja ya Wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na hizi hoja, nitachukua furasa hii kujaribu kueleza hatua ambazo Serikali tumechukua katika kukabiliana na hoja hizi ambazo ni sahihi kabisa. Mbali ya hoja hizi suala la msongamano magerezani ni pana zaidi na upana wake unatokana na hatua ambazo Serikali tumechukua kuliangalia hili, lakini kuangalia kwa ujumla wake utendaji kazi wa Vyombo vyetu vya Usalama kwa ujumla wake na ndipo tukaja na mpango kabambe wa kufanya maboresho makubwa katika vyombo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapofanya *reforms* katika jambo lolote changamoto yake ni kwamba, unaweza usipate matokeo haraka, inahitaji ustahimilivu na uvumilivu katika kupata matokeo kwa sababu inahusisha tafiti mbalimbali, inahusisha vilevile marekebisho ya mifumo,

marekebisho ya sheria, marekebisho ya mazoea, marekebisho ya aina mbalimbali. Kwa hiyo, naomba nitoe mfano mmoja wa hii kauli yangu ambayo nimeizungumza ya umuhimu wa kuliangalia kwa mapana yake zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama siku mbili nyuma nilipita hapa kwenye Kituo cha *Police Central,* Dodoma na sikuwa nimemwambia mtu yeyote kama naenda, nilipita tu nikasimama, nikaingia ndani, nikawaambia naomba nizungumze na hawa mahabusu walioko huku ndani. Kwa hiyo nikaingia kwenye mahabusu, nikajaribu kuwauliza hivi kuna mahabusu yeyote hapa anahitaji kueleza jambo lolote kwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakajitokeza waliokuwa na hoja zao mbalimbali. Mmoja ambaye nataka nimtolee mfano hapa, aliyejitokeza akalalamika kuonewa na Jeshi la Polisi. Akasema bwana mimi nimekamatwa hapa nimekaa mahabusu muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofanya utafiti baada ya kuzungumza naye na utafiti mbalimbali kuhusiana na yule mtu, niligundua yule mtu aliwahi kufungwa miaka 30 Ruvuma kwa kosa la ubakaji na alikaa miaka michache gerezani akapata msamaha. Baada ya kupata msamaha, hivi karibuni amekamatwa kwa tuhuma za kubaka watoto wa madrasa, sio mmoja, sio wawili, sio watatu, sio wanne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio Mahakama, kuna utaratibu wake wa kuweza kutoa hukumu, lakini mazingira ya uchunguzi wangu mimi wa juu juu umenipa imani juu ya umuhimu wa yeye kuendelea kukaa mahabusu. Nina uhakika hata kama ataachiwa leo hivi, pengine akienda huko wanaweza wakamuua wale wazazi wa wale watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nini maana ya kutoa mfano huu? Maana yangu ni kwamba, hata utaratibu huu wa misamaha, utaratibu huu wa *parole* ambao

Waheshimiwa Wabunge wanaulalamikia kwamba tunaufanya kwa kusuasua, na wenyewe unahitaji maboresho na kuangaliwa, kwamba, je, utaratibu tunaoutumia hautoi mianya kwa watu wengine ambao hawastahili kutumia fursa hizi? Kwa hiyo, pengine mambo haya ambayo tunayafanya yanasababisha kuonekana tunachelewa kutumia hizi fursa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusiana na wahamiaji haramu. Ni kweli, tatizo la wahamiaji haramu ni kubwa sana. Hatua ambazo tunaendanazo mpaka sasa hivi ni nzuri na za kuridhisha, kwa sababu, hivi sasa tunavyozungumza wahamiaji haramu hawa wa Ethiopia waliko gerezani wanakadiriwa kufika 2,673. Katika kipindi cha mwezi Januari na Februari tu peke yake ambapo mwezi Februari ni tarehe za mwanzo tu, tarehe 7, leo tunazungumzia wahamiaji waliorudi kwao Ethiopia kwa miezi hiyo miwili wanakadiriwa kufika 1,538.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipozungumza leo asubuhi nimewasilishiwa *release orders* za kusaini wahamiaji ambao wako tayari kuondoka 397, hivyo kufanya jumla ya wahamiaji haramu wa Ethiopia 1,903 ambao wanaondoka kwa miezi miwili. Sasa hii ni hatua kubwa sana. Hatua hizi zimesababishwa na nini? Kwanza ni jinsi ambavyo tumelichukulia kwa uzito tatizo hili na kuweza kutoa maamuzi ya muhimu sana. Maamuzi yenyewe ni kuhakikisha kwamba tunaiondoa nchi ya Ethiopia katika nchi ambazo zinatumia utaratibu wa *Visa* Rejea. Sasa tumefikia katika hatua nzuri kwa sababu tayari tumeshabadilisha kanuni na hivi sasa tunapozungumza tayari *GN* Namba 37 ya mwaka 2023 imeshatangazwa na hivyo basi, utaratibu wa matumizi ya *Visa* kwa wananchi wa Ethiopia kuja Tanzania utaendelea kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itasaidia sana kwanza kuua hii biashara ya usafarishaji binadamu haramu. Itasaidia

pia kufanya Serikali iweze kuongeza mapato kwa sababu, hawa watakuwa wanalipa *Visa*. Pia itaondoa ile changamoto ya kuiingiza hasara ya Serikali ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiipigia kelele. Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Bunge wamezungumza hapa juu ya takwimu kwamba, pengine kwa kipindi kifupi tu kulingana na takwimu zao tumepoteza karibu shilingi bilioni 5.6, wakashauri wahamiaji hao waondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuondoa wahamiaji haramu kwa kutumia gharama za Serikali ni changamoto kubwa. Kwa sababu tulipiga hesabu kwa hawa wahamiaji ambao nimewazungumza, elfu mbili na kitu, kama ingekuwa tumewaondoa kwa fedha ya Serikali, tungetumia takribani Shilingi bilioni tisa, ambapo kama ukijumlisha na hesabu ile ya Waheshimiwa Wabunge madawati, badala ta kupata madawati 31,000 unazungumzia madawati zaidi ya 129,000. Kwa hiyo, ndiyo maana tukatumia njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ambazo tumetumia, ya kwanza, tumeweza kuzungumza na washirika wa maendeleo, na wameweza kuondoa wahamiaji haramu zaidi ya 504. Sasa hivi tuna utaratibu mzuri ambapo ndugu wa hawa wahamiaji haramu wenyewe wanakuja sasa kuwaondoa ndugu zao kwa gharama zao wenyewe. Ndiyo maana sasa hivi nazungumzia jitihada hizo kwamba zinakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii hoja ya kuiondoa Ethiopia kwenye utaratibu wa *Visa* Rejea imeweza kuleta hamasa katika nchi yao kuona kwamba, sasa hivi hakuna sababu tena ya kuweza kutumia njia ya kificho kuweza kusafiri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba nilizungumzie kwa haraka haraka…

**MWENYEKITI:** Haya, nakuongeza dakika moja Mheshimiwa umalizie jambo lingine.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja?

**MWENYEKITI:** Hitimisha ndiyo. Muda wako ulikuwa umeisha Mheshimiwa. Unaweza ukamalizia lakini jambo lako moja ambalo umelisema.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jambo ambalo nilitaka nilihitimishe kwa haraka haraka ni eneo la Jeshi la Polisi na hasa katika eneo la usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili kuna mambo makubwa mawili ambayo tunafanya; la kwanza kabisa, ni kufanya *reform* ambayo juzi nilishuhudia jinsi Mheshimiwa Rais alivyounda tume. Ile tume pamoja na mambo mengine, inakwenda kuangalia mambo mengi; inakwenda kuangalia maslahi, utaratibu wa ajira, na vitu mbalimbali. Pia kuna vitu ambavyo tayari tumeshavianza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema lazima Jeshi la Polisi liwe la kisasa ili tudhibiti uhalifu kwa ufanisi zaidi, ili tudhibiti ajali za barabarani, ili tupunguze kero au malalamiko ya wananchi kuhusu rushwa kwenye Jeshi la Polisi na mengineyo, lazima Jeshi la Polisi liwe la kisasa. Hivyo, kwa upande wa ajali barabarani kwa mfano, kuna mambo makubwa mawili ambayo wakati wowote kuanzia sasa tunaweza kuanzanayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni kwamba, tunaanza hivi karibuni kutangaza utaratibu wa kuweza kufanya ukaguzi wa lazima wa magari. Kwa hiyo, naomba kuchukua fursa hii kutoa wito kwa taasisi ama kampuni yoyote duniani ambayo inajihisi inaweza kuja kushirikiana na Serikali. Maana mambo haya yote ya *modernization* ya Jeshi la Polisi na majeshi mengine, hatuwezi kuyafanya kwa kutegemea bajeti ya Serikali peke yake. Kwa hiyo, kuna utaratibu ambao tunaweza tukashirikisha taasisi binafsi kwa ajili ya kwenda kukabiliananayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni jambo jema kabisa, ni kitu muhimu sana kuweza kuwa na mifumo ambayo itasaidia Jeshi letu la Polisi kuweza kubaini makosa ya uhalifu kwa haraka, ikiwemo makosa ya jinai, makosa ya ajali barabarani na mengineyo. Kwa hiyo, hatuwezi kuepuka katika karne ya leo kuwa na matumizi ya mifumo ya kisasa ya kamera.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna mpango vilevile katika muda siyo mrefu kuanza utaratibu wa kuwa na mifumo ya miji salama katika nchi hii. Haya mambo niliyazungumza katika bajeti iliyosomwa mwaka uliopita 2021/2022 na katika utekelezaji wake tumefikia katika hatua ya kuridhisha. Tutaanza na Mji wa Dodoma, Mji wa Dar es Salaam, Mji wa Arusha na baadaye tutaelekea na miji mingine mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna hoja nyingine ya vitendeakazi. Katika hili Mheshimiwa Rais Samia suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua unataka kunikatisha, lakini angalau moja niliseme la muhimu kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakizungumza sana katika maswali mbalimbali hapa Bungeni wakiuliza Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, sasa hivi tunakamilisha utaratibu wa kuweza kupeleka magari katika kila Wilaya katika nchi hii. Kwa hiyo, kila Mbunge ambaye ana changamoto ya gari katika jimbo lake, sasa inaendelea kupatiwa ufumbuzi. Fedha hiyo Mheshimiwa Rais ameshaitoa na wakati wowote magari haya, taratibu za manunuzi zitakapokamilika yataingia na tutaweza kukabiliana na changamoto hiyo ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo yanahusu masuala ya makazi na vituo vya Polisi…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni. Nilikuongeza dakika mpaka zikafika kumi kutoka tano, na naona sekta yako inataka muda wa kutosha, nafikiri hapo baadaye pengine utapewa kwa muda mwingine.

Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, Waziri wa Mambo ya Nje aweze kuchangia pia.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu, nianze kwa kuzipongeza Kamati zote kwa taarifa nzuri walizowasilisha. Pia kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Vita Kawawa, Mwenyekiti wa Kamati ya NUU na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia, ushauri wanaotupatia ambao unatuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea michango mingi kutoka kwenye Kamati na Wajumbe mbalimbali waliochangia. Naomba niwashukuru na niwahakikishie kwamba michango hii yote ni muhimu na tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa mambo yaliyojadiliwa na kwa uchache wa muda, nitajaribu kuongea machache na kwa ufupi sana. Mtanisamehe Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, napenda niweze kuongelea mengi kadiri nitakavyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa mojawapo lililoongelewa kwa umuhimu na kuchangiwa na watu wengi ni kuhusu diplomasia ya uchumi, kufunganishwa na uchumi, ushirikishwaji wa sekta, limekwenda mpaka Halmashauri na kupanua uelewa wa diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kusema kwamba diplomasia ya uchumi ni kitu muhimu sana na imekuwa na mafanikio makubwa sana kibiashara, kiuwekezaji, kiutalii na hata miradi. Pengine Waheshimiwa Wabunge hamfahamu kwamba baadhi ya miradi mikubwa mnayoona ikitekelezwa hapa nchini imeibuliwa na Balozi zetu ikiwa ni sehmu ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kipindi hiki au katika awamu hii ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, diplomasia ya uchumi imeshika kasi kubwa sana. Tumemwona yeye mwenyewe akitangaza fursa mbalimbali katika mataifa mbalimbali, tumemwona jinsi ambavyo amekuwa akitangaza utalii, tumemwona ambavyo amevutia wawekezaji mbalimbali, na hii yote imechangia katika kukuza diplomasia ya uchumi. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, diplomasia ya uchumi imekuwa na mafanikio makubwa, lakini hata hivyo siyo kwamba, hakuna changamoto. Tumefanya tathmini kama Wizara na kubaini kwamba zipo changamoto ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na masuala ambayo yameainishwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, tunaandaa Mpango wa Kitaifa wa Kisekta wa Kutekeleza Diplomasia ya Uchumi. Madhumuni ni kuhakikisha kwamba tunaibua maeneo ya kimkakati, tunaainisha watekelezaji wote ikiwa ni pamoja na sekta binafsi na tunapanga utaratibu wa kutekeleza ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya umma kama ilivyoelezewa na kuwaleta wadau wote pamoja. Kama nilivyosema, matarajio yetu ni kwamba, tutakamilisha kazi hii mwezi Desemba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mchango kwamba pengine tuangalie kuajiri kutoka sekta binafsi. Katika kuandaa mkakati huu, tutaona kama kuna haja ya kuajiri au tunaweza kuishirikisha sekta binafsi kwa utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, katika Taarifa ya Kamati, aya ya 3.2.1, sijui ni ibara au *section* (b) na (c), Kamati ilipendekeza tuandae mikakati miwili na mpango mmoja; Mkakati wa kuainisha fursa za kiuchumi, mkakati wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, na mpango wa ushirikishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba tuandae mkakati mmoja ambao tunaendelea kuuandaa na utajumuisha yote haya. Hii itakuwa na ufanisi zaidi. Kwa muktadha huo, naomba azimio hilo lisomeke namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nitapenda kuliongelea ni uratibu maalum wa kuwaandikisha *diaspora*. Hili ni jambo kubwa, na ni kweli, kama ilivyosemwa, limesimamiwa sana na Mheshimiwa Rais. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, siyo kweli kwamba hatuyajali maagizo ya Mheshimiwa Rais, la hasha, tunafanya kazi kubwa na tumefika pazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshaanza kuandaa mfumo wa kidijitali ambao mpaka sasa hivi umefika mbali na tunatarajia kufika mwezi Juni mwaka huu utakuwa umekamilika. Mpaka sasahivi *prototype* iko tayari, tumeshaandaa *design* na kilichobaki sasa ni kukamilisha mfumo huu. Kwa hiyo, hili limekwishakamilika, ni muda mchache tu mtaweza kuona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine muhimu ambacho kilijitokeza katika mazungumzo, mijadala au michango ni hadhi maalum kwa *diaspora*. Hapa ndipo tulipoambiwa tunamkwamisha Mheshimiwa Rais. La hasha, hatumkwamishi, na hatuwezi kufanya hivyo. Sisi ni jeshi lake, tuko nyuma yake, tunafanya kazi kuhakikisha yale yote aliyotuagiza kuyafanya, tunayatekeleza kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika mbali sana. Mpaka sasa hivi tulishakusanya maoni ya wadau, tulishakusanya mapendekezo kutoka *diaspora,* tumeshayachambua, tumeshashirikisha wadau wote na tumeshaainisha maeneo ambayo tuna imani kwamba yanakwenda na matarajio na matakwa ya *diaspora* ambayo sasa mfumo umeshawekwa na utaratibu umeandaliwa, lakini kilichobaki sasa hivi tunapeleka kwenye Baraza la Mawaziri. Kitakachofuata baada ya hapo, kwa sababu yapo maeneo ya kisheria ambayo yatatakiwa kufanyiwa kazi, kwa hiyo, baada ya Baraza kupitisha waraka huu, tutaendelea na mabadiliko ya sheria ili hadhi hii maalum iweze kufanyiwa kazi. Tumefika mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa ruhusa yako, ni uendelezaji wa balozi na vitega uchumi, limeongelewa sana na ninawashukuru sana kwa kuliongelea hili. Hili ni jambo kubwa sana na ni kweli kabisa kwamba taswira ya nchi yetu inaonekana pia kupitia balozi zetu tulizonazo nchi mbalimbali, lakini ni suala kubwa linalohitaji rasilimali nyingi. Mjumbe mmoja ameeleza kwamba, kati ya majengo 110,

majengo 67 yanahitaji aidha kujengwa upya, kukarabatiwa au kubomolewa kabisa na kujengwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba hatuwezi kufanya kazi hii peke yetu, na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tunafanya kazi hii kwa kushirikiana na sekta binafsi. Tayari nimeshaunda Kamati ya Kitaasisi inayojumuisha sekta binafsi na sisi wenyewe. Kwanza kuainisha nini tunaweza kufanya kwa haraka? Mahitaji tunayoyahitaji sasa hivi ni nini? Wizara ya Fedha inaweza ikatenga kiasi gani? Tuko katika mchakato wa bajeti ili iweze kuingia katika bajeti inayofuata, lakini sekta binafsi na yenyewe inaweza ikashiriki namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la sheria ambalo pia lilikuwa linatusumbua, lakini sasa hivi tayari *PPP* inafanyiwa maboresho na tuna imani kwamba sekta binafsi itaweza kushirikiana nasi na mtaona matokeo baada ya muda siyo mrefu. Ni kazi kubwa kwa sababu inahitaji uandae *concept note,* uwe na *feasibility study,* uwe na *design;* yote haya yanaandaliwa na Kamati ili hata pale tukapopata fedha tuweze sasa kwenda na kuanza kutekeleza kazi hii. Hata ukipata fedha sasa hivi Waheshimiwa Wabunge unaweza usifanye kazi hii kama haya maandalizi hayajawa tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kama utaniruhusu, ni suala la kujitoa katika *COMESA*. Naomba tu kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, hatujapata hasara yoyote. Sisi tulikuwa wanachama wa jumuiya tatu, na tukiwa pekee wanachama wa jumuiya tatu. Tumebaki tukiwa Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*. Baada ya kuwa tumejitoa, tuliona kwamba hatuwezi kuwapoteza wale wachache ambao hatukonao ambao walibaki katika *COMESA* na nchi zote zilikuwa zikihangaika wakati huo, kwamba tuko katika *configurations* nyingi. Inatusumbua,

tunalipa michango mingi, lakini pia kuna *obligations* ambazo zinapandana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukakubaliana kuanzisha utatu unaoleta pamoja *COMESA, EAC* na *SADC* na tunashirikiana katika mihimili yote mitatu; uendelezaji wa viwanda, uendelezaji wa miundombinu, na pia uendelezaji wa masoko na biashara. Pia ipo miradi ambayo tunatekeleza pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 ulizinduliwa ukanda huru wa biashara *(FTA),* kilichobaki sasa hivi ni kufanya *ratification.* Katika hii *tripartite* inatuwezesha sasa kufanya biashara kwa pamoja kama ambavyo tungefanya na *COMESA* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ilikuja hoja kwamba, tunapoteza biashara kubwa na *DRC*. Kuna utoafauti kati ya ushirikiano wa kikanda na ushirikiano wa nchi na nchi. Vinapotokea vikwazo ambavyo ni baina ya nchi na nchi tunavitatua baina ya nchi na nchi. Tumeendelea kutatua vikwazo mbalimbali kama ilivyoelezewa kati ya Kenya na Tanzania na hata kati ya *DRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuthibitisha kwamba hatujapoteza biashara katika *DRC,* biashara hii imeendelea kukua mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2012 biashara yetu ilikuwa ni Shilingi bilioni 50.2 lakini miaka minane baadaye kufikia mwaka 2020 biashara yetu ilikua kufikia Shilingi bilioni 334 kutoka Shilingi bilioni 50. Kwa hiyo, biashara inaendelea na hatujapoteza kitu chochote na urari wetu kati ya *DRC* na Tanzania ni chanya. Hivyo hakuna tulichopoteza, bali tumenedelea kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua umenivumilia, umeniongezea muda. Nakushukuru sana, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote nipokee maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge, tumeyapokea, tutayafanyia kazi na mengine tutaendelea kupeana mrejesho kwa sababu, tukimaliza Bunge hili litakuja Bunge lingine ambalo litakuwa linahusisha bajeti, panapo Mungu akitujalia afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo ambayo niliona pamoja na kupokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge waliyoyatoa, ningependa nitolee ufafanuzi hoja chache. Hoja ya kwanza ambayo Waheshimiwa Wabunge wameongelea kwa sauti kubwa ni kuhusu uchache wa wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato *(TRA)*. Kwanza kabisa niliombe Bunge lako tukufu liridhie tumpongeze Mheshimiwa Rais kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa *TRA* walikuwa hawajaajiriwa katika kipindi cha muda mrefu kidogo, miaka yapata mitano sita saba hivi, lakini tulipokuja kwenye mwaka wa fedha uliopita hapa Bunge lako lilielekeza Serikali kuweka uzito kwenye uajiri wa watumishi wa Mamlaka ya Mapato - *TRA*, hivi tunavyoongea ndani ya mwaka huu mmoja, kibali kilitolewa na Mheshimiwa Rais kuajiri watumishi kwa mpigo 2,100 wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa taratibu za kiutumishi, sekta moja kupata watumishi 2,100 kwa mpigo siyo jambo dogo na hivi tunavyoongea 1,500 tayari walishaajiriwa na wengine 500 wako hatua za mwisho za taratibu za kiuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii ni namna gani unaweza tukawaambia jinsi Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inavyopokea na kuyafanyia kazi mapendekezo ya Bunge. Ni ndani ya mwaka huu wa fedha tupo nusu mwaka tu, wafanyakazi 2000 wameshaajiriwa na 170 wako hatua za mwisho kwenye taratibu za masuala ya vibali wakati wanakamilisha usaili wa

hao wengine. Kwa hiyo, maoni yenu Serikali inayapokea na inayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kama mwaka mmoja wameajiriwa 2100 kama wangekuwa wanaajiriwa hivyo hivyo kwa miaka kumi tungekuwa na watumishi wangapi. Sasa pengo la Watumishi wa Umma wakiwa hawajaajiriwa kwa muda mrefu huwezi ukaliziba kwa mara moja, ukiajiri wengi kwa mara moja pia, kwa sababu watakuwa bado hawajazalisha utatengeneza tatizo tena kwenye upande wa mishahara, kwa sababu utakuwa umeajiri wengi ambao bado hawazalishi. Kwa hiyo, ninawaomba mridhie Serikali hatua hizi inazochukua, iwaajiri hawa waingie kazini waendelee kuzalisha, wakati huo tutakuwa tunaendelea pia kutekeleza masuala ya kimfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliongea Mheshimiwa Esther Matiko nami nakubaliana naye, tatizo siyo watumishi peke yake, siyo idadi peke yake, tunayo maeneo mengine ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi, masuala ya uadilifu, masuala ya matumizi ya *EFD* na masuala ya hamasa tu ya wananchi wenyewe kuwianisha kodi na maendeleo yao. Kwamba kila mmoja awiwe kulipa kodi anapo nunua bidhaa na anapofanya biashara nyingine yoyote ile. Kwa hiyo, hili tunaenda nalo lakini kama nilivyosema ni jambo ambalo linatakiwa liende hatua kwa hatua, niliona nilisemee hilo kwa sababu lilijitokeza lakini tunaendelea kulifanyia kazi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ni mashahidi mtaona kwamba makusanyo yameongezeka siyo tu kwa kuwianisha malengo na makusanyo lakini hata kwa namba, Machi 2021 makusanyo ya mwezi yalikuwa trilioni 1.2 lakini Disemba hii tumepiga zaidi ya trilioni 2.7, kwa hiyo mnaweza mkaona kwamba hata kwa *real terms* makusanyo yameendelea kuongezeka. Niliona nilisemee hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili na ninaomba hapa tuelewane vizuri sana Waheshimiwa Wabunge, vinginevyo tutabadilisha Bunge hili kuwa *platform* ya kujadili matukio. Hiki chombo ni kikubwa sana siyo chombo cha kujadili matukio tu. Kinatakiwa kiishauri pia Serikali ni namna gani inaweza ikaweka mipango yake ya kuwatoa Watanzania kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivi, ukiangalia *Hansard* za Bunge letu hili, utaweza kuona michango ya Wabunge inavyokuwa tofauti Bunge moja na Bunge lingine linalofatia. Leo hii kwa sababu inasikika vizuri kwa watu ikionekana unasemea bei, kila mmoja anaongelea bei lakini twendeni katika hali ya uhalisia. Nchi hii ina wazalishaji na ina walaji lazima mara zote tukumbuke hilo. Nchi hii ina wazalishaji na walaji, na hivyo vyakula vinavyozalishwa havizalishwi kwa mashamba ya Vijiji vya Ujamaa ni watu binafsi wanaingia gharama zao kuzalisha, ni mtu binafsi anajipinda anahangaika anazalisha, kuna upande mmoja unazalisha kuna upande mmoja unatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama watunga sera kama watunga sheria ni lazima tuwe makini sana ku-*balance* haya maeneo mawili. Tujiulize kwa nini nchi hii ina wakulima wengi sana halafu inakuwa ni nchi maskini na ardhi inayo! Tujiulize jibu sahihi utakalolipata ni kwa sababu wamekuwa wakizalisha wanapata hasara katika uzalishaji wao, ndiyo jibu sahihi hilo. Wanafanya kazi kwa bidii anazalisha magunia 400 anaambiwa usiuze popote halafu yanakutwa na mvua yananyeshewa yako hadharani. Wakati huo yananyeshewa yule aliyeelekeza kwamba usiuze popote hayupo kwenda kuyafidia yanakutana na mazao mengine, hii inatengeneza umaskini kwa wakulima wetu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachokifanya ni kipi, leo hii imetokea, mazao tunayotumia sasa hivi kama alivyosema Waziri wa Kilimo ni yale mazao ambayo uzalishaji wake mbolea ilikuwa zaidi ya shilingi 120,000. Bunge hili lilipiga kelele kubwa sana kuhusu bei ya juu sana ya mbolea mwaka jana! Haya ndiyo mazao yanayotumika sasa hivi, yamezalishwa kwa gharama za juu sana. Mafuta yalikuwa juu ilikuwa kabla ya ruzuku, mbolea ilikuwa juu ilikuwa kabla ya ruzuku, ndiyo yaliyozalishwa sasa hivi. Itakuwa ni ukatili sana kwa Serikali ukienda tu uweke maelekezo tu ya moja kwa moja kwamba wewe uza shilingi 100 debe hili hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya nini kwa kutambua hivyo? Serikali ndiyo hicho alichofanya Mheshimiwa Samia katika mwaka huu wa Fedha, katika haya mazao ambayo ndiyo tunatarajia kuyavuna, ameweka nusu bei ya mbolea kwenye kila mfuko Serikali ibebe, impunguzie gharama mzalishaji kwenye mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikaweka ruzuku kwenye mafuta Bilioni 100 kila mwezi ili kupunguza gharama ya usafirishaji na gharama ya uzalishaji. Sasa mazao yatakayovunwa yaliyotumia ruzuku tunayatarajia yawe na bei ya chini. Hivyo ndivyo uchumi unavyopaswa kwenda lakini leo hii tukisema tu kwamba, mtu yuko pale kwenye uzalishaji anasema Serikali inajificha tu kwenye Ukraine, Sisi tumezalisha hapa hapa kwa nini bei iko juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezalisha hapo kwenu ndiyo mmezalisha Mwanzugi lakini Mwanzugi hamtengenezi Mbolea. Mbolea mliyotumia kuzalishia ni ya bei ya juu, ndiyo hiyo iliyosababisha yale yatakayozalishwa kama mfuko ulitumia wa shilingi 140,000 au shilingi 120,000 ni lazima yale mazao hata kama umeyazalisha kijijini kwako yatakuwa ya bei ya juu. Bado usafiri, kama mafuta unayotumia kusafirisha yako juu utazalisha nyumbani kwako pale pale lakini bado

yatakuwa na bei ya juu! Ndiyo maana Mheshimiwa Rais akasema tuweke ruzuku ili kupunguza pale mtu alipozalishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu Serikali haijaishia hapo kushughulika na suala la mfumuko wa bei. Baada ya kuwa imefanya hivyo imetoa akiba yake kwenye maghala ya chakula kwenda kupeleka kwenye soko na kuwapelekea wale ambao ni kaya zenye uwezo mdogo kukabiliana na jambo la aina hii. Ni lazima tunapoelezea matatizo yaliyopo tuelezee na hatua zinazochukuliwa, tusioneshe ufahari katika kuwatajia Watanzania matatizo. Unawatajia tu bei kwamba kuna bei hii, bei hii iko juu wanazijua kila siku wananunua hivyo vitu. Taja kama unaona hatua zilizochukuliwa na Serikali hazitoshi taja za kwako mbadala kwamba Serikali iongeze hatua hii, hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokuwa makini tutafanya kila kitu kwa kuhemka, leo hii tunavyoongea ninyi Wabunge mmetoka wiki moja kule Majimboni, mkirudi wengine wanakaribia kuanza kuvuna mazao yao, sasa mnataka leo tuagize mahindi ya Pakistan, tuagize mchele wa Pakistan uje ukutane na uzalishaji wa wazalishaji wetu, Bunge lijalo usimamishe shughuli za Bunge tujadili mazao ya wakulima hayana bei yatakuwa yamekutana *flooding*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara zote ukiona kelele zinapigwa kwenye haya mambo ya dharura kuwa makini sana, wakati mwingine unaweza ukabeba na *deal* za watu humo humo, lazima tuwalinde wakulima wetu na lazima tuwalinde walaji wetu, ni lazima tu-*balance*. Wananchi wengi wanaona umachinga unaweza ukalipa kuliko kilimo, kwa sababu gani? Kwa sababu tunaki-*mistreat* kilimo. Mimi nimekulia huko najua jinsi ilivyo kazi kulima asubuhi mpaka jioni halafu uhangaike kutunza yale mazao, halafu uvune. Lazima tuwalinde hao watu, halafu ushuhudie yananyeshewa

mvua hayana pa kupeleka. Tulinganishe hata hizo bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie lingine ameongea tena Ndugu yangu na jirani yangu kwamba *reserve* zinashuka sana, akilinganisha kwamba mwaka juzi *reserve* zilikuwa Dola bilioni 6,000 sasa zimesharudi bilioni 4,500. Jamani haya masomo ya uchumi ni sayansi, narudia tena, twendeni tufuatilie kwa makini *reserve* zina-*build* vipi, *reserve* zinaongezeka vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipokuwa 6,300 tulikuwa na Trilioni Moja tumeitoa *IMF* ndiyo ikaongeza ile *reserve,* sasa tumeichukua ile tumejengea madarasa yote unategemeaje *reserve* iwe ile ile? Iliongezeka kwa sababu tulipokea kwa mkupuo trilioni 1.3, tulipoitoa tukajengea madarasa ni kweli itashuka, sasa shida iko wapi? Haya ndiyo matatizo ya kutaka kuonea huruma mbegu, unaogopa kupanda mbegu kwa sababu ghala litapungua, panda ili uvune zaidi, ndicho tulichofanya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulileta kwa ajili ya madarasa na vitu vingine, baada ya hapo tumeitoa, ni kweli *reserve* zitashuka! Lakini siyo hilo tu, *reserve* pia ni *function* ya *import* na *export,* uwiano au mizania yetu ya *importation* ni kubwa kuliko *exportation,* sababu moja ya msingi ni kwamba tunayo miradi mikubwa kuliko nchi zote za *SADC,* vitendea kazi vyote tunavyojengea miradi hii tuna-*import*. Uki-*import* kilo moja ya tumbaku na vyuma vilivyoenda kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere mizania yake hailingani. Uki-*export* kilo kadhaa za mafuta ya alizeti hapa, galoni kadhaa za mafuta ya alizeti ya Singida, mizania yake na *importation* ya *material* tunayotumia kwenye reli, mizania ya reli ni kubwa, kwa maana hiyo mizania ya *export* na *import, import* ziko juu kwa sababu ya miradi mikubwa. Tuna daraja la Busisi unategemeaje *reserve* ziwe zile zile tu. *You can't eat the cake and have it!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi sana kutumia Bunge lako kufundisha mtu yule yule ambae ametaka kwa maksudi kutokuelewa! Haiwezekani tukawa tunatumia muda wa Bunge kujadili kitu kile kile tunataka ku-*achieve* kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna mashaka kuhusu *reserve* nchi yetu iko na zaidi ya miezi ya 4.7 ya *importation*. Wastani ni miezi Minne tu, tuko makini kwenye hilo. Hata ya Deni la Taifa tuna asilimia 73 ya mikopo yetu tangu uhuru imekopwa kwa *consessional* miaka 40 kipindi cha malipo na *grace period* miaka 10, *interest rate* 0.75, asilimia 73 ya mikopo ni *consessional*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia hii 26 inayosalia ni *commercial* ambayo tumeamua kukopa kwa sababu miradi hiyo isingeungwa mkono. Jamani, tumesahau sasa hivi tu vita ya kiuchumi tumeimba muda siyo mrefu. Ulikuwa na *option* moja tu ama uache miradi hiyo, ama tukope *commercial*, tukasema tukope *commercial* tuweke *back born* ya uchumi wetu na *backbone* ya uchumi wetu tunao uhakika italipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhakika reli italipa, bwawa la Mwalimu Nyerere litalipa, sasa hapa unatishatisha watu kwa ajili ya nini? Ni wahakikishie na wala hata siyo mbaya kwa sababu hii siyo *Honorary Doctorate* nimeingia darasani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Samia mbinu alizochukua na *vision* aliyoiweka kwenye masuala ya kiuchumi siyo ya kutiliwa mashaka. Wafuatilieni wabobezi wa IMF, *World Bank*, wafuatilieni Wachumi wote wanao-*classify* kuhusu uchumi, wanasema uchumi wa Tanzania unaelekea pazuri, uko pazuri na unaelekea pazuri. Haya siyo maneno ya Mwigulu! *IMF* wamesema hivyo, *World Bank* wamesema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache kujidharau dharau, Watanzania tumezoea sana kujidharau. Hata juzi imetoka *classification* kwamba *league* ya Tanzania ni ya Tano, jamaa mmoja anasema haiwezekani *league* yetu haiwezekani *league* yetu ikawa ya tano. Sasa wewe unaumwa nini Tanzania ikiwa inafanya vizuri!*(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majirani wote wanasema Mheshimiwa Rais Samia unaupiga mwingi majirani wote, kote juzi tulikuwa kwenye jukwaa la uchumi la Dunia, *(World Economic Forum)*, miadi ya watu kumuona Mheshimiwa Rais ilikuwa haina hata nafasi, wanaona uchumi wa Tanzania ulivyo imara na matarajio yake yalivyo imara. Halafu sisi kutwa tunaona hatuendi vizuri!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutofautishe mfumuko wa bei na bei, mfumuko wa bei ambacho ndiyo Wachumi huwa wanapambana nacho kila wakati ni kiwango cha kubadilika kwa bei siyo bei! *Inflation is the rate of average change of prices, not prices*. Bei ni *function* ya *cost of production* na *cost of transportation*. Kama mtu kanenepesha ng'ombe wake kwa Milioni Moja huwezi kumwambia bei yake iwe Laki Mbili, hiyo ni kuu sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei wa Tanzania siyo kama nchi zile ambazo asubuhi unabadilika, saa nne unabadilika, saa tano unabadilika, saa sita unabadilika, huo ndiyo mfumuko wa bei ambao *it is a problem* kwenye uchumi. Kama tatizo ni bei zinashughulikiwa kwa hatua hizi ambazo Mheshimiwa Rais amezichukua za kuongeza uzalishaji. Hatuwezi kuwa unatumia udikteta kwenye shughuli ambazo watu wamewekeza nguvu, wamewekeza fedha, wamewekeza muda. Kwa hiyo, hii hatua ambayo Mheshimiwa Rais amelchukua *actually* ni *long-term* na itaenda kuhamisha watu kutoka mijini kwenda vijijini siyo siku nyingi. Tukifanya kilimo kikawa kinalipa tutaondoa *rate* hii ya

*unemployment* na hii misongamano ya mjini lakini pia *GDP* itaongezeka. siyo hilo tu, *per capital income* itaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasema mwenyewe tu leo, Mzee Kimei kasema, Balozi wa Kodi Mheshimiwa Subira Mgalu pia kasema, na wengine nao humu wameyaona kwa namna hiyo. Ningeshauri sana Bunge lako Tukufu liwe linatoa ushauri kwenye jambo la dharura, tulenge hilo la dharura halafu tumalize tuendelee na mambo mengine tusiwafanye wananchi wa-*panic* wananchi. Tunawapanikisha wananchi. Uchumi ni basi tu *stock exchange* hai-*determine* sana maisha mengine, nchi zingine ukitoa kauli moja tu unashusha uchumi chini kabisa, kwa hiyo tusiwe tunatoa toa kauli za unazuiwa hapa unapita hii, unazuiwa hapa unapita hii! Tuna-*hinder investment*, Rais anafanya kazi kubwa ya kuita *investment* sisi tumekazana kusema hii mbaya hii mbaya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakuongeza dakika nyingine moja kwa ajili ya kuhitimisha hoja yako.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niliseme hili kwa msisitizo kwamba unaenda vizuri, yale yaliyo maoni tumeyapokea tutayaboresha, bahati nzuri sana maoni haya mengi tunatumia tunapokea kwenye Kamati lakini pia na Bunge zima hili. Kwa hiyo, tutaendelea kuyafanyia kazi yale lakini nitahadharishe tena, tusije tukawa tunajipaka taswira ambayo hatuna. Hali ya Dunia nzima wameongea pia Wabunge wengine, ina madhara kwa namna moja ama nyingine ndiyo maana tunachukua hatua za ndani kuweza kukabiliana nayo, Mheshimiwa Rais jitihada alizofanya ndiyo zinazotofautisha na maeneo mengine, tunakoenda tutakuwa hata imara zaidi kuliko hata hivi tulivyo. Nakushukuru sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ninawaita watoa hoja, tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya

Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Vita Kawawa aweze kuhitimisha hoja yake.

**MHE. VITA R. KAWAWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja niliyowasilisha asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ya NUU - Nje, Ulinzi na Usalama imechangiwa na wachangiaji Tisa, nikianza na Mchangiaji wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Mbogo ambaye alizungumzia diplomasia ya uchumi, alieleza Mikoa ya pembezoni mipakani ipewe elimu ya diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tulishatoa mapendekezo kwamba Bunge liazimie Serikali iandae mpango mkakati wa utekelezaji wa kidiplomasia ya uchumi nchini ikiwemo kuwapa elimu ngazi za Mikoa na Wilaya. Tunashukuru Wizara hapa imejibu na kuomba iruhusiwe ipate kuanza na mkakati mmoja, nasi kwa niaba ya Kamati tunakubali hilo. Pili, kupatiwa fedha Wizara ya Mambo ya Nje kukarabati Balozi zetu na kujenga, Kamati tulishatoa mapendekezo kushirikisha sekta binafsi, na sekta za umma katika ujenzi wa majengo ya Balozi na vitega uchumi kutarahisisha upatikanaji wa fedha na ujenzi wake kukamilika kwa haraka na hivyo kuwa na majengo ambayo yanastahili kwa hadhi ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa pili, alikuwa Mheshimiwa Felister Njau, yeye amesisitiza upatiakanaji wa fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge, kwamba mtiririko wake hauridhishi kwa Wizara zetu tunazo zisimamia, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa hili mimi sina la kusema zaidi, ninaamini Serikali imekusikia na ninaamini italifanyia kazi. Kwa nyongeza tu Bunge linapotoa maazimio kuhusu mambo mahsusi linafanya kazi hiyo ili kuhakikisha

kwamba tija iliyokusudiwa inafikiwa kwa ustawi wa wananchi. Hivyo ulinzi na usalama wa raia ni ustawi wa wananchi wake. Tukiwa na amani ndivyo hata tunaweza kufanya kazi nyingine. Hata hivyo, tuko hapa Bungeni kwa sababu ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vyema sana Bunge linapotenga na kuidhinisha fedha kwa ajili ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, tunaiomba Serikali ivipe kipaumbele vyombo vya ulinzi na usalama ili waweze kufanya kazi yake inavyotakiwa. *(makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Faharia pia alizungumzia *PAROLE;* Kamati ya NUU ilikwishatoa maelekezo kwa Wizara ya Mamabo ya Ndani ya Nchi kufanya tathmini ili kubaini changamoto ya utekelezaji wa Sheria ya *PAROLE* ili kuchukua hatua stahiki kuziboresha. Hata hivyo alizungumzia kuhusu Sera ya Mambo ya Nje; ni matumaini yetu Kamati na Bunge, Serikali itakamilisha maboresho ya Sera ya Mambo ya Nje mapema kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Condester Sichalwe, naye alizungumzia kuhusu *COMESA*. Serikali imesikia na imetoa ufafanuzi hapa; ila ushauri wetu sisi kama Kamati, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ije kutupa elimu, kutueleza kwa kina ili tuwe na uelewa wa pamoja kuhusiana na hii *COMESA*. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri amepata muda mchache akalielezea kwa uchache; lakini kama akipata nafasi tunaomba uweze kuja na timu yako kulielezea Bunge kuhusiana na huu mtangamano na kujitoa kwetu *COMESA* na nini maana yake. Hata hivyo, tunafahamu kuna hii *Tripartite,* kuna *EAC* na *SADC*. Faida tunazozipata umezielezea hapa kwa ufupi. Hata hivyo, tungependa pia ungekuja kulielezea Bunge zima kama semina ili liweze kuelewa kwa makini kuhusiana na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Neema Lugangira, yeye alizungumzia ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa *diaspora* kupata hadhi maalumu? Nadhani Waziri amelijibu vizuri suala hili, lakini sisi kama Kamati tunasisitiza Serikali ikamilishe mchakato huo ili hii kazi iweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chumi naye alieleza kuhusu vijana waliopelekwa Israel kusomea kilimo cha kisasa, kwamba wanaporudi waunganishwe na vijana wa JKT na *block farming* zinazoanzishwa na vijana wengine. Mheshimiwa Chumi hili naamini Serikali imekusikia na naamini watalifanyia kazi. Serikali ina wajibu pia wa kuisaidia *NIDA*. Hoja yake ya pili, kuhakikisha inakamalisha utoaji wa vitambulish. Ni kweli, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuiwezesha *NIDA* kwa wakati ili kukamilisha zoezi hili; na tumesisistiza sana jambo hili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Mheshimiwa Getere pia aliongezea kwenye hili, alisema tuambiwe ni lini kazi ya kutoa vitambulisho inakamilika au inaisha lini kazi hii? Ushauri wa Kamati, Serikali iendelee kuipatia fedha kwa wakati *NIDA* kama zilivotengwa na kuidhinishwa na Bunge ili kuharakisha utambuzi, usajili na kuchapisha vitambulisho na kuvisambaza kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Londo naye alitoa ushauri kuhusu diplomasia ya uchumi. Kamati imepokea ushauri wake na tunaamini Serikali pia imemsikia ushauri wake, na kama haikumsikia vizuri, basi tunaomba iitishe *Hansard* ili iweze kumsikia na kuona jinsi gani ya kutekeleza ushauri wa Mheshimiwa Londo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Ally Kassinge naye alizungumzia mtiririko wa upatikanaji wa fedha katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Mimi ninaamini Serikali na Wizara ya Fedha, hususani Wizara ya Fedha imekusikia vizuri sana. Hata hivyo Kamati inapendekeza

maazimio na haya yote ambayo yamo tunaomba Bunge liridhie ili yawe maazimio ya Bunge na Serikali iyafanyie kazi. Maazimio yetu yote tuliyoomba tunaomba Bunge liweze kuridhia ili yafanye kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengine walikuwa Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Bashe Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa *Engineer* Masauni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Stegomena Tax Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Innocent Bashungwa Waziri wa Ulinzi na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Fedha. Tunawashukuru sana wote mliochangia mchango huu na ninaamini Serikali imewasikia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo baada ya kutoa ufafanuzi wangu naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Pamoja na maoni na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(makofi)*

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyeiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa Mkono. Sasa nitawahoji na nitalihoji Bunge. Wanaoafiki hoja ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo waseme ndiyo, na wasioafiki waseme siyo. Basi hoja imeungwa mkono kwa asilimia 100.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti ili sasa aweze kuhitimisha hoja yake; Mheshimiwa Sillo!

**MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kwa kushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuhitimisha hoja ambayo iko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamechangia Waheshimiwa Wabunge 15 na Waheshimiwa Mawaziri watu; Mheshimiwa Waziri wa kilimo, Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi Mheshimiwa Bashungwa pamoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Mawaziri kwa sababu wote wameunga mkono hoja. Nawapongeza na ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni mengi yamechukuliwa na Serikali katika kuyafanyia kazi lakini ningependa kuongeza mambo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, limezungumzwa sana kuhusu Deni la Serikali. Naomba niwahakikishie na niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wabunge kwamba, Deni la Serikali kwa Biashara zote za kimataifa liko himilivu kwa viwango vyote vya kimataifa. kwa hiyo, tusiwe na wasi wasi Deni liko salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati ya Bajeti tumejiridhisha, tumepitia hii mikopo yote inayokuja na tumehakikisha kwamba hakuna kifungu chochote cha Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya Serikali Sura ya 130 ambacho kimevunjwa. Kwa hiyo, mikopo imekopwa katika uhalali wake na iko ndani ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Tano cha Sheria ya Matumizi, kinampa Mamlaka Waziri wa Fedha kukopa kiwango chochote cha Fedha ambacho kimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo mikopo yote imekopwa kutokana na sheria ambayo imetu-*guide,* Sheria ya Matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye deni hilo hilo mwezi Juni, 2022 deni lilikuwa trilioni 71.56 lakini kufika Disemba, 2022 deni lilikuwa ni shilingi trilioni 74.64, ongezeko la shilingi trilioni 3.08 ambayo ni *growth rate* ya asilimia 4.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo Mjumbe alichangia limekuwa kwa asilimia 12,13 lakini uhalali ni kwamba imekua kwa asilimia 4.3, kwa hiyo deni liko salama na liko himilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu mfumuko wa bei. Kwa nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo iko na asilimia tano mpaka sasa. Ukiangalia nchi kama Rwanda asilimia 23.7, Kenya asilimia 9.7 na Uganda asilimia 9. 7. Kwa hiyo sisi tuko salama kwa maana ya mfumuko wa bei pamoja na changamoto ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa kwamba mfumuko wa bei unatokana na usimamizi mbovu wa sera za fedha pamoja na Bajeti. Kwa hiyo, naomba niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wabunge, kwamba nchi iko salama katika suala hili la mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni eneo la mifumo ya TEHAMA ya kukusanyia mapato. Mifumo ya *TRA* tuna mifumo ya *TANCIS* Pamoja na Mfumo wa *IDRAS***.** Mifumo hii haisomani na Mfumo wa *TPA* wala Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo niombe sana Serikali katika eneo hili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha unanisikia, naombeni sana mkaboreshe mifumo ya ukusanyaji wa Mapato. Mifumo inapokuwa haisomi na ni ya taasisi moja ni changamoto. *TRA* wenyewe kuna Mfumo wa Forodha wa

*TANSIC* lakini kuna kodi za ndani wa *IDRAS* hii yote yenyewe haisomani. Kuna changamoto na Mapato yanapotea. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri hili mlichukue mboreshe sana maeneo haya mifumo iweze kusomana ili tuweze kukusanya mapato yetu ya Serikali kwa ajili ya kusaidia shughuli za maendeleo pamoja na huduma za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuiwezesha kampuni ya Mbolea. Kampuni ya mbolea imeomba ipatiwe mtaji wa bilioni 60 ili iweze kusambaza mbolea kwa wakulima wetu. Tuiombe sana Wizara ya Kilimo kampuni hii ya mbolea muiwezeshe ili iweze kuagiza mbolea moja kwa moja kutoka kwa ma-*supplier.* Hivi sasa wananunua kwa mawakala kwa hiyo hawawezi kushindana na wauzaji wengine wa mbolea hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwenye huu Mkopo wa *ECF* ambao ni trilioni 2.4. Mkopo huu wa trilioni 2.4 si wa mwaka mmoja, huu ni mkopo wa miezi 40 kuanzia Julai, 2022 hadi Julai, 2025. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na ambao tumepitisha ndani ya Bunge lako Tukufu, kwenye bajeti tumetenga shilingi bilioni 760; na mwezi Agosti, 2022 tumepokea awamu ya kwanza ya bilioni 349.8 na awamu ya pili mwaka wa fedha 2023 tutapokea mwezi machi, 2023. Kwa hiyo mkopo huu si kwamba wote umepokelewa kwa mara moja. Maana kuna Mjumbe ameongea kuwa kuna hela zinaingia nje ya bajeti, hapana. Ndani ya bajeti mwaka wa fedha 2022/2023 ni bilioni 720 na awamu ya kwanza kama nilivyosema ni bilioni 349. Niiombe tu Serikali, kule ambako mkopo umeelekezwa muweze kuusimamia vizuri hasa zile za uzalishaji. Umeenda kilimo, nishati na mifugo na uvuvi, hizi zote ni sekta za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mkopo huu ni katika kuboresha urali wa malipo na urali wa biashara kati ya nchi yetu na nchi nyingine hapa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja pia nizungumze, kuhusu *reallocation* ndani ya mafungu na pia nje ya mafungu. Kifungu cha 41(8) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Kanuni zake zinamtaka Waziri wa Fedha kuwasilisha taarifa ya uhamisho wa ndani *(within the votes)* au nje au *between votes* mara baada ya nusu mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge lako Tukufu, kwamba uhamisho kwa mwaka wa fedha 2021/2022 uliwasilishwa kwenye Ofisi ya Bunge tarehe 1o Novemba, 2022. Hata hivyo, kwa nusu mwaka hii ya mwaka wa fedha ambao tunaendelea nao, wa 2022/2023, ripoti hii itawasilisha kwenye Ofisi ya Bunge Mwezi Machi 2023. Taarifa hii inapatikana kwenye ukurasa wa 72 wa taarifa ya Kamati ya Bajeti kipengele cha 7.7 na kiambatisho (B) ambacho pia kimeambatishwa kwenye taarifa yetu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa pia kulizungumzia ni eneo la Sheria yetu ya Manunuzi. Sheria yetu ya manunuzi ina changamoto, wote tunakubali; kwamba Sheria yetu ya Manunuzi inachukua muda mrefu sana. Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kuishauri Serikali na Serikali ilikubali, kwamba sheria hii itafanyiwa marekebisho. Sasa tuiombe Serikali iwaishe muswada wa sheria katika mwaka huu wa fedha wa 2023/2024 ili Sheria ya Manunuzi tuibadilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna miradi mingi sana, Mheshimiwa Bashe amezungumza hapa, kwa mfano kwenye Tume ya Umwagiliaji tumetengea shilingi bilioni 215 lakini utoaji wa fedha mpaka sasa ni asilimia kidogo sana. Hata hivyo ukiongea na Serikali wanasema tayari fedha ziko kwenye *commitment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* hii inacheleweshwa na Sheria hii ya Manunuzi. Kwa hiyo naomba muswada huu uletwe haraka iwezekananvyo ili Sheria hii ya Manunuzi tuibadilishe. Tusiicheleweshe wenyewe, nchi hii ni yetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja la mwisho, si kwa umuhimu, ni miradi ya muda mrefu; amezungumza Mheshimiwa Waziri Kiongozi Mstaafu, Mheshimiwa Shamsi Vuai Naohodha, kuhusu Miradi ya Mchuchuma na Liganga pamoja na gesi asilia. Miradi hii ikikamilika itaokoa sana fedha za kigeni tunazoagiza chuma kutoka nje pamoja na maeneo mengine. Kwa hiyo niombe sana Serikali iharakishe majadiliano ya miradi hii ili iweze kukamilika kwa wakati ili kuokoa fedha za kigeni ambazo zinatumika kuagiza chuma na bidhaa nyingine nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninaomba sasa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti yawe Maazimio ya Bunge zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na idadi ya kutosha kabisa ya Wabunge, sasa nitawahoji. Wanaoafiki hoja ya Kamati ya Bajeti pamoja na Maoni na Mapendekezo yake yaliyomo katika taarifa hii waseme ndiyo, na wasioafiki waseme siyo. Hoja imeungwa mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Nitumie nafasi hii kushukuru Kamati zetu zote mbili, kwa maana ya Kamati ya Bajeti na Kamati ya

Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa ripoti nzuri sana na wajumbe husika wa Kamati hizo. Pia tuwashukuru Wabunge wote waliochangia leo na *flexibility* ya Serikali katika kuchukua maoni ya Wabunge na kwenda kuyafanyia kazi. yapo ambayo yamezungumzwa kwa sababu ya muda yapo pengine yasingeweza kuzungumzwa lakini tunaamini kwa ujumla wake Serikali itayachukua na kwenda kuyafanyia kazi.

Shughuli tulizopanga kuzifanya leo zimekwisha hivyo ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 19:57 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 7 Februari, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*